**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 1 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:**

Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa miaka ya 2003/2004 na 2004/2005.

**NAIBU WAZIRI WA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. JANETH M. MASSABURI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha uliopita pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 328

**Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. LUCAS L.SELELII (K.n.y. MHE. LEKULE L. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa, uharibifu wa mazingira unaendelea katika maeneo mengi na hivyo kusababisha hasara na maji kupungua kwenye maziwa kama Victoria na Jipe:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuokoa maziwa hayo?

(b) Kwa kuwa, Ziwa Jipe limejaa magugu maji yaliyoanza kuelekea Bwawa la Nyumba ya Mungu na kusababisha samaki kupungua na wengine kutoweka je, Serikali ina utaratibu bani wa kuondoa magugu maji hayo ili kuokoa Ziwa hilo?

(c) Kwa kuwa, wananchi wanaotegemea samaki wa Ziwa Jipe hawana kipato tena kutokana na kupungua kwa samaki. Je, Serikali itawasaidiaje ili wapate kipato mbadala?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali, kwa kushirikiana na taasisi nyingi na wananchi, inatekeleza programu, mipango na miradi mbalimbali ya kuyanusuru maziwa yetu. Kwa Ziwa Victoria juhudi za muda wa kati za Tanzania na nchi zilizo jirani zimelenga katika kuboresha mazingira ya bonde kupitia Programu za Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*LVEMP*) na Bonde la Mto *Nile*.

Udhibiti wa magugu maji (*water hyacinth*) katika Ziwa Victoria chini ya awamu ya kwanza ya programu umehusu, ujenzi wa vituo vya kuzalisha na kusambaza wadudu wa kushambulia magugu maji waitwao mbawakavu (*weevils*). Hadi sasa vipo vituo 14 na mbawakavu waliozalishwa ni milioni 60. Juhudi nyingine zimehusu kutumia zana nyepesi kuondoa magugu maji ziwani.

Awamu ya pili ya programu itahusu kubuni njia mbalimbali za kuyaondoa magugu maji, kudhibiti uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria, hifadhi ya maji na udongo katika bonde la Ziwa na uvuvi endelevu. Awamu hii, itazihusisha pia Rwanda na Burundi hasa tukizingatia kwamba, Mto Kagera umeendelea kuingiza magugu maji Ziwani kwa kasi zaidi

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira, Serikali imeandaa Mkakati wa Hatua za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mabwawa na Mito. Katika kutekeleza Mkakati huu, Serikali itachukua hatua za muda mfupi, muda wa kati, na muda mrefu kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira ya maeneo haya.

(b) Mheshimiwa Spika, inakisiwa kuwa asilimia 65 za Ziwa Jipe kwa upande wa Tanzania tayari imefunikwa na magugu yanayojulikana kama *makurovira* kwa Kipare na Kitaveta, nimelipata hili kwa hisani ya Mheshimiwa Prof. Maghembe, au *Typha demongensis*, Kilatini.

Serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi imefanya tafiti kuhusu jinsi ya kuondoa magugu maji hayo. Baadhi ya mapendekezo yamekuwa kuyaondoa kwa kuyaburuza au kuyakatakata, kutumia mashine, kutumia wadudu na kutumia madawa ya kuua mimea.

Matumizi ya madawa yanaweza kuleta athari kubwa zaidi kwa mazingira ya binadamu na viumbe. Matumizi ya wadudu kama mbawakavu si rahisi kwa mazingira ya Ziwa Jipe. Kwani magugu hayo ni ya asilia katika ikolojia ya Afrika kuanzia Mto Limpopo mpaka Kaskazini mwa Sudan katika bonde la *Nile*. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya inaandaa programu ya pamoja na usimamizi wa ikolojia za Ziwa Jipe, Ziwa Chala, Mto Lumi na Mto Umba ambayo itahusu matumizi endelevu, hifadhi, na usimamizi wa maliasili ya ikolojia hiyo. Programu itahusika pia na uondoaji wa magugu maji katika Ziwa Jipe. Kwa upande wa Tanzania programu hii inasimamiwa na Wizara ya Maji, kupitia Ofisi ya Maji ya Bonde la Pangani, tarehe 9 Oktoba, 2006 nilipata nafasi ya kutembelea Ziwa Jipe.

(c) Mheshimiwa Spika, Uharibifu wa mazingira na umaskini ni sehemu mbili za sarafu moja. Kuongezeka kwa magugu maji katika Ziwa Jipe kumeathiri sana kipato kwa jamii inayotegemea samaki wa Ziwa hili. Shughuli mbadala za kupunguza kutegemea uvuvi katika Ziwa Jipe ni pamoja na:- Ufugaji endelevu wa samaki; ufugaji bora wa mifugo; ufugaji wa nyuki na kurina asali; kilimo endelevu; uanzishaji wa vitalu vya miche; kupanda miti; kilimo cha mseto; uondoaji wa magugu Ziwani; na biashara ndogo ndogo. La msingi katika juhudi hizi ni kuwawezesha wananchi wapate mikopo kupitia benki ya *SACCOS*. Katika hili wananchi wa Mwanga wana bahati kubwa ya kuwa na Benki ya Jamii ya Mwanga. Wanashauriana wajiunge katika vikundi ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo hiyo. Kwa kuuliza swali hili Mheshimiwa Laizer amethihirisha kwamba hakika yeye ni mwana mazingira.

**MHE. LUCAS L.SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika Ziwa Jipe ambao ni ziwa liko katika nchi mbili yaani mpakani kabisa mwa Tanzania na mpakani kabisa mwa nchi ya Kenya, jirani zetu. Lakini cha ajabu kwa upande wa Tanzania Ziwa Jipe hili limejaa mgugu mengi zaidi kuliko upande wa pili wa majirani zetu upande wa Kenya. Je, ni sababu zilizosababisha upande wetu wa Tanzania kukawa na magugu maji na upande wa pili wa jirani zetu kukawa hakuna magugu maji?

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu Ziwa Victoria, miaka ya hivi karibuni magugu maji yaliyotoweka kabisa katika Ziwa Victoria lakini sasa yameanza kuonekana yakija kwa kasi kubwa sana kuliko hata ilivyokuwa kule awali. Pamoja na juhudi za kuwa mbawa kavu je, ni hatua gani za ziada ambazo zinaweza kunusuru Ziwa hili lisiingiliwe na magugu maji kama ambavyo ilifanyika hapo awali?

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selelii kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba Ziwa Jipe limejaa magugu maji upande wetu zaidi kuliko upande wa Kenya na kuna sababu mbili, sababu ya kwanza ni kwamba upande wa Kenya ni tambarare na upande wa Tanzania Ziwa Jipe linapakana na milima ya upare, kwa maana hiyo upande wetu limejaa tabaki zaidi kuliko upande wa Kenya kwa maana udongo ambao unapelekea mgugu kuota zaidi upande wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini sababu ya pili ni kwamba upepo unavuma kutoka Mashariki kwenda Magharibi katika eneo hilo kwa hiyo magugu maji mengi ambayo yako upande wa Kenya yameletwa upande wa Tanzania kama Visiwa na upepo ambao unatoka Mashariki kuja Magharibi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ambalo linahusu magugu maji katika Ziwa Victoria, tuliweza kufanikiwa kwa asilimia 90 kuyaondoa magugu maji katika Ziwa Victoria katika mradi wa *LVEMP* mradi wa kwanza wa hifadhi ya mazingira ya Ziwa Victoria, sana sana kwa kutumia mbawa kavu lakini vile vile kwa kutumia njia mbadala kama vile kuyang'oa na kutumia mashine katika maeneo mengi hasa katika mialo katika Ziwa Victoria. Wote tumegundua kwamba kuna ongezeko kubwa la magugu maji na kama nilivyosema Rwanda na Burundi ambao vile vile wako katika Bonde la Mto Kagera walikuwa hawajahusika na mradi mkubwa wa *LVEMP* hapo mwanzo na tumegundua kwamba magugu maji mengi bado yanaendelea kuja kutoka maeneo ya Kagera kupitia Mto Kagera kuingia katika Ziwa Victoria.

Kwa maana hiyo katika awamu ya pili ya mradi wa *LVEMP* ndio maana tunaingiza nchi za Rwanda na Burundi katika mpango mzima wa kuendelea kutafuta jibu la hili tatizo ambalo linaonekana ni sugu lakini tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Ziwa Jipe linatumika kwa utalii upande wa Tanzania na Kenya, upande wa Kenya ziko

boti kazi yake ni kusukuma yale magugu yaje upande wa Tanzania na upande wa Kenya unabaki hauna magugu. Kwa hiyo, unakuwa *free* kwa watalii. Je, Waziri anasemaje kuhusu hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce Kimaro kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, hatuna taarifa kuhusu matumizi ya boti upande wa Kenya kuyasukuma magugu maji kuja upande wa Tanzania lakini kama hilo linafanyika basi ule mpango niliosema tunauandaa kwa pamoja kati ya Tanzania na Kenya kuhusu hifadhi ya Bonde la Jipe tutalishughulikia katika mpangilio huo na katika uhusiano mwema na ujirani tulio nao kati ya Kenya na Tanzania.

Na. 329

**Viwanda vya Usindikaji Mazao ya Mifugo**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa Maendeleo ya Sekta ya Mifugo yanategemea sana kuwepo kwa viwanda na masoko kwa ajili ya usindikaji wa mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali imebaini na kutekeleza mikakati gani ya kuwashirikisha wadau katika kuanzisha na kuendeleza viwanda vya usindikaji nchini na upatikanaji wa masoko ya mifugo nje ya nchi?

(b) Je, Serikali inakabili vipi tatizo la muda mrefu la kutopatikana kwa mikopo kwa wadau kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa viwanda vya usindikaji wenye hadhi ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ili sekta ya mifugo iweze kuendelea ni muhimu kuwa na masoko ya mifugo na viwanda vya kusindika mazao yake. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali kupitia Wizara yangu imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali inayowashirikisha wadau katika kuanzisha na kuendeleza viwanda vya usindikaji na masoko ya mifugo

Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ambayo ni mwongozo kwa wadau ikiwemo sekta binafsi ya kuwekeza katika viwanda vya kusindika bidhaa za mifugo na kuendeleza masoko yake. Aidha sheria mbalimbali zinazosimamia na kuratibu mwenendo wa sekta ya mifugo zimeandaliwa na kuboreshwa kuendana na mazingira ya sasa ya uchumi wa soko, mfano Sheria ya Maziwa ya mwaka 2004 na ya Sheria ya Nyama ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia imeendelea kuwahamasisha wadau wa mazao mbalimbali ya mifugo kupitia semina, vyombo vya habari na machapisho mbalimbali ili waunde umoja kuwawezesha kupata masoko, teknolojia, mitaji na huduma nyingine.

Baada ya kuhamasishwa, wadau hao wameanzisha vyama na vikundi vya usindikaji na uendelezaji wa masoko ya nyama na maziwa. Baadhi ya vyama na vikundi hivyo ni pamoja na Chama cha Usindikaji wa Maziwa (*TAMPA*), Chama cha Wazalishaji wa Maziwa (*TAMPRODA*), Chama cha Ushirika wa Maziwa Tanga (*TDCU*), Chama cha Wafanyabiashara wa Nyama (*TALIMETA*) na Chama cha Wasindikaji wa Ngozi (*LAT*).

Mheshimiwa Spika, wadau hao pia wameshirikiana kwa kuuziwa viwanda vilivyokuwa vya Serikali kama vile Viwanda vya kusindika maziwa vya Musoma na Tanga, Viwanda vya kusindika ngozi vya Morogoro, Mwanza na Moshi na kushirikishwa, kumilki na kuendesha machinjio ya Dodoma na kiwanda cha Nyama cha Shinyanga. Aidha, Serikali imedhamiria kushirikiana na watu binafsi kuanzisha viwanda vipya vya kusindika mazao ya mifugo tuna mfano wa Kiwanda cha Nyama cha Mvomero Morogoro na Kiwanda cha Safi Sumbawanga na pia hivi karibuni tulitangaza kwenye vyombo vya habari mwezi Julai, 2007 kuhusu uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo hususan nyama.

Mheshimiwa Spika, Katika juhudi za kukuza viwanda vya kusindika maziwa nchini, Serikali imeweka kodi mbalimbali kwenye bidhaa za maziwa zinazoingizwa kutoka nje. Kodi hizo ni pamoja na *Suspended Duty 25%,* kodi ya ongezeko la thamani 20% na ushuru forodha 25%.

Hatua hii inasaidia bei ya maziwa yanayosindikwa nchini kuwavutia walaji, maziwa yetu kununuliwa zaidi hivyo viwanda husika kuwa endelevu. Aidha Serikali imeweka kodi ya asilimia 20 kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa nje kama hatua ya kuhamasisha usindikaji nchini na inaangalia uwezekano wa kuongeza kodi ili kwenda sambamba na nchi zingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masoko ya mifugo ya mipakani, Serikali imejenga minada 13 mpakani maeneo ya Arusha, (Longido na Waso), Kilimanjaro (Kileo na Munga), Mbeya (Mpemba, Mara (Magena), Kagera (Mtukura), Rukole, Murusagamba na Rusumo, Kigoma (Buhigwe na Kakonko), Rukwa (Kasesya), ili kurahisisha biashara hiyo. Hata hivyo azma ya Serikali ni kukuza biashara ya nyama kuliko mauzo ya mifugo nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kukabiliana na tatizo la muda mrefu la kutopatikana kwa mikopo, Serikali imeweka utaratibu wa kudhamini wasindikaji na wajasiriamali wengine kupata mikopo kupitia benki za biashara. Taratibu hizo ni kupitia *Government Guarantee Scheme*, na *Export Processing Zones* na kutumia msaada na maelezo ya Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (*TIC*). Aidha, Serikali inahamasisha uundaji wa vyama vya kuweka na kukopa (*SACCOS*) kwa lengo la kupanua mitaji ya biashara.

Mheshmiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge hususan wale wanaotoka kwenye maeneo yenye mifugo mingi kushirikiana na Serikali kikamilifu kuhamasisha uwekezaji katika biashara ya mifugo na viwanda vya kisasa vya kusindika mazao ya mifugo. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri waliyonipatia lakini nilikuwa naomba kumwuliza maswali mawili madogo nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba tayari mikakati madhubuti imeshaandaliwa kwa ajili ya kujenga viwanda hivi vya kusindika mazao ya mifugo. Je, ni lini sasa viwanda hivyo vitajengwa katika mikoa mingi katika mikoa ambayo ina mifugo mingi ukiwemo Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika masoko au minada mingi ya kuuzia mifugo imebainika kwamba mizani mingi ni mibovu na hivyo inawasababishia wafugaji washindwe kupima wale wanyama wanapokuwa wanataka kuwauza. Je, ni lini sasa mizani hiyo katika minada hiyo itakarabatiwa? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosemary Kirigini, kama ifuatavyo. Kwanza ninamshukuru kwa kunipongeza kwa kujibu vizuri kwa sababu alihitaji jibu la makini.

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyopo kama nilivyosema tumeshatangaza ili kusudi wawekezaji wengine wengi zaidi waje, azma ya Serikali ni kuona kuwa ifikapo mwaka 2010 tuwe na viwanda na machinjio ya kisasa takriban kama 10 na katika matangazo tuliyotoa Mkoa wa Mara ni kati ya Mikoa ambayo tunahamasisha uwekezaji kwa makusudi kabisa kwa sababu ni kati ya mikoa ambayo ina mifugo mingi. Ninamuwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Mara washirikiane na Wizara ili kuona azma hii ya Serikali ya kuwa na machinjio au viwanda vya kusindika vya kisasa kule Mara kinajengwa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mizani nyingi kwenye minada haifanyi kazi na kusema kweli wafanyabiashara wengi hawapendi kuitumia. Azma ya Serikali hususan Wizara yetu ni kuona kuwa wafugaji wanauza mifugo yao kwa kupima kwa sababu hiyo itawezesha kupata fedha nyingi zaidi kuliko hali ilivyo sasa hivi na mara viwanda vitakapojengwa tunaamini kwamba mtandao huu wa uuzaji wa kisasa wa ng'ombe bora kwa kupima kwenye mizani utakuwa endelevu na kwa hiyo Wizara itahakikisha kuwa minada yote ina mizani ambayo inatumika barabara.

**MHE. DR. CHRISSANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kweli kuwa Serikali imeanzisha utaratibu wa kuweza ku-*guarantee* wananchi wajasiriamali na wanaokopa kuanzisha viwanda lakini Waziri atakubaliana nami kwamba benki zilizopo sasa ni Benki za Bishara na kwamba mikopo yao wanayotoa ni ya muda mrefu na riba ya juu kuliko kama vile tungekuwa na benki ambayo ni maalum kwa kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Chrissant Mzindakaya kama ifuatavyo. Ni kweli kwa sasa Benki zetu za Biashara zinatoa mikopo lakini mara nyingi mikopo hii ni ya muda mfupi na siyo muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko kwenye harakati za kukamilisha kuweka taratibu ambapo mabenki yataweza kutoa mikopo ya muda mrefu ili kuwawezesha wajasiriamali wengi kuweza kukopa lakini pia Serikali inajiandaa ili kuweza kuweka utaratibu ambapo kutakuta na benki zitakazotoa mikopo yenye riba nafuu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, kwa kuwa njia ya kuweza kwenda kwenye masoko kwa wafugaji zaidi wa Kanda ya Ziwa ni kuswaga mifugo yao na kwa kuwa njiani hawa wafugaji kila mara wanawekewa vizingiti vikubwa sana na watendaji na pia kwa kuwa kule mpakani inakuwa ni vigumu sana huu utaratibu uliopo wa Serikali kuweza kupitisha wale ng'ombe zao kwa mfano kwenda Kenya.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kurahisisha mauzo haya ya wafugaji ili iwe njia pia ya kujipatia pesa na pia njia ya kuweza kupunguza mifugo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Momose Cheyo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika Mashariki zimeweka taratibu za kuhakikisha kuwa biashara ya mipakani inafanywa kwa mujibu wa taratibu zinazolinda biashara endelevu ikiwemo biashara za mifugo. Kuhusu suala la wafugaji kuwekewa vizingiti katika uswagaji taratibu zipo za wazi kabisa kwamba kabla mfanyabiashara hajaswaga mifugo yake kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine anapewa vibali vinavyohakikisha kuwa mifugo ni salama dhidi ya magonjwa na kwa hiyo katika vituo vyovyote anavyopita ukaguzi ambao lazima ufanyike unazingatia kuwa ana vibali halali ili kumwezesha kufika kule anakoenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sioni kama kuna tatizo hasa kwenye suala hili la uswagaji wa mifugo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine katika maana ya biashara.

Na. 330

**Hali ya Watoto Yatima – Makete**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa UKIMWI ni janga la Taifa, linaloathiri vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa kwa ujumla; na kwa kuwa; Wilaya ya Makete ni Wilaya yenye watu wengi walioathirika na inao watoto yatima wasiopungua mia tatu (300) na wanaishi katika mazingira magumu majumbani; na kwa kuwa, baadhi yao wanaishi na dada zao wenye umri kati ya miaka 10 – 16 na mama wakubwa wanaosimamia watoto hamsini (50) kila mmoja; na kwa kuwa baadhi ya misaada wanayopelekewa kutoka katika Mashirika au Serikali haiwafikii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea nyumba watoto hao ili kuwakusanya pamoja kama ilivyo kwa Kituo cha Kuleana Mwanza na *Msimbazi Center* – Dar es Salaam ili kuwapunguzia makali ya maisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, ninaomba kutoa maelezo yafuatayo.

Ni kweli janga la UKIMWI limeathiri Wilaya karibu zote hapa nchini. Hata hivyo, Wilaya ya Makete imeathirika zaidi kwani taarifa na takwimu mbambali zinaonyesha kwamba Wilaya hiyo ina kiwango kikubwa cha watoto wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI, ambapo asilimia 22.4 ya kaya zote zimepoteza angalau mtu mmoja tangu mwaka 1998.

Kiwango kikubwa cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI na athari zake kimesababisha kuwepo idadi kubwa ya watoto na vijana wanaoishi katika mazingira magumu wilayani humo, kutokana a kufarikia kwa wazazi na au walezi wao. Kulingana na utafiti uliofanyika Wilayani Makete kuhusu utambuzi na uchambuzi wa watoto walio katika mazingira magumu, asilimia 16.3 ya watoto wote wilayani humo wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kutokana na ukubwa wa tatizo la watoto yatima katika Wilaya ya Makete, wengi wamekuwa wanalelewa na dada na kaka zao pamoja na mama wakubwa. Serikali kwa kupitia Programu ya Ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), imekuwa ikitoa misaada mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya malezi ya watoto yatima waliotambuliwa na kufanyiwa uchambuzi.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali yakiwemo Masharika yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Kidini, itaendelea kutoa misaada hiyo kwa kadri uwezo utakavyoruhusu. Hivi sasa Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kuwasaidia Watoto Yatima na Walio katika Mazingira Magumu zaidi, kwa lengo la kuhakikisha wanapata haki zao za msingi na huduma bora. Lengo la Serikali sio kuwaweka watoto hao katika vituo, kwa sababu kwa kufanya hivyo, watoto huathirika kisaikolojia. Serikali kwa kupitia Mkakati huo itahakikisha kuwa watoto hawa wanalelewa ndani ya familia zao ikiwa hapana budi, basi na jamii husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iko haja ya kuziwezesha familia na jamii mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kuwalea na kuwalinda watoto hao. Hii ni pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa familia na asasi za kiraia ndani ya jamii, kuandaa na kuteleza mipango ya kuhudumia watoto hao kwa kutumia rasilimali na fursa walizonazo kabla ya kuomba msaada kutoka nje ya mazingira yao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kabla sijakuita Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, kwa sababu tunazungumzia watoto napenda Waheshimiwa Wabunge mtambue kurejea Bungeni kwa Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, aliyekuwa katika likizo ya uzazi. Amejifungua salama tarehe 31 Mei, 2007 katika Hospitali ya Muhimbili, Saa nane usiku kwa *Scissorion Operation* lakini amerudi salama na mtoto wake ni wa kike anayeitwa Nazareth Mwampeta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika karibu.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, wahisani wanaotoa misaada hiyo wamebaini kuwa kuna ubadhilifu wa misaada yao. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa atakayebainika na ubadhilifu wa misaada inayotolewa na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na ya Kiserikali kuhakikisha inawafikia walengwa waliokusudiwa?

Kwa nini nchi nzima wameathirika na maandali haya ni kwa nini hayafanywi kwa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, kwa kupata mtoto aitwaye Nazareth Mwampeta, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ambao wanaonyesha ubadhilifu wa misaada ambayo inatolewa na asasi au *NGOs* pamoja na Mashirika ya Kimataifa hata pamoja na Serikali ni lazima wafuatiliwe na waadhibiwe kwa sababu watoto hawa wanahitaji mahitaji muhimu kwa mfano afya, elimu, upendo na kulindwa kwa kila aina. Kwa hiyo, wabadhilifu hawa kwa kweli ni wa kuadhibiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwamba nchi nzima imeathirika na kuna maandalizi gani ni kwamba, ni kweli kama nilivyosema Wilaya zote zimeathirika na tatizo hili la UKIMWI lakini tunajua kuna mipango mbalimbali ikiwemo juzi tu Mheshimiwa Rais kwa kuonyesha mfano amekwenda kupima, sote tunatakiwa kwanza tupime tujue hali zetu ili tuweze kujua tutasaidiwa namna gani aidha kwa kupewa dawa za kurefusha maisha na vilevile tukijijua tunaweza tukajilinda zaidi kwa lishe bora na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuko nyuma ya muda sana sasa lakini tuko katika Wizara hiyohiyo na swali linaulizwa na Mheshimiwa Charles Keenja.

Na. 331

**Huduma kwa Watoto Yatima**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:

Kwa kuwa, uchunguzi uliofanywa katika baadhi ya Shule za awali na za msingi katika Jimbo la Ubungo zinaonyesha kwamb zaidi ya asilimia 10 (10%) ya watoto wanaosoma kwenye shule hizo ni yatima na wengi wao wanaishi katika mazingira magumu sana.

(a) Je, tatizo la watoto yatima ni kubwa kiasi gani kitaifa na ni Mikoa ipi inayoongoza kwa kuwa na watoto yatima?

(b) Je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kuwahudumia watoto yatima na ni asilimia gani ya watoto yatima wanaofaidika na mipango hiyo, au jukumu hilo limeachiwa *NGOs?*

(c) Je, katika miaka miwli iliyopita, Serikali ilitenga kiasi gani cha fedha katika bajeti zakei li kuhudumia watoto yatima na inakusudia kutenga kiasi gani katika bajeti ya 2006/2007 na kitahudumia watoto wangapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye vipingele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tatizo la watoto yatima kitaifa ni kubwa. Takwimu za 2004 za *Rapid Assessment Analysis and Plan of Action* zinaonyesha kuwa idadi ya watoto yatima na walio katika mazingira magumu inakadiriwa kuwa ni 2,500,000 ambayo ni sawa na asilimia 12 ya watoto wote nchini. katika watoto hao, asilimia 53 wanaishi na kulelewa na mababu au mabibi zao, wakati asilimi 31 wanaishi na ndugu. Aidha asilimia 12 wanaishi na dada au kaka zao na asilimia 3 wanaishi na walezi wa kambo au wameasiliwa yaani wamekuwa *adopted*.

Kufuatana na takwimu ya sensa ya idadi ya watu na makazi ya mwaka 2002 idadi ya watoto wanaoongoza kaya nchini, ilikuwa ni zaidi ya 66,000. Tatizo la Watoto yatima ni kubwa na ongezeko lake ni la kasi kubwa na linachangiwa kwa kiasi kikubwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu umefanyika katika Wilaya 18 Tanzania Bara. Wilaya hizo ni Bagamoyo, Bunda, Jiji la Mwanza, Kibaha, Karagwe, Kibondo, Kisarawe, Magu, Makete, Masasi, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya Mtwara, Manispaa ya Temeke, Musoma Vijijini, Ngara, Singida Mjini, Singida Vijijini na Songea. Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa, kwa mwaka 2005 Wilaya zilizokuwa zinaongoza kwa idadi ya watoto yatima ni Karagwe watoto 13,765, Jiji la Mwanza watoto 10,270, Singida Vijijini watoto 10,252, Bunda watoto 9,968, Temeke watoto 9,645, na Makete watoto 6,889.

Mikoa inayoongoza kwa kuwa na watoto yatima wengi zaidi ni Mbeya, Dar es Salaam, Kagera na Iringa. Serikali ina mpango wa kufanya utambuzi wa watoto yatima

na walio latika mazingira magumu kwa nchi nzima kwa kuwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kupata takwimu za kila Wilaya. *(Makofi)*

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kasi ya ongezeko la watoto yatima na wale walio katika mazingira magumu zaidi, ilichukua hatua za haraka za kuhakikisha watoto hao wanapata huduma muhimu. Huduma hizo ni pamoja na kuwaendeleza kielimu kwa kuwaptia vifaa vya shule kama vile madaftari, sare pamoja na karo za shule. Mpango huu unatekelezwa nchini kote. Mpaka sasa watoto 6,091 wamenufaika na mpango huo ambao ni sawa na asilimia 1.2 ya watoto yatima wanaohitaji msaada, wakiwemo watoto yatima wanaoishi katika Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia, inaandaa mkakati wa Taifa wa kuwasaidia watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi. Lengo ni kuhakikisha watoto hao wanapata haki zao za msingi, huduma bora na mahitaji muhimu ndani ya familia zao. Utekelezaji wa mkakati huo utashirikisha jamii yote katika ngazi ya familia, kijiji, Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa jukumu la kuwalea watoto yatima Serikali haijaachia Asasi zisizo za Kiserikali peke yake, bali Serikali inashirikiana nao kwa pamoja kama wadau wetu. Aidha, ni jukumu la familia na jamii kuhakikisha kuwa watoto hawa wanalelewa katika familia zao na suala la kuwaweka katika makao iwe ni hatua ya mwisho kabisa. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutekeleza MKUKUTA mwaka 2005/2006 ambapo katika mwaka huo masuala ya watoto wakiwemo watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu yalipewa kipaumbele. Hivyo, kwa kuzingatia tatizo la watoto yatima, katika mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya kuwasaidia watoto hao.

Matarajio ya Serikali ni kwamba, fedha hizi zitawahudumia watoto yatima na walio katika mazingira magumu kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles N. Keenja swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu niliyopewa.

Kwa kuwa, kuna uwezakano mkubwa sana kwamba hawa watoto wameathirika na virusi vya UKIMWI na kwa hiyo wanahitaji matibabu maalum. Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba wanapata matibabu hayo na wanapata lishe inayoendana na matibabu hayo?

Pili, ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri anatueleza juu ya mikakati nafikiri tunachohitaji ni mipango inayotekelezeka ya kuwahudumia watoto hao na hii inahitajika sasa siyo mikakati ya kutekelezwa baadaye. Je, Serikali imeiandaaje jamii sasa ili jamii iweze kutambua tatizo hilo na kutimiza wajibu wake?

Mheshihimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles N. Keenja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba watoto wengi wameathirika na Serikali ina mpango gani ni kwamba katika mkakati wa Maendeleo ya mtoto ambao vilevile unawa – *cover* watoto walioathirika na UKIMWI kwanza Serikali inahakikisha kwamba wanapata lishe bora na pili wanakaa katika mazingira mazuri.

Lakini vilevile watoto hawa wakiwa ni sehemu ya jamii na wao wanaingia katika mpango mzima kwanza wa kuangalia kama wameathirika na ndiyo maana wako katika mazingira hayo lakini vilevile wanapatiwa dawa za kuongeza maisha na tuna mifano kwa mfano kuna taasisi Dar es Salaam ambayo inahangaika na watoto hawa kwa kuhakikisha kwamba wana lishe bora na wanapata hii *ARVs* za kuongeza maisha. Kwa hiyo, na wao wako katika utaratibu mzima ambao umeandaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili tunaongea juu ya mikakati tu na je ni lini tutapanga mipango.

Mheshimiwa Spika, nina furaha ya kuwaaarifu Bunge lako kwamba Serikali sasa hivi inaunda mfuko wa kuhudumia watoto walioathirika na UKIMWI na wanaoishi katika mazingira magumu. Mfuko huu utachangiwa na asasi mbalimbali zikiwemo asazi za nje lakini vilevile utachangiwa na Serikali na utachangiwa na TAMISEMI vilevile.

Kwa hiyo, mfuko huu utaangalia watoto hawa kuhakikisha kwamba wanapata lishe bora lakini vilevile wanapata elimu, wanatibiwa vizuri, haki zao zinalindwa, wanaishi katika hali ya usalama na kadhalika. Kaw hiyo, mfuko huu unakuja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, swali linaulizwa na Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, lakini kwa niaba yake Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni .

Na. 332

**Nafasi za Ajira kwa Vijana**

**MHE. DR. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (K.n.y. MHE. LUCY T. MAYENGA)** aliuliza :

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kutatua tatizo la ajira kwa vijana na kwa kuwa kumekuwepo na wageni waliothibitika kufanya kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania na hasa katika maeneo ya viwanda na mahoteli ;

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakaikisha kuwa nafasi hizo za ajira zinarudi kwa Watanzania ?

(b) Je, ni wageni wangapi waliorejeshwa katika nchi zao baada ya kudhihirika kuwa walikuwa wakifanya kazi kinyume na Sheria hizo za Ajira katika maeneo hayo ?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (AJIRA) (MHE. DR. EMMANUEL JOHN NCHIMBI)** alijibu-:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mbunge Viti Maalumu, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sera ya Ajira inaelekeza kwamba uchumi wa Tanzania utaendeshwa na kumilikiwa kwa kiasi kikubwa na Watanzania wenyewe wenye elimu na ujuzi katika fani mbalimbali za kazi. Sambamba na Sera hiyo vibali vya Ajira hutolewa kwa watalaamu wa kigeni wenye elimu na utaalamu ambao haupatikani katika Soko la Ndani la Ajira. Hivyo waajiri wanatakiwa kuomba Vibali kwa wataalamu nchini. Wanatakiwa pia kutoa mafunzo kwa Watanzania wanaofanya kazi chini ya watalaamu wa wageni ili hatimaye wachukue nafasi zao pindi wamalizapo muda wao wa vibali.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba vibali vinatolewa kwa Wataalamu wanaostahili kwa mujibu wa Sheria, Wizara yangu imeunda upya Kamati ya kutoa vibali vya ajira kwa wataalamu wa kigeni kwa kuwateua wajumbe kutoka Idara ya Vijana, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Chama cha Waajiri *(ATE),*

Idara ya Uhamiaji, Kituo cha Soko la Ajira na Kituo cha Uwekezaji *(TIC).* Jukumu la Kamati hii ni kuhakikisha kwamba nafasi za ajira kwa wageni ambazo zinaweza kushikwa na watanzania zinarudi kwa vijana watanzania. Wageni wa aina hiyo hawapewi vibali.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya wageni 432 walirejeshwa katika nchi zao baada ya kudhihirika kuwa walikuwa wakifanya kazi kinyume na Sheria za Ajira katika maeneo ya viwanda na mahoteli. Kazi ya ukaguzi wa maeneo ya kazi ili kuwabaini wageni waofanya kazi kazi kinyume cha Sheria ni ya kudumu. Natoa wito kuwa wananchi wenye taarifa za wageni wanaofanya kazi kinyume cha Sheria watoe taarifa katika Wizara yangu au Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara ya Uhamiaji

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda tu kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado kuna tatizo la vijana wengi ambao wako katika Taasisi na hasa za fedha wanashindwa kushika nafasi zile kubwakubwa yaani nono na hizi nafasi wanapewa sana wageni kutoka nje ya nchi na hasa nchi jirani, na kigezo kikubwa ni kwamba kwa vile wale watu wanajua kuzungumza zaidi kingereza lakini si kwa sababu ni wataalamu zaidi ya Watanzania.

Je, Serikali ina mpango sasa kuhakikisha kwamba vijana wetu wasomi wanapatiwa fursa sawa za kupata madaraka katika taasisi mbalimbali hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (AJIRA) (MHE. DR. EMMANUEL JOHN NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, kama ifuatavyo;

Kwanza nakiri kwamba ni kweli baadhi ya vijana wetu wenye sifa wanashindwa kupata nafasi kubwakubwa katika baadhi ya taasisi kwa sababu ya kasumba ya lugha ambayo waajiri wengi wanayo.

Lakini Wizara yangu kuanzia mwaka jana yaani 2006 tumeanza mkakati mkubwa wa kuwabana waajiri wa aina hiyo na moja ni kuwalazimisha kuweka mpango wa kukabidhi madaraka kwa Watanzania wenye ujuzi na ndiyo maana hata wale tunaowapa ajira sasa hivi tunawataarifu tangu mapema kwamba ajira hii kibali chako hakitaidhinishwa upya baada ya muda kuisha na tunataka watupe mkakati wao wa nani atafuata baada ya yeye kutoka tunaiita *succession plan*.

Kwa hiyo, tatizo hili lipo tutaendelea kulikabili kwa nguvu zetu zote na tunachukua hatua kila itakapobidi katika kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru**.**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu sasa hivi ina upungufu mkubwa wa wataalamu wanaoweza kuendesha mahoteli hivyo kulazimika kuwatumia watalaamu walewale kwa mahoteli tofauti au kuagiza wengine kutoka nchi za nje.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo maalumu kwa wafanyakazi wa fani hii ili kupata watalaamu wa kutosha wa kuendesha maholi yetu na kukuza utalii?

Mheshimiwa Spika, Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (AJIRA) (MHE. DR. EMMANUEL JOHN NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba tunao upungufu wa watalaamu katika fani ya hoteli, changamoto ya Serikali ni kuwaomba watu wote ambao wanajihusisha na mambo ya elimu na wawekezaji kufunguza zaidi vyuo vya mafunzo vya sekta hii na Serikali itatoa ushirikiano wa kutosha kwa wale ambao watakuwa na nia ya kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mipango mbalimbali ya kuhakikisha kwamba tunaongeza ubora wa huduma katika sekta ya hoteli. Sehemu ya kwanza ya mpango huu ni ushirikiano kati ya Serikali na Jumuiya ya Ulaya ambapo Jumuiya ya Ulaya imetupatia dola za Kimarekani milioni 2.5 kwa ajili ya *In service Training* kwa ajili wafanyakazi wa mahoteli katika nchi yetu na mpango huu utaanza katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nchi yetu imeanzisha Chuo cha Utalii cha Taifa ambacho kimeanza kutoa mafunzo katika *level* ya Stashahada mwaka huu wa elimu na tatu Chuo cha Mataifa cha Biashara au *World Tourism University* itashirikiana na sisi kujenga Chuo cha Utalii cha Dunia hapa Tanzania. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kwa ufafanuzi huo na sasa swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mwichoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni.

Na. 333

**Ujenzi wa Nyumba za Bei Nafuu - Kigamboni**

**MHE. MWICHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, *NSSF* ina mpango wa kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya kuwakopesha wananchi katika maeneo ya Tarafa ya Kigamboni, na kwa kuwa, ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambao ulikuwa ni kikwazo cha mradi huo sasa unategemea kuanza mwaka 2007/2008 chini ya *NSSF* na Uholanzi:-

(a) Je, Mpango wa ujenzi wa nyumba hizi umefikia hatua gani sasa?

(b) Je, ni lini ujenzi huo utaanza rasmi?

**NAIBU WAZIRI KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi (Kigamboni) swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu uliobuniwa na Shirika la *NSSF* katika eneo la Kigamboni unatarajia kuanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2007/2008. Kwa sasa hivi mradi huu upo katika hatua za usanifu na upembuzi yakinifu. Lengo ni kuanza ujenzi wa nyumba za bei nafuu kati ya 300 na 400 kwenye viwanja vilivyopo Tuangoma, Vijibweni na *Nadungu Farm* ambazo zitazingatia mahitaji na uwezo wa wananchi wa kawaida.

Baada ya hatua hizi Wakandarasi watateuliwa ili kuanza ujenzi. Aidha, ni muhimu pia kueleza kuwa uharaka na ubora wa mradi huu utategemea sana ujenzi wa daraja la Kigamboni na uwekaji wa miundombinu ya barabara, maji safi/taka, pamoja na umeme. Ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na *NSSF* unahitajika pia katika kufanikisha mradi huu. *(Makofi)*

**MHE. MWICHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini kwa kuwa *NSSF* matarajio yao makubwa ni baada ya daraja la Kigamboni.

Je, kwa vile hali ya vivuko vya Kigamboni hivi sasa inaridhisha kidogo na tunararajia kupata pantoni mpya mwaka ujao pamoja na kukwama kwa daraja letu la Kigamboni. Je, kwa misingi hiyo vivuko vitakuwa katika hali nzuri haioni kwamba kuna umuhimu wa kuendeleza mradi huo bila kutegemea zaidi daraja la Kigamboni?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza si kweli kwamba ujenzi wa daraja la Kigamboni umekwama, matayarisho ya ujenzi wa daraja hili ulianza mwaka 2003, mwaka 2005 ushauri ulipelekwa Serikalini sasa hivi ujenzi wa daraja hili uko kwenye ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, tunategemea kwamba itakapomaliza kwenye ngazi hiyo itakwenda kwenye ngazi ifuatayo ya Makatibu Wakuu wa *MTC.*

Baadaye kama Baraza la Mawaziri likiona inafaa basi litamshauri Mheshimiwa Rais na daraja hilo litaaanza kujengwa kama ilivyotajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Kuhusu kuanza ujenzi wa nyumba hizi kwa kutumia njia ya *Pontoon* na kubaliana naye lakini pamoja na hilo tukubaliane vilevile kwamba njia zote mbili hizi za kutumia vivuko pamoja na daraja zote zitatumika pale daraja litakapokamilika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Usalama wa Raia swali linaulizwa na Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara. Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni sidhani kama nitakuruhusu kama hayupo mwingine basi tutaliacha tu. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwa niaba tafadhali.

Na. 334

**Kituo Kikuu cha Polisi Kibaha**

**MHE. MHE. HAFIDH ALI TAHIR ( K.n.y. CHARLES M. KAJEGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Polisi cha Kibara ndicho Kituo Kikuu cha Polisi Jimbo la Mwibara, na kwa kuwa, kituo hicho hutekeleza majukumu yake ya kulinda amani na usalama wa raia pamoja na mali zao kwa kushirikiana na vituo vingine vinne vidogo

vidogo vilivyomo Jimboni humo; na kwa kuwa, kituo hicho kinafanyia kazi zake katika nyumba ya kupanga, ambapo hakuna nyumba za wafanyakazi na mawasiliano ya uhakika kati yake na vituo vidogo vidogo vilivyomo Jimboni humo pamoja na gari la kufanyia kazi:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga ofisi ya kudumu na nyumba za wafanyakazi kwa ajili ya kituo hicho?

(b) Je, ni lini serikali itakipatia kituo hicho gari na mawasiliano ya uhakika ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa urahisi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuwapatia Askari wake ofisi nzuri na makazi mazuri. Hata hivyo, nia hiyo ya Serikali inakwamishwa na uwezo wetu mdogo kiuchumi, kwani ni maeneo mengi nchini ambayo hayana kabisa Vituo na Makazi au majengo yanayohitaji kukarabatiwa.

Hivyo, kwa kadri uwezo wetu kifedha utakavyoruhusu, Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya kujenga vituo na makazi nchi nzima awamu kwa awamu.

(b)Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti na uwezo mdogo wa Serikali, juhudi zinafanyika kuhakikisha kwamba Vituo vya Polisi hapa nchini vinapatiwa zana za kisasa yakiwemo magari, pikipiki na vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya kupambana na uhalifu nchini, ikiwa ni pamoja na Kituo cha Polisi Kibara.

Kwa sasa, Jeshi la Polisi linaifanyia matengenezo gari lililopo katika Kituo cha Polisi cha Bulamba ambacho kipo karibu na Vituo vya Polisi vya Kibara, Kisorya na Kekombyo ili kutoa huduma ya usafiri kwa kushirikiana na gari kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Bunda.

Hata hivyo, kwa sasa tunaangalia uwezekano wa kuwapatia japo pikipiki kwa ajili ya kuhudumia eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir swali la nyongeza.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa jawabu la Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulieleza Bunge hili Tukufu kwamba ni vituo vingapi vya Jeshi la Polisi ambayo hivi sasa vinapanga katika nyumba za watu binafsi hapa Tanzania? Na je, Askari wa Kituo hiki hivi sasa wanaishi wapi kama hawana nyumba za kukaa katika eneo hilo?

**SPIKA:** Hili swali linahitaji takwimu ninaomba liandaliwe kwa ajili ya kuulizwa kwa sababu sidhani kama Waziri anaweza kuwa na takwimu za Askari wangapi wanaishi katika nyumba za kupanga. Kwa hiyo, basi tunahamia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba Mbunge wa Mikumi.

Na. 335

**Hitaji la Hospitali – Mikumi**

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya watu Mikumi ni kubwa sana, na kwa kuwa, Mikumi ipo katikati ya Mji wa Iringa na Morogoro umbali wa kilomita zisizopungua 115 kila upande hali inayosababisha usumbufu na mateso makali kwa majeruhi kila zinapotokea ajali za magari kwani husafirishwa hadi Iringa au Morogoro.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kujenga Hospitali inayoweza kutoa huduma za msingi kwa majeruhi sambamba au kutoa kibali cha kupandishwa gredi kwa Kituo cha Afya kinachoendeshwa na Madhehebu ya Katoliki ya Mkumi kiwe Hospitali ili kukabiliana na ongezeko kubwa la mahitaji ya huduma za tiba kwa wakazi na jamii nzima ya Mikumi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa mji mdogo wa Mikumi ambao uko katika Wilaya ya Kilosa katika njia itokayo Mrogoro kwenda Iringa unakuwa kwa haraka. Hali inahitaji huduma za jamii ikiwemo afya ziboreshwe ili kukabiliana na ongezeko la watu. Naomba nitumie fursa hii kulishukuru kwa dhati

Kanisa Katoliki la Mikumi kwa huduma nzuri za afya zinazotolewa kwa wananchi katika kituo chao cha Afya.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali inayoweza kutoa huduma za msingi kwa majeruhi ni jukumu la Halmashauri na Sekretarieti ya Mkoa. Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya yake pamoja na Sekretarieti ya Mkoa ili kuona uwezekano wa kuingiza mradi huu kwenye Mipango yao ya Maendeleo. Wizara yangu iko tayari kutoa ushauri, ramani, wataalam, vitendea kazi, vitendanishi pamoja na dawa.

Mheshimiwa Spika, ili kituo cha Afya kiweze kupandishwa daraja ni lazima mmiliki wa kituo aongeze na kuboresha huduma kwa maana ya idadi na aina ya watalaam, nyongeza ya wingi na aina ya huduma kama vile chumba cha kupasulia, maabara vyumba vya kulala wagonjwa na kadhalika. Wakaguzi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wakiridhika na vigezo vilivyowekwa hadhi ya kituo itapandishwa bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Bunge lako Tukufu, pamoja na wananchi kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Tufanye juhudi za makusudi kukinga ajali za barabarani kwa kushirikisha wadau wote kama Askari wa usalama barabarani, wananchi, madereva, abiria na kadhalika, kwani zaidi ya asilimia 80 ya ajali za barabarani hutokana na makosa ya binadamu na zinaweza kuzuilika.

Mheshimiwa Spika, magari mengi mabovu na yenye hitilavu za kiufundi yanayoonekana barabani na hivyo husababisha ajali barabarani. Baadhi ya magari hayana viashiria na hivyo yakiharibika madereva hutumia majani na matawi ya miti ambayo ni vigumu kuonekana kwa urahisi hasa usiku na matokeo yake yanaweza kuwa mabaya kwa magari mengine. *(Makofi)*

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ustawi wa Jamii, kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, kituo cha Afya Mikumi kimeshawasilisha maombi Wizarani kwa ajili ya kupandishwa gredi kuwa hospitali na kwa kuwa, vifaa vyote muhimu alivyovitaja Naibu Waziri vimeshatimizwa isipokuwa ni upungufu wa wauguzi 42, lakini kwa kuwa pia kituo hiki kinatoa huduma za gredi za juu sana kiasi kwamba hata wagonjwa wa kutoka Tarafa nyingine wote wanakuja kumiminika Mikumi na kusababisha misongamano mikubwa ya wagonjwa.

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa kipaumbele katika kupanga na ku – *allocate* wauguzi wa ziada kupunguza pengo hilo ili huduma zizidi kuendelea kabla ya kufikia hatua ya kukamilika na kupewa kibali cha kuwa hospitali kamili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda tena kuisifia hospitali hiyo kwamba imeweza kujiwezesha ili kuweza kukidhi haja ya kupandishwa kuwa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba kama kweli imekidhi mahitaji Wizara yangu itapeleka wataalam kwenda kukagua na kuona kwamba inastahili kupandishwa daraja ili kuweza kupandishwa daraja. Vilevile kuhusu watumishi tutaweza kutoa kipaumbele kutokana na hali halisi. Tunawasubiri wataalam watakaohitimu tukiona kwamba watakuwepo wa kutosha basi hatuna sababu ya kuacha kuwasaidia kwa sababu wanawasaidia wananchi kwa jumla.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho kwa asubuhi hii linaelekezwa Wizara hiyo hiyo na linaulizwa na Mheshimiwa Martha Mlata. Mtaona kwamba napitiliza kidogo kwa sababu tulitumia muda wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali mezani kabla ya kipindi cha maswali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Martha Mlata hayupo, Mheshimiwa Faida Bakar, uliza kwa niaba yake.

Na. 336

**Upungufu wa Madaktari Bingwa – Singida**

**MHE. FAIDA M. BAKAR (K.n.y. MHE. MARTHA MOSSES MLATA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Singida unakabiliwa na upungufu wa Madaktari Bingwa hasa katika magonjwa ya akina mama na watoto na hivyo kusababisha makundi haya kukosa tiba maalumu hali inayosababisha vifo vinavyoweza kuepukika:-

(a) Je, akinamama na watoto wangapi waliopoteza maisha yao kutokana na ukosefu wa Madaktari bingwa kwa mwaka 2000 – 2005?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na upungufu wa Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mkoa wa Singida pamoja na Mikoa mengine nchi inakabiliwa na upungufu wa Madaktari Bingwa hasa wa magonjwa ya akinamama na watoto na hivyo kusababisha makundi haya kukosa huduma za kitalaamu zaidi na kwa wakati pale zinazpohitajika. Hata hivyo, vifo vya akinamama na watoto haviwezi kuhusishwa moja kwa moja na ukosefu wa madaktari bingwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 – 2005 jumla ya akinamama 270 walipoteza maisha. Sababu za vifo hivi ni pamoja na:-

Ukosefu wa damu, Malaria, kutokwa na damu kabla na baada ya kujifungua, uambukizo kwenye kizazi baada ya kujifungua, kifafa cha mimba, *Obstructed labour*, kuchanika mfuko wa uzazi, UKIMWI, Mimba kuharibika na matumizi ya dawa za kienyeji wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi hicho 2000 – 2005 jumla ya watoto 1912 walipoteza maisha. Sababu za vifo ni UKIMWI, Malaria, Pungufu wa Damu, Kuharisha, Lishe duni, Malaria Kali na Maambukizo katika njia ya hewa (*pneumonia*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya juhudi ya kuongeza idadi ya madaktari wanaochukua shahada za uzamili wa fani za afya kila mwaka. Kwa mwaka uliopita 2006/2007, jumla ya madaktari 77 wanaosomea mafunzo ya ubingwa wanatarajiwa kuhitimu katika Vyuo vya Muhimbili na *KCMC* na pia nje ya nchi. Madaktari hawa watakapohitimu watapangiwa kwenye hospitali za Mikoa ikiwa ni pamoja na Singida.

Hatua ya muda mfupi iliyochukuliwa na Serikali ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa Madakatari pamoja na watumishi wengine wa afya nchini na Singida ikiwemo kwa kulegeza masharti ya ajira. Katika utaratibu huu Wizara yangu imepewa kibali cha kuwapangia vituo vya kazi watumishi wa afya wakiwemo Madaktari Bingwa kwenye Halmashauri na Mikoa kulingana na nafasi zilizoidhinishiwa fedha.

Aidha, hatua ya muda mrefu ni kuongeza idadi ya wanafunzi watakaojiunga na mafunzo mbalimbali ya afya yakiwemo ya ubingwa. Tayari Wizara yangu, imekwishafanya makubaliano na Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili kutekeleza mpango huu. Pia, Wizara inahamasisha vyuo binafsi kutoa mafunzo ya ubingwa katika fani mbalimbali za afya ili kuongeza nafasi ya watalaamu wetu kujiunga na hivyo kuongeza idadi ya mabingwa. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo hili la Madaktari Mabingwa katika Mkoa wa Singida ni la muda mrefu sana na kila wakati linapoulizwa hapa Bungeni Serikali inaahidi kutekeleza. Lakini mpaka sasa bado. Je, akinamama na watoto watapoteza maisha yao mpaka lini na Serikali haioni kwamba inawakosesha haki hiyo ambayo ni haki yao kuipata huduma hiyo kutoka kwa Madaktari bingwa? *(Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Faida Bakar leo sauti yako kama inakwaruza kwaruza hivi. Lakini kwa kuwa unamwuliza Waziri wa Afya pengine baada ya hapa mnaweza mkaonana ili upate huduma. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Bakar napenda kuchukua nafasi hii kumpa pole na ninaahidi nitamwona na nitampatia matibabu na atapona. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nikijibu maswali mengine katika Kikao hiki cha Bunge, ni kweli kuna upungufu wa madaktari bingwa na Singida imekuwa ikiomba na ikizungumzia sana kwamba ina upungufu mkubwa wa madaktari bingwa. Lakini nilikwisha kusema hapa tuna upungufu mkubwa wa Madaktari bingwa. Lakini Wizara tayari imekwishapeleka Daktari Bingwa wa akinamama na ameisharipoti Singida na yuko kule anafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane kwa sababu si tatizo la Singida pekee hatuwezi tukachukua wahitimu wote watakaokuwa wamefuzu ubingwa tukawapeleka Singida kwa sababu mahitaji ni makubwa na kila Mkoa unahitaji. Kwa hiyo, kwa kweli tunaahidi na tunajua umuhimu wa watoto. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba watakapokuwa wanatosheleza Mikoa yote watapatiwa wataalam ili kukidhi mahitaji ya akinamama na watoto. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kama yalivyo matatizo ya Singida na Mkoa wa Kigoma matatizo yetu ni makubwa zaidi. Mkoa mzima wa Kigoma tuna madaktari wawili tu. Ningependa Naibu Waziri anisaidie kuna njia gani za kufanya ili asaidie Mkoa wa Kigoma ili hao watoto na akinamama wa Kigoma nao waweze kuokoa maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama jibu langu la msingi lilivyojieleza ni kwamba tuna uhaba mkubwa na yeye kama Kigoma ana madaktari bingwa wawili, mimi ninasema kwamba aishukuru Serikali kwamba wapo wale wawili kwani Mkoa wa Singida walikuwa hawana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba Serikali inaliona tatizo hilo, lakini tatizo hili ni kubwa na wataalam hao ni wachache. Ndiyo maana nimesema katika jibu la msingi wahitimu 77 watakaohitimu tutahakikisha kwamba tunawapeleka ili kuweza kuona kwamba sehemu zote zinapata wahitimu hao na jinsi watakavyokuwa wanaongezeka tutakuwa tunaongeza idadi. Kwa hiyo, nawaomba watuvumilie. Suala hili tunalifahamu na tunalifanyia kazi kwa kadri ya uwezo wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Sasa matangazo ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga la Taifa anao wageni wake kama ifuatavyo:- Kwanza, ni Jenerali George Waitara, Mkuu wa Majeshi ya Tanzania. Karibu sana Jenerali. Ningependa yeye pamoja na Wanajeshi wetu wafahamu kwamba tunajivunia sana Jeshi la Tanzania. Wanafanya kazi nzuri sana wakati wa amani na hata wakati wa mapambano na wana historia iliyotukuka. Tunawashukuru sana kuwaona. Pamoja naye yupo Major Jenerali Abdulrahman Shimbo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa. Karibu sana. Mtakuwa mmesikia katika wiki hii maswali na vitu vingine kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa. Waheshimiwa Wabunge wana matazamio makubwa sana ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa siku zijazo kuzidi kutuunganisha katika nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ningewaomba pia Makamanda na viongozi wa Vikosi popote walipo pale walipo wasimame ili Waheshimiwa Wabunge, waweze

kuwatambua. Naona wote wapo pale, Jeshi la Nchi Kavu, Anga na *Navy* naona wapo. Bahati nzuri pia ni mchanganyiko wapo pia Makamanda ambao ni wanawake, Tunafurahi sana kuona hivyo. Ahsante sana. Hamuoni aliyevaa ushungi mnadhani ni mwanamume. *(Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo natambua kuwepo kwa Katibu Mkuu wa Wizara, alikuwa kwenye matibabu kwa muda mrefu Ndugu Abel Mwaisumo, amerudi na afya njema tu. Karibu sana Ndugu Abel Mwaisumo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kama ambavyo imekuwa ni utamaduni wetu, mke wa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, amekuja hapa na ninaomba sasa asimame. Pia pamoja na Mama Tatu Kapuya, amekuja na mtoto wao ambaye anaitwa Kulwa na wanafamilia ya Mheshimiwa Waziri Prof. Juma Kapuya. Pamoja na Ndugu kumi kutoka Jimbo la Urambo Magharibi. Kwa kweli wametia uzi sawasawa. Hali hii ndiyo inafanana na Jimbo ambalo lina mafanikio kama vile Urambo Magharibi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, ambaye ni Mheshimiwa Hassan Said Shinda, Diwani wa *Ward* ya Kwamtipura, Naibu Meya wa Manispaa ya Mji wa Zanzibar. Lakini ningeomba ambaye ni Meya kwanza ndiyo asimame. Naibu Meya. Karibu sana Mstahiki. Halafu Mheshimiwa Khamis Abdallah Amour Diwani wa *Ward* ya Mkeli katika Jimbo hilo hilo. Sijui tulionana siku ile nilikuja Kwamtipura. Ahsante sana kwa mapokezi mazuri pale Kwamtipura. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wanafunzi 60 kutoka shule ya Sekondari ya Kikuyu Dodoma, bila shaka na walimu wao. Ningeomba wasimame karibuni sana. Tunafurahi kuwaona. Ni jambo nzuri kutembelea Bunge. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 41 na walimu nadhani hao ni sehemu ya wale waliokuwepo hapa juzi kutoka shule ya msingi ya Kizota. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mwisho, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi ana wageni wake Alfred Nchimbi ambaye ni kaka yake, wanafanana vizuri tu. Halafu Ndugu Bageorge Zakari Katibu wa CCM wa Wilaya ya Mbarali. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi nilikuwa nasikiliza *Radio Clouds* walikuwa wanatania jinsi Spika anavyotambulisha wageni. Lakini hatuwezi kuacha Bunge hili ni la watu, lazima liweze kuwa karibu na watu. Kuna mambo ambayo tunayatengeneza ni utamaduni. Inawezekana Mabunge mengine hayafanyi, lakini sisi tunaona ni jambo nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya Vikao vya Kamati. Leo saa 4.00 katika ukumbi namba 133 Mheshimiwa Mgana Msindai, anaomba wajumbe wote wa Kamati

ya Hesabu za Serikali za Mitaa wakutane na Maafisa wa Benki ya *Standard Charted*. Kwa hiyo, ni sasa hivi.

Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali wakutane chumba namba 231 saa 5.00 asubuhi.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi anatoa wito kwa wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane katika ukumbi namba 219 jengo la utawala saa 6.00 mchana. Hayo ndiyo matangazo. Sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Kuhusu taarifa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kikao cha Kamati ya *LAAC* ni kesho saa 4.00 siyo leo.

**SPIKA:** Ni kweli nilighafilika kumbe imeandikwa ni kesho tarehe 2 Agosti, 2007 - saa 4.00 asubuhi, Kamati ya *LAAC.* Ahsante sana Mheshimiwa Mgana Msindai. Katibu endelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea, kujadili na kisha kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuiweka nchi yetu na sisi wenyewe salama na kutuwezesha kukutana tena baada ya mwaka mmoja

kwa ajili ya Bunge la Bajeti. Kwa sababu hiyo, naomba kutoa shukrani maalum kwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye kwa uongozi wake makini na usiyoyumba, chini ya sera thabiti za Chama Cha Mapinduzi (CCM), amehakikisha usalama tulionao nchini mwetu unalindwa na kudumishwa. Aidha, namshukuru kwa msimamo na hatua anazozichukua kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vinawezeshwa na vinatekeleza kikamilifu wajibu wao wa kulinda uhuru na usalama wa nchi yetu. Hatua hizi zimeendelea kuimarisha amani na utulivu tunaouhitaji kwa ajili ya Maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya makadirio haya. Napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Kusilla, Mbunge wa Bahi, kwa kuchambua kwa makini mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2007/2008 na kutupa ushauri na changamoto zilizochangia katika kuyaboresha na kuyakamilisha.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, Katibu Mkuu, Bwana Abel W.R. Mwaisumo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Goerge M. Waitara, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Davis A. Mwamunyange, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Abdurahman A. Shimbo, Makamanda, Maafisa, Wapigaji na Watumishi wa Umma wote. Nawashukuru wote kwa ushauri wao ulio makini na ushirikiano mkubwa walionipa wenye uaminifu. Mwisho namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali na watumishi walio chini yake kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa hotuba yake ya kina ambayo imeelezea mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2006/2007. Aidha, nawapongeza, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji; Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao zilizoelezea mwelekeo wa uchumi wa Taifa na bajeti ya Serikali. Vile vile, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa hotuba zao nzuri ambazo zimekwisha kujadiliwa na kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliomalizika tumeshuhudia mambo mengi mazuri na ya kufurahisha. Katika mwaka huo tumepata Wabunge wenzetu watatu ambao ni Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba (Mbunge wa Kuteuliwa), Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura (Mbunge wa Tunduru) na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya (Mbunge wa Viti Maalum). Napenda kutumia fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kuwapongeza sana na kuwakaribisha hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa, kupitia Bunge lako Tukufu, kuiwakilisha nchi yetu ya Tanzania katika Bunge la Afrika ya Mashariki, ambao ni Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Aman Walid kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate

Kamba, Mheshimiwa Sepetu Nasoro, Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortinatus Lwanyatika Masha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza kwa dhati aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dkt. Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi wake kwenye nafasi hiyo ya uongozi ni heshima kubwa kwake na kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushuhudia matukio haya mazuri na ya kufurahisha katika mwaka uliomalizika, yamekuwepo pia yale ya huzuni. Tumempoteza mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge). Pia tumempoteza mwenzetu Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole na rambirambi zangu kwa familia, jamaa na marafiki wa marehemu Akukweti na Chifupa. Mwenyenzi Mungu azipumzishe roho zao mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika**,** Hali ya Ulinzi na Usalama katika mwaka 2006/2007.
Usalama wa Mipaka. Katika mwaka 2006/2007 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliendelea kusimamia jukumu la ulinzi wa nchi yetu dhidi ya tishio la usalama kutoka nje. Kwa ujumla mipaka yote ya Tanzania na nchi jirani ilikuwa shwari na tulivu. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (Jeshi), lenye jukumu la ulinzi, limefuatilia hali hiyo kwa karibu na kuweza kuidumisha kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, utulivu huu ni kutokana na hali ya kisiasa na kijamii katika nchi jirani za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kuendelea kuimarika, hatua ambayo imeimarisha usalama wa mipaka ya nchi yetu ya upande wa magharibi katika mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa.

Hali ya wasiwasi iliyokuwepo katika mipaka na maeneo hayo kwa kipindi cha ziadi ya miaka kumi, imeendelea kutengemana kutokana na kupungua kwa vurugu za wakimbizi na vitendo viovu vya wahamiaji haramu kutoka nchi hizo jirani. Aidha, zoezi linaloendelea sasa la kuwarejesha makwao wakimbizi na wahamiaji haramu limeendelea kuimarisha hali ya amani na utulivu miongoni mwa wananchi katika maeneo yote ya magharibi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo hali hiyo ya utulivu, katika baadhi ya mipaka yetu yamekuwepo matatizo ambayo kwa kiwango fulani yanaweza kutishia utulivu uliopo. Hivyo Jeshi limekuwa likifuatia kwa karibu na kutoa tahadhari kwa Serikali. Mipaka hiyo na matatizo husika, ambayo yameshughulikiwa na mamlaka husika za hapa nchini kwa kushirikiana na zile za nchi jirani, ni haya yafuatayo:-

(a) Mpaka wa Tanzania na Kenya Uharibifu wa mawe ya kuonyesha mpaka *(beacons*) kati ya Tanzania na Kenya katika Wilaya za Tarime (Tanzania) na Migori (Kenya).

(b) Mpaka wa Tanzania na MsumbijiWimbi la wahamiaji haramu na wasafiri wasio na hati halali za kusafiria kutoka nchi jirani kwenye mpaka wa kaskazini ambao huingia Tanzania na kuelekea nchi za kusini mwa nchi yetu kwa kuvuka mpaka huu.

(c) Mpaka wa Tanzania na MalawiUkosefu wa ufumbuzi wa tatizo la mpaka katika Ziwa Nyasa.

(d) Mpaka wa Tanzania na Zambia Ongezeko la migogoro kati ya wafanya biashara kutokana na wananchi wa pande zote mbili kuhamia na kujenga katika eneo hilo kunakosababishwa na kupanuka kwa shughuli za biashara. Hali hii inaongeza wimbi la uhalifu sambamba na kulipunguzia Taifa mapato yake.

(e) Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Vitendo vya uporaji na unyang'anyi vinavyofanywa na wahamiaji haramu, wakimbizi na wahalifu wengine.

(f) Mpaka wa Tanzania na Burundi Vikundi vya waasi wa Burundi kuvinjari karibu na mpaka na kuingia Tanzania na kufanya uhalifu.

(g) Mpaka wa Tanzania na Uganda Uharibifu wa mawe ya kuonyesha mpaka kati ya Tanzania na Uganda bado unaendelea. Uharibifu huo unasababishwa na shughuli za ufugaji mpakani, mvua kubwa zinazonyesha katika maeneo hayo na wananchi waishio jirani na mpaka kuharibu mawe hayo wakidhani chini yake kuna dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Ndani ya Nchi. Pamoja na kuhakikisha usalama wa mipaka ya Tanzania, Jeshi pia limeshirikiana na vyombo vingine vya dola kuhakikisha usalama wa ndani ya nchi. Jeshi limeshiriki katika kudhibiti uzagaaji wa mabomu ya kutupwa kwa mkono yaliyokuwa yakihatarisha usalama wa wananchi katika baadhi ya maeneo, hasa viwanda vinavyojihusisha na biashara ya vyuma chakavu katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pia Jeshi la Ulinzi lilishiriki katika zoezi la kupambana na wimbi la ujambazi wa kutumia silaha na vitendo vingine viovu katika miji mikubwa hapa nchini ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Mbeya. Kufuatia zoezi hilo, ujambazi na vitendo hivyo viovu vilivyokuwa vikitishia usalama wa wananchi na mali zao pamoja na utulivu uliopo hapa nchini, vimeandelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Jeshi limeshiriki katika kudhibiti tatizo la ujambazi unaofanywa na watu wenye asili ya Kisomali katika maeneo ya karibu na mpaka wetu wa kaskazini. Hatua hizo zimehuisha pia kuongeza udhibiti wa uingiaji na utokaji wa wageni katika mipaka yetu kwa lengo la kuwasaka wale wanaojipenyeza visivyo halali.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2006/2007. Mwaka jana, wakati wa kufunga mjadala kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2006/2007, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kwa niaba ya Kamati yake, na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla, katika kuchangia mjadala huo, walitoa maelekezo na ushauri wa jinsi ya kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu ya wizara yetu.

Kwa heshima na taadhima napenda kutoa taarifa kwamba tulizingatia maelekezo na ushauri huo kulingana na uwezo wa bajeti ulivyoruhusu. Hivyo, pamoja na kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2006/2007, taarifa rasmi ya utekelezaji wa ahadi tulizotoa hapa Bungeni imeandaliwa na Waheshimiwa Wabunge wamepewa nakala kama sehemu ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, shabaha kuu za kisera za ulinzi wa Taifa letu ni:-

(a) Kuendelea kuunda jeshi dogo la kisasa, lililo madhubuti na lenye uwezo na ufanisi mkubwa katika utendaji kivita kwa ajili ya:-

(i) Kulinda mipaka ya nchi dhidi ya tishio la usalama wa Tanzania.

(ii) Kuandaa mgambo ambao utakuwa ndiyo nguvu kuu ya akiba ya ulinzi wa Taifa.

(iii) Kusaidia mamlaka za kiraia hapa nchini wakati wa dharura na maafa ili kuokoa maisha na mali za wananchi, na kudhibiti vitendo vinavyohatarisha usalama.

(iv) Kutekeleza majukumu ya kimataifa yatokanayo na makubaliano na/au mikataba kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani.

(v) Kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, mshikamano na umoja wa kitaifa, na kuwaandaa katika jukumu la uzalishaji mali na stadi za kazi kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

(b) Kuendelea kujenga uhusiano na ushirikiano mwema na nchi nyingine duniani, hususan nchi jirani, kwa lengo la kudumisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, ili kuzifikia shabaha hizo, malengo ya ulinzi wa Taifa yaliyokuwa pia malengo ya bajeti ya mwaka 2006/2007 ni:-

(a) Kuajiri wanajeshi wenye sifa zinazohitajika kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa Taifa.

(b) Kuimarisha Jeshi kiutendaji ili liwe na uwezo na ufanisi mkubwa kwa:-

Kuwapatia wanajeshi mafunzo na mazoezi ya kijeshi ili wawe na utaalam na ujuzi wa hali ya juu kwenye fani zao.ii.Kulipatia Jeshi zana na vifaa bora vya kisasa kimapigano na kuliandaa kwa ajili ya majukumu mengine ya ndani na nje ya nchi.

(c) Kuhifadhi, kutunza, kutengeneza na kukarabati kikamilifu vifaa na zana za kijeshi ili ziweze kutumika kikamilifu katika jukumu la ulinzi wa nchi.

(d) Kuboresha teknolojia ya kijeshi kwa kuendeleza shughuli za utafiti na uzalishaji kwa lengo la kujenga uwezo wa kujitegemea katika vifaa na zana za kijeshi, na kuzalisha bidhaa zingine kwa ajili ya matumizi ya kiraia

(e) Kuwapatia wanajeshi mazingira bora ya kufanyia kazi, ikiwa ni pamoja na nyumba za kuishi, huduma za tiba na elimu, majengo ya kufanyia kazi, na maeneo salama ya kufanyia mafunzo kwa vitendo.

(f) Kuwapatia wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) huduma na mahitaji muhimu katika viwango vinavyoridhisha, ikiwemo chakula, sare, vifaa vya malazi, mabwalo na kadhalika.

(g) Kuwapatia wanajeshi na watumishi wa umma stahili zao kwa wakati, ikiwemo mishahara, likizo na kadhalika.

(h) Kuwalipa wanajeshi wastaafu mafao yao kwa wakati.

(i) Kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi na vifaa mbalimbali kwa ajili ya shughuli za utawala ikiwa ni pamoja na uendeshaji, mafunzo, mazoezi na michezo.

(j) Kuendeleza huduma bora za tiba na juhudi za kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI.

Ongezeko la wastani la bajeti pamoja na mkopo toka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* katika mwaka 2006/2007 liliongeza kasi ya utekelezaji wa baadhi ya malengo ya ulinzi wa Taifa ikilinganishwa na mwaka 2005/2006.

Kwa mfano, huduma muhimu kwa wanajeshi, kama vile chakula, tiba, sare, mishahara, makazi na usafiri pamoja na huduma za kijamii za maji, umeme na simu ziliimarika kwa kiwango cha kuridhisha.

Vilevile, hali ya vitendea kazi hususan vifaa na zana kwa ajili ya utendaji kivita, michezo, mafunzo na mazoezi imeendelea kuboreshwa. Hali ya utekelezaji katika kila eneo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Uimarisha wa Jeshi Kiutendaji. Vifaa, Zana na Vitendea kazi. Mpango wa kuimarisha Jeshi kiutendaji chini ya shabaha kuu ya kuunda jeshi dogo la kisasa, lililoimara katika utayari na utendaji kivita, kama inavyobainishwa katika

Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi (CCM) (mwaka 2000 hadi 2010), umeendelea kutekelezwa kulingana na uwezo wa Serikali kiuchumi.

Aidha, katika kuendeleza utekelezaji wa mpango huo, katika mwaka 2006/2007 Jeshi limeweza kununua baadhi ya vitendea kazi, vifaa na zana ili kuliimarisha katika utekelezaji wa majukumu yake muhimu, kama vile kufanya doria mipakani, baharini na kwenye maziwa, na majukumu mengine ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi. Pia Serikali imeendelea kuchukua hatua kuhakikisha Jeshi linapata uwezo wa kuwapatia wanajeshi wake mafunzo na mazoezi ya elimu ya kijeshi hususan kuhusu matumizi ya teknolojia mpya ya kijeshi, mbinu za kisasa za kivita na utendaji katika majukumu yake mapya.

Hivyo, katika mwaka 2006/2007 wanajeshi wetu wamewezeshwa kufanya mafunzo na mazoezi kuanzia ngazi ya mtu binafsi (*individual training*) hadi mafunzo na mazoezi ya pamoja na makundi (*collective formation training exercises*). Mazoezi ya pamoja na makundi yaliyofanyika katika mwaka 2006/2007 ni haya yafuatayo:-

Mazoezi ya Ndani ya Nchii.Zoezi la medani la "Pima Uwezo" lililoendeshwa na Brigedi ya Mashariki eneo la Msata tarehe 9 Novemba, 2006. Zoezi la Askari wa Mgambo Tabora lililofanyika mwezi Novemba, 2006 kwa askari wa mgambo kujifunza mbinu mbalimbali za kivita. Kikosi cha Jeshi *25 KJ* Tabora kilishiriki katika zoezi hilo. *(Makofi)*

(i) Zoezi la ulinzi wa amani la Monile Bambo lililofanyika Songea Desemba, 2006 chini ya Brugedi ya Kanda ya Kusini.

(ii) Zoezi la kivita la Juhudi lililofanywa na Kikosi cha Jeshi 27 KJ mkoani Mara, mwezi Februari, 2007.

Mazoezi ya Kimataif i.Zoezi la *Natural Fire* 2006 (*Field Training Exercise*) Zoezi hili lililohusu ulinzi wa amani, kupambana na maafa pamoja na kuzuia ugaidi, lilifanyika nchini Kenya kuanzia tarehe 8 hadi 19 Agosti, 2006.

Zoezi hili lilishirikisha Majeshi ya Ulinzi ya nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Marekani.ii.Zoezi la *Hot Springs***.**

Zoezi hili lilifanyika nchini Uganda kuanzia tarehe 20 hadi 30 Septemba, 2006 chini ya Ushirikiano wa Afrika Mashiriki na lililenga katika kupambana na maafa.

(iii) Zoezi la Blue Ruvuma (*Disaster Management*). Zoezi hili lilifanyika nchini Tanzania kuanzia tarehe 9 hadi 13 Oktoba, 2006 na kushirikisha Majeshi ya Anga ya nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, mbali ya wanajeshi wetu kupatiwa mafunzo katika vyuo na shule za kijeshi za hapa nchini, pia wamewezeshwa kuhudhuria kozi, semina na warsha mbalimbali kuhusu elimu ya kijeshi nje ya nchi.

Katika mwaka 2006/2007 jumla ya maafisa na askari 211 walipelekwa nje ya nchi, hususan katika nchi rafiki, kuhudhuria mafunzo ya kijeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu ya mafunzo na mazoezi hayo imehusisha pia uboreshaji wa masomo yatolewayo katika vyuo na shule za kijeshi za hapa nchini ili kuendana na mahitaji na majukumu ya sasa ya Jeshi letu. Kwa mwelekeo huo, na hasa kutokana na jukumu la kulinda amani kuchukua umuhimu katika majukumu ya Jeshi, kumeanzishwa kitengo cha *Peace Keeping Training Centre (PTC* kinachoendesha mafunzo ya ulinzi wa amani kwa maafisa na askari wetu.

Katika mwaka 2006/2007 kitengo hicho kiliendesha mafunzo kadhaa, kwa mfano maandalizi ya maafisa na askari walioko Lebanon, kozi ya unadhimu kwa maafisa kuhusu kazi za Umoja wa Mataifa katika operesheni za kulinda amani (*United Nations Staff Officers Course*), kozi ya Ukufunzi wa Sheria za Kivita (*Law of Armed Conflict Instructors Course*) na kozi ya maafisa wadogo wa kazi za Umoja wa Mataifa katika operesheni za kulinda amani (*United Nations Junior Officers Course*). Ushiriki wa Jeshi letu katika majukumu ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na ulinzi na uangalizi wa amani katika nchi zenye migogoro duniani, ni njia mojawapo ya kuwapatia wanajeshi wetu elimu zaidi ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na vyombo vingine vya usalama nchini, Jeshi limeendelea kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa umma ili kutekekeleza azma ya Serikali ya kuendelea kuimarisha amani na utulivu nchini.

Miongoni mwa majukumu yaliyofanywa na Jeshi ni pamoja na uundaji wa kombania za mgambo katika mikoa yote 21 Tanzania Bara. Jukumu la kombania hizo ni kuendelea kuwa nguvu ya akiba na kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi katika maeneo yao.Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Serikali imelinunulia Jeshi baadhi ya vifaa na vitendea kazi, na kuliwezesha kutoa mafunzo kwa watendaji wake katika jukumu lake la kusaidia mamlaka za kiraia katika kukabiliana na madhara ya maafa na dharura hapa nchini. Kutokana na kuimarika kiuwezo katika jukumu hili, Jeshi liliitikia na kutekeleza wajibu wake huo katika matukio na majukumu yafuatayo:-

Jeshi lilishiriki katika shughuli za uokoaji wakati wa mafuriko mkoani Shinyanga na Mtwara, ajali ya garimoshi huko Tabora na kusaidia katika tatizo la kuharibika kwa kivuko cha Kigamboni, Dar es Salaam. Aidha, Jeshi lilishiriki kikamilifu katika mazishi ya watu waliofariki katika ajali ya basi iliyotokea nje kidogo ya mji wa Singida tarehe 15 Juni, 2007.Hospitali za Jeshi zimeendelea kutoa huduma za tiba kwa wananchi wanaoishi jirani na makambi husika ikiwa ni pamoja na Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo kwa wananchi wa Dar es Salaam.

Jeshi liliandaa gwaride katika sherehe za kitaifa hususan Kumbukumbu ya Sikukuu ya Uhuru, Mapinduzi ya Zanzibar, Muungano na Siku ya Mashujaa.Kama ilivyokuwa kwa miaka ya nyuma, Jeshi lilitoa burudani kwa wananchi kupitia vikundi vyake vya utamaduni, muziki wa dansi, taarabu, sarakasi, *brassband*, maigizo na michezo mingine.Mheshimiwa Spika, juhudi za kulipatia Jeshi zana na vifaa vya kisasa zimefanywa sambamba na hatua za kuimarisha usalama wa vyombo hivyo kwa kuboresha hifadhi na matunzo yake.

Hivyo, katika mwaka 2006/2007 maghala ya kuhifadhia milipuko, zana na vifaa katika baadhi ya vikosi vya Jeshi yamefanyiwa ukarabati kama hatua ya kuvikinga dhidi ya jua, mvua na vumbi ili kuzuia kuchakaa haraka vyombo hivyo vinavyonunuliwa kwa gharama kubwa.

Aidha, hatua hiyo imelenga katika kuimarisha usalama wa silaha na milipuko hatari, ambayo isipopatiwa hifadhi ipasavyo, inaweza kulipuka na kusababisha majanga makubwa kwa maeneo yaliyo jirani na vikosi.Mheshimiwa Spika, vile vile hatua zimechukuliwa kuhakikisha Jeshi linajenga uwezo wa kufanyia matengenezo na ukarabati wa vifaa na zana zake ili ziweze kutumika kikamilifu katika jukumu la ulinzi wa nchi. Kwa mfano, katika mikataba ya ununuzi wa zana na vifaa, masuala ya huduma baada ya mauzo (*after sales services*), mafunzo kwa mafundi na watendaji, upatikanaji wa vipuli na uhawilishaji wa teknolojia (*transfer of technology*) yamepewa umuhimu mkubwa.

Aidha, hatua zimechukuliwa kuimarisha karakana mbalimbali za Jeshi kwa kuzipatia vifaa na vipuli, na kutoa mafunzo ya ujuzi kwa mafundi na watendaji wa karakana hizo. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 ushirikiano wetu na nchi rafiki katika nyanja za ulinzi na kijeshi uliendelea kuimarika kwa kupata misaada ya vifaa na teknolojia ya kijeshi, mafunzo ya elimu ya kijeshi na uzoefu kutoka majeshi mengine. Mambo muhimu yaliyotokea katika mwaka 2006/2007 kuhusu ushirikiano wetu wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine duniani ni yafuatayo:-

(a)Ushirikiano na Serikali za Nchi Moja Moja (*Bilateral Cooperation)*

(i) Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imetoa vifaa na nafasi za kozi mbalimbali za elimu ya kijeshi kwa maafisa na askari wa Jeshi katika vyuo vya kijeshi nchini China. Vile vile, katika kudumisha ushirikiano kati ya nchi hizi mbili kumekuwepo na ziara za kirafiki za kutembeleana baina ya viongozi wa ngazi za juu, ikiwemo ziara ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nchini China mwezi Mei 2007.

(ii) Serikali ya Shirikisho la Ujerumani Serikali ya Shirikisho la Ujerumani iliendelea kusaidia katika ujenzi na ukarabati wa karakana ya Jeshi na Hospitali Kuu ya Jeshi, Lugalo, Hospitali za kanda katika mikoa ya Arusha, Mwanza na Mbeya. Ujenzi wa Hospitali ya Bububu, Zanzibar ulikamilika na kukabidhiwa rasmi kwa Serikali mwezi Machi, 2007.

Vile vile Serikali ya Ujerumani imetoa nafasi za kozi za kijeshi na kitalaam katika fani mbalimbali kwenye vyuo vya nchi hiyo.

(iii) Serikali ya Canada Serikali ya Canada ilisaidia nafasi za kozi za ulinzi wa amani, ukamanda wa unadhimu mdogo na lugha ya Kifaransa kwa jeshi letu. Aidha, nchi hiyo kupitia jeshi lake inatarajia kuendesha kozi maalum kwa ajili ya wanasheria wa jeshi letu ili kuboresha utendaji katika taaluma hiyo.

(b)Ushirikiano wa Kikanda *(Regional Cooperation):-*

Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kusaidia kuratibu utekelezaji wa mkataba wa ushirikiano kati yetu na nchi za Afrika Mashariki katika sekta ya ulinzi. Mambo muhimu yanayotekelezwa katika mpango huo ni kutolewa kwa nafasi za mafunzo katika vyuo vya nchi za jumuiya hii, ubadilishanaji wa wanafunzi, wakufunzi na mazoezi ya medani. Aidha, utamaduni na michezo imefanyika kila mwaka kwa mzunguko wa kila nchi kuwa mwenyeji wa michezo hiyo. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)*Chini ya Ushirikiano wa nchi za *SADC* mambo yafuatayo yametekelezwa**:-**

•Tanzania hivi sasa ni Mwenyekiti wa Organ ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya *SADC*. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa makubaliano ya kiulinzi na usalama ya jumuiya hii kwa kushiriki katika vikao vya ngazi mbali mbali.

•Majeshi ya nchi za *SADC* yameshirikiana kwa karibu katika kutoa nafasi za mafunzo kwenye vyuo vya kijeshi ili kubadilishana uzoefu na ujuzi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa majeshi hayo.•Wakuu na maafisa wengine wa majeshi hayo wamekuwa wakitembeleana ili kudumisha uhusiano.

•Jeshi letu limeendelea na mpango wa kukamilisha mikakati ya kuunda kikosi ambacho kitakuwa chini ya Brigedi ya *SADC* itakayoundwa katika jeshi la pamoja la Afrika. Tanzania, kama Mwenyekiti wa *SADC* Organ, ina jukumu la kufanikisha uzinduzi wa Brigedi ya *SADC* ambao unatarajiwa kufanyika tarehe 17 Agosti, 2007 nchini Zambia.

(c)Ushiriki katika utatuzi wa migogoro duniani. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya nchi mbalimbali chini ya mwavuli wa jumuiya za kikanda.

(d)Operesheni za Ulinzi wa Amani Jeshi limeshiriki katika operesheni za Umoja wa Mataifa za kulinda amani katika nchi mbalimbali za Afrika na Asia zilizokumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika mwaka 2006/2007 Jeshi lilipeleka maafisa katika operesheni za kulinda amani katika mgogoro wa nchi za Ethiopia na Eritrea, Lebanon, Ivory Coast na Sudan kama waangalizi wa amani na wanadhimu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ukakamavu, ulinzi, uimarishaji wa umoja wa kitaifa na kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo wa nchi yao, yaliendelea kutolewa katika makambi mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Taifa. Sambamba na mafunzo hayo, vijana hao walipatiwa mafunzo ya stadi za kazi na uzalishaji mali katika fani za uvuvi, kilimo, ufugaji bora wa wanyama na elimu ya hifadhi ya mazingira. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, hali ya utoaji mafunzo hayo kwa vijana katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ilikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Vijana 3,156 wa Operesheni Jiajiri kati ya 3,354 (wavulana 2,486 na wasichana 868) waliojiunga na mafunzo mwezi Machi 2005 walimaliza mafunzo yao ya miaka miwili mwezi Machi, 2007. Vijana 1,139 kati ya waliomaliza mafunzo, waliweza

kupata ajira katika taasisi mbalimbali hapa nchini ambapo Jeshi la Magereza lilichukua vijana 89, Kampuni ya madini Anglo Mine Geita ilichukua vijana 104 na Jeshi la Wananchi liliandikisha vijana 946 kwa mafunzo ya kijeshi.

(b)Vijana 2,454 (wasichana 479 na wavulana 1,975) wa Operesheni Kasi Mpya walijiunga na mafunzo hayo mwezi Machi 2006. Baada ya kumaliza mafunzo ya awamu ya kwanza ya ukakamavu na uzalendo vijana 518 kati yao waliandikishwa kujiunga na Jeshi na waliobakia kwa sasa wanaendelea na mafunzo ya awamu ya pili ya stadi za kazi na uzalishaji mali katika makambi mbalimbali.

(c) Vijana 3,902 (wavulana 3,240 na wasichana 662) wa Operesheni Maisha Bora wameanza mafunzo yao ya miaka miwili mwezi Juni 2007 katika makambi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) liliendelea kuendesha miradi katika sekta ya viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, uhandisi na ujenzi pamoja na biashara. Lengo la shirika ni kuzalisha mali, na faida inayopatikana kusaidia Serikali kugharamia uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa. Katika mwaka 2006/2007, SUMA JKT ilitekeleza majukumu mbali mbali ya uzalishaji mali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shughuli za kilimo na ufugaji ziliendelea kutekelezwa katika vikosi mbalimbali. Kilimo cha mazao ya muda mrefu na mfupi ya chakula na biashara kilifanyika. Mazao hayo ni mahindi, mpunga, kahawa, zabibu, alizeti na korosho. Aidha, kilimo cha zao jipya la nishati mbadala la mibono kiliendelea vizuri na hadi sasa hekta 300 zimelimwa na kupandwa. Ufugaji wa kuku, ngo'mbe, mbuzi, kondoo na nguruwe uliendelea kutekelezwa katika vikosi vya Ruvu na Mafinga, na kwa kiasi kidogo katika vikosi vingine. Juhudi za kuwapata wawekezaji wenye uwezo kimtaji, toka ndani na nje ya nchi, ili kushirikiana nao katika uzalishaji kwenye maeneo hayo zinaendelea kufanywa.Shughuli za SUMA JKT katika sekta ya viwanda zilikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kiwanda CAMISUMA kilishona sare za thamani ya jumla ya shs 214.**2** milioni kwa ajili ya taasisi mbalimbali ikiwemo JKT yenyewe, Jeshi la Magereza, Mgambo, Hotel za White Sands na Peacock.

(ii) Kiwanda cha Ushonaji cha JKT Ruvu kilishona sare za vijana wa JKT jozi 4,000 zenye thamani ya Shs 152.0 milioni na sare za mgambo jozi 100 zilizouzwa thamani ya shs 0.6 milioni

(iii) Kiwanda cha *TANZANSINO* kilitengeneza dawa ya malaria ya *Dihydrotan* yenye thamani ya shs 78.0 milioni.

(iv) Kiwanda cha Samani cha Chang'ombe kilitengeneza samani za watu binafsi na taasisi mbalimbali zenye thamani ya shs 268.9 milioni.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT iliingia mkataba na Serikali kujenga nyumba za maafisa na askari wa Jeshi katika vituo vya Dar es Salaam na Arusha zenye thamani ya shs 5.1 bilioni. Pamoja na kazi hizi, SUMA JKT iliendelea kukamilisha miradi ya ujenzi wa majengo kwenye wilaya mpya za Chato, Siha, Mkinga, Nanyumbu na Tandahimba.

Aidha, SUMA JKT ilikabidhi mradi wa nyumba 250 za Serikali za Mwangaza, zilizopo mjini Dodoma na magorofa 25 ya kuishi watumishi wa umma Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, uwezo mdogo wa Serikali kifedha uliendelea kuwa kikwazo cha uwekezaji katika mitambo na utaalam ili kuimarisha shughuli za viwanda, utafiti na maendeleo ya teknolojia ya kijeshi kwenye mashirika yetu ya Mzinga na Nyumbu.

Kutokana na hali hii, bado hatujafanikiwa kupata mitambo ya kisasa kwa ajili ya kukarabati au kuimarisha uzalishaji katika Shirika la Mzinga, na hatujaweza kuendeleza teknolojia ya gari la Nyumbu kwa uzalishaji kibiashara. Pamoja na kuwepo hali hii, shughuli za viwanda, utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya kijeshi zilikwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika hili, ambalo hushughulika na utafiti na uzalishaji wa vifaa vya kijeshi, lilitekeleza shughuli zake kwa kutumia mitambo ya zamani iliyopo. Hivyo uzalishaji hakuweza kufikia kiwango kinachohitajika. Hata hivyo Shirika hili lilifanya shughuli za utafiti na uboreshaji wa bidhaa na vifaa mbalimbali kwa matumizi ya Jeshi, pamoja na kufufua na kukarabati vifaa na zana zilizokuwa zimeharibika kiwandani na pia vipuli mbalimbali vya Shirika la Reli Tanzania. Vile vile, Shirika lilifanya ukarabati mkubwa wa baadhi ya majengo yake kama sehemu ya maandalizi ya uimarishaji na uboreshaji wa shughuli za uzalishaji katika kiwanda chake pindi mitambo ya kisasa itakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumbu, ambalo hushughulika na utafiti na uendelezaji wa tekinolojia ya magari ya kijeshi, liliendelea kuongeza ubora wa teknolojia ya gari la Nyumbu kwa kurekebisha kasoro zilizogundulika wakati wa majaribio yake. Aidha, Shirika limeunda magari matano yatakayogawiwa katika baadhi ya vikosi vya Jeshi kwa ajili ya majaribio. Idadi hiyo inafanya magari yote yaliyokwishaundwa tangu mwaka 2004/2005 kufikia 26.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2006/2007, awamu ya tatu ya mradi wa ITN iliendelea kutekelezwa ambapo mtambo chotara wa satelaiti wenye kutumia mawimbi ya masafa ya “C” na “Ku” ulisimikwa. Huu ni msingi mkuu wa kuwezesha kutoa huduma ya mawasiliano kwa mfumo wa Serikali Mtandao *(e-Government*). Wakati huo huo huduma ya *ITN* kwa Jeshi iliendelea kuwa ya kuridhisha ingawa athari za uchakavu wa mitambo kwa vikosi vilivyojengewa mitambo ya mtandao huu katika awamu ya kwanza mwaka 1989 zinaanza kujitokeza. Kuanzia mwaka 2007/2008 tunatarajia kuanza kazi ya kubadilisha mitambo ya zamani kwenye vituo mbalimbali vya *ITN.*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kupunguza kero na kuboresha huduma na utendaji katika maeneo mbalimbali jeshini ili kuwawezesha wanajeshi kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Lengo la Serikali ni kutoa huduma nzuri katika mahitaji muhimu ambayo ni mavazi, chakula, usarifi makazi na mabwalo pamoja na malipo ya mishahara na marupurupu kadri uwezo wa Serikali kifedha unavyoboreka. Katika mwaka 2006/2007 hali ya utoaji wa huduma hizi kwa wanajeshi ilikuwa kama ifuatavyo:-

Kero ya ukosefu wa sare za Jeshi hususan mavazi ya kufanyia kazi za kila siku (*working dress*) na medani (*combat*) imeondolewa. Ununuzi wa mavazi uliendelea kufanyika ili kuhakikisha upungufu uliokuwepo siku za nyuma hautokei tena.

Huduma ya chakula imeendelea kuboreshwa ambapo kuanzia Januari, 2007 Serikali imeongeza kiwango cha kumlisha Mwanajeshi kutoka shs 60,000.0 hadi shs 75,000.0 kwa mwezi. Aidha, utaratibu wa "*canteen system*" uliopo sasa umeliwezesha Jeshi kuondokana na madeni ambayo yalikuwa yanatokana na chakula miaka ya nyuma.

Ukarabati wa nyumba za kuishi, mabwalo na maofisi ulifanyika Makao Makuu ya Jeshi, makambi ya Kigamboni, Kinonko, Lugalo, Makao Makuu ya Jeshi na Potoa. Aidha, ukarabati wa mifumo ya maji safi na maji taka ulifanyika katika makambi ya Mirambo, Lugalo, Monduli na Chukwani. Hali kadhalika ukarabati wa njia za umeme ulifanyika katika makambi ya Kinonko, Ngerengere na Potoa. Kwa upande wa zahanati, ukarabati ulifanyika Pemba. Ukarabati pia ulifanyika kwenye vituo vyote vya malipo vya kanda.

Huduma ya usafiri wa nchi kavu na anga jeshini imeendelea kuboreshwa. Kutokana na hali hiyo, usafiri wa kawaida wa wanajeshi (kwa kutumia ndege na magari) sasa ni nafuu na hivyo shughuli za kupeleka huduma za kiutawala maeneo yenye ugumu unapatikana. Aidha, usafiri wa dharura au maalum (*special flights*) kwa ndege upo.Serikali iliendelea kuboresha mishahara na marupurupu ya wanajeshi na watumishi wa Umma na kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Desemba, 2006, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilianza kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba mpya 270 za kuishi maafisa na askari pamoja na mabwalo mawili kwenye makambi yaliyoko katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Ujenzi huo, unaotekelezwa kwa gharama ya Shs 21.0 bilioni ambazo ni mkopo toka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* unategemewa kukamililka mwezi Septemba, 2007.Sambamba na mkopo huo, Serikali imepata mkopo mwingine wa Shs 23.0 bilioni pia toka *NSSF*. Kati ya fedha hizo, Shs 16.0 bilioni zimetumika katika ununuzi wa mtambo wa kujenga nyumba za wanajeshi, na Shs 7.0 bilioni kununulia mali ghafi ya ujenzi wa nyumba hizo kwa kutumia mtambo huo toka Marekani. Ujenzi wa nyumba za awali kwa kutumia mtambo huo yatafanyika mwezi Agosti, 2007. Madhumuni ya kununua mtambo huo ni kutokana na azma ya Serikali ya kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi, na hivyo kupunguza makali ya tatizo sugu la uhaba wa huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, programu ya kuyapima, kuyalipia fidia na kasha kuyamiliki kisheria maeneo yote ya Jeshi kwa ajili ya makazi, mabwalo, maghala, Ofisi, maeneo ya michezo na mafunzo/mazoezi ya kijeshi pamoja na uzalishaji mali iliendelea kutekelezwa. Katika mwaka 2006/2007 maeneo ya Chenene Farm JKT, Dodoma na Tunduru yalipimwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inakusudia kuyamiliki kisheria maeneo yote ya Jeshi ambayo yamepimwa na hayana migogoro ya fidia. Tunatarajia kufanya kazi hii

katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa kuanzia kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inafanya kazi zake kwa malengo na ufanisi mkubwa, Wizara imehuisha Mpango Mkakati kwa kipindi cha 2004/2005 hadi 2006/2007 na kuandaa mwingine kwa mwaka 2007/2008 hadi 2009/2010. Mpango Mkakati huu, unaozingatia shabaha za kisera na malengo ya ulinzi wa Taifa kulingana na Mwelekeo wa Sera za CCM (mwaka 2000 hadi 2010) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, umeainisha malengo ya Wizara kwa uwazi na kujikita zaidi katika malengo ambayo yanatekelezeka.

Aidha, Mpango Mkakati huu umeainisha kazi ambazo inabidi zitekelezwe kwa muda mfupi zaidi ili kukidhi mahitaji yaliyopo sasa ya wadau wote wa Wizara.Katika mwaka 2006/2007, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilisimamia ipasavyo uendeshaji wa shughuli zake kwa misingi ya sheria katika maeneo ya nidhamu, ajira na uadilifu ili kudumisha dhana ya utawala bora. Kubwa zaidi, Wizara imehimiza viongozi na watendaji wa ngazi zote kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine lililoendelea kusimamiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni utunzaji wa mali za Serikali na udhibiti wa matumizi bora ya fedha za umma. Mambo hayo yote mawili ndiyo yanayopima uwajibikikaji mahsusi wa utendaji kazi unaozingatia utawala bora na ustawi wa wananchi. Wizara kwa kutambua hivyo, imetekeleza kazi zake kwa kuzingatia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 na Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inategemea kuzingatia na kutoa msukumo zaidi katika udhibiti wa matumizi bora ya rasilimali zake ikiwa ni pamoja na fedha ili ziweze kuleta matunda yanayolingana na thamani yake. Vilevile, Wizara itaendelea na mpango wake wa kuhakikisha kuwa vituo vyote vya malipo mikoani vimeunganishwa kwenye mtandao na Makao Makuu. Hatua hii itaongeza udhibiti na uwajibikaji wa fedha za umma na utoaji wa taarifa za fedha zilizo sahihi na kwa uharaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatambua umuhimu wa raslimali watu. Pamoja na uwezo mdogo wa fedha uliokuwepo, tumeweza kutumia fedha hizo kwa ufanisi na kwa kufuata mpango wa mafunzo uliopo. Wizara imeajiri jumla ya watumishi 15 na kupandisha vyeo watumishi 346 na kuthibitisha kazini watumishi 38. Vile vile, watumishi 320 ambao walikuwa wamekaa kwa muda mrefu bila ya kupandishwa vyeo (mlundikano) wamepandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa jeshi kwa mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kuwapatia elimu maafisa, askari na watumishi wa umma katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mpango huu una lengo la kutoa mafunzo kwa makundi hayo hadi kufikia kiwango cha juu ikiwa ni pamoja na shahada. Hadi sasa wanafunzi

wanaoendelea na masomo vyuoni ndani ya nchi ni 137 na nje ni wanane (8). Aidha, Jeshi liliwapandisha askari na maafisa wake kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, juhudi za lazima zinazofanyika na zinazohitaji nguvu na busara ni zile za kupigana na janga la UKIMWI. Tunalipa umuhimu na uzito unaostahili suala hili kwa kuhakikisha kuwa dawa kwa ajili ya kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI na magonjwa nyemelezi zinatolewa. Aidha, huduma zinazotolewa kwa wagonjwa wa UKIMWI haziishii tu kwa wanajeshi na watumishi wa Wizara, bali hutolewa pia kwa familia zao na watu wa maeneo yanayozunguka kambi za Jeshi.

Mheshimiwa Spika, katika shughuli za kila siku za majeshi yetu zimo pia huduma za elimu zinazotolewa kwa jamii ya Watanzania. Hili ni jukumu mojawapo linaloendeleza uhusiano mwema na mshikamano kati ya Jeshi na wananchi. Aidha, utoaji wa elimu hiyo ni mchango muhimu na mzuri katika utekelezaji wa azima ya Serikali ya kupambana na adui ujinga.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya limepiga hatua kubwa katika kuimarisha elimu ya msingi kwa watoto wa familia za maafisa na askari pamoja na watoto wa wananchi waishio katika maeneo yanayozunguka makambi ya jeshi hili. Jeshi la Kujenga Taifa limeweza kuimarisha ubora wa elimu ya msingi kwa ushirikiano mkubwa na Halmashauri za Wilaya ambako kuna makambi yake, yaani usimamizi, uratibu na uendeshaji wa elimu ya msingi ulifanyika katika makambi ya Mlale, Oljoro, Maramba, Mgambo, Makutupora, Chita na Bulombora. Elimu ya Sekondari na Ufundi Stadi. Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kutoa elimu ya sekondari katika shule za Chabruma, Kawawa, Jitegemee, Kizuka, Nyuki, Kigamboni, Unyanyembe, Ruhuniko, Makongo na Air Wing. Elimu hii, licha ya kutolewa kwa vijana wa maafisa na askari, pia hutolewa kwa watoto wa familia za wananchi waishio katika maeneo yaliyopo jirani na shule hizo. Kwa upande wa Dar es Salaam, shule hizi hupokea wanafunzi wengi sana sio tu kutoka maeneo ya karibu, bali jiji lote.

Aidha, elimu ya ufundi staid, pia imetolewa kwa vijana wa familia za wananchi waishio jirani na makambi ya Mlale, Mgulani, Maramba na Makutupora kwa gharama nafuu. Katika mwaka 2006/2007 Serikali iliendelea kuwalipa majenerali wastaafu stahili zao kulingana na sheria iliyopo, kutoa huduma muhimu kama vile matibabu, viungo bandia na malipo wanayostahili walemavu wa vita.

Aidha, Sera ya Ulinzi wa Taifa, ambayo iko hatua za mwisho za maandalizi inatamka kuwa jukumu la kuhudumia walemavu hao ni la Taifa. Kwa hiyo, huduma hiyo itatolewa kulingana na mikakati itakayobainishwa kwenye sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililoshughulikiwa kwa makini ni mirathi na matatizo yaliyopo kutokana na kutokufahamu taratibu za wasimamizi wa mirathi. Jambo hili husababisha kuchelewa kwa malipo ya mirathi kwa wahusika. Juhudi zinafanyika kulitanzua kwa kuongeza idadi ya maafisa wa kushughulikia mirathi na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Makao Makuu ya Jeshi, Makao Makuu ya JKT pamoja na Wizara ya Fedha kuhusu utayarishaji wa nyaraka na malipo kwa wasimamizi wa mirathi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 jumla ya majalada 2,020 ya wastaafu, 269 ya walemavu na 116 ya mirathi yalishughulikiwa. Majalada 668 yamepelekwa Hazina kwa ajili ya malipo. Ili kupunguza kero ya kuchelewa malipo kwa wastaafu, warithi na walemavu, Jeshi liliendesha semina mbalimbali kuhusu taratibu za kufuata katika kupata mafao yao. Vilevile, Jeshi lilitoa vijarida kuhusu elimu ya pensheni ya maafisa na askari wastaafu.

Mheshimiwa Spika, suala la jinsia nalo limezingatiwa kwa ukamilifu katika ajira na upandishwaji vyeo. Wizara imeshirikiana na taasisi zingine katika mafunzo ya jinsia ili suala hili lieleweke kwa watumishi wake. Kwa kutambua umuhimu huo, wizara inalo dawati (*desk)* la jinsia kwa ajili ya kuratibu shughuli mbalimbali za utekelezaji.Mheshimiwa Spika, suala la michezo jeshini ni muhimu kwani linajenga ukakamavu, afya, ubunifu na umoja. Katika mwaka 2006/2007 majeshi yetu yalishiriki katika michezo mbalimbali.

Tukio kubwa zaidi ni michezo ya Majeshi ya Afrika Mashariki ambayo mwaka huo yalifanyika mjini Zanzibar kuanzia tarehe 20 hadi 30 Mei, 2007. Katika michezo hiyo, jeshi letu lilipata ushindi wa kwanza. Kwa mwaka ujao wa 2008 michezo hiyo itaendelea kwa mzunguko na kufanyika nchini Uganda, ambapo nchi za Burundi na Rwanda nazo zitashiriki. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watumishi wa Umma, Wizara imeshiriki katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, (SHIMIWI) yaliyofanyika mjini Tanga mwezi Septemba, 2006.

Lakini wizara haikuweza kushiriki katika michezo ya Mei Mosi, iliyofanyika mjini Mwanza kutokana na sababu mbalimbali. Tunaamini kuwa mambo yakienda sawa,mwaka 2007/2008 wizara itashiriki michezo ya Shimiwi na Mei Mosi. Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, kwa pamoja zinabainisha kwamba, amani na usalama ni mihimili muhimu na lazima kwa maendeleo na maslahi ya Taifa.

Bila amani na usalama wa wananchi na mali zao, matarajio na malengo ya maendeleo ya Taifa hayataweza kufikiwa. Kwa hiyo, kama Taifa tunahitaji wakati wote kujijengea mazingira ya amani ikiwa ni kwa kuhakikisha kuwa inakuwepo kinga thabiti dhidi ya tishio la ulinzi na usalama wa nchi yetu. Nguvu ya kijeshi, kwa maana ya kuwa na Jeshi lililo na utayari na utimamu mkubwa kiutendaji, ndiyo kinga kuu dhidi ya tishio la ulinzi na usalama wa nchi yetu. Utayari na utimamu wa Jeshi utapatikana kwa kuwapatia kikamilifu wanajeshi wetu mafunzo ya elimu ya kijeshi, huduma nzuri za chakula na malazi, zana na vifaa vya teknolojia ya kisasa kuwawezesha kutekeleza jukumu lao la kulinda nchi yetu katika mazingira ya sasa ya dunia.

Tukiwa dhaifu kijeshi, ni wazi kuwa tunashawishi wazo la kuvamiwa na maadui na hivyo kuweka hatarini usalama, maendeleo na maslahi ya Taifa letu.Kwa misingi hiyo, ni dhahiri kuwa pamoja na hatua tunazochukua za kudumisha amani na utulivu na nchi nyingine duniani, tunahitaji tuwe na nguvu za kijeshi za kutosha kuhakikisha ulinzi na usalama wetu na hivyo kudhoofisha mawazo ya maadui kutaka kutuvamia.

Ili kukidhi mahitaji haya, hatuna budi kuchukua hatua zaidi kuimarisha ulinzi wa Taifa letu ikiwa ni pamoja na kutekeleza malengo ya bajeti ya wizara hii kwa mwaka 2007/2008, ambayo kwa heshima na taadhima, naiwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mpango na bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inazingatia shabaha kuu za kisera na malengo ya ulinzi wa Taifa, Mpango Mkakati wa Wizara na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Mwaka 2005. Kwa hiyo kazi zitakazofanyika katika mwaka huu ni:-

(a) Kuimarisha uwezo wa majeshi yetu kwa kuwa na kiwango cha juu cha utayari kiutendaji.

(b)Kuboresha mazingira ya kazi, vitendeakazi, huduma na mahitaji muhimu kwa wanajeshi, watumishi na vijana watakaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

(c)Kuendeleza juhudi za kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI na kutoa huduma ya dawa kwa waathirika wa ugonjwa huu.

(d) Kuwapatia wanajeshi na watumishi wa umma stahili zao za kisheria kikamilifu.

(e)Kuendeleza ushirikiano wa kijeshi kati ya nchi yetu na nchi jirani na rafiki katika nyanja zinazohusu mafunzo ya pamoja, taaluma mbalimbali na kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa katika ushirikiano kiulinzi hususan Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC).*

(f)Kuendeleza tafiti na kuboresha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali toka mashirika yetu kwa ajili ya matumizi ya Jeshi letu.

(g)Kuendeleza mafunzo ya kijeshi, ufundi stadi, kilimo na taaluma nyinginezo kwa vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

(h)Kugharamia mafunzo ili kuongeza ufanisi kwa watumishi wa umma na pia kuyaimarisha majeshi yetu.

(i)Kuendelea na utekelezaji miradi ya maendeleo hasa yenye mikataba, kama vile ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi, kulipia ununuzi wa magari na kuendeleza mtandao wa mawasiliano jeshini *(ITN).*

(j)Kuboresha utumishi wa Umma kama ilivyoelekezwa katika *"Public Service Reform Programme".*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama ilivyoelezwa katika Hotuba hii, kwa mwaka 2007/2008, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 309,636,963,000.00 ambapo kati yake shilingi 255,202,963,000.0 zitatumika kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 54,434,000,000.0 ni Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Fungu 38 - Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania - Bajeti ya Matumizi ya Kawaida – shilingi 198,693,067,000.0. Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo- shilingi 203,000,000.0

(b) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa - Bajeti ya Matumizi ya Kawaida – shilingi 47,650,625,000.0. Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo – shilingi 203,000,000.0. (c) (c) Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Bajeti ya Matumizi ya Kawaida – shilingi 8,859,271,000.0 . Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo – shilingi 54,028,000,000.0.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama nilikuwa napenda muone kwamba kuna kijitabu kingine kidogo kimesambazwa na Mheshimiwa Waziri ambacho kinahusu Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni kwa mwaka wa fedha uliopita.

Napenda kwa niaba yenu nimpongeze sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu ni utaratibu mzuri sana na inakuwa rahisi hata kufanya rejea kwa sababu yale ya mwaka jana unayaona hapa hapa wakati unataka kuchangia. Ni utaratibu mzuri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

**MHE. JANETH M. MASSABURI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge - Toleo la Mwaka 2004, ninatumia fursa hii kuwasilisha Taarifa na maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadiro ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika**,** Maoni na Ushauri wa Kamati unatokana na Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu ulinzi na usalama wa Mipaka ya nchi na Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara iliyowasilishwa mbele ya Kamati

Tarehe 7 Juni, 2007 Jijini Dar es salaam. Kwa kuzingatia Kanuni Na. 81(1) na Na. 81(4) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004.

Kamati ilipitia na Kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 pamoja na Ushauri wa Bunge uliotolewa kwa Wizara hii.

Aidha, Kamati ilipitia Mafungu ya Makadirio kwa Mwaka 2007/2008 ya Fungu 38 (Ngome) na Fungu 39 (Jeshi la Kujenga Taifa) na Fungu 57 (Wizara na Mashirika).

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa William Kusila,-Mwenyekiti wa Kamati kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba yake na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kipekee kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uwezo wa kuwepo hapa leo.

Pia napenda kumshukuru sana mume wangu mpendwa Mheshimiwa Dr. Didas Massaburi, watoto wetu, wazazi wangu na wapiga kura wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam na hasa wanawake kwa kuwa karibu nami na kunipa ujasiri kama mama na hivyo kuweza kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kabla ya kutoa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutumia nafasi hii Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi zake za kuboresha utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yusuph Mzee, Katibu Mkuu, Ndugu Abel Mwaisumo na Wataalam wote wa Wizara kwa juhudi wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha Utendaji wa Wizara hii.Aidha, ninapenda kutoa pongezi kwa Wizara kwa kuweza kuandaa na kuwasilisha mbele ya Kamati Taarifa inayoelezea bayana utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2006/2007.

Napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa namna ambavyo wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe wa Kamati wamekuwa bega kwa bega katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kufanya ziara katika Vikosi mbali mbali vya Majeshi ya Ulinzi na pia kwa kutoa maoni yao na ushauri ambao

Wizara imekuwa ikifanyia kazi. Ningelipenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kama Ifuatavyo:- Mheshimiwa William J. Kusila, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Capt.(Rtd) George H. Mkuchika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati wakati wajumbe ni Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col.(Rtd) Saleh A. Farrah na Mheshimiwa Maria I. Hewa.

Wajumbe wengin e ni Mheshimiwa . Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Col.(Rtd) Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, MheshimiwaBrig. Gen.(Rtd) Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda na Mheshimiwa Janeth M. Massaburi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka na Sekretarieti ya Kamati, Ndugu Peter Magati, Hussein Athuman na Ndugu Patson A. Sobha, kwa kazi na huduma nzuri walizozitoa kwa Kamati na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na pia kukamilisha taarifa hii. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, iliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati na taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Kamati ilipokea na kuchambua kwa kina taarifa hizo.Kamati ilipata malezo ya kina toka kwa Waziri ambaye alieleza Dira, Mwelekeo na Majukumu ya Wizara, Utekelezaji wa Maagizo/Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2006/2007 pamoja na kuelezea mafanikio na matatizo ya utekelezaji katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Aidha, Kamati ilipata maelezo ya kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na yalitolewa Maombi ya Fedha za Matumizi kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Wizara hii imetekeleza kwa kiasi kikubwa majukumu yake na pia imefanyia kazi Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na utekelezaji wake unaonekana dhahiri. Pamoja na Mambo mengine, Wizara imeonyesha mafanikio katika utekelezaji wa masuala mbali mbali ya malengo yaliyokusudiwa kwa mwaka 2006/2007 ambayo ni pamoja na:Utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Majeshi kiutendaji ambao unahusu mikataba mbali mbali ikiwemo: Ununuzi wa Helkopta, Ununuzi wa magari na vipuri naKufanikiwa kupata boti ziendazo kasi (*speed boats).*

Mradi wa ujenzi wa makazi ambapo jitihada zimefanyika kuwajengea wanajeshi nyumba za kuishi ikiwa ni pamoja na mabwalo na ukarabati wa baadhi ya miundombinu. Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za kuweza kuchukua jumla ya familia 270, lengo likiwa kuwawezesha wanajeshi wengi kukaa makambini. Kuboresha mtandao wa mawasiliano ya pekee Jeshini *(ITN).* Mapambano dhidi ya UKIMWI hasa kwa kuzuia maambukizi mapya. Hospitali za Jeshi zinatoa huduma ya dawa kwa waathirika waliojitokeza na pia kutoa ushauri nasaha na kuhamasisha wanajeshi na watumishi wa Umma waweze kupima afya zao. Majeshi yameendelea na mafunzo ya kinadharia na vitendo ikiwa ni pamoja na yale yaliyotolewa ndani ya Jeshi lenyewe kikanda kwa mfano Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, majeshi kushiriki katikakulinda. amani ambapo hivi karibuni wanajeshi walipelekwa kulinda amani nchini Lebanon na wanaendelea vizuri. Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ni Mzinga, SUMA na Nyumbu yameendelea na tafiti mbali mbali na uzalishaji wa bidhaa za kijeshi na uzalishaji. Kuendeleza mafunzo ya JKT kwa vijana ambapo wanajifunza mambo mbali mbali ikiwemo uzalendo na utaifa. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika maeneo mengine ambako Kamati imeona kuna upungufu na juhudi zaidi zinahitajika, imeweza kushauri ipasavyo katika masuala mbali

mbali likiwemo suala la: Ufinyu wa bajeti ambao haukidhi mahitaji halisi ya kulifanya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwa bora na la kisasa kwa kuwezesha kuwa na idadi ya wanajeshi inayokidhi na pia zana bora na za kisasą.Ongezeko la posho ya chakula kwa wanajeshi, bado halitoshelezi mahitaji ya chakula kwa sikų.Kuongezeka kwa majukumu ambayo awali hayakukasimiwa kwenye bajeti na hivyo kulazimika kuyatekeleza kwa kutumia fedha zilizokuwepo na hivyo kutofanikiwa kutekeleza baadhi ya malengo yaliyopangwa. Kwa mfano, Jeshi kupeleka wanajeshi nchini Lebanoņ.Suala la ulinzi wa mipaka ya nchi, kuna sehemuambazo alama za mipaka *(beacons*) zimeondolewa ama hazipo, mfano: kati ya mpaka wa Tanzania na Zambia na pia katika mpaka wa Tanzania na Kenya. Vilevile swala la *no man's land* litiliwe mkazo kwenye mipaka yetu yotę. Mpaka wa Malawi na Tanzania katika Ziwa Nyasa na pia jina la Ziwa Nyasa kuitwa Lake Malawi kwa upande wa Malawį. Umhimu wa kuboresha uundaji wa Sera ya Ulinzi nchinį. Suala la wafugaji kutoka Uganda kuingia Tanzania na mifugo yaọ. Urasimu katika utaratibu wa kupitisha zana, vifaa, magari na nyezo za Majeshi bandarini.

Maafisa wa Jeshi wastaafu wafikiriwe kuongezewa muda zaidi wa kuwepo kazini ili kuziba pengo la idadi ya wataalam wanaostaafu. Tofauti za viwango vya pensheni kwa Majenerali wastaafu zifanyiwe marekebisho. Aidha pensheni za maafisa na maaskari wengine wastaafu iangaliwe upya kwa nia ya kuboresha masilahi yao kutegemeana na hali iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, Waziri aliieleza Kamati ya Ulinzi na Usalama kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 pamoja na kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka huo.

Katika Makadirio hayo Kamati imeelezwa kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Jumla ya Shilingi 198,693,067,000/=.kwa Fungu 38 - (Ngome), Shilingi 47,650,625,000/=, kwa Fungu 39 - (Jeshi la Kujenga Taifa) na Shilingi 8,859,271,000/= kwa Fungu 57 (Wizara na Mashirika).

Aidha, kwa upande wa Maendeleo, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 54,028,000,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2007/2008, sasa naomba kutoa ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2007/2008:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba utaratibu wa kupitisha bandarini zana, vifaa, magari na nyenzo za Majeshi ya Ulinzi uweze kuangaliwa upya ili kuondoa urasimu na hivyo kuharakisha utekelezaji wa majukumu ya majeshi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa iharakishe mchakato wa uboreshaji wa Sera ya Ulinzi nchini pamoja na sheria za jeshi. Vilevile Kamati inashauri

Serikali iwaongezee muda zaidi Wanajeshi wanaostaafu hivi karibuni ambao ni wengi sana na hivyo kusababisha idadi ya Wanajeshi Kupungua Sana katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la Malipo ya Pensheni kwa Majenerali Wastaafu kuzingatia asilimia ya mshahara wao wakati wakiwa Jeshini, linawafanya Wastaafu wa zamani kupata kiasi kidogo sana kulinganisha na Wastaafu wa hivi karibuni kwa kuwa mishahara inatofautiana sana. Serikali itafute utaratibu wa kuwaongezea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa, Kamati inashauri kwamba Serikali iharakishe kusawazisha suala hilo na pia Ramani zote zinazouzwa nchini hasa mitaani ambazo zinaonyesha kuwa Mpaka wa Tanzania na Malawi upo katika Ufukwe wa Ziwa Nyasa kwa upande wa Tanzania badala ya Mpaka halisi kuwa kati kati ya Ziwa kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa, Serikali ipige marufuku uingizwaji wa ramani hizo na zile zilizopo nchini ziteketezwe.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa JKT wanafundishwa stadi za kazi, Serikali iangalie namna ya kuwawezesha pindi wamalizapo mafunzo yao. Aidha Serikali iendelee kuiimalisha na kuiendeleza ili izidi kuimarika kwenye masuala ya ujenzi. Pia Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu kwa Vikosi vya Wana-Anga na Wana-Maji kuwa na Vifungu (*Votes*) vyao vya Bajeti vinavyojitegemea ili kuboresha utendaji wao wa majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Janeth Massaburi ikiwakilisha Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Ni mara yako ya kwanza kusoma kitu kama hicho na umesoma kwa utulivu mkubwa sana na nakupongeza sana. Sasa napenda kumwita Mheshimiwa Masoud Salim Mbunge wa Mtambile ambaye ndiye msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama. Karibu Mheshimiwa.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Nachukua furaha hii kukushukuru wewe Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote kwa jinsi mnavyojitahidi kuimarisha demokrasia ndani ya Bunge, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Juma Athumani Kapuya Waziri na

Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee Naibu waziri kwa jinsi wanavyojituma katika kukabili majukumu ya askari wetu. Pia niwapongeze Makamanda wa Brigedia zote katika Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Viongozi na Wabunge wa Kambi ya Upinzani inayoongozwa kwa umahiri mkubwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Dr. Wilbroad Peter Slaa, ambao kwa kweli busara zao na maelekezo yao yameifanya Kambi ya Upinzani kuwa ni yenye muelekeo mzuri katika masuala kadhaa ya kitaifa yanayopelekea kutoa taswira ya wapi tupo hivi sasa na wapi tunakoelekea.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile kwa imani yao na dua zao na mashirikiano yao kwangu siku hadi siku ambayo yamepelekea kufanya kazi zangu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa. Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa ni ya zamani, na katika kipindi cha miaka 41 sasa, bado sheria hizi haijafanyiwa marekebisho makubwa yanayostahili, na kukidhi mahitaji katika kuboresha mfumo wa haki na kujenga ufanisi katika dhana nzima ya Utendaji ndani ya majeshi ya Ulinzi, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuifanyia mapitio Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa kwa kuyaangalia mambo ya msingi kwa mfano; mfumo wa Mahakama ya Kijeshi na Viwango vya adhabu zinazotolewa viangaliwe upya kwa lengo la kuboresha nidhamu na utoaji wa haki kwa wanajeshi.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sehemu ya Tatu (Fungu la 29 – 55) ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa, inatoa fursa ya haki ya mwanajeshi kulalamika ngazi ya juu pale anapoona amekandamizwa au amenyanyaswa, hivyo Kambi ya Upinzani inataka kujua ni matukio mangapi yamelalamikiwa na yameripotiwa na kupatiwa ufumbuzi katika Wizara ya Ulinzi kwa mwaka wa fedha 2006/2007. na mangapi hayapatiwa ufumbuzi na kwanini.

Mheshimiwa Spika, Nidhamu Jeshini. Nidhamu Jeshini ni jambo la muhimu sana, na sote tunafahamu Jeshi letu limejengeka kwa nidhamu ya hali ya juu, na hii imetokana na misingi imara ya Hayati Baba wa Taifa Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani hairidhishwi na baadhi ya askari wachache sana waliolitia doa jeshi letu kwa kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu, kama lile la ubungo la uvamizi wa benki, ambapo askari mmoja alihusishwa, lakini kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni, kitendo cha kukutwa na risasi 2,593 askari wa jeshi la ulinzi la Tanzania MT80186 PT Henry Mwisongo mkazi wa Keko Machungwa Dar es Salaam ambaye anatoka kikosi cha 83 (83KJ) kinasikitisha jamii.

Mheshimiwa Spika, inaonekana dhahiri Mwanajeshi huyu kwa mazingira yalivyo anajihusisha na ujambazi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu kwa mwanajeshi; hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka kujua ukweli wa suala hili.Na iwapo baada ya uchunguzi

itabainika kuwa ni mhalifu wa ujambazi basi hatua kali zichukuliwe dhidi yake ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika Makazi ya Askari. Askari kubakia makambini ni muhimu katika kujenga heshima na ufanisi wa kazi yenyewe. Kwa bahati mbaya Askari wa JWTZ asilimia 70 hukaa Uraiani, hali ambayo inapelekea kikwazo katika dhana nzima ya Nidhamu katika jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuwa na mpango wa kutekeleza miradi ya Ujenzi wa Nyumba zenye uwezo wa kuishi jumla ya familia 270 kwa mkopo wa *NSSF*, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kutafuta vyanzo vingine vya fedha za ujenzi wa nyumba za askari toka kwenye mashirika na Taasisi mbalimbali ili lengo la kuwaweka Askari makambini litimie.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanajeshi kuishi uraiani ni kasoro kubwa, ambapo sio tu kero la kwenda na kurudi Uraiani pia inampelekea Askari kutokuwa na Maadili, na miiko ya kazi yenyewe, ambapo wakati mwingine inawapelekea Askari wetu kuhusishwa na matukio ya uhalifu hali ambayo sio tu kuwa inamnyima heshima mtuhumiwa aliyeko uraiani bali inalinyima heshima Jeshi lenyewe ambalo hadi sasa Askari wetu wamekuwa ni mfano wa heshima nzuri, watiifu na majasiri ndani ya Ulinzi wa Taifa hili

Mheshimiwa Spika, Askari wa JWTZ walio nje ya Kambi wanatakiwa wapewe 10% ya mshahara wao kwa ajili ya pango lakini utaratibu huu bado haufuatwi, wengine wanaambulia 9,000/- kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia upya kwa makini suala hili kwa kipindi hiki ambacho askari wanakaa uraiani, vinginevyo Serikali iwaelekeze ni ni wapi askari atapata chumba chenye umeme na maji kwa Shs.9,000/- kwa mwezi.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Jeshi ya Lugalo kwa umuhimu wake ulivyo, nyumba wanazoishi askari kwa kweli haziendani na jeshi letu na askari wetu. Nyumba hizo katika hali zinavyoonekana zinawakilisha nyumba za askari katika makambi mengine hapa Tanzania. Jambo la kujiuliza ni je kambi zingine ambazo ziko nje ya upeo wa wakuu wa nchi ziko katika hali gani?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Mwanyanya Zanzibar zina upungufu mkubwa sana wa nyumba za kuishi askari. Kambi hii pia na Afisi moja na ya zamani iliyochakaa, hivyo ndio kusema Kambi ya Mwanyanya Zanzibar inasikitisha kutokana na hali ilivyo, hali ambayo inapunguza ufanisi wa utendaji wa wanajeshi wetu.Kambi ya Mwanyanga imezungukwa na makaazi ya raia huku Kambi ikiwa haina uzio wa kutenganisha maeneo ya Jeshi na raia, kwani jicho huona popote hivyo kuna uwezekano wa kuonekana lolote linalofanyika katika eneo la jeshi jambo ambalo si sahihi kwa miiko na maadili ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, Kambi hii haina gari la usafiri lenye sifa ya kukidhi haja ya Kambi yenyewe. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwajengea nyumba za kutosha

Askari katika Kambi ya Mwanyanya sambamba na kuweka uzio utakaotenganisha raia na Kambi.

Mheshimiwa Spika, majengo katika Kambi ya Mtoni Zanzibar ni ya zamani ambayo inaonekana kama hayo nayo haijapewa umuhimu wake unaostahili, ni imani ya Kambi ya Upinzani kuwa Serikali itaiangalia kwa jicho la huruma, sambamba na kuzikarabati nyumba za Kambi ya Bavuai zilizoko Migombani ambazo zinahitaji maboresho kulingana na hadhi na umuhimu wa kambi yenyewe. Sambamba na hilo, Kambi ya Kisakasaka na Ubago nazo zinafaa zifikiriwe kutokana na hali zake zilivyo.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya jeshi ya Uelezo haina umeme, jambo ambalo linakwamisha taratibu nyingine za kuchunguza magonjwa mbali mbali, hivyo ni imani ya Kambi ya Upinzani kwa Serikali kuweza kuipatia umeme kambi ya uelezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa nyumba unaoendelea katika Kambi ya Ali Khamis Vitongoji Pemba tunaishauri Serikali kuzikarabati kwa dharura zile nyumba ambazo askari wetu wanaendelea kuishi, kwani askari wetu wanaishi kwa sababu hawana mahali pengine tu.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Mipakani na Vituo Teule *(Detarches)*. Vituo teule (*detarches*) vina umuhimu wa pekee katika ulinzi wa Taifa letu hasa katika maeneo ambayo vituo hivyo viko mpakani hasa maeneo yenye matukio ya uhalifu wa mara kwa mara katika mikoa kama vile Kagera, Kigoma na Mara.

Mheshimiwa Spika, makazi ya wanajeshi wetu katika vituo teule bado hayaridhishi na haviendani na hali halisi ya Jeshi lenyewe lililojengeka kwa nidhamu na ukakamavu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika vituo teule, barabara zinazotoka Wilaya husika mpaka kwenye vituo hivyo nyingi ni za udongo na huwa hazipitiki wakati wa msimu wa mvua jambo ambalo ni hatari likitokea lolote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani naishauri Serikali kuwajengea nyumba zinazostahili katika vituo husika, sambamba na kuweka angalau changarawe katika barabara hizo angalau ziweze kupitika hata wakati wa mvua.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imebainika, vituo hivi vingi vina gari moja iliyochoka au hakuna kabisa. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali vituo hivi vipatiwe gari za kisasa zinazolingana na mazingira yenyewe kukabiliana na lolote linaloweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kudhibiti mipaka yetu, Kambi ya Upinzani inataka kujua kwanini beacons zilizong’olewa miaka iliyopita katika Mipaka ya Tarime (Tanzania) na Migori - Kenya mpaka leo hazijarejeshwa hasa ukitilia maanani vijiji vya Panyakoo, Ronche, na Ikoma ndio maeneo yaliyoripotiwa kuondolewa kwa beacons hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu uhakika wa mipaka yetu na nchi jirani katika maeneo ya Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika ili wavuvi wetu wanaoendelea kudhalilishwa na hata kuuawa waweze kujua mipaka halisi ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni matukio mangapi ya uhalifu yameripotiwa katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika na ni wananchi wangapi wamepoteza maisha kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2007 na Je, jeshi letu la wananchi limewasaidaje wavuvi kuokoa mali zao toka kwa majangili wa nchi jirani ?

Mheshimiwa Spika, haipe ndezi hata kidogo kuona kwamba mpaka wa Tanzania na Zambia kule Tunduma umekuwa na mwingiliano mkubwa wa nyumba ndani ya alama za mipaka (*beacons*) hali ambayo inazua utata wa kuwajua ni raia gani wa Tanzania na ni wapi raia wa Zambia. Hivyo tunajiuliza, hivi vitambulisho vya uraia vya watanzania vitakavyotolewa hata baada ya uhakiki, je, vitatoa haki kwa watanzania?

Mheshimiwa Spika, eneo linalotakiwa kuwa wazi katika mipaka kimataifa, kama utaratibu ukifuatwa ipasavyo utaondosha utata wa mipaka baina ya nchi moja na nyingine, hivi tunajiuliza uongozi wa Serikali unakuwa wapi wakati wote ambapo wananchi wanaleta vifaa vya kujengea katika maeneo yasiyostahili mipakani na kuachiwa kujenga hadi nyumba kukamilika bila ya kikwazo chochote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua iwapo mipaka hiyo inataka kuwekwa kwa utaratibu wa kimataifa na wananchi kuamriwa wavunje nyumba zao, ni nani atatoa fidia?

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kisasa. Ni dhahiri kabisa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika Sekta ya ulinzi ni jambo lisilopingika katika kuimarisha Ulinzi wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika wa kutekeleza ajira zetu katika taaluma mbalimbali kama Utawala, Sheria, Ujenzi, Sayansi, Uhandisi katika ngazi ya Shahada ya kwanza na ya pili.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwatumia vijana wenye uwezo mkubwa kielimu katika lengo la kudumu la kuunda jeshi dogo na la kisasa ambalo litafikia viwango vya maendeleo ya Sayansi na Teknolojia sambamba na kuwapatia nyenzo zenye kukidhi hoja ya Jeshi lenyewe.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya Jeshi limeandaliwa kwa ulinzi, au kukabiliana na vita, na asilimia ndogo ni ile ya uzalishaji hivyo inasikitisha kuona bajeti ya Wizara ya Ulinzi katika baadhi ya maeneo kadhaa haitoshelezi hata kidogo; kwa dhana ya kulinganisha na Wizara nyingine juu ya uzalishaji, hili si sahihi, ikumbukwe kuwa hakuna maendeleo kama hakuna amani inayoletwa na Ulinzi ulio imara.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali inunue vifaa vipya na vya kisasa vinavyoendana na hali halisi ya maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, ili askari wetu wapate mafunzo ya nadharia na vitendo ili kupata ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamandi ya *Navy* Kigamboni. Ni faraja kubwa kupatikana kwa boti ziendazo kwa kasi kwa ajili ya ulinzi wa baharini katika azma ya kufanya doria, lakini uzoefu unaonyesha boti zilizoko hivi sasa hazifanyi mazoezi ya kiulinzi ipasavyo kwa sababu ya kukosa mafuta hali ambayo si tu inakwamisha utendaji bali inapelekea kutofika lengo.

Mheshimiwa Spika, mbali ya jitihada za Serikali kuunda boti mpya katika chelezo ya Navy Kigamboni, lakini boti zetu tulizonazo ni chakavu na ni za zamani sana na ni ndogo na haziwezi kufika bahari kuu kwa ulinzi huku tukijua meli za kigeni zinaendelea kuvuna rasilimali zetu siku hadi siku bila hofu nasi tukijiuliza maswali kadhaa yasiyopata majibu.

Mheshimiwa Spika, uimara wa boti au meli ni pamoja na kufanyiwa mazoezi ya matembezi baharini, lakini inasikitisha baadhi ya meli na boti, katika Kamanda ya Navy Kigamboni hazitembei kwa muda mrefu kwa ukosefu wa mafuta hali ambayo inapelekea baadhi ya boti kutoboka kwa kubakia eneo moja tu bila kutembea hivi tukijiuliza hasara ya mafuta na hasara ya kutoboka meli na isishindwe kutembea, ni ipi itagharimu Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuipatia Kamandi ya Navy Kigamboni mafuta ya kutosha kwa kufanya doria ili kudhibiti meli zetu ili zisitoboke.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kukosekana kwa mafuta katika boti zetu situ inaadhiri utendaji wa kazi bali inawapelekea vijana wetu wapya walio katika ajira ya Kamandi wa Navy kuchelewa kupata ujuzi wa uhakika huku kukiwa na wimbi la kustaafu kwa wataalam asilimia kubwa bila ya kurithisha utaalam kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Automative Technology Centre (Tact)* Nyumbu. Kwa kuwa lengo la kuanzishwa kwa MEREMETA ilikuwa ni kuisaidia Nyumbu kujiendesha. Wakati sasa umefika Serikali kuchukua hatua za maksudi ya kuboresha miradi huu muhimu nchini kwetu ambao magari ya aina mbalimbali yanazalishwa na hata shughuli zingine za utafiti.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ikumbukwe baadhi ya zana za mradi wa Nyumbu zinahitaji ukarabati wa hali ya juu, kuepuka kutofanya kazi kabisa hali ambayo itapelekea Serikali kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuwa Shirika la Nyumbu ambalo linazalisha bidhaa za kijeshi na kufanya utafiti, katika mwaka huu wa fedha shirika halikutengenewa fedha, hivyo sijui uzalishaji utaenda vipi, na utafiti utafanyika namna gani katika hali ya kutokuwa na fedha, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali

kuangalia namna ya kutafuta fedha kwa njia yoyote kuinusuru Nyumbu isije ikafa kama yalivyokufa mashirika mengine.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Hospitali ya Nyumbu yenye uwezo wa kuchukua au kulaza wagonjwa 60, yamechakaa na pia majengo hayo hayana vifaa vinavyojenga sifa ya kuitwa Hospitali. Hali ambayo kama Serikali ingalikamilisha vifaa si tu ni faraja kwa Jeshi bali hata raia wanachi za Kibaha.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuikamilisha Hospitali hiyo kwa matengenezo na vifaa vya kisasa na kama shauri hilo litakubaliwa ni lini basi ukarabati na vifaa vitakamilishwa.Itakuwa jambo la faraja kama Serikali itaiwezesha Nyumbu kifedha ili iweze kuzalisha magari na vifaa vya aina mbalimbali kwa matumizi ndani ya na nje ya Tanzania. Uajiri katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Pamoja na utaratibu wa kuwapata vijana wa kujiunga na JWTZ kupitia JKT na JKU ni jambo zuri iwapo dhana nzima ya kuwapata vijana hao haitokani na ubaguzi wa itikadi za kisiasa katika maeneo wanayotoka.

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa nia ya kujenga na kwa vile watanzania wote ni sawa mbele ya sheria, lakini inasikitisha sana utaratibu wa uchujaji wa vijana wa kujiunga na JWTZ, kuanzia ngazi za wilaya hadi mkoa haziendani na dhamira ya Jeshi lenyewe linalohitaji vijana wenye sifa katika fani zinazohitajika bali zaidi nafasi zinakwenda ni mtoto wa nani, ni wa itikadi gani, jambo ambalo haliisaidii Serikali. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuangalia utaratibu mwingine wa kuwapata vijana wanaojiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi siku hadi siku katika taratibu za kuwapata vijana kutokana na baadhi ya viongozi hasa wa Mikoa kushindwa kutekeleza utaratibu wa uadilifu, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iandae utaratibu mpya utakaowezesha kutoa haki kwa vijana wenye uwezo na sifa za kujiunga na JWTZ, bila ubaguzi wa aina yoyote. Jeshi katika mfumo wa vyama vingi Ibara ya 147 limetolewa kujiingiza katika siasa, iweje leo viongozi wa mkoa nafasi hizo wazitoe kiitikadi.

Mheshimiwa Spika, Wastaafu na Stahili zao. Askari wa JWTZ wanapostaafu wanachukua muda mrefu kupata mafao yao ikiwemo kiinua mgongo. Hii imedhihirika Wizara ya Ulinzi na JKT bado haijaandaa utaratibu unaorahisisha kwa wastaafu hawa kujipatia haki au stahili zao kwa wakati muafaka, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuunda Kitengo maalum cha kuhakiki askari wanaotarajiwa kustaafu kabla ya miaka 3 ili kuweka mawasiliano ya kuhakikisha wakati ukifika anapata haki zao bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mwingine hata fedha zao wanazopaswa kupata kila miezi 6 baada ya kustaafu huwa hawapati, hali ambayo inasababisha wale wanaokaa mikoa ya mbali na HAZINA Dar es Salaam, inawawia vigumu kufuatilia kutokana na

hali ya maisha inavyokuwa mabaya kwa wastaafu, huku kukiwa na masuala kadhaa wanayojiuliza wastaafu, utumishi wao wa utiifu, nguvu zao zilizolinda Taifa, zimethaminiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiri bado haijachukua jitihada za maksudi za kuwaenzi wastaafu wa JWTZ na badala yake mara nyingi sifa za askari na umuhimu wake unaonekana pale anapofariki kwa kutangazwa sifa zake ambazo hazisaidii kitu wakati alipokuwa hai hakutunzwa kikamilifu.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwapatia wastaafu mafao yao kwa wakati na pensheni stahili. Pia Serikali iandae utaratibu wa kutoa mikopo midogo midogo na pia wapatiwe mikopo ya kujengea nyumba hasa ukitilia maanani hali za maisha za wastaafu walio wengi zinakuwa ni za kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, kuna manung'uniko juu ya wastaafu wa zamani kupata kiasi kidogo cha fedha ukilinganisha na wastaafu wa hivi karibuni, hali ambayo siyo tu katika ngazi ya ma-Jenerali wastaafu lakini hata maafisa wastaafu na askari wastaafu wa kawaida. Hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia utaratibu muafaka ambao utawapelekea wastaafu wote katika ngazi mbalimbali, kutopishana kwa mbali kwa viwango vya fedha zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa ambayo tunataka Serikali ituthibitishie, kwamba baadhi ya wanajeshi wastaafu wanaajiriwa nchi za jirani kama Uganda na *DRC* Kongo huku umri wao ukiwaruhusu kulitumikia Jeshi kiafya.

Hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali umri wa kustaafu kwa wanajeshi wa miaka 47 hadi 55 uangaliwe upya kulingana na afya za wajeshi wenyewe na mapendekezo ya mwajiriwa wa JWTZ hata hivyo kama hilo ni kweli wastaafu kuajiriwa nchi za jirani kwa kujitafutia maisha Serikali haioni kuwa haijawatendea haki inayostahili na haijawapangia mipango madhubuti ya mafao yanayokidhi maisha yao ya baadae, na je hii si fedheha na aibu kwa Taifa?

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuandaa mazingira ya wastaafu ili waondokane na aibu ya kwenda nchi za jirani kutafuta kazi.Kambi ya Upinzani inataka kujua ni askari wangapi waliostaafu walioajiriwa katika nchi za jirani katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi sasa; na Jee, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha wastaafu wake hawayumbi kimaisha?

Mheshimiwa Spika, kipindi tunachoendelea baadhi ya wanajeshi wengi watastaafu hivyo watastahili kupatiwa stahili zao bila usumbufu, huku baadhi yao wanastaafu wakiwa na ujuzi na utaalam wao wa fani mbalimbali, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwaajiri tena kwa mkataba wataalam hao baada ya kupata stahili zao zote, kwani imegundulika idadi ya wataalam wanaostaafu ni kubwa huku kukiwa na idadi ndogo ya kuziba pengo la wanaostaafu, hii ni kutoa fursa kwa kipindi hicho kuwatumia wataalam hao kuwapa elimu ya ziada vijana kabla ya kumaliza mkataba wao.

Siku ya Mashujaa. Tunaipongeza Serikali kwa kufanikisha vyema maadhimisho ya siku ya mashujaa, chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Mhe. Jakaya M. Kikwete ambaye ni Amir Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hii ni siku muhimu sana katika Taifa letu katika umuhimu wa pekee na kwamba huu ni mchango mkubwa wa mashujaa wetu katika kulinda nchi yetu, ambapo kitendo hiki ni miongoni mwa dalili za kuwaenzi. Baadhi ya mashujaa wetu walioshiriki vita vya Kagera mwaka 1978 wengine wameisha kufa na wengine wamekuwa walemavu, hivyo Kambi ya Upinzani inahoji, Je, Serikali inafuatiliaje maisha ya familia za marehemu mashujaa au familia za mashujaa walioko hai hadi leo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha baadhi ya mashujaa walioshiriki vita hivyo ambao bado wako hai na wengine wamepata ulemavu wakiwa vitani hawashirikishwi kwa namna yoyote juu ya siku ya mashujaa, kwa mfano, Askari mstaafu *TR4786 Copl.* Mohamed Haji Hamad maarufu mkobozi wa Vitongoji Pemba ambaye alipata ulemavu kwa kukatwa mguu akiwa vitani ameachwa katika mazingira magumu nay a kusikitisha akiwa hana hata baiskeli ya kutembelea.

Hii ni sambamba na Askari mstaafu *MT 30608 PTE* Samwel Raphael Obiero mlemavu wa vita vya Kagera ameachwa katika hali ngumu kimaisha, Kwa ujumla kuna mashujaa wengi ambao wametelekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mara baada ya vita Mwalimu Nyerere, baba wa taifa letu aliwathibitishia mashujaa hawa kwamba kamwe hawataachwa na kutelekezwa kwa aina yeyote ile na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, maneno haya bado mashujaa walio hai wanayakumbuka na kauli hiyo ya Mwalimu ilisisitizwa na Mhe. waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Naibu wake wakati huo. Mashujaa wanajiuliza kama kweli tunayotamka ya kumuenzi Baba wa Taifa ni kwa maneno au kwa vitendo?

Mheshimiwa Spika, Baadhi ya mashujaa ambao ni walemavu wamekuwa na huzuni kubwa kwa kutoshirikishwa kwa namna yoyote ile siku ya mashujaa, huku wakijiuliza mbona mashujaa walemavu hawapewi taarifa yoyote, lakini mashujaa wengine wasio na ulemavu wanashirikishwa, walemavu hao wanauliza je kuna nini hapa,kupata ulemavu katika kuitetea nchi hii ni adhabu?(*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuandaa mazingira na utaratibu mzuri katika suala hili ili kuondoa dhana ya kubaguana inayojengeka miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, Hati Miliki Maeneo ya JWTZ na JKT. Wizara ya Ulinzi na JKT inaendelea na utaratibu wa Upimaji wa maeneo ya Jeshi na JKT na hatimaye kuyaptia hatimiliki sambamba na taratibu za kulipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za Jeshi la Ulinzi na JKT.

Kambi ya Upinzani inataka kujua hatua iliyofikiwa na baadhi tu ya maeneo ya Jeshi la JKT na utoaji wa hatimiliki na hata fidia, katika maeneo yafuatayo:-

| | | |
|---|---|---|
| KUNDUCHI TRANSIT CAMP | - | Dar es Salaam |
| UBUNGO KIBANGU (691 det) | - | Dar es Salaam |
| MAKUTUPORA JKT | - | Dodoma |
| BIHARAMULO (23 KJ | - | Kagera |
| RWANKOMA JKT | - | Mara |
| MLALE JKT | - | Ruvuma |
| TUNDURU | - | *TPDF* |
| MARAMBA-JKT | - | TANGA |

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo yaliyokwishafanyiwa uthamini na kusubiri fedha tangu 2006, hivyo Kambi ya Upinzani inataka kujua ni maeneo gani yameshatolewa fidia kwa wananchi na kama hakuna fidia hadi sasa ni sababu zipi zilizokwamisha. Mfano: *Duluti Estate* – Tengeru JWTZ (*CSC*), Singino – Kilwa JWTZ, Mapinga – Bagamoyo JWTZ. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni maeneo gani yanayomilikiwa na JWTZ na JKT bado hayajapimwa hadi sasa na kupatiwa hatimiliki na maeneo gani bado yana mgogoro na wananchi na hatua gani zilizochukuliwa na Wizara kutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, Chakula cha Askari. Kiwango cha Shs.2,500/- kama posho ya chakula cha Askari ni kidogo mno na hakiendani kabisa na hali halisi ya kupanda kwa gharama za maisha, katika hali ya kawaida ya binadamu angalau apate milo mitatu. Shs.2,500/- ni ya Chai ya asubuhi tu kama kweli tunataka Askari wetu awe na afya nzuri inayotakiwa, hivyo kuna maswali kadhaa ya kujiuliza Jeshi lisilopata fedha za kutosha za chakula litakuwa na afya gani ya kupambana na adui, hivyo Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwapatia Askari wa JWTZ posho ya chakula angalau Shs.8000/- kwa siku, ili kuweza kumjenga mwanajeshi kiafya.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Kutokana na sera ya uanzishwaji wa Jeshi la kujenga Taifa. JKT inatakiwa kuzalisha kwa asilimia 75% na mafunzo ya kijeshi asilimia 25% hivyo ni vyema wakati sasa umefika wa kulifanya Jeshi la Kujenga Taifa likazalisha zaidi kuliko ilivyo sasa kwa kuwapatia wataalam wa kutosha na zana za kutosha yakiwemo matrekta ili kuweza kuendeleza kilimo cha kisasa chenye tija sambamba na kuipatia JKT masoko ya uhakika ya bidhaa zitakazozalishwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali SUMA JKT ambalo limeonyesha mabadiliko makubwa ya Uzalishaji hata kilimo, ujenzi, uvuvi n.k. ambapo wanaendeleza miradi midogo na mikubwa kwani bado wanaonekana SUMA JKT ni wakandarasi wahodari wenye uwezo na wa bei nafuu.

Hali ya majengo ya Bulombora JKT bado hayaridhishi, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuyafanyia ukarabati majengo hayo kwani ili na hao askari waone kweli Serikali na wananchi wake wanathamini kazi zao kwa maendeleo ya Taifa letu.Vijana wa JKT Chita katika tarehe 02 Julai, 2006, 7 Julai, 2006, 12 Julai, 2006, 15 Julai 2006, 28 Julai na 29 Julai, 2006, yalitokea matukio mengi ya kupigwa na kuporwa mali kwa wananchi wa Kijiji cha Chita; ambapo hasara ya mali ya jumla ya Sh.1,634,850, na fedha taslimu Sh.860,500/- zilichukuliwa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kujua ni hatua gani za kinidhamu zilizochukuliwa kwa vijana hao waliopelekea kulitia doa JKT.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Nawashukuruni waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud Salim, inaelekea kuna utafiti wa kila namna ambao umeufanya nah ii ndiyo kazi ya Upinzani kuweza kufanya utafiti. Sasa Waheshimiwa Wabunge ninao wachangaiji kumi na moja walioomba kuchangia katika Wizara hii. Waliochangia mara moja, wananafasi nzuri ya kupata nafasi ya kuchangia leo. Lakini hawa mara mbili na tatu tutaona.

Sasa naomba niwataje ni orodha fupi tu ili wajiandae. Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, wa pili Mheshimiwa Ali Said Salim. Watatu Mheshimiwa Esther Nyawazwa, wanne Mheshimiwa Issa Kassim Issa, watano Mheshimiwa Benito Malangalila, wa sita Mheshimiwa Kanali Sarehe Farrah, wasaba Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, hawa ndiyo waliochangia mara moja.

Wa mara mbili ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, aliyechangia mara tatu ni Mheshimiwa Felix Kijiko. Kutugemea kama Waheshimiwa hawatachukua dakika zote kumi na tano kuna uwezekano wote wa kupata nafasi.

Kwa hiyo, watatu wa mwanzo ni Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Ali Said Salim na Mheshimiwa Esther Nyawazwa kwa mpangilio huo sasa namwita Mheshimiwa Mohamed Missanga.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia kwenye hoja hii ya leo inayohusu Wizara yetu muhimu, nyeti, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania kwa kazi nzuri anayofanya ya kuhakikisha kwamba Jeshi letu na majeshi yetu yanatimiza wajibu wake pamoja na kuona kwamba wanafanikiwa kusaidiwa vitu ambavyo vinawahusu ili waweze kutimiza majukumu yao sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri - Mleta hoja, ndugu yangu, rafiki yangu, mtani wangu, jirani yangu, Mheshimiwa Kapuya kwa maandalizi mazuri ya hotuba yake hii. Lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri anayofanya, majibu yetu ya maswali anayotupa hapa, anatupatia majibu mazuri yenye kueleweka. Na vile vile nimpongeze Katibu Mkuu, Amiri Jeshi Mkuu kama ulivyomtambulisha, Makamanda wote na Wapiganaji wote kwa ujumla, naomba niwapongeze sana, hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kwanza, kulipongeza Jeshi kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayofanya kwa sababu nyingi tu. Mheshimiwa Spika, kwanza, wewe unafahamu historia ya Jeshi letu miaka ya 1970 wametusaidia sana kutuongoza katika vita dhidi ya Nduli amini na wakatuongoza vizuri sisi wananchi ikiwa ni pamoja na Mgambo na tukamchapa jamaa mpaka akakimbia akaenda zake. Hili ni jambo ambalo inawezekana vijana wa sasa hawalifahamu, ni vizuri tukalizungumza likakaa kwenye *record* ili kujua kwamba ni kazi nzuri ambayo imefanywa na Jeshi letu, kwa hiyo, wanastahili pongezi za kila aina.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Jeshi limeendelea kufanya kazi nzuri katika mipaka yetu, ndani na nje ya nchi kiasi kwamba hakuna yeyote ambaye mpaka sasa ametusumbua na hawajafanya hivyo, siyo kwa sababu labda wana nini... lakini wanajua kwamba vijana wetu kule mipakani wako timilifu na wako imara, wanaweza kabisa wakamshughulikia yeyote yule ambaye angetaka kuleta matatizo kwenye mipaka yetu. Hili nalo ni jambo ambalo tunastahili kuwapongeza sana wenzetu hawa na naomba sana waendele na kazi nzuri ambayo wanaifanya. Ninawapongeza sana juu ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile toka tumeanza chaguzi hizi za Vyama vingi vya kisiasa, wewe unafahamu vishindo vishindo vinavyotokea wakati wa chaguzi hizi, mwaka 1995, mwaka 2000, mwaka 2005, harakati za hapa na pale zimekuwepo. Pamoja na kwamba kazi nzuri imefanywa na Jeshi letu la Usalama wa Raia au Polisi, lakini nina hakika mchango wa Jeshi la wananchi katika kutuliza na kuiweka nchi salama ndani ya nchi na nje ya nchi, umesaidia sana katika kuiweka nchi yetu kuwa katika hali hii ya usalama na amani. Naomba niendelee kuwapongeza, nilipongeze Jeshi kwa kazi nzuri ambayo wamefanya ya kuhakikisha kwamba tumepita katika vipindi vyote vile. Mwaka 1993 tumepita salama, mwaka 2000 tumekwenda salama hata juzi mwaka 2005 tumekwenda salama na *Inshallah* jinsi tunavyoendelea kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na viongozi hawa na wanajeshi kwa ujumla, nchi yetu itaendelea kuwa salama na amani na itaendelea kuwa kioo cha Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoambiwa na kama tunavyofahamu, Jeshi letu sasa limekuwa mfano katika nchi za nje, tayari wapo vijana wetu kule Lebanon wanafanya kazi nzuri na si kazi ndogo hiyo kwa nchi maskini kama Tanzania, lakini vijana wake wakaonekana kwamba wanastahili na wanafaa kwenda kuwasaidia wenzetu kule nchi za nje kama Lebanon, nafahamu na Ivory Coast, Ethiopia na Eritrea, Sudan na kadhalika.

Vyote hivyo ni vielelezo vya kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu, inafanywa vizuri na viongozi wetu wa Jeshi, Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Jeshi na wengineo. Kwa

hiyo, kwa kweli sisi kama Bunge tunastahili kuwapongeza na kuwaombea heri kwamba waendelee kufanya kazi nzuri ambayo itaendelea kuipa sifa nchi yetu na kwamba itaendelea kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa na utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, hapa niseme jambo moja tu kwamba sera yetu ya Ulinzi na busara za viongozi wetu na hasa busara ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo alifanya kutumia hekima na busara kwa kuwachukua wanajeshi kufanya kazi za kiuongozi, za kiutawala. Wakati wa Chama kimoja kulikuwa na Ma-*Dc* Wanajeshi, Wakuu wa Mikoa n.k. Mwanzoni mimi sikuelewa hii ni kwa nini, lakini jinsi nilivyoendelea kupata maarifa na uzoefu, nikaona hekima ambayo mwalimu aliitumia katika kuwachukua wenzetu hawa kutoka *Ballacks* na kuwapa nafasi za uongozi mbali mbali kama ambavyo alikuwa amewapa.

Hali hiyo inaendelea mpaka sasa, ingawa sasa waliopo katika nafasi za uongozi kama za Uwaziri, u-*RC*, za Ubalozi ni wale wenzetu Makamanda waliostaafu. Lakini nasema hiyo sidhani kama ipo katika nchi zingine! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mtu anaweza akajiuliza hapa imekuwaje na imewezekana vipi! Lakini, nataka kusema hiyo ni moja ya kichocheo ambacho kimesaidia nchi yetu kuwa na utulivu na amani kwamba “wenzetu katika *Balacks* au katika Majeshi, hebu njooni na ninyi katika sehemu ya uongozi muone ugumu wa uongozi, urahisi wa uongozi. Sasa wakati mwingine mnaposema hivi na hiki, lakini na ninyi mnashiriki katika kuongoza nchi hii, wote tuchangie kwa pamoja”. Mimi nadhani hizo ndizo busara ambazo Mwalimu Nyerere alitumia na kuhakisha kwamba wenzetu hawa wanafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utulivu uliopo ni katika busara na hekima ambazo alitumia Mheshimiwa Mwalimu au Hayati Mwalimu katika taratibu hizo. Kwa mfano hivi sasa, tunao Mabalozi; yuko Balozi wetu kule Burundi, Francis Mndolwa, kama cheo chake nimekosea, anisamehe, anafanya kazi nzuri, yuko *General* Makame kule Malawi, anafanya kazi nzuri. Lakini, vile vile yuko Mkurugenzi wa Upelelezi wa zamani *(DCI)*, ndugu yetu Adad Rajab, yuko pale Zimbabwe. Hili lisionekane ni jambo la kawaida tu, kwamba unatoka huku, unaingia kwenye upande wa pili. Hizi ni busara na hekima ambazo zimefanywa na Waasisi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya nchi hapa, kule Kigoma yuko *RC*, Mheshimiwa Simba Kalia anachapa kazi nzuri pamoja na kwamba yeye ni Kamanda. Kule Kagera yuko Kanali Mfulu, anafanya kazi nzuri na yeye ni Mwanajeshi lakini anafanya kazi za uongozi. Kule Shinyanga yuko Mheshimiwa Balele anafanya kazi nzuri, ametoka *Ballacks* amekuja kule. Yuko ndugu yangu Tarimo, yuko Mtwara sasa. Ningeweza nikawaorodhesha wengi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba busara za viongozi wetu za kuwachukua wenzetu hawa na kutokuwaacha huko walikokuwa peke yake, wakaja huku

wakajumuika na viongozi wengine katika kuiongoza nchi yetu ndio zimechangia sana hali ya utulivu na amani iliyopo hapa nchini, ni busara ambazo zinatakiwa kuenziwa.

Kwa hiyo, niwapongeze Waasisi wetu kwa busara hii, lakini niwapongeze sana wote wanajeshi na viongozi wao kwa kuona kwamba na wao wanashiriki na kwa kweli ndio maana hali yetu ni nzuri kama unavyoiona.

Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na wenzetu hawa kama tunavyoiona hakuna matatizo, hakuna makelele. Matatizo yapo, wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wanajua namna ya kutatua matatizo yao. Kwa kweli ushauri wangu ni kwamba kama dhana iliyopo, tuwe na Jeshi dogo, lakini la kisasa. Maana yake ni kwamba Serikali yetu ijitahidi kuhakisha kwamba inawapa nyenzo za kisasa, inawapa vifaa vya kutosha ili waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la maslahi ni suala la msingi, mimi sitarajii Mwanajeshi au Makamanda hawa watoke tena wakafanye kazi ya kuhangaika, mara wafungue kibishara hiki, mara kibiashara hiki, wakipewa maslahi mazuri, watatulia Kambini, watafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Makaazi: Makaazi ya pamoja Makambini ni jambo moja ambalo ni vizuri likaweza likazingatiwa, likawasaidia. Suala la Pensheni ni suala muhimu hasa kwa wajane. Wajane wanahangaika sana katika pensheni za kawaida hata hizi pensheni za jeshini. Mimi naomba Serikali isaidie sana kuona kwamba suala la pensheni linaboreshwa katika majeshi na katika sehemu zingine, lakini hasa kwa wanajeshi na hasa kwa wajane wasihangaike baada ya kufiwa na waume zao, wakati waume zao wengine wanakufa wakitetea nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yakiboreshwa hayo, itakuwa jambo zuri. Ombi langu makambi ya Jeshi na Makambi ya JKT yako karibu Tanzania nzima hasa ya JKT. Singida hatuna! Hivi sisi tuna makosa gani kule Singida sisi? Ukienda wapi, Kambi ya JKT, sijui Oldonyo, wapi, sijui Usambaru, sijui nini, yaani kila utakapotaja utakuta makambi ya JKT. Mara nyingine unakuta Mkoa mmoja makambi mawili/matatu, Singida hatuna hata kambi moja ya JKT kwa nini? Hali ya hewa ni nzuri, mandhari ni nzuri, eneo kubwa, eneo la kilimo ni zuri, sisi ni wafugaji, wakitaka kufuga watafuga, wakitaka kulima wanalima.

Mheshimiwa Spika, naomba sana na sisi tufikiriwe kuwa na kambi ya JKT kama siyo kambi ya Jeshi. Vile vile vijana wetu inapotokea nafasi wa Singida wachukuliwe. Siku hizi umeanza utaratibu ikitokea nafasi ya JKT, basi watu wanapigiana simu, anapigiwa simu kutoka Kagera, kutoka Mtwara, "njoo nafasi zipo za Mkoa wa Singida". Sasa watoto wa pale pale Mkoa wa Singida hawapati, lakini wanapata watoto kutoka Mikoa mingine. Huo ndio utaratibu ulioko, watu wanapigiana simu! Naomba sana Wizara iliangalie hili, wafaidike watu wa Mkoa wa Singida kwa sababu kila Mkoa unapata *share* yake, sasa kwa nini wewe wa Mkoa mwingine uje uchukue *share* ya Mkoa mwingine. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho nilipongeze Jeshi kwa mambo ya michezo, wamefanya mambo mazuri sana. Wanajeshi wetu wametusaidia katika riadha, katika mambo mbali mbali na bahati nzuri wamempata rafiki yangu Waziri ambaye anapenda michezo ingawa bahati mbaya anaipenda sana Simba, maana hata vitabu vyake vyekundu, sasa angalia vitabu vyote; hiki cha kwanza chekundu, hiki cha pili ulichompongeza wewe chekundu, unataka kielelezo gani kama rafiki yangu anaipenda sana Simba zaidi kuliko timu nyingine! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Na wewe Mheshimiwa Missanga ungekuwa Waziri, nina hakika vitabu vingekuwa vya njano! *(Kicheko/Kicheko)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ndio hapo utakaponipigia ndogo ndogo, ningeupata, halafu utaona! *(Kicheko)*

Kwa hiyo, wamempata Waziri ambaye kwa kweli kimsingi anapenda michezo. Kazi nzuri ambayo inafanywa na Wanajeshi naomba aiendeleze. Mimi ushauri wangu ni mmoja tu: Ningeomba kuwe na *specialization*. Tusirundikane wote kwenye mpira wa miguu. Naomba kwa mfano, JKT ambao wanafanya vizuri kwenye mpira, wafanye mpira, Jeshi lenyewe *proper* waende kwenye *netball*, sijui Polisi waende kwenye *Basketball*. Magereza wanafanya vizuri katika *handball*, waende kwenye *handball* na riadha wengine. Ngumi, ndugu zangu wa Uhamiaji wale *at sometime* walikuwa wakifanya vizuri sana katika ngumi. Kuwe na *specialization*, kitu kama hicho kitatusaidia hata wakati wa kwenda kwenye Olimpiki tutakuwa na wachezaji wazuri na Jeshi ndio lina nafasi nzuri sana ya kutusaidia kuinua kiwango chetu cha mpira, siyo kila… Polisi mpira, JKT mpira, sijui nani, mpira, hapana! Naomba Mheshimiwa Kapuya kwa busara alizo nazo jinsi anavyopenda michezo, ni muombe sana aangalie uwezekano kwamba kama kuna kijana mzuri mzuri yuko Polisi, lakini tumekubaliana kwamba Jeshi ndio wafanye mambo ya *netball*, basi apelekwe *netball*. Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, asante na mimi kunipa nafasi niweze kuzungumza machache katika hoja ambayo Waziri Kapuya katuwasilishia hapa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa asuhuhi hii ya leo, sote tukaamka na afya, wengi walipenda waamke na afya, lakini wengi leo hawakuamka. Kwa hiyo, sote tumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka nichukue nafasi hii nimshukuru *Captain* mmoja wa Jeshi kule Kambi ya Alhamisi *Camp* ya Vitongoji anaitwa kama sijui ni *Major General* au ni *Captain*, vyovyote itakavyo kuwa ndio hivyo hivyo, anaitwa Lingoe. Nimshukuru kwa jinsi juhudi aliyoichukua katika kushirikiana na sisi kuweza kutatua lile tatizo ambalo lilijitokeza Piki katika uchaguzi uliopita. Naomba nimshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, salaam za rambi rambi nimetoa katika mchango wangu nilipokuwa nachangia Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa naomba nijielekeze moja kwa moja kwa hii ajenda ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kama muda utaniruhusu nina mambo manne. Nianze la kwanza; La kwanza, nataka nizungumzie maslahi ya wanajeshi. Kwanza, nichukue nafasi hii niwapongeze wananchi wote wanaokubali kujiunga katika kazi hii ya jeshi. Niseme hivyo kwa kuwa kwa kweli ni kazi ngumu, mpaka mtu akakubali kujiunga maana yake ni kuweka rehani maisha yake hasa panapotokea zahama. Ni nzuri kazi ya jeshi ikiwa ni salama, lakini pakitokea zahama, kwa kweli ni mtihani. Sasa kwa kweli tuwapongeze hawa ndugu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa inasikitisha sana, inasikitisha sana pale inapofikia kwamba wanajeshi wetu wamefanya kazi nzuri katika ulinzi wa nchi hii, lakini hatimaye *at the end of the day*, kwa kweli Jeshi linawatelekeza. Hii kwa kweli inasikitisha sana. Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu nakumbuka wakati nachangia mwaka jana nilileta hapa Bungeni suala la kijana mmoja mwanajeshi ambaye ametumikia katika Jeshi hili, lakini kwa bahati mbaya akapata ugonjwa wa ku-*paralyse*. Bada ya kupata ugonjwa, ikawa kwa kweli hawezi kutekeleza majukumu yake. La kusikitisha ni kwamba Jeshi lilimtelekeza.

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo Waziri wa Ulinzi alikuwa Mheshimiwa Prof. Sarungi, nilimpelekea suala hili na baada ya kumwendea, nashukuru sana kwamba alichukua juhudi angalau ya kuweza kumfuatilia yule kijana Pemba, akaenda akachukuliwa, akaletwa katika Hospitali ya Jeshi, akapata matibabu. Kwa kiasi fulani angalau unafuu umepatikana. Lakini, Mheshimiwa Waziri wakati huo akaniambia kwamba baada ya kazi hii tutahakikisha kwamba tunamstaafisha na kumpa mafao yake. Nikatakiwa nilete *document* zake zote, zote nikazileta, nikamkabidhi mama mmoja ambaye ndiye anayehusika na mambo ya Jeshi hapa anaitwa mama Veronica, nikampa *document* zote naye akaniambia “suala hili nitalishughulikia”. Baada ya muda akanijia na lugha nyingine mpya, akaniambia kwamba huyu bwana baada ya kufanya uchunguzi akaniambia kwamba kaishastaafishwa na kwamba fedha zake zote kaishalipwa. Mimi nikashangaa sana na nikastaajabu sana. Na kwa kuwa nilichukia kwamba huyu kijana wangu kwa nini aniambie suala la kuwa yeye bado hajastaafishwa na anadai haki zake wakati kaishastaafishwa! Nikarudi kumwendea. Nilipokwenda akaribie kulia!

Mheshimiwa Spika, huyu kijana ni mlemavu, basi pamoja na ulemavu wake akaniambia “mimi Mheshimiwa ni mlemavu wa viungo, si mlemavu wa akili, akili yangu ni timamu.

Ninachokuhakikishia ni kwamba mimi bado sijastaafishwa na sijapewa hata shilingi moja”. Sasa, nilishangaa sana kwamba mama Veronica kanipa taarifa kwamba huyu mtu kaishastaafishwa na fedha keshalipa. Lakini, yeye mwenyewe hata shilingi kumi hajaipata! Sasa, inawezekana huu mchezo uko katika Jeshi na kama upo kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana katika Serikali hii ambayo tunapiga kelele suala la Utawala Bora, lakini inafika hatua mnachukua mtu mlemavu, mnamstaafisha kimya kimya, halafu fedha yake inaliwa. Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama ni kweli, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri suala hili afuatilie kwa kina, halafu naomba nipate majibu ya kina. Lakini kwa kweli yeye mwenyewe bado ananiambia sijastaafishwa na wala sijapewa hata shilingi na taarifa hizi anayezijua kwa kina ndani nje ni mama anayeitwa Veronica anayeshughuliia mambo ya Jeshi hapa Bungeni. Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri haya masuala aweze kuyafuatilia, halafu niweze kupata jibu.

Lakini pia napeleka ombi maalum kwamba atakapokuja Pemba Mheshimiwa Waziri, namuomba sana angalau amfariji angalau kwa kumuona huyo mgonjwa ambaye anaitwa Said Abdallah Bakari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba niingie kwenye suala la pili, suala la JKT. Mheshimiwa Spika, niliuliza swali hapa katika Mkutano huu huu kutaka ufafanuzi suala la JKT na JKU na nikasema kwamba kuna ulazima gani wa kuweko JKU na JKT kwa pamoja katika nchi? Mheshimiwa Naibu Waziri akajibu kwamba JKT si Jeshi la Muungano, ni Jeshi la Tanzania Bara, JKU ni Jeshi la Unguja, ni tofauti kabisa. Sasa mimi hapa nimechanganyikiwa, naomba ufafanuzi mzuri, Mheshimiwa Waziri. JKT, Jeshi la Kujenga Taifa, tunaambiwa ni Jeshi la Tanzania Bara. Hii tafsiri ya JKT – Jeshi la Kujenga Taifa, taifa, Tanzania Bara ni Taifa? JKT, hivi Tanzania Bara ni Taifa?

Sasa ikiwa Tanzania Bara ni Taifa, Tanzania tutasema ni nini? Halafu isitoshe hii inaitwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hiyo inaonekana hii Wizara nusu ni Muungano, nusu si ya Muungano! Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mnatuambiaje kwamba JKT sasa si Jeshi la Tanzania? Kwa hiyo kama hivyo ndivyo, mmeishakubali kwamba JKT ni Jeshi la Bara, basi naomba sasa Wizara iitwe Wizara ya Ulinzi mbali na halafu muunde Wizara nyingine iitwe Wizara ya JKT.

Kama si hivyo, basi bado ukweli unabaki pale pale kwamba bado mimi naona JKT ni Jeshi la Muungano na kama si Jeshi la Muungano, basi lifanywe la Muungano kwa kuzingatia hizo hoja ambazo mmezitoa. Au mtwambie kwamba leo Tanzania Bara sasa ni Taifa. Sasa ikiwa Tanzania Bara ni Taifa, sijui na Zanzibar tutaitaje na Tanzania tutaitaje! Naomba ufafanuzi wa kina katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni sheria ya Jeshi. Mheshimiwa Spika, kuna sheria ya Jeshi inasema kwamba Mwanajeshi kama ni mwanamke ama ni mwanamme anapojiunga katika Jeshi ni lazima akae kipindi cha miaka mitano bila ya kuoa au kuolewa. Ah! Hii sheria kwa kweli ni ngumu! Mheshimiwa Spika, tunapiga kelele suala la kupambana na magonjwa ya UKIMWI. Sasa Jeshi mtapambanaje katika suala hili huku mnawakandamiza watu wakae miaka mitano bila kuoa wala kuolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sisi tuna miezi miwili tu hapa Dodoma na kwa kweli ni mtihani mzito kuweza kukaa bila kunanihii na nanihii! Leo inakuwaje mtu umweke

miaka mitano? Hapa miezi miwili kwa kweli inatakiwa uadilifu mkubwa, upate mtu mcha Mungu na mtu aliye karibu na Mungu kama mimi ndio atapona kabisa kabisa. Lakini wengi tunafeli mtihani huu, ni wachache ambao tunapasi.

Kwa hiyo, kwa kweli mimi nadhani bado Jeshi hebu angalieni zaidi tena suala la kuwaambia watu wakae miaka mitano bila kuoa bila kuolewa. Hili mimi nadhani itakuwa badala ya kupunguza UKIMWI mnaongeza UKIMWI. Kwa hiyo ni vizuri mkaangalia basi mkasema angalau mwaka mmoja utatosha kuweza kukaa angalau na kujizuia zuia kidogo, vinginevyo kwa kweli itakuwa ni mtihani mzito. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ni suala la malazi na chakula kwa wanajeshi wetu. Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba kwa kweli hii kazi ni kazi ngumu na kwa kuwa ni kazi ngumu, ni vizuri vijana wetu wa Jeshi tukawajengea mazingira mazuri. Lakini kama yalivyosema maoni yetu ya Upinzani kwamba mtu analipwa shilingi 2500/= iwe ni chakula cha siku nzima, sasa mwanajeshi gani huyo! Labda awe ni mwanajeshi wa kimalaika.

Lakini kwa maisha ya leo, shilingi 2500/= haziwezi kumsaidia mwanajeshi kabisa kabisa! Tusidanganyane! Kama tunataka kijana wetu awe mkakamavu, awe madhubuti, aweze kukabiliana na shughuli yote ambayo itatokea, basi lazima tuhakikishe kwamba tunamlipa ili aweze kula chakula vizuri na pia aweze kulala mahala pazuri. Sasa tulipendekleza kwamba angalau zifikishe shilingi 8,000/=, basi angalau shilingi 8,000/= tunaweza kusema mtu anaweza kula asubuhi, akala mchana na akala na usiku. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani bado Jeshi mmeomba hela si kidogo hii bilioni mia tatu na… jaribuni kupunguza shughuli nyingine, sasa hivi kwa sababu hatuna vita, tuko salama, fedha ambayo pengine mnaipeleka kwenye mambo ya kununua silaha, hebu zitengeni muweze kuwapa wanajeshi waweze kupata chakula na malazi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipata nafasi ya kuonana na shemeji yangu katika Kambi ya Sangasanga Morogoro. Kwa kweli ile hali niliyoiona pale ya makazi, hairidhishi. Makaazi yao hata vyoo vyao, mimi mwenyewe nilishindwa.

Mimi naomba Wizara hii ijitahidi sana kuhakikisha kwamba inajenga mazingita mazuri kwa wanajeshi wetu katika suala la chakula na malazi ili waweze kufanya shughuli zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nichukue tena nafasi hii kuwashukuru Vijana wote ambao wanakubali kujiunga katika Jeshi kwa nia ya kulinda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, asante sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Ali Said Salim na naomba pia nikupongeze kwa kuwa mwadilifu sana katika miezi yote hii miwili. *(Kicheko)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii kuungana na wezangu waliotangulia kuchangia Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza, kwa kumpongeza Amiri Jeshi wetu Mkuu, Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa msimamizi Mkuu wa Jeshi hili na hatimaye Tanzania tumekuwa mfano wa nchi nyingi zionazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Jeshi la Ulinzi na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri wanazomsaidia Mheshimiwa Waziri kusimamia majeshi yote mawili na Tanzania tumekuwa mfano mzuri. Hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuwaombea wote kwa Mwenyezi Mungu awalinde, awape ushupavu, awape moyo wa kuhakikisha kwamba Tanzania bado tutaendelea na amani na utulivu kama tulivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende moja kwa moja katika kuchangia katika sheria iliyo katika waajiriwa ndani ya Jeshi letu letu la Ulinzi. Mheshimiwa Spika, kuna sheria ambayo tuseme ukifikia kiwango fulani cha cheo chako ulichopewa kama hujaongezea, inabidi ustaafu. Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala hili.

Kama ni sheria hiyo, imepitwa na wakati, imeanza kufikia vijana wengi wanafikia umri huo wa kustaafu bado ni vijana na sheria inamwambia astaafu, anarudi kijijini kwetu, anaingia na kwa sababu alishafundishwa mbinu zote za kijeshi, unategemea kule kwetu atafanya nini! Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, tunaomba basi, kama hao vijana wanaostahili, kwa nini basi kama ni vyeo tusiwaendeleze huko Jeshini? Kama ni marupurupu, kwa nini tusihakikishe tunapowapa hivyo vyeo, tuongeze marupurupu yao ili yaweze kuwasaidia huko huko jeshini kuliko umri wao mdogo ambao una walazimisha kurudi huu mitaani, kwanza, kutakuwa na madhara makubwa sana, tutakuwa na jeshi la vijana ambalo litajiunda kisirisiri, litatusumbua sana. Naomba nilifikishe hili kwa Mheshimiwa Waziri aliangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi kuzungumzia Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu baada ya kuamua sasa tena turudishe mafunzo ya vijana wetu kwenye Kambi za JKT.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wamepewa muda wa miaka miwili, vijana hawa wanafundishwa mbinu zote za ulinzi, vijana hawa wote wanafundishwa mbinu za kutumia silaha. Inapofikia miaka miwili, wanalazimika kurudishwa majumbani. Tunategemea nini! Kama tumeamua kuwachukua vijana hawa, kwa nini basi na kwenye JKT ni mahali ambapo wanajifunza kujenga Taifa.

Kuna kilimo, ufundi, ulinzi wenyewe. Kwa nini sasa Jeshi hili lisiwapike hawa vijana baada ya kuwafundisha Ulinzi ikawaweka basi hata kwenye maeneo ikawawezesha hawa vijana maeneo ya mashamba huko huko JKT wajisaidie wenyewe kwa kujitegemea kuliko kuwa tunawarudisha tena huko huko uraiani? Hapo hapo bado nilikuwa nasisitiza Mheshimiwa Waziri aliangalie upya ombi langu. Waziri atusaidie kwa nini sasa wasiwawezeshe hawa vijana?

Hivi sasa kumekuwa na *security guard* nyingi sana za ulinzi kwenye maeneo yetu. Tuna vijana wetu ambao tunawafundisha JKT, kwa nini Serikali isiliangalie hili kwa sababu vijana tunawapika sisi wenyewe? Hao *security guards* wanapewa silaha unakuta hata mafunzo hawajapata. Lakini vijana wetu hawa wameonyesha mafunzo yote huko kambini kwetu tumewafundisha miaka miwili. Kwa nini sasa tusichukue jukumu hili JKT tuwaandae vijana kuwaanzishia hizi *security guard* ziende zikawasaidia hawa raia wakipata ajira? Hivi tunaizungumzia ajira, ni ajira ya namna gani tukiwaacha vijana wetu wanarudi wanahangaika huko mitaani! Hilo lilikuwa la pili.

Mheshimiwa Spika, naomba niende katika suala la usafiri. Naomba niipongeze Serikali yetu kwa kuwajali wanajeshi wetu wa Ulinzi pamoja na JKT kuhakikishia kwamba wanawawekea makazi. Makazi hayatoshi na mimi nakubaliana bajeti ni ndogo lakini cha kufurahisha kabla ya kusikitika ni kuwashukuru. Askari hawa wamejiwekea akiba kidogo kidogo kwa kupewa hata mikopo, wakajenga makazi yao wenyewe nje ya jeshi. Nawapongeza sana waliokuwa na mawazo kama haya. (*Makofi*)

Lakini sasa imefikia mahali kwamba wanapotoka sasa makazini kwao kwenda kwenye kambi inasikitisha asubuhi saa kumi na mbili ukienda kituo cha mabasi hapa Dodoma kwa mfano wale wanajeshi wanaokwenda Ihumwa, unakuta wanaomba *lift* ya mabasi. Inadhalilisha, mwenye gari akikubali atamchukua, asipokubali atamwambia subri kwanza nijaze basi langu ndiyo awaingize mle ndani, inasikitisha. Kwa nini wanajeshi letu tusiwaweke katika mazingira mazuri. Kama hatuwezi kuwakopesha pikipiki, kwa nini basi tusiandae utaratibu wa mabasi yale makubwa yakawa yanawasomba yanawapeleka kazini? Hilo Mheshimiwa Waziri alione ili awasaidie wananchi wetu, wanafanyakazi ambayo ni ya moyo, ni ya kujitolea, wameamua kujenga makazi yao. Sasa kwa nini tusiwatafutie hata usafiri? Mheshimiwa Spika, nimelisema kwa uchungu kwa sababu ukiwakuta askari wetu ambao ni wa kuwalindi nyinyi wananchi, wanabembeleza *lift*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sasa suala la Ukimwi. Limeongelewa na Mheshimiwa aliyekaa sasa hivi. Naomba na mimi niungane na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kusisitiza kwamba ile sheria ya miaka mitano kijana anapoajiriwa Jeshini, ni muda mrefu sana hatutaupunguza Ukimwi. Unamwambia kwamba anapoingia Jeshini masharti kwamba akae miaka mitano ndipo aoe, na huyu ni kijana kabisa, bado damu inachemka.

Mheshimiwa Mbunge mwenzangu amesema kuna nini? Ni kweli, ni kitu muhimu katika mwili wa kijana. Sasa itasikitisha kwetu jeshini tunapambana na Ukimwi kijana huyu unampa miaka mitano afanyaje sasa? Na hili ni jambo la muhimu. Naomba

Mheshimiwa Waziri alegeze suala hili ili ahakikishe kwamba ampe haki huyu kijana ili aweze kufanya kazi zake vizuri na afurahie maisha yake aliyoumbwa hapa duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee lingine la vyeo ndani ya jeshi. Leo nasikitika sana umetambulisha wakuu wetu wa majeshi, viongozi wetu wa majeshi. Kwenye hotuba ya Waziri ameeleza kwamba ataangalia suala la jinsia. Inasikitisha nikiangalia maafisa wa jeshi waliokaa pale, mwanamke ni mmoja tu! Hii ndiyo jinsia? Naomba tunapozungumza suala la jinsia ndani ya midomo yetu tujaribu kuangalia uwiano; ina maana wanawake kule jeshini hawapo? Ina maana hawajui kushika bunduki au hawawezi kwenda kwenye vyuo vyao hivi? Hivi hii *fifty fifty* ni ndani hata ya jeshi?

Naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie mwishoni anapoeleza majumuisho yote alivyozingatia suala la jinsia ndani ya jeshi. Je, wanawake wako wapi? Naomba alipe umuhimu sana kwa sababu sisi tuliomo ndani ya Bunge ndiyo kazi yetu kwamba tunaomba kuwe na wanawake huko jeshini. Pale yupo mwanamke mmoja, je, huyo atapingana nini na wanaume alipokaa? Atatoa hoja gani? Kweli atasikilizwa?

**MBUNGE FULANI:** Hawezi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Naomba hili lizingatiwe hata wanapokuja kwenye bajeti wanawake tuwaone nao kama ni watano, sita, kumi, tu-*balance fifty fifty* mpaka kwenye jeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Wizara hii wanatufanyia kazi nzuri sana, naomba sana fedha walizoomba waongezewe kwa kuwa ni kidogo. Inatakiwa wapiganaji wetu hawa tuwaweke katika hali ya kuwashika kama *glass*. Hawa wamejitolea maisha yao, askari anakwenda vitani vita vinapotokea na kuwaacha mke na watoto wake aliowazaa mwenyewe. Naomba tujali maslahi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba bajeti ni ndogo tuhakikishe basi askari hawa wa vyeo vya chini maslahi yao yanaboreshwa. Maana wakati inapotokea vita hawa ndiyo wanapelekwa mstari wa mbele, ukweli mwenye nyota yeye anaamrisha tu. Lakini hawa vijana wa chini ndiyo wanapelekwa mbele kwanza. Tuhakikishe basi na marupurupu yao yanakuwa ya kuridhisha, kwa hiki kidogo tunachopewa tuhakikishe kuwa kinawafikia hawa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naomba niendelee kuipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri wanayotufanyia Tanzania. Niwahakikishie makamanda kuwa mmepata Waziri mzuri anayeweza kuwasimamia masuala yenu. Anaweza kuwasemea ndani ya Bunge mpaka kwenye Baraza la Mawaziri, naomba mumsaidie sana na yeye yuko tayari kuwatumikia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Jambo la kwanza, nakushuru

wewe mwenyewe pamoja na wapiga kura wangu wa jimbo la Mpendae. Namshukuru kaka yangu Yahya Kassim Issa kwa kuniongoza vizuri toka kuingia katika Bunge hili Tukufu. Namshukuru na aendelee kuniongoza kama kawaida.

Vile vile nawashukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi pamoja na Makamanda wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wapiganaji wenzangu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa kazi yao nzuri. Pongezi zaidi ziende kwa kamanda wa Brigedia ya Nyuki Zanzibar, kwa ushirikiano mzuri anaonionyesha kwenye Jimbo la Mpendae kwa sababu makao makuu haya yako katika jimbo la Mpendae. Aendelee kuniongoza na kushirikiana nami na wapiganaji. Wapiganaji wa nyuki brigedia ni vijana wa mfano linapotokea lolote kwenye jimbo langu wanashiriki kikamilifu, nawapa hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii nyeti sana. Wizara yoyote inayohusika na ulinzi wa taifa ni Wizara ya kuheshimika sana na vijana wetu wana haki na kila sifa ya kuweza kuwapa lakini la kusitikitisha ni ufunyu wa bajeti wanayopewa haitoshi. Kwa sababu mpishi ndio anayejua moto siyo mmenya vitunguu na ngome ndiyo wanaojua gharama na thamani ya matumizi ya jeshi wakishirikiana na Wizara ya Ulinzi. Kwa hali hii wanaopewa makisio ya bajeti, kila siku tutalaumiana Wizara pamoja na ngome fedha wanazopewa hazitoshi, ndiyo wanaojua matumizi na gharama. Tunawasifu, wanafanya kazi nzuri. Lakini tuwasifu na mafanikio ya mafao ya baadaye na hapa wanapofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kusitikisha tutalaumiana kila siku kwa madeni waliokuwa nayo wanajeshi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa sababu Wizara ya Ulinzi ina mihimili miwili, Wizara yenyewe na Ngome. Ngome wanatengeneza bajeti yao na Wizara wanatengeneza bajeti yao. Watakapoileta kwa wahusika hawapati wanavyotaka. Wakati huo huo hizi hizi tunazozipitisha Bungeni Wizara husika hawawapi. Tunawapeleka wapi wanajeshi hawa? Au Wizara hii tunampeleka wapi Waziri na Naibu Waziri na Katibu Mkuu? Lazima tuwafikirie sana kuhusu suala la bajeti. Si vema kuzungumza mambo ya ndani ya jeshi kwa sababu ni sehemu nyeti katika taifa letu. Tunasema tunakuwa katika amani na utulivu, wao vijana ndiyo wanaopata tabu, kazi hii ni nzito!

Mimi nimefanya kazi na kama umelelewa kwa vigari huiwezi. Lazima uinukie mgongo wa mama au kiambaza ndiyo uiweze kazi ya jeshi. Lakini kwa mtoto hivi hivi tu huiwezi kazi hii, tusidanganyane! Lazima tuwahurumie vijana wetu. Kila siku ni aibu kusikia kwamba jeshi linadaiwa. Mwanajeshi lazima ale, lazima atumie, hata ikibidi awe na madeni. Tuwahurumie Wizara ya Ulinzi kwa majukumu waliyonayo. Hatuwezi kuwa na kilimo safi kama hatuna usalama wa nchi hii. Hatuwezi kuwa na wanafunzi bora kama hatuna ulinzi mzuri. (*Makofi*)

Leo mimi naondoka hapo katika suala hilo, hiyo itakuwa salamu imefika lakini tunalolizungumza zaidi ni suala la kuwaboresha askari. Watu wengi wamesimama hapa wanasema kwamba huduma ya askari kweli ni ndogo na nazungumza kwa ushahidi kamili. Shilingi 2,500 kwa askari haimfanyii kitu kwa *ration allowance*. Enzi zangu

nilipokuwa askari nilikuwa *store men* wakati huo jeshi lilikuwa linatumia kuliko sasa baada ya kuja utaratibu wa *coupon*.

Askari anatakiwa ale nyama gramu 240. Kilo moja askari wanne, mchele gramu 270, kilo moja ya mchele shilingi 1000, sembe gramu 240, sembe shilingi 350, samaki anatakiwa ale gramu 180, kilo moja shilingi 4000; je, shilingi 2500 zinamtosheleza nini askari yule? Kwa *ration allowance* anatakiwa apatiwe na wakati huo huo kuna mzabuni anayetoa huduma ile, umlipe shilingi 2500. Wakati wa nyuma jeshi lilikuwa linanunua kuni (*firewood*), masufuria, wapishi wenyewe wanajeshi, linajihudumia lenyewe.

Sasa hivi anatafutwa mzabuni alihudumie jeshi. Atafute wafanyakazi, wapishi, mpaka waosha sahani! Shilingi 2500 zitatosha wapi? Ipo haja maalumu lazima Serikali iionee huruma Wizara ya Ulinzi kuwapatia mafao au *ration allowance* ili mzabuni naye anufaike katika kutoa huduma. Ni huduma ngumu sana *ration* kutoa kuponi katika kantini za jeshi, siyo nyepesi, tofauti na tunavyoiona. Utakuja kusema kwamba askari wengi wanakula, itakuwa tumejumlisha kwa fuata *ratio* ya askari anayotakiwa ale. Tunataka askari wawe wazuri. Mheshimiwa Spika, nafikiri suala hili litaangaliwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, makazi ya askari hayatoshi, na haya yanatokana na bajeti finyu. Leo mimi nitaona aibu kwamba nyumba za askari wanazolala na familia zao yakija masika itabidi magodoro wayaondoe na yapo yanatokea na ushahidi kamili ninao. Anza Kambi ya Ubago *Merrad. Quarter* zilizopo huko ni aibu, zaidi nyumba ziko barabarani zimepasuka, ukiambiwa hii ni nyumba analala askari na familia yake huamini. Njoo kambini kwangu kabisa makao makuu ya brigedi, hali kadhalika familia za askari zinalalamika. Leo hapo tunawapa sifa nzuri kweli wafanyaji kazi wetu wazuri na ni kweli watiifu kutokana na misingi tuliyolelewa toka enzi yetu ya wazee wetu na Mwenyezi Mungu, awarehemu walioliunda jeshi na kuwa umadhubuti mpaka namna hii leo. Mungu awasaidie sana na awalaze mahali pema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuja sehemu ya mafao ya maaskari. Inasikitisha na inahuzunisha. Askari aliyeacha kazi mwaka 2002 na mwaka 2004, aliyeacha mwaka 2002 anapata mafao makubwa zaidi kuliko aliyeacha 2004. Nilileta suala hili hapa Bungeni na Naibu Waziri, akaniambia nimpelee, hivi kweli hakuna kumbukumbu za askari hawa mpaka nipeleke mimi Mbunge katika Wizara? Naomba hili suala Mheshimiwa Waziri mliangalie. (*Makofi*)

Suala jingine katika haya haya marupurupu, wastaafu wa jeshi wanapoacha kazi, Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara ya Fedha askari wanaoacha kazi wote wako kwenye mihimili yao. Leo kule Zanzibar kuna kijana mmoja ni *agent* wa Wizara ya Ulinzi au Wizara ya Fedha anaitwa Mahalua. Mwanajeshi anapoacha kazi anakwenda Wizara ya Fedha anaambiwa nenda kamuone Mahalua aje hapa keshapata orodha ya askari wetu waliostaafu *cheque* zao zitakuwa tayari.

Nawashukuru Wizara ya Ulinzi, wamemfukuza kijana huyu. Lakini donda ndugu lile lile liko vile vile Wizara ya Ulinzi kwa sababu hao watu wako kwenye miliki yao.

Wawashughulikie wapate haki zao Mahalua ni nani katika nchi hii? Vijana wanasikitika sana. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana suala hili mliendee mbio, hayo matatizo madogo madogo ya maudhi yasitokee na yasiendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeshapigiwa kengele ya kwanza, sasa hivi nitaongelea suala la askari wanaoacha kazi katika pensheni yao. Muda uliowekwa wa miezi sita jamani ni mingi, hali ya maisha ni ngumu, basi tuwaonee huruma wastaafu angalau miezi miwili miwili. Leo uje uniambie unaniwekea miezi sita tutagombana! Lakini kulingana na hali ilivyo walivyolelewa wanastahili, tuondoleni hili tatizo la miezi sita. Tatizo la miezi liondoke angalau miezi miwili ili wapate kujikidhi. Leo ni aibu utamwona Luteni Kanali ameacha kazi anatengeneza baiskeli. Mimi sipendezewi au namuona kepteni wangu mlangoni analinda. Si jambo la busara hata kidogo, mimi Koplo niliyeacha kazi ya jeshi siwezi kwenda kulinda; leo Kapteni utamkuta mlinzi, anakumulika wewe, amekwishaacha jeshi anakwenda kuwekwa mlangoni kulinda. Jamani hawa wafungue milango au awe *watchman* ni sahihi? Jamani tuangalie maslahi ya askari wetu waliostaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo ili nisije kupigiwa kengele ya pili, napendekeza kwa Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara husika inayowapa fedha kwamba wanaodai madeni ya jeshi ni wananchi wa Tanzania hivyo madai yao yashughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**SPIKA:** Ahsante sana ulitakiwa toka mwanzo kwa mujibu wa kanuni utueleze kwamba una maslahi na hoja ya Waziri huyu, kumbe wewe ni mwanajeshi, ahsante! (*Makofi*)

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja ya Wizara hii ya Ulinzi na JKT. Awali ya yote napenda nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Ndugu yetu Mheshimiwa Waziri Juma Kapuya, pamoja na viongozi wetu wa jeshi walioko katika ukumbi huu na popote pale walipo katika nchi yetu. Nawapongeza kwa sababu wanatuhakikishia usalama na ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imetuhakikishia kwamba mipaka ya nchi yetu yote kabisa ni shwari. Hili ni jambo zuri linalotufariji sisi Watanzania wote kwa ujumla wetu. Ni vizuri tukafurahia ushwari na usalama wa mipaka yetu, lakini nadhani inakuwa muhimu kuwafahamu sana majirani zetu, kufahamu nguvu zao za kijeshi walizonazo. Kwa sababu jirani yako ndiye mtu hatari ambaye unaweza kupigana naye vita wakati wowote. Kwa hivyo, ningependekeza kwamba kile kitengo kinachohusika ndani ya jeshi na usalama kingeimarishwa zaidi. Lakini pamoja na hayo ningependa niungane na wenzangu ambao wamezungumzia sana maslahi na mafao na mishahara ya hawa askari wadogo wadogo pamoja na posho zao.

Mheshimiwa Spika, kuwaangalia sana askari wa chini ni jambo la maana kwa sababu hawa ndiyo wapiganaji wa mstari wa mbele katika jeshi la nchi yoyote ile. Miaka

michache iliyopita nilitembelea majeshi yetu nikiwa katika Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, nilifika kule Kibondo, nilikuta askari wanalala katika mahandaki, kwa kweli walitoa malalamiko mengi. Sisi sote tuliokuwa wajumbe wa Kamati ile tuliwaonea huruma. Tulikuwa na Kamanda wa Kanda ya Magharibi, tukamuulizia kuhusu maisha ya hawa vinajana wanavyoishi.

Kwa namna alivyotueleza, kwa kweli hatukuridhika kwamba wao wanaacha watoto wao wanaenda kulinda mipaka ya nchi yetu huko pembeni kabisa, lakini ule mshahara askari akipata inabidi sehemu aache nyumbani na sehemu imsaidie yeye huko porini. Lakini tumesema tunataka jeshi dogo lenye uwezo. Basi ni vyema pia tukawa na jeshi dogo ambalo tutaliwezesha kwa maana ya kuwa *night allowances* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu gani kila kazi ndani ya Serikali ina taratibu zake, lakini Serikali hii hii mtu mwingine akienda nje ya kituo chake analipwa posho (*night allowance)*. Sasa mimi najiuliza, kwa nini wanajeshi hawalipwi wakitoka nje ya vituo vyao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi swali hili ni la msingi sana. Brigedia Kamanda alitujibu lakini kwa kweli sisi wajumbe wote wa Kamati hatukuridhika na nakumbuka Mwenyekiti wa Kamati ile alikuwa Mbunge wetu, Mheshimiwa John Samuel Malecela, alisema atakuja kumwona Waziri Mkuu. Mpaka naondoka Kamati ile, hatukupata jibu, lakini kwa sababu si mjumbe tena, nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri atakapotoa majuisho yake, atueleze juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, napenda kulipongeza jeshi letu kuhusu mazoezi ya kijeshi, hili ni jambo kubwa sana na ni nzuri. Unajua nchi inapofanya mazoezi ya kijeshi hata majirani wanauona uwezo wenu. Si lazima uingie katika vita lakini mazoezi yale tu yanavyofanyika yanatikisika majirani wanaotufikiria vibaya. Nimesoma hapa, mmefanya mazoezi ndani ya nchi kama manne nadhani. Na niliwahi kuhudhuria maonyesho ya kijeshi kule Msata, kwa kweli yalikuwa ni maonyesho ambayo kila mtu alijiridhisha kwamba Tanzania tunalo jeshi.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kuzungumzia juu ya askari wastaafu. Wengi wetu hapa wamezungumza kwamba kwa kweli inasikitisha unaona mtu alikuwa *Col*. wa jeshi, alikuwa ni mtu anaheshimika sana ndani ya jeshi, kila akipita anapigiwa saluti, leo amekuwa mlinzi, hiyo mifano iko wazi kabisa. Kule Mafinga kuna *Col*. Mmoja, ni mlizi, ni kiongozi wa walinzi. Kuna kiwanda cha *Sao Hill*, kuna Luteni mmoja yeye ndiye mlinzi kabisa, wala sio kiongozi, ni *watchman*!

Sasa vitu kama hivi vinaleta matokeo kwamba mtu akipata kazi Uganda kwenda kufundisha majeshi ya Uganda au nchi yoyote atakwenda. Sasa huu mojapowapo ya upungufu ambao nadhani ni vizuri kabisa Serikali yetu kwa ujumla wake ikaona namna gani itawatumia watu waliofikisha umri wa kustaafu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia umri wa kustaafu katika majeshi yetu yote ni mdogo sana, sijui naambiwa miaka 53 ambao takriban ndiyo umri wangu mimi. Hivi

jamani mimi sifai kuwa mwanajeshi katika umri huu? Tena Ofisa, Luteni, Kapteni au Meja. Kwa hiyo, naungana kabisa na Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia juu ya umri wa kustaafu wanajeshi wetu. *(Makofi)*

Wanajeshi wetu wanastaafu katika umri mdogo mno. Unajua mtu akistaafu jeshi akienda nchi ya jirani kwenda kutoa utaalamu wake huko na wewe ukaruhusu na umemgharamia, umemfundisha, ina maana kwamba elimu uliokuwa unampa, unampa adui yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu si lazima jirani yako awe rafiki yako wakati wote, nitoe mifano ya wazi kabisa. Tulikuwa na Dikteta Idd Amin wa Uganda, katika kipindi kile cha Serikali yetu ya Awamu ya Kwanza. Kuna kipindi aliwahi kuja kule Mwanza, tena bila kukaribishwa, kaja katua ule uwanja wa ndege wa Mwanza, alipokelewa na Waziri akaenda akakutana na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wakafanya mazungumzo. Kwa maana hiyo, ningependa kusema kwa ufupi sana kwamba si lazima jirani yako awe rafiki yako wakati wote. *(Makofi)*

Pia ningependa nizungumzie juu ya baadhi ya vikosi vya majeshi yetu. Kipo kile kikosi cha *Navy* Kigamboni, kimekwisha zungumzwa. Kile kikosi ni muhimu sana katika ulinzi wa Taifa letu, lakini boti zilizoko pale wengi ambao tunapitapita maeneo yale tunaziona. Kwa kweli zimechoka sana. Sasa kama tunaamini kwamba maji nayo ni sehemu ya ulinzi wetu basi tukiimarishe kikosi kile ili kifanane na kikosi cha miguu, kiwe na nguvu za kweli za kijeshi, siyo kusema tu kwamba tuna *Navy,* lakini *Navy* yenyewe haina nguvu yoyote ya kijeshi, haina vifaa vya kijeshi! Vilevile, katika kikosi kile; sijui ni mfumo wa kupanda vyeo; askari wa kikosi kile kupanda vyeo kwao inakuwa tabu sana. Basi hili kama ni suala la mfumo basi waupanue ili angalau vijana wanaofanya kazi katika kikosi kile waweze kupata vyeo kama vile askari wa miguu. Sina hakika na askari wa anga lakini nina hakika na askari wa miguu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie JKT. Mimi natoka Mufindi, kule tuna kambi ya JKT Mafinga, ni kambi kubwa, wana ardhi kubwa sana, na mara nyingi nimekuwa nikiomba Serikali ikiwezekana ikigeuze kile kiwe kikosi cha Jeshi la Wananchi. Hilo ni ombi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningependa kuongelea juu ya SUMA JKT, Shirika letu ambalo ni la ujenzi. Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba Shirika hili limesajiliwa katika Bodi ya Usajili wa Kandarasi kwamba ni Shirika ambalo liko daraja la kwanza. Daraja kubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi sioni kwa nini Serikali inaendelea kuhangaika kutafuta watu wa kujenga majengo yake. Tunalo tayari shirika letu. Mimi ningeishauri Serikali itoe amri kwa Taasisi zote za Serikali, Wizara au Idara zote kwamba pale ambapo kuna kambi ya JKT ambapo watu wa JKT wanaweza kufanya kazi, wanaweza kufika maeneo hayo, kazi hizi wapewe wao. Hapa mmesema zimepatikana shilingi bilioni 5 kwa mwaka, ni fedha kidogo sana. Mimi nimeshuhudia wale vijana wanavyochapa kazi.

Unajua wanajeshi ni tofauti na raia. Ni vijana hodari. Kwa hivi ningeshauri kwamba kazi nyingi wawe wanapewa vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda nilionao ni kidogo, ningependa pia kuzungumzia MZINGA. MZINGA ni taasisi ya Serikali. Nimewahi kupata bahati ya kutembelea taasisi ile, kwa kweli ni taasisi ambayo kimsingi ina uwezo mkubwa sana wa kutengeneza risasi na vitu kama hivyo. Lakini ninachoomba Wizara yenyewe iwe inanunua risasi zile. Wizara hii ndiyo inasimamia ile Taasisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Namwita Col. Saleh Ali Farrah na Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kaskazini, ameomba dakika 10 ambazo nadhani tutazipata akishamaliza Mheshimiwa Kanal Mstaafu Farrah.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimiwa Spika, na mimi sina budi kujiunga katika msafara huu pamoja na wenzangu katika kuchangia Wizara hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema, ijapokuwa kwa leo sikutulizana sana kwa sababu nina mgonjwa nyumbani, naye ni mke wangu amelazwa. Kwa hiyo, naomba radhi kama nitaonekana sijatulizana, ana *low pressure*.

**SPIKA:** Pole sana Mheshimiwa.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Lakini ilinibidi tu nikae *otherwise* ningekuwa nimeondoka; ilibidi nikae ili niweze na mimi kutoa mawazo yangu machache niliyokuwa nayo na nafikiri kwamba labda yanaweza yakasaidia.

Sina budi kumshukuru Rais wangu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, na vilevile, sina budi kuwashukuru wananchi wa jimbo langu ambao ndiyo walionipa uwezo wa kusimama hapa. Ninatoa pole kwa wote waliopata maafa katika kipindi ambacho sisi tuko hapa ndani ya Bunge na ninatoa pongezi kwa wote waliokuwa wamefanikiwa kupata vyeo mbalimbali wakati sisi tuko hapa. Vilevile naomba kwa haya machache kama nitakosea, ninaomba radhi mapema kwa sababu ulimi unaweza ukapokonyoka. Wizara tunayoizungumzia ni Wizara nyeti au ni Wizara ngumu sana kwa namna moja au nyingine, inatakiwa mimi hasa binafsi niwe makini kidogo.

Mheshimiwa Spika, mimi nina sehemu moja kubwa au mbili nilizokuwa nataka nizizungumzie mchana huu wa leo na kama nitapata nafasi basi nitaweza kuzungumzia sehemu nyingine ya tatu. Sehemu ya kwanza nilikuwa nimejipanga kulizungumzia jeshi lenyewe kama Sera ilivyokuwa inatamkwa toka enzi za Mwalimu na mpaka sasa. Tumesema au Sera ilikuwa inasema kwamba jeshi liwe dogo na liwe la wataalamu. Lakini ukitazama jeshi liwe dogo kiasi gani na wataalam wawe wangapi?

Ninavyofahamu jeshi la nchi yoyote huwa linakwenda na *percentage* ya *population* ya nchi na *population* hiyo inaweza ikawa *2%, 3% maximum to five percentage*. Sisi nchi yetu ni maskini, hatutaweza kuingia kufika katika 5%, itakuwa ni watu wengi sana hatutaweza kuwahudumia. Lakini pale tunaposema kwamba jeshi liwe dogo na liwe la

kitaalamu basi tugawanyike ndani ya jeshi hili. Mimi naona ndani ya jeshi letu tumejifinya. Wizara, Makao Makuu ya Jeshi kuna *Brigade* basi yameisha.

Nilichokuwa najaribu kuomba mimi ni kwamba sasa tuingie ndani ya *commands* hapo ndipo kutakuwa na siri kubwa ndani ya jeshi kutokueleweka japokuwa siyo dawa. Lakini tutakuwa na siri kubwa ya kusema kwamba jeshi letu ni dogo kiasi gani, na litakuwa na wataalamu kiasi gani. Mpaka sasa hivi hatumo ndani ya *commands*, hakuna *infantry commands*, hakuna *communication commands, commands* zote hakuna. Sasa hili jeshi letu tunavyolisema liwe dogo, dogo kiasi gani?

Wenzetu wakati wamekaa wanaimarisha majeshi yao, kuna *navy command*, kuna *air command*, kuna *infantry command*, kuna *communication command.* Sisi tunasema dogo. Kwa hiyo, la kwanza kabisa naomba jeshi lingejipanga sasa hivi ni *time* muafaka tuwe na *command* na kuwepo na *general chief of staff* awepo anashughulikia *commands* hizo mbalimbali. *(Makofi)*

Kwa namna hiyo nilikuwa nahisi kwamba tutalitania jeshi letu kwa kuchelewa kwetu kuundwa kuwa *commands, commands* zitakuwa na wataalamu, wataalamu watakuwa wamegawanyika na tutakuwa tunapiga hatua kidogo kidogo. Hili moja ambalo niliona nilizungumzie kwa kifupi sana. Wataalamu wapo wengi wananisikiliza, kwa hiyo, nina wasiwasi nisije nikateleza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilikuwa najaribu kulizungumzia, ingawa nilikuwa nafikiria sana nisiliingie mno ndani lakini nijaribu kulisema. Wakati tumekaa hapa sisi kama Wabunge na ni wanasiasa, tunajaribu kusema maneno mengi, tunajaribu sana kuingia ndani ya *policy* yenyewe kuliendesha Jeshi, nitatoa mfano mmoja.

Kwa mfano, Mbunge mwenzangu alisimama hapa akalalamika kuhusu mwanajeshi. Wanajeshi waruhusiwe mapema kuoa. Hii ni *policy* ya ndani ya jeshi, ni nidhamu ndani ya jeshi inayoweza kumfanya mwanajeshi aweze kufanya kazi sawasawa, na hii *policy* haiko mbali sana hata kwa Wamasai ipo, kuna Morani, haruhusiwi kuoa mpaka afikie *stage* fulani. Nafikiri hili tu lazima tuombewe semina itakayoelekeza *policy* ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, naomba utufanyie semina, uitishe semina moja ya wanajeshi, waje wazungumzie kidogo *policies* zao kwa nini mwanajeshi ndani ya Jeshi kwa kipindi cha miaka mitano hana ruhusa ya kuoa au kuolewa. Ukishaoa basi ujue umeshaingia katika matatizo mengi sana. Huyu hataweza kuwa bingwa wa fani mbalimbali na kuweza kuzi-*master* katika kichwa chake na kujiweka tayari kupigana. Sote tunajua kwamba wanajeshi wote wanatakiwa wawe shupavu na wapiganaji katika ngazi za chini. Sasa huyu kama hukumnoa akawa jeuri, akawa shupavu, yuko tayari kufanya kitu chochote unataka sasa hivi akakumbatiane na mama mara baada ya kumaliza tu *recruitment* itakuwaje? *(Makofi)*

Mimi ningeomba Wabunge wenzangu msiingie sana katika *policy* ya jeshi. Nakubali kwamba kweli tuna haki na wajibu wote wa kuwalinda wanajeshi wetu na

namna za kujikinga na Ukimwi lakini pia wanajeshi na makamanda wanajua sana. Kwa sababu wanakuwa na mazoezi mengi yanayoweza kufanyika ambayo yanambana huyu mwanajeshi asiweze kutoka nje au akaweza kuhimili hili la miaka mitano. Kwa vile mimi nimekwishastaafu, sina *interest* hapa kabisa.

Mheshimiwa Spika, hiyo kengele ya kwanza? Ya pili? Bado! Suala la pili, nataka kuzungumzia upande wa kustaafu. Kwa kweli nilishakwishawahi kuzungumzia sana kwamba wastaafu wa jeshi wana hali ngumu, wengine bado wanapata tabu kupata pesa zao. Kuna maudhi mengi madogo madogo ambayo yanawakabili. Mimi najaribu kushauri kwamba kwa idadi ya hao askari na maafisa waliomo ndani ya vikosi mbalimbali hawawezi kuwashughulikia wastaafu na matatizo yao. Vyema kuwe na utaratibu mzuri wa kuweza kuwafikiria hawa wastaafu ili waweze kupata mafao yao vizuri.

Lakini kuna kitu ambacho kinaniuma, nitakizungumzia kwa uangalifu sana. Ndani ya jeshi kuna ngazi mbalimbali kama sijakosea (*other ranks)* kuna ngazi tisa au kumi lakini katika *officers* kuna ngazi 10 au 11 ukichukua pamoja na *cadet*. Hao wamegawanyika, kuna *Officer Cadet, a Second Lieutnant, Lieutnant, Capt., Major*, kuna *Lieutnant Colonel* na *Colonel,* huu ni mkanda mmoja. Halafu kuna Brigedia mpaka *General.* Sasa mkanda huu wanaitwa *general staff*. Kuna *Brigedia General, Major General*, *Lieutnant General* na kuna *General.*

Katika kustaafu hapa utakuta ni vikundi vitatu tu ndio vina hali nzuri. Hawa ni maofisa wakubwa wanaotegemewa kesho kama nchi yetu itatokewa na vita. *Brigedia* katika kustaafu kwake kwa kweli kunasikitisha. Mimi naomba *Brigedia* aingie ndani ya mkumbo wa *general stall* ili katika kustaafu kwake awe anapata huduma na viwango vinavyolingana na maafisa wengine. Ninaamini kama juu patakuwa pazuri, basi na chini vilevile tutapaweka vizuri zaidi. Mabrigedia kwa kweli na wao ni majenerali vilevile. Jenerali wa nyota moja, mbili, tatu, nne. Afande Waitara, unamwachaje huyu jenerali wako wa nyota moja? Kwa nini yeye hapati maslahi kama mnavyopata nyinyi?

Nalizungumzia hili sina *interest* yoyote, mimi nimestaafu na *full colonel*, nashukuru Mungu kwamba nayajua mengi, najisomea na naendelea kusoma, nayajua mengi kidogo. Lakini hili nilikuwa nataka nilizungumzie kwa kweli ni baya mno. Tabaka za namna hii zikianza kuwepo, haipendezi, na kama ningepata nafasi ningesema na vijitabaka vingine vidogo vidogo ambavyo ndani ya jeshi vinatakiwa kwa kweli viondoke vinginevyo tutakuja kumtafuta mchawi na hatumjui yuko wapi. Wewe huwezi kumwacha leo brigedia analalamika ovyo na alikuwa anakufanyia kazi vizuri. Niachie hapo, nizungumzie kitu kingine zaidi. Sijui kama wakati utaniruhusu!

Tumepigana vita ndani ya nchi hii, tuna walemavu ndani ya nchi hii. Hawa walemavu wa vita wana hali mbaya sana, moja. Pili, tumepigana vita ndani ya nchi hii na kuna veterani ambao wamepigana vita. Je, hawa Serikali yetu inawafikiriaje? Licha ya kwamba wastaafu lakini wanawafikiriaje, nchi za wenzetu wanafanyaje? Watu waliopigana vita na kurudi salama hatuwezi kuwaita mashujaa ila wanakaribia ushujaa. Kwa sababu ndani ya jeshi shujaa ni yule aliyekufa, huwezi kuwa shujaa kama upo hai.

Ndani ya *policy* za jeshi huwezi kuwa shujaa kabla hujafa. Kwa hiyo, vilevile naomba hawa ambao wamepigana vita na sasa hivi wako hai, Serikali ijaribu kuwatazama vizuri. Sina *interest* yoyote hapo katika suala hili ijapokuwa nimestaafu lakini ninatazama ile hadhi kwa sababu tusidanganyane ndugu zangu, Wabunge wenzangu kwamba kama pakitokezea vita Bunge hili halikaliki.

La mwisho nauliza *Ministry of Defence* ina asilimia ngapi ya bajeti hii kama kweli tunasema kwamba tuna ulinzi? Tuna asilimia ngapi katika bajeti hii? Mimi naelewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina asilimia 18 je, jeshi ina asilimia ngapi? Na wanaweza wakajikidhi? Mazoezi yatafanyika, watalishana vizuri, watavaa vizuri, wataendesha *training* zao vizuri? Baadaye pakitokea matatizo mnataka kuja kumkamata *Chief of Staff* mumpeleke *Court Marshal*. Uwezo ni kitu kikubwa sana katika kuendesha taasisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kukushukuru sana kukubali kunipa dakika chache hizi ili niweze kuzungumza katika hoja hii. Kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Nampongeza mtoa hoja amewasilisha vizuri na kwa hiyo naenda moja kwa moja kueleza haya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Muleba Kaskazini kipo Kikosi cha Jeshi kinaitwa Kaboya 21KJ. Kila mwaka ninapopata nafasi ya kuchangia huwa nalisemea hili. Nisiwe mwizi wa fadhila, nishukuru kwa ajili ya *ambulance,* nashukuru kwa ajili ya gari kubwa lori ambalo sasa hivi linatoa huduma mbalimbali pale kambini. Lakini basi nielezee tatizo la kiafya linalokabili kambi hii ya Kaboya pamoja na vijiji vilivyozunguka. Hapa kuna huduma inayotolewa ya tiba lakini hawana jengo zuri la zahanati. Zahanati yao ambayo ilikuwa inajengwa baada ya vita ya Nduli Idd Amin, iliendelea kusimama mpaka leo haijaendelezwa. Nadhani inasemekana ilipigwa mabomu kwa hiyo haikuendelea tena. Huduma wanayotoa ni nzuri na gharama zake nafuu, kwa hali hiyo kama ingeliwezekana wakapata zahanati wangetoa huduma nzuri zaidi na wananchi wanapendelea sana kwenda kupata huduma hapa kuliko mahali pengine kwa sababu gharama yake ni nafuu.

Mheshimiwa Spika, makubwa ninayopenda kuyazungumza hapa ni mambo mawili. Kwanza, ninasemea mipaka ya kikosi cha 21KJ. Mipaka hii awali ilikuwa kwa upande unaoelekea kijiji cha Kata ya Mayondwe, ilikuwa nyuma kabisa ya Chama Cha Msingi. Lakini sasa hivi imekwenda mpaka imeiachia Shule ya Msingi Mayondwe na walipojenga shule ya Sekondari Mayondwe ni takriban mita kama mita 2 au 2 kasoro. Unaweza kupita tu kwa gari, ni kiasi cha mita 2.

Mheshimiwa Spika, sasa mipaka hii imesogea sana. Bunge lililopita nilizungumzia juu ya mipaka hii na nikauliza na Kagera wamepima wakasema ndiyo wamepima. Safari hii niliweza kufika nikajionea mipaka, kwa kweli kiasi hicho ambapo imesogezwa kwa namna fulani mimi naona jeshi lilichelewa kuitambua. Likaacha wanakijiji wakakaa mle, wameshakaa miaka mingi. Wameshajenga, wameshaishi,

wameshatengeneza mashamba, ni kijiji kabisa, unapokuja kuweka mpaka pale unasema mwisho ni hapa, hata shule tu hawawezi kuchimba shimo la taka, hapo ni eneo dogo tu.

Nadhani hilo waliacha kwa heshima tu ili uweze kupita nyuma ya shule kuelekea katika shule ya Sekondari. Naomba hii mipaka iangaliwe upya katika eneo hili. Hata kama kuna wachache ambao watabaki sina matatizo, hata ule mpaka ukisogezwa mpaka ninaposema, ukirudishwa nyuma bado kuna wanakijiji wengine watabaki. Lakini hawa watakaobaki tulikuwa tunafahamu kwamba walikuwemo ndani ya Kambi tangu muda mrefu. Napo hawa wanasema wanakijiji kwamba mipaka ilikuwa nyuma bado ikasogezwa wakaingia ndani ya kambi sasa imesogezwa zaidi. Mimi naliangalia hili naona kama silipendelei sana. Naomba Serikali ilitazame upya.

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda kuzungumzia kero. Nilipo hapa nimewekwa njia panda. Kambi ya Kabo ya 21KJ ni wananchi wangu licha ya kwamba ni askari, ni wapiga kura wangu. Majukumu yao makubwa hawa ni ulinzi wa nchi na mipaka, na mambo mengine ambayo wanatakiwa kuyafanya kwa mujibu wa *vision* na *mission* yao. Lakini sasa hapo wanavijiji waliowazunguka ni wapiga kura wangu, pia na wao ni wananchi wangu. Hivi unapotokea mgogoro kati ya wananchi na jeshi hivi Mbunge unasimama wapi?

Mheshimiwa Spika, nadhani hapo sasa lazima usimamie ukweli. Mwaka 2005 kulitokea tatizo kwenye mbuga ya Kaboya, ikachomwa moto. Baada ya ile mbuga kuchomwa moto, moto umeshazimwa tayari, saa zimeshapita, kukatokea kikosi cha askari kikaingia kijijini. Kikapiga wananchi vibaya mno, wakajeruhiwa wakalazwa hospitalini, wakajiuguza, waliowapiga hawakuonekana. Wale askari wakarudi kikosini, wale wa hospitali wakaishia kufunguliwa kesi, ikapelekwa Mahakamani, mpaka leo kesi hiyo nadhani haijaamuliwa. Bado hao waliopigwa walionewa kwa sababu siyo waliokuwa wamechoma moto. Waliochoma moto walikwishaondoka na vijana walikimbia.

Sasa kubwa sana kuamkia jana tarehe 31 juzi usiku wa saa 3 kasoro dakika 5 nilipokea simu ya mwananchi kutoka kijiji cha Mayondwe. Vita imefumuka kati ya wanajeshi na hawa wanakijiji na mimi namshukuru Mkuu wa Kikosi cha Kaboya *CO* yule. Nilimpigia simu kama saa 3 kamili nikamwambia bwana kuna vijana wako wapo wanasababisha matatizo kijijini. Namshukuru alienda akaweza kusitisha yale mapigano. Lakini mpaka anayastisha wananchi 18 wamelazwa tena katika hospitali ya binafsi.

Mheshimiwa Spika, haya siyo mahusiano mazuri. Wala nilipopeleleza wakasema unajua eti jana yake sijui kulitokea mapigano huko kijijini wakampiga askari. Askari akipigwa ananyanyua kombania nzima kwenda kupigana na wananchi. Hii mimi inanitia katikati ya njia panda na kwa kweli nasema sikulipendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali igharamie yale matibabu ya wale wananchi wote waliolazwa kwa kipigo hicho, kwa sababu hawana sababu yoyote ya kutoa pesa kwa ajili ya kujitibia. Pili, wale ambao waliongoza jambo hili wasiachwe kwa sababu hapa hakuna ujirani, kuna uadui na kama hali itaendelea namna hii hakutakalika. Kaboya

hakutakalika, Mayondwe hakutakalika na vijiji vilivyoizunguka. Hawa wachukuliwe hatua za kinidhamu ili jambo hili lisiendelee. Lakini lingine nalo ninaloliomba ni kwamba kama tunasema raia asipigane na raia mwenzake, hata askari asimpige raia, ampeleke katika chombo kinachohusika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ombi langu ni kwamba baada ya hatua hizi za kinidhamu, kwa sababu *CO* alifika pale pale amewatambua, naomba wahamishwe mara moja, kwa kufanya hivyo wanakijiji waliopigwa watakaporejea wataweza kupata amani ya kuendelea kuishi pale na kufanya kazi. Na wale waliobaki kikosini wajue kwamba kitendo hiki hakiruhusiwi na kuwe na amani na wananchi waweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, basi niwatakie afya njema waweze kupona haraka wanakijiji waliopata majeraha haya. Nimpe pole Mheshimiwa Diwani wa Kata husika; nimpe pole Mkuu wa Wilaya, ambao wote wako wanahangaika sasa katika hii heka heka ambayo ilikuwa haikutegemewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hilo nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Msafiri. Natumaini mtaiweka hali hii vizuri ili Kambi ya Jeshi na wananchi waweze kukaa salama. Waheshimiwa Wabunge, niseme tu wakati wa saa 11 atatangulia Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwenegoha na nadhani Kamati.

Kwa kuwa Wizara hii si ndefu sana, tutamruhusu Mheshimiwa Felix Kijiko na baada ya hapo basi Mheshimiwa Naibu Waziri ataongea kwa dakika 20 na itahitimishwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa dakika 40. Sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.

*(Saa 7 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alikalia kiti.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa wakati Bunge linasitishwa kipindi cha mchana tulikuwa na wenzetu ambao walipaswa waendelee kujadili Mheshimiwa Aziza Ali, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, na Mheshimiwa Felix Kijiko.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuomba radhi, sauti yangu si nzuri sana kwa sababu nina mafua. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanazofanya pamoja na Mheshimiwa Waitara, Mwamnyange na Katibu Mkuu na watendaji wote wa idara pamoja na kuwapongeza wao na watendaji wote lakini pia nawapongeza na wake zao kwa kuwapa nguvu kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu jambo kubwa tunalolitegemea ni jeshi, lakini napenda kupongeza jeshi letu la Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa

umahiri mkubwa sana. Lakini napenda kuchangia sehemu kama tatu au nne. Sehemu ya kwanza ni sehemu ya mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waswahili wanasema nyumba ni mlango, na kama nyumba ni mlango lazima iangaliwe, na ukiacha mlango wazi anaweza akaingia mnyama au mwizi au mambo mengine yanaweza yakatoekea. Nazungumza hivyo kwa sababu mipaka yetu ya nchi, ni mipaka ambayo inayohitaji ipate ulinzi mkubwa. Kutokana na ufinyu wa bajeti ambayo inapewa Wizara hii, naomba Wizara ya Fedha ikaiangalia kwa undani kabisa Wizara kwa kuiangalia mipaka iliyokuwa pembeni ya nchi yetu. Mfano Kigoma, Arusha, Ruvuma na sehemu nyingine ambazo mipaka hiyo ipo, ni kweli wako wanajeshi ambao wanaishi huko, walinzi wetu lakini wale walinzi wanaoishi huko, basi tuwaweke katika mazingira mazuri ili waweze kweli kulinda maeneo hayo.

Kama tutawaweka katika mazingira mazuri ya kuwajengea nyumba zilizo bora wataishi kwa amani na wataishi vizuri zaidi. Sasa hivi tumeona kuna wimbi la ujambazi, lakini wimbi hilo la ujambazi tunajikuta wanaingia watu mbalimbali, wanaingilia wapi? Juzi Mbeya walikamatwa Wasomali wengi tu, lakini laiti kule kwenye mipaka zingewekwa nyumba nzuri wakapata huduma nzuri, nina imani kuwa wangelinda vizuri zaidi. Kwa hiyo, Serikali yetu hasa Wizara ya Fedha ingeiangalia Wizara hii kwa kuangalia mipaka yake. Nchi ikiwa haina amani hata hizi fedha na mengine mengi tunayofanya hayatokaa vizuri na kukosa amani zaidi. Naomba sana Wizara hii ikafikiriwa kuweza kupata asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili la mafunzo ya jeshi, mimi nina maono kwamba jeshi lina mahusiano na majeshi ya nchi mbalimbali, mahusiano yale yazidi kuboreshwa na kuimarishwa katika nchi nyingi kama Urusi, na naamini walikuwa na ushirikiano na China. Nasema hivi kwa sababu watakapokwenda kujifunza huko, watajifunza mambo mengi. Lakini mambo mengine watakayojifunza ya kuwasaidia ni kwamba madaktari watapatikana kutoka katika jeshi la Ulinzi na Usalama. Vilevile marubani watapatikana. Juzi tu hapa kama mwaka mmoja kama sikosei madaktari wa Muhimbili waligoma, walipogoma madaktari wa jeshi walikwenda kufanya kazi Muhimbili. Mimi nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo waliyokwenda kuifanya pale, kwa kweli ni kazi ambayo lazima tuwashukuru na kuwapa moyo, walifanya kazi nzuri ya kuwaokoa wananchi wao. (*Makofi*)

Mheshinmiwa Naibu Spika, na bado itatusaidia hata kwa hawa marubani, nchi yetu inaweza ikawapa watu *scholarship* ya kwenda kusoma nje, na inawezekana watakapokwenda kusoma na mazingira watakayokuta kule watazamia huko moja kwa moja hawatarudi. Lakini kufuata utaratibu wa heshima ya jeshi watarudi katika nchi yetu na kuja kufanya kazi na hivyo kuweza kupata wasomi wengi wenye ujuzi mwingi watakaobaki hapa hapa kwetu.

Sasa kuna kuna videge vidogo vingi tu ambavyo vinazunguka, lakini marubani wale wanatoka nje, si kutoka nchini kwetu, na wanalipwa pesa nyingi sana. Laiti kama wangekuwa wakipelekwa kwa *scholarship* za kusomeshwa na Serikali ya Tanzania wangekuwepo hapa, nina imani zile pesa wangepata marubani wa Tanzania na

Watanzania wangeweza kuendelea zaidi. Kwa hiyo, uhusiano uendelezwe na kuimarishwa na hata kutafuta marafiki wengine wa kuweza kusaidia askari wetu waweze kuishi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni mafao ya pensheni. Mafao ya pensheni kwa kweli ni mafao ya kuzingatiwa na ya kuangaliwa mapema kabla askari hawa hawajastaafu. Kwa sababu si suala la kigugumizi kuangalia ni lini atastaafu, inajulikana na kama inajulikana mtu huyu aweze kuandaliwa mapema zaidi ili kuepuka matatizo ya madai ya mara kwa mara. Katika Bunge lako hili hili yapo maswali mengi sana yameulizwa kuhusu suala la pensheni. Ni kweli wanapata shida na ni kweli wanashawishika kwenda kushirika katika mambo mbalimbali kutokana na udhaifu wao, si kama moja kwa moja pamoja na kuwa pensheni inasababisha lakini kila mmoja kutokana na udhaifu wake. Pengine hiyo inaweza ikawa inampelekea akafanya mambo kama haya.

Lakini hilo hilo bado kwenye pensheni, si hapa tu katika jeshi, katika sehemu mbalimbali natolea mfano wa juzi tu katika hizi pesa za Afrika Mashariki, yuko mtu mmoja ambaye ametoka Tabora alikuja hapa kudai pesa zake za Afrika Mashariki. Lakini alipofika kule mkoani kwenda kuangalia pesa zake alizoletewa, alikuta yeye ameshaandikwa amekufa, na mrithi alishapatikana na mahakama ilishamuidhinisha kuwa yeye ni mrithi, kwa hiyo, akachukua zile pesa. Hii yote inatokana na ile taratibu ya kucheleweshа pensheni zao.Hivyo, naomba uwepo utaratibu mahususi utakaoweza kuwasaidia waweze kupata pensheni zao ili kuepukana na matatizo mbalimbali hasa matizo mengi yanayojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine napenda kuzungumzia kuhusu suala la michezo. Jeshi letu ni jeshi ambalo kwa kweli linajitahidi sana na katika kujitahidi kwake linaimarisha sana michezo. Natolea mfano kwa timu ya Tabora *rhino* pale, *rhino* imeweza kushinda kuingia kwenye daraja la kwanza, lakini nina imani wananchi wa Tabora wasivunjike moyo zaidi. Wale *rhino* watazidi kuendela na tutazidi kuwatia moyo ili waweze kufika juu zaidi. Kwa hiyo, naomba jeshi letu liweze kuimarisha michezo zaidi, hata wachezaji wa Taifa wanaweza wakatoka wengi katika timu ya jeshi ili kuweza kutusaidia si mpira wa miguu tu, hata *netball*, *volleyball*, na michezo mingine mingi inayochezwa. Hata ngoma Mheshimiwa Waziri pale ananikumbusha ngoma ya sanaa na wao pia wanacheza, ni wachezaji wazuri zaidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, napenda kusema michezo iimarishwe ili iweze kuendelea zaidi, lakini nilikuwa nasema kwamba Tabora tuna kambi la jeshi. Kambi la Jeshi ipo Tabora, nilikuwa na mawazo ambayo kama utaratibu unaruhusu, kwa nini pale Tabora wasijenge uwanja wa ndege kwa sababu kuna ndege ambazo, pamoja na kuwa uwanja wetu wa Serikali upo, lakini mdogo sana hautoweza kumudu.

Lakini bado pia wanaweza kujenga uwanja wao wa ndege kwa usalama zaidi waweze kujitegemea wao wenyewe sio lazima kutegemea huu uwanja wa ndege wa kawaida. Itatusaidia zaidi pale kwetu kuwa na uwanja wao wa ndege na shughuli zao

wakazifanya wakiwa wao wenyewe peke yao. Hii itatusaidia zaidi kwa sababu yako mambo mengi katika mkoa wetu wa Tabora yanaweza yakafanyika na yakawa ni siri ya kwao wenyewe sio lazima liweze kupitishwa katika uwanja wetu wa ndege wa kawaida.

Lakini la pili kuna nyumba za jeshi nyingi sana, naomba nao watengenezewe zile nyumba zikarabatiwe waweze kuishi katika nyumba nzuri. Kwa kweli sisemi kama ni nyumba mbaya sana lakini kuboreshwa si vibaya. Ziboreshwe ili ziweze kukaa katika mazingira ambayo yanapendeza ya kuwatia moyo katika kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani kulikuwa pia na mabasi, mabasi yale sasa hivi siyaoni, walikuwa wakitoka na mabasi wanarudishwa. Hapo hapo kwenye mabasi nimeweza kukumbuka na kitu kingine. Kuna wanajeshi wengi ambao wanakaa nje ya makambi. Mimi nina mtazamo ambao ni tofati, kwa nini kusiwe na utaratibu wa kuweza kurudishwa kwenye makambi? Waishi makambini. Hatuoni kwamba kuishi nje ya makambi ni sehemu moja ambayo inaweza ikaleta vishawishi mbalimbali.

Sasa hivi ujambazi unaotokea baadhi ya watuhumiwa ni wanajeshi. Hatuoni kuwa mtu anaweza akapata tamaa au akashawishika na vitu fulani kwa kuwa yeye ni mwanajeshi kwa kuwa yuko nje ya jeshi. Lakini akiwa ndani ya jeshi itasaidia zaidi ili waweze kushiriki ndani badala ya kushiriki uraiani.

Kwa hiyo, hata kama utaratibu unaeleweka kuwa watasema bado pesa ni ndogo, lakini kama pesa ni ndogo tuangalie utaratibu gani tunaweza kufanya tukawaweka ndani, na si kama itashindakana, kama tukiamua tutafanya na tutaweza. Kwa hiyo, naomba warudishwe katika makambi yao waweze kuishi kuepukana na matatizo mbalimbali yanayayojitokeza.

Mheshimiwa Naib Spika, sitopenda kuongea mengi zaidi lakini napenda kukushukuru na kuwapongeza viongozi wote, lakini zaidi napenda kumpongeza mama Kapuya kwa kazi nzuri anayofanya kwa kuweza kumlinda Mheshimiwa Kapuya, na mama Omar, kwa kazi nzuri anayofanya. Nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kidogo tu juu ya Hotuba hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza, nianze na pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watalaamu ndani ya Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya na hotuba nzuri ambayo imekuwa fupi na inayoeleweka. Hali kadhalika napenda kuwapongeza viongozi wakuu wa Jeshi ndugu yangu *General* George Waitara na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa. Nawapongeza sana kwa sababu wanafanya kazi nzuri. Niende moja kwa moja kwenye hoja zangu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni wakati mzuri sasa na wakati muafaka umefika kabisa kwa jeshi letu kuweza kujengewa nyumba nzuri za makazi ya jeshi wakaenda kukaa kwenye makazi yao. Wakati sasa umefika kwamba wawe kwenye makazi ambayo yanatambuliwa kwamba ni makazi ya wanajeshi. Kuchanganyika sana na wananchi nadhani vilevile kunawasahaulisha kidogo nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda kuzungumzia ni juu ya uwezo wa jeshi letu kutumika wakati wa amani. Jeshi la Wananchi lina uwezo mkubwa sana na kampuni yake ya SUMA ni mkandarasi *grade one*. Lakini hatumtumii mkandarasi huyu hata kidogo kwa sababu tuna majengo.

Sisi tuna fedha tunakwenda kwenye Halmashauri, barabara za Wilaya hazipo kule, nyumba zinataka kujengwa, mkandarasi huyu hatumtumii sisi, lakini ndiye mkandarasi ambaye kwa kweli anakupa bei sahihi. Atakupa muda kamili wa kumaliza kazi, atajenga kitu chako kama unavyokitaka na hata kukuletea bei ya nyongeza ya kila mlichopatana.

Nazungumza hili kutokana na uzoefu kwamba nilipokuwa Naibu Waziri wa Ujenzi tumewatumia hawa kujenga nyumba za kisasa na mnaweza kuona uwezo wao. Lakini vilevile uwezo wao mkubwa wa kujenga madaraja na barabara ulionekana wakati wa vita vya Idd Amin. Waliweza kufanya kazi nzuri sana. Lakini tunangojea tu kuwasifu wakati wa vita. Sasa hivi kuna kampuni Ngerengere kiko kikosi kizima cha ujenzi hatukitumii. Nacho kingeweza kabisa kutengeneza barabara angalau hizi za Wilaya, basi kwa fedha hizi ambazo nyingi tunazipeleka Halmashauri, na mara nyingi fedha hizo hazitumiki vizuri kwa sababu makandarasi wetu hawamalizi kazi.

Hali kadhalika majengo haya ya elimu, nyumba za walimu na baadhi ya madarasa kampuni hii ya *SUMA* ingeweza kujenga katika muda muafaka kabisa na tukapata nyumba nzuri za walimu na ambazo bei zake hazitakuwa na nyongeza. Mimi naomba tuangalie suala hilo sana tuwatumie, wenzetu wana ujuzi, wana nyenzo za kufanyia kazi na kampuni yao inaweza kuwa ni kampuni kiongozi kwa kufanya kazi wakati wa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja limezungumzwa, mimi kidogo nimekerwa nalo, suala la kuwapa wanajeshi posho wakienda mahali kufanya kazi. Nidhamu ya jeshi haiendani hata kidogo na madai ya posho na vinginevyo. Ukianza kumpa nafasi mwanajeshi adai kabla ya kukubali amri ya kiongozi, basi jeshi linakuwa halina nidhamu. Mimi hapa nimesema waachieni wanajeshi watumie utaratibu wao ambao wanaujua.

Nina uzoefu kabisa wa suala hili, kwa mfano, mwaka 1972 mimi nilikuwa JKT Makutupora na ghafla tukapata vita ya Mtukula, kule Idd Amin. Saa tisa mchana unapigiwa *bugle,* unakwenda unaambiwa kachukue vitu vyako, safari! Ingekuwa suala la kungoja posho tusingeondoka. Tungekuwa kwanza tugawiwe posho zetu halafu ndiyo twende vitani. Lakini hili ni suala la nidhamu, unaingia kwenye gari unaondoka, unakwenda Kaboya, asubuhi unaambiwa Mtukura, hakuna posho! Posho utaikuta huko huko, kama ni dona, ugali, huko huko na hicho ndicho utakachofuata.

Mimi naogopa sana kuzungumzia posho katika jeshi kwa sababu ukianza kuzungumzia posho askari mdogo atakuja atapiga saluti kubwa sana kwa mkubwa wake na mkubwa wake ataitikia kwa saluti, atakaposhusha mkono yule askari mdogo atamwambia mzee posho je? Hapo nidhamu hakuna! Kwenye suala la posho kusema

kweli naomba Waheshimiwa Wabunge, muwaachie viongozi wa jeshi wapange utaratibu wao kwa nidhamu inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kingine nadhani hiki nacho kinanikera, ni kizuri sana kwa wanajeshi wetu, lakini kwa bahati mbaya tunatembea mitaani, vitu vinavyouzwa kwa wanajeshi wetu ambapo wanauziwa wanajeshi bila ya kodi lakini havina alama ya jeshi. Kwa hiyo, vinatembea mitaani vinauzwa upya.

Mimi naomba vile vyote ambavyo wanajeshi wetu wanauziwa kwa nia njema kabisa na kwa sababu nzuri tu ya kuwakidhi haja zao basi viwe na alama ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili vikikutwa kwenye duka ama na mtu mwingine yeyote ataulizwa alivyovipata au uhusiano wake na vitu hivyo. Ili tuweze kupunguza wenzetu wajanja kutumia mali hizi ambazo hazina kodi wao wanazitumia kuuza. Hii kusema kweli inashusha hadhi ya jeshi. Mimi ningependa kila mali ya jeshi iwe na alama kwamba hii ni mali ya jeshi la wananchi Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia, ni kusifu Jeshi la Tanzania. Jeshi la Tanzania lina vyuo vyake, linafundisha viongozi wake mpaka imefikia hatua kwamba Monduli sasa inakuwa *an African Institute,* viongozi wengine wa Afrika wanataka wanajeshi wao wafundishwe hapo. Hii ni sifa kubwa sana na ndiyo maana unaona kutokana na nidhamu kubwa na uwezo mkubwa wa kufundisha wa askari wetu sasa wanajeshi hao wanachukuliwa kulinda sehemu zingine za amani na Umoja wa Mataifa na Jeshi la Afrika. Na kutokana na uwezo huo siyo tu tunakuwa bahati mbaya tunachaguliwa, hapa ni ile nidhamu ambayo wanajeshi hawa wakubwa wanafundisha wanajeshi wetu na viongozi wengine wa Afrika wanaleta wanajeshi wote kufundishwa hapa.

Hii ni sifa kubwa sana kwa sababu tunao sasa ujeuri wa kusema tunatoa viongozi katika Jeshi sisi wenyewe badala ya kuwapeleka nje. Zamani walikuwa wanajeshi wengi wanakwenda *Sandhouse* Uingereza na wakirudi huko wanajivunia *Sandhouse*. Sasa hivi tunajivunia hapa hapa Arusha Monduli na hii ni sifa kubwa sana. Lakini lingine Morogoro Vijijini, niwie radhi nizungumzie Morogoro Vijijini hatuna jeshi, hatuna JKT, hatuna kambi ya aina yoyote na sisi tupo tunapakana na Rufiji, tunapakana na Lindi, tunapakana na Kisarawe na tunapakana na sehemu ya *Selous*.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo yale niliyonayo kwa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza, napenda nitoe pongezi zangu za dhati sana kwa Amiri Jeshi Mkuu, *CDF, Chief of Staff, Chief of National Service* pamoja na makamanda wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

La pili, nataka nimpongeze Mtoa Hoja, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa taarifa yake ambayo ametusomea hapa, taarifa nzuri kabisa na nina hakika wameipitia vizuri sana na Naibu Waziri wake na ndiyo maana taarifa imeandikwa vizuri.

Imeandika kijeshi kifupi, sio kuandika karatasi nyingi sana. Huu ndiyo utaratibu wa jeshi, wanafanya hivyo hawana mambo ya kurefusha maneno, ni kazi moja tu, nampongeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Napenda pia niwapongeze wapiganaji wote kwa ujumla kokote waliko kwa sababu kusema kweli Jeshi la ulinzi ni jeshi ambalo tunashuhudia kwamba amani tuliyonayo katika nchi hii ya Tanzania inatokana na msimamo na uongozi mzuri ambao wanapata kutoka kwa viongozi wa jeshi. Lakini sio hilo tu, lakini pia ni lazima tujue kwamba askari nao wana nidhamu ya hali ya juu nidhamu ya kuweza kuwatii viongozi wao, nawapongezeni sana wapiganaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona yanayozungumzwa yanarudiwa rudiwa ni kwamba yana maana sana. Sasa nilikuwa nazungumza muda mfupi hapa nikasema wameni-*empty* kwa yale niliyokuwa nayo, hata hivyo, sina budi niyazungumze kwa kifupi ili yaweze kutiliwa mkazo kwa Serikali. Serikali, kusema kweli naomba bajeti ya jeshi kama NGOME isingezungumzwa hapa labda ingebaki ni Wizara peke yake, lakini NGOME tukawaacha na mipango yao kwa sababu hatuwezi tukarekebisha kitu kwenye bajeti yao, na miaka yote iko hivyo. Kwa hiyo, kama Serikali inanisikia basi nadhani kwa bajeti ijayo NGOME tungewatoa pembeni wakawa na bajeti yao, kwani wana mambo mengi sana ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo moja la kuzungumza ambalo nitaanza nalo. Kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya Watanzania ambao walipigana vita vya pili vya dunia. Taarifa walizonazo wanaeleza kwamba malipo ya kwao yalilipwa na Jeshi la Uingireza na fedha hizo zikaletwa Tanzania, sijui ilipokea Serikali au labda kama ni Jeshi! Inawezekana Waziri atafafanua hili na ningeomba afafanue kwa sababu imekuwa ni kero sana kwa Wabunge, tunaulizwa sana huko majimboni. Hawa wananchi wanaodai haki zao wakitaka hayo malipo, na bahati mbaya wengine wameanza kupoteza maisha wamefariki bila ya kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hili naomba kusema tufuatilie tujue taarifa zilizopo ni kama fedha zilikwishatumwa kutoka Jeshi la Uingereza kuja Tanzania; je, aliyepokea fedha hizo ni nani? Na kwa nini kama amepokea hizo fedha hazijagawiwa kwa watu wanaohusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopigana wapo mpaka watu wanakufa bila kufaidi jasho lao na kama akibainika huyo mimi nilikuwa nashauri achukuliwe hatua kwa sababu naweza nikasema ni mwizi mkubwa sana anayewatesa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni la kwanza ambalo Mheshimiwa Waziri pamoja na ripoti nzuri lakini ningeomba utusaidie. Nadhani na wewe kwako kuna wazee ambao wanakudai malipo hayo ambayo kwa kweli Wabunge inabidi tuwapooze kwa kugusa mfukoni.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu analijua na amelisimamia na kuna wengine wameanza, yeye mwenyewe kwa kujikamua anapunguza hasira za hawa wazee. Lakini nadhani kuwe na utaratibu sasa wa Serikali wa kuwalipa hawa watu ila tusikilizwe huko tunakokwenda Majimboni. Hivi tuko hapa, tunapumzika, tukienda karibu kila

Mheshimiwa Mbunge anadaiwa hizo fedha ambazo hazijui, mimi sijui ukiniambia habari za vita vya pili vya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kama ushauri ambao umezungumzwa na wasemaji waliotangulia kwa makusudi mazima nilikuwa nadhani sasa ni muda muafaka kwamba Serikali iingilie kati kusaidia askari wetu. Askari wanaishi uraiani, wanachanganyika na raia wenye tabia mbovu. Naamini askari mwenye nidhamu ya hali ya juu katika kuchanganyikana huko anaweza kujifunza tabia mbovu na mifano ipo ambayo inawahusisha baadhi ya askari kujiingiza kwenye tamaa ya maisha ya kufanya ujambazi ili waishi maisha mazuri. Kwa sababu askari kama huyo akija kwangu akakuta mimi Kijiko nina maisha mazuri na yeye atataka aishi hivyo. Sasa hii chachu yake ni hiyo ya kuruhusu kutoa mwanya askari wakae uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi msemaji mmoja amezungumzia habari ya matatizo ambayo wanajeshi wetu wanapata matatizo ya usafiri. Asubuhi ukiwa kama Dar es Salaam ambapo kuna vikosi vingi, ukipita barabarani kwa kweli utawahurumia askari. Kwa sababu utakuta wamejaa barabarani wakati kwanza wanatakiwa wafanye mazoezi ya mwili asubuhi saa 11. Askari wa Jeshi tangu saa 10 wanatakiwa wameshaamka, askari anaamka saa moja ili aingie kazini saa moja na nusu, sasa tunawarudisha nyuma, tunaharibu *ethics* za jeshi, haziendi namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwamba ni muda muafaka kabisa kwamba sasa Serikali iongeze nguvu, itoe nguvu kwa Jeshi la Wananchi ili waweze kujengewa nyumba kwenye *barracks*, askari wakae kwenye *barracks* na siyo uraiani. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeepusha lawama ambazo mara nyingi wamekuwa wakizipata za kujiingiza kwenye vitendo vibovu wakati tumebariki wao kuchanganyikana na wapenda anasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili au nikiendeleza hilo, ni hili la usafiri ambalo kwa kweli limekuwa ni zito sana. Karibu miaka 10 iliyopita kulikuwa na utaratibu mzuri sana, mimi niliupenda, wanajeshi walipokopeshwa magari, vifaa vya ujenzi na magari hayo tunayoyaona sasa yameshakwisha, yameandikwa *TZJ*, hizi *pickup*. Magari yameshakwisha kabisa. Sasa hivi lakini askari huyu ili afanye kazi ngumu anayoifanya ya kulinda nchi ni lazima apewe motisha, motisha ni vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani ufike wakati tuwahurumie wanajeshi wetu. Hii tunasema wanakaa barabarani kusubiri mabasi, mwanajeshi anapanda Daladala na kuomba *lift*, kama angekuwa amekopeshwa chombo cha usafiri kwa awamu nyingine tungekuwa tumesaidia sana na wangefanya kazi kwa uaminifu mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie askari wetu wanaolinda mipaka kama mzungumzaji mmoja alivyozungumza hapa. Mimi natoka kwenye mkoa ambao upo mpakani. Napakana na nchi jirani za Burundi, Kongo, ile mipaka inalindwa. Nashauri kwamba hawa askari wasikae muda mrefu kwa sababu hii ni mikoa iliyoko mipakani na hasa sisi mikoa ambayo ina wakimbizi ni mikoa ambayo imevunja rekodi kwa kuwa na vitendo vya ujambazi. Inakuwa ni kazi kubwa kutofautisha ujambazi umefanywa na

silaha ipi; ni ya kutoka nje ya nchi au ni ya ndani ya nchi kwa maana silaha ambazo zinatumiwa na askari wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama nilivyosema kukata tamaa ya maisha askari anaweza akajihusisha na kitu kama hicho kwa sababu kwanza amekaa muda mrefu sana kwenye kituo cha kazi, kwa hiyo, napendekeza kwamba askari wasikae muda mrefu kwenye vituo hivi vilivyoko mpakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine ambalo kusema kweli nadhani halina budi lifanyiwe kazi ya kuwasaidia wanajeshi wetu kama njia mojawapo ya kuhamasisha au kuwapa motisha, hili ni mafunzo. Mheshimiwa Mwenegoha amezungumza kuhusu chuo chetu cha kule Monduli kinavyotoa mafunzo mazito kwa *East Africa* na hata Afrika. Nadhani chuo hicho kitumike kutoa mafunzo kwa askari wetu, kisiwe na muda wa kukaa bila kuwa na wanafunzi, muda wote kiwe na wanafunzi. Nakumbuka Mgulani pia pamekuwa kama kituo cha kufundisha, ni chuo kinafundisha askari wa ngazi ya chini.

Muda mwingi askari wawe katika mafunzo ambayo kwa kweli yatasaidia kuwa na jeshi ambalo liko timamu. Sisemi kwamba jeshi letu haliko timamu, liko timamu vizuri sana. Lakini mafunzo yanatakiwa yatolewe mara kwa mara ili kuhakikisha jeshi linaimarika zaidi na yawe ya kisasa kwa sababu kwenye hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri ametusomea hapa, ameeleza ni siri ya jeshi tukija kwenye silaha tunazozitumia. Kama tutakuwa na silaha za kisasa ambazo hazina mafunzo ya kisasa kwa kweli itakuwa sawa na mtu kupewa bunduki umuue adui wakati wewe hujui kutumia bunduki, utakimbia. Lakini kwa uongozi wa jeshi tulionao, nina hakika kwamba mambo yote yataenda sawa sawa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Naibu Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Omar Yusuph, alikuja kule kwangu nadhani baada ya taarifa kupokea taarifa kwamba ujambazi ulikuwa umeshamiri kule katika Wilaya ya Kibondo. Kweli baada ya kufika kule alijionea mwenyewe, na hakuweza kufanya ziara hiyo akiwa peke yake, alikuwa na ulinzi mkali, ulinzi mzito, ndio hiyo nasema kwamba adha kubwa ambayo tunaipata sisi tunaoishi kule mpakani kutokana na hawa wakimbizi ambao tunawalea. Tunawalea kwa manufaa yetu wenyewe, manufaa ya watu wachache lakini sio kwa wananchi walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema mambo ambayo nilitaka kuyazungumza mengi yamezungumzwa, lakini naiomba Serikali iangalie upya kama inawezekana bajeti ya Ngome tusiijadili hapa hadharani kwa sababu inaenda na usiri, ni nyeti sana, nakushukuru sana. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi zao nzuri za kusimamia ulinzi wa nchi yetu.

Kuhusu ukosefu wa magari katika Kambi ya Potoa Zanzibar, Kambi ya Jeshi Potoa haina magari ya kufanyia kazi kwani gari iliyopo ni moja tu *Nissan* ndogo ambayo ina umri zaidi ya miaka 15 na imechakaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alione tatizo hilo na alisaidie utatuzi wake. Kambi ya Potoa si ndogo ambayo ndio Kambi kongwe kwa mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kuhusu michezo, kwa nini Jeshi letu halina timu nzuri ya mpira wa miguu kama vile polisi? Nashauri Jeshi liwe na timu ya *football* nzuri kama vile inavyokuwa na timu nzuri ya riadha

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote na makamanda wote wa majeshi yetu chini ya uongozi wa Mkuu wa Majeshi, kwa kazi nzuri sana wanazofanya kuilinda nchi yetu na kuwaimarisha vijana wetu kwa ukakamavu wa kuitumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya Kambi za Jeshi na Vijiji Manispaa ya Shinyanga. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aambatane nami baadaye mwaka huu 2007 kutembelea na kutatua matatizo ya mipaka ya Kambi za Jeshi na Vijiji katika Kata za Chibe na Kizumbi.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote. Natoa pongeza maalumu kwa Jenerali Waitara na jeshi kwa kazi nzuri ya kuilinda nchi yetu na uhusiano mzuri wa kijeshi na majeshi ya nchi jirani na nyinginezo duniani kama hotuba ya Bajeti ya Wizara ilivyotueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wangu yanalenga katika maeneo mawili yafuatayo:-

Kwanza ni kuwapatia wanajeshi wetu zana za kisasa na makazi bora na pili kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa ambalo tumeliunda upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zana na makazi bora, pamoja na zana za kisasa nasisitiza umuhimu wa kuboresha mawasiliano ya kisasa ili jeshi letu lipate uwezo wa kugundua mbinu za maadui wetu kutoka kokote kabla hawajaleta madhara kwa hiyo, rada yetu tuliyoinunua kwa mamilioni ya fedha, itumike vizuri na ifanyiwe matengenezo ya mara kwa mara ili ifanye shughuli zilizokusudiwa, vile vile wapatiwe vifaa vingine vya mawasiliano viendavyo na wakati.

Kuhusu nyumba nasisitiza kuwa Wizara irejeshe utaratibu ule wa zamani wa majeshi yetu yote kupatiwa makazi ya pamoja badala ya kuwaacha baadhi ya pamoja badala ya kuwaacha baadhi ya wanajeshi kupanga nyumba uraiani. Hali kama hii inarudisha nyuma hadhi ya jeshi na askari wake waone hadhi ya jeshi na askari wake waonekane kama ni sawa na wananchi wa kawaida na wanajeshi wenyewe wajione kuwa

sawa na raia wa kusaidia. Hali kama hiyo inarudisha nyuma nidhamu ya wanajeshi. Kuna umuhimu pia wa kuhakikisha katika maeneo ya bahari na maziwa, jeshi la uhamiaji linapatiwa boti ziendazo kasi ili kupambana na ujambazi unaoongezeka hasa katika maziwa kutokana na majambazi toka nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uimarishaji wa JKT, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kulijenga upya Jeshi la Kujenga Taifa kwani mbali ya vijana wetu kujifunza masuala ya ulinzi, huko nyuma walishiriki sana katika masuala ya kiuchumi kwenye sekta za kilimo, ufugaji, useremala, ushonaji na viwanda vingine mbalimbali.

Kwa hiyo, nashauri kuwa Serikali iwape maeneo (ardhi) ya kutosha sana (vitendea kazi) za kisasa na za kutosha ili wazamie zaidi katika uzalishaji wawe mfano bora kwa Taifa. Pia wanapotoka jeshini, Serikali iwawezeshe kupata mitaji ili wajiajiri na hatimaye wawaajiri wenzao. Utaratibu ukienea nchini tutakuwa tumepunguza tatizo la ajira kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kila la heri, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuwapongeza kwa kazi nzuri Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na makamanda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya wananchi wa Wawi, jimbo la Wawi ni moja kati ya majimbo yenye vikosi vingi vya ulinzi vikiwemo jeshi la wananchi Visiwa vya Unguja na Pemba vinauhaba mkubwa wa ardhi na kwa wakulima wa Wawi hawana tena ardhi ya kulima kutokana na maeneo yao ya asili kuchukuliwa na vyombo hivi vya ulinzi. Namwomba Waziri afanye ziara katika jimbo la Wawi, asikilize kilio cha wananchi juu ya uwezekano wa kupatiwa angalau ile ardhi waliokuwa nayo kabla kambi haijapanuliwa na kuchukua ardhi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya nyumba za jeshi, *Ali Khamis Camp* ni kambi kongwe hapa nchini pamoja na ukongwe huo kambi pamoja na mradi wa ujenzi kuanza kwa kasi, lakini iliibua kama zimamoto hadi leo mradi haujakamilika, je, ni lini mradi huu ulipangiwa kukamilika?

Kuhusu posho ya chakula, vinywaji kwa wanajeshi, Serikali inaelewa ikitoa fedha kwa ajili ya wapiganaji kupata mahitaji yao. Pamoja na juhudi hizo bado yapo malalamiko na upungufu wa huduma hii. Nashauri ili kuondoa manung'uniko ni vyema posho zote za wapiganaji ziingizwe katika mishahra yao. Kwa mfano, vinywaji wanavyopewa mara nyingi unavikuta katika maduka ya mitaani, hivyo kukosesha Serikali kodi. Ni vyema utaratibu unaofanyika Uganda wa kumpa mpiganaji *package* yake ili akajinunulie mwenyewe ili mradi kunakuwa na huduma hiyo kila kambi.

Kutokana na taarifa ya *CAG,* yapo matumizi yasiyo mazuri katika vyombo vya ulinzi, eneo moja ni la manunuzi.Wakati umefika wa Wizara kutumia ununuzi wa vifaa vya kawaida kwa kutumia mtandao *E-Procurement* ambao utasaidia kupunguza gharama,

uwazi wa vifaa vyenye umadhubuti. Aidha, ni vyema jeshi likanunua vifaa vyake kwa wazalishaji na sio kupitia kwa mawakala na kadhalika.

Kuhusu kuendelezwa vijana wa JKT, mwaka jana nilishauri matumizi mazuri ya vijana wetu wanaomaliza mafunzo ya JKT ni kupatiwa vifaa vya kazi kwa fani waliozosomea ili wajiendeleze kwa kujiajiri wenyewe. Aidha, kampuni ya ujenzi ya JKT ni vyema ikaingia katika ubia na makampuni yenye teknolojia ya ujenzi wa nyumba ya *pre-fabricated,* teknolojia hii ingemaliza tatizo la nyumba na makambi, aidha, gharama za ujenzi zingepungua sana. Nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nampongeza mtoa hoja Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Kwanza, nishukuru kwa yaliyofanyika jimboni kwangu, kikosi cha 21 KJ Kaboya tumefanikiwa kupata *ambulance* kipindi kilichopita na mwaka wa fedha 2006/2007 tumepewa lori kubwa la kufanyia shughuli mbalimbali za askari na kazi zingine za Kiserikali. Nawapongeza na nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru pia Serikali ilikubali kuongeza posho ya chakula kutoka shilingi 60,000/= hadi 75,000/= kwa mwezi. Hata hivyo, naomba waongezwe walau ifikie shilingi 5000/= kwa mwezi sawa na mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tanzania. Huyu mwanafunzi akimaliza chuo, atajiunga na jeshi na hatoridhika na kiasi hiki kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nieleze matatizo ya 21 KJ. Kwanza, ipo huduma ndogo ya tiba kwa askari na wananchi. Naomba zahanati iboreshwe na hasa ijengwe zahanati kabisa. 21 KJ tangu jengo lake lilipopigwa wakati wa vita vya nduli wa Uganda hadi sasa halijajengwa. Naomba wapate zahanati, huduma wanayotoa ni nzuri, ni nafuu kifedha na lugha ya madaktari na wahudumu inaridhisha. Hawana eneo la kutosha kutoa huduma hii ya tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la pili ni kwamba mipaka ya kambi ya 21 KJ iangaliwe upya yaani imesogezwa kiasi ambacho kinatisha sana. Imesogezwa kiasi ambacho kinatisha sana. Eneo kubwa la kijiji cha Mayandwe limemegwa, shule ya msingi Mayondwe imeachiwa mita kama nne tu na shule ya sekondari. Eneo hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia na kero kubwa inayoanza kujitokeza kwa baadhi ya askari wa 21 KJ na vikosi vingine. Nilisoma gazetini askari aliyemjeruhi raia kule Kibaha kwa sababu tu alikatisha mbele ya gari lake akipanda baiskeli wakati yeye alikuwa karibu naye, lilinisikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwangu, mwaka juzi baadhi ya askari wa 21 KJ walipigana na kuwajeruhi vibaya wananchi wa kijiji cha Bisole kwa madai kwamba wamechoma moto mbuga, cha ajabu hakuna askari waliyekamatwa lakini raia walilazwa hospitali akiwemo Bwana Yazid. Juzi sasa kuamkia jana saa 2:55 usiku nilipokea simu nami nikamjulisha haraka *CO* wa kikosi cha 21 KJ kwamba baadhi ya askari walikuwa wamevamia wananchi wa kijiji cha Mayandwe wakiwapiga kwa marungu na fimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru *CO* kwa alivyochukua hatua haraka kwenda kusitisha vipigo hivyo. Hata hivyo tayari wananchi 18 walikuwa wamejeruhiwa na wamelazwa hospitali ya Kagondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole wananchi hao wapone na warejee katika kazi zao. Naomba Serikali igharimie matibabu ya wananchi wote walioumia na kulazwa hospitalini. Naomba wale walioongoza jambo hili la kiharamia kinachochafua sifa nzuri ya jeshi wasiachwe bila kuchukuliwa hatua za nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ujirani mwema upewe uzito izingatiwe hali ya amani kati ya jeshi na kijiji. Jeshi letu ni la wananchi wasiwageuke wenyewe. Izingatiwe na isisitizwe kwamba hakuna raia anayetakiwa kujichukulia sheria mkononi. Polisi Waheshimiwa na wapewe nafasi ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wote waliohusika katika vurugu hizi baada ya hatua za kinidhamu wahamishwe mara moja ili kuleta/kurudisha amani na kurejesha upendo miongoni mwa jeshi na wananchi na kati ya 21 KJ na kijiji cha Mayondwe.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kushukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza naanza kwa kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii ya kutekeleza maagizo na ushauri wa Kamati na kuleta ufanisi mkubwa katika kuimarisha majeshi kiutekelezaji.

Pamoja na kazi nzuri zilizofanywa na Wizara hii za kuongeza nyumba za kuishi askari na ukarabati wa miundombinu, bado kuna tatizo kubwa la nyumba za kuishi askari katika vikosi mbalimbali, hivyo bado kuna jukumu kubwa la kuongeza nyumba za kuishi na miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu huo Serikali ina jukumu kubwa la kuangalia uwezekano wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii, ili kuondoa kabisa tatizo hili ndani ya jeshi letu. Naomba nichukue nafasi hii kuwazungumzia askari wa jeshi la ulinzi ambao wamepewa jukumu la kufundisha mgambo katika Wilaya zetu. Askari hawa ni muhimu sana kwa kuwa kazi wanayoifanya imeweza kutuzalishia askari wa mgambo wa kutosha na kuongeza idadi ya walinzi hadi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi hasa Wilaya ya Masasi, askari hawa hawana ofisi ya mgambo, hawana usafiri, vitendea kazi vya ofisi kwa mfano kompyuta

ambazo zingewawezesha kutunza kumbukumbu vizuri, meza za ofisi, makabati na kadhalika. Ukosefu huu wa ofisi unatokana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuwa finyu na kukosa vyumba vya kutosha kwa matumizi ya ofisi ya mgambo. Chumba ambacho wanakitumia hivi sasa ni kidogo mno mfano wa *store,* hivyo, naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kujenga ofisi ya mgambo ya kisasa na kuwapatia vitendea kazi vya kisasa ili kuboresha zaidi utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani wanalazimika kuishi nyumba za kupanga kwa wale waliooa huku wakiwa hawana usafiri wa kuwawezesha kutumia pale wanapokuwa vijijini kwa ajili ya kutoa mafunzo, hivyo ninachoomba Wizara ione umuhimu wa kutoa magari kwa Wilaya zetu maalumu kwa shughuli za mgambo kwani shughuli hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningeomba askari hawa wanapokuwa vijijini kwa ajili ya kutoa mafunzo waweze kupewa posho za ziada kwa ajili ya kujikimu kwa sababu kipindi hicho hulazimika kuishi huko huko vijijini. Naomba sana Wizara ione umuhimu wa kuboresha kitengo hiki cha ushauri wa mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuitakia heri Wizara hii iweze kuikamilisha mipango yake iliyopangwa kutekeleza kwa mwaka 2007/2008. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia tena kwa maandishi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri na wataalamu wao.

Pia ikumbukwe jeshi ndio chombo pekee kinachotegemewa na wananchi kwa kulinda usalama wa nchi na ili jeshi lifanye haki katika ulinzi bila kuonekana wanapendelea hasa katika ulinzi wa siku za uchaguzi wa nchi, mfano hai ni uchaguzi wa Zanzibar, nguvu kubwa ya kijeshi ilitumika, hivi ni jambo gani lililosababisha kuchukuliwa nguvu kubwa ya kijeshi na kuwafanya raia kukosa amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa Serikali iangalie jinsi gani itawasaidia wanajeshi walioathirika katika vita na wale wanaostaafishwa wapate haki zao bila ya usumbufu ili kuondoa utata na malalamiko yaliojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza jeshi kwa kazi nzuri wanaoifanya kwa kushiriki katika ulinzi wa Kitaifa na Kimataifa na jinsi jeshi linavyoshiriki katika kazi za kujitolea za maafa. Hivi karibuni nimesikia katika vyombo vya habari kuwa jeshi litasaidia katika suala zima la ujambazi lililojitokeza nchini, naomba ufafanuzi kuhusu suala hili na ushiriki wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi ni chombo muhimu, ni vizuri likaongezewa Bajeti Wizara hii ili iweze kujitosheleza kwa angalau kiasi fulani katika usafiri na mambo mengine yanayoikabili katika maisha ya kila siku. Pia suala la jeshi baadhi yao kuwapiga raia matukio ambayo hujitokeza mara kwa mara, hasa katika maeneo ya Tegeta

Jijini Dar es Salaam, nitaomba jeshi liwadhibiti askari hawa ambao hawana nidhamu na kuwachukulia hatua, ili wasiendelee kulitia aibu jeshi letu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyoandaa hotuba yao hii na jinsi wanavyotekeleza majukumu yao siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi ni la wananchi wa Tanzania hivyo nina imani kwamba katika kuajiri basi ajira hupaswa kutolewa kwa Watanzania wa pande zote za Jamhuri hii ya Tanzania kwa wale wanaohitaji ajira hiyo na wenye sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kushangaza ni kwamba wakati wa usaili kule Zanzibar/Pemba hutolewa vijana kutoka Bara na Unguja kuja kufanyiwa usaili kule Pemba na nafasi zile nadhani huwa ni kwa ajili ya Pemba, je, hiyo si kuwanyima fursa vijana wa kisiwa cha pili kujiunga na jeshi na wao. Hivyo tunaomba mgawanyo wa nafasi uheshimiwe ili kujenga na kuimarisha Muungano wetu uwe Muungano wa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI, ukifanya uchunguzi wa kina utagundua kwamba kambi za jeshi zinaathirika zaidi na janga la ukimwi hii inachangiwa zaidi wanajeshi wetu kuwa na tatizo la makazi na kupelekea kuishi mbali na familia zao, na kulazimika kufanya vitendo vya ngono ovyo ovyo. Hivyo naomba basi suala la ujenzi wa nyumba za kutosha kwa wanajeshi wetu ili waweze kuungana na familia zao wanapokuwa kambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haina dini lakini Watanzania wenyewe wana dini tofauti, na kila mmoja anapashwa kuheshimu dini ya mwenzake, lakini katika makambi ya jeshi inaonekana heshima ya dini haipewi kipaumbele. Kwa mfano, nguruwe wanawekwa ovyo ovyo huko makambini mwa Jeshi mpaka kupelekea WaislamU kulalamikia hali hii, hivyo tunaomba hali hii isiendelee na hatua za haraka zichukuliwe kurekebisha hali hiyo ili kudumisha umoja, udugu na upendo wa dhati kwa Watanzania. Ahsante.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Makamanda wote wakiongozwa na *CDF* Waitara, kwa pamoja na wasaidizi wake kwa kusimamia vizuri Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo Wizara inayochukua pesa nyingi katika Bajeti ya nchi yetu na hii ni kutokana na unyeti wa Wizara yenyewe, ili kuongeza pato na jeshi au Wizara hii iweze kupata pesa nyingi, naiomba jeshi litumie rada yake kubaini wavuvi haramu wanaovuna katika bahari yetu *high sea* ili waweze kuwaita waje wajitambulishe na waulizwe kwenye nchi yao wamevuna tani ngapi na taarifa ziwafikie *TRA* ili wawatoze ushuru kuliko kuvuna katika bahari yetu na kuondoka bila ya kulipa chochote. Kwa kutumia rada ya jeshi ambayo nina uhakika wavuvi hao huwa mnawaona mtasaidia kuongeza mapato ya nchi kupitia rada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiombe Wizara iangalie utaratibu mzuri wa malipo ya wastaafu kutokana na ukokotoaji wa mahesabu, mahesabu yanayotumika hayafanani, lipo tatizo la nauli baada ya kustaafu, mstaafu wakati mwingine hulazimishwa kusafirishwa sehemu ambayo hakuzaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie vifaa vya jeshi, sare za jeshi bado zinavaliwa ovyo mitaani kwa watu wasiokuwa askari (JWTZ), bado askari wako sare zao zimechakaa, viatu vimeenda upande hasa kwa askari wa ngazi ya chini, suala hili litazamwe vizuri ili kuwatendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara huwa naulizia kuhusu ndege 11 za kivita zilizoko uwanja wa Mwanza, ndege hizo za kivita bado ni nzima, lakini tangu kuwekwa pale, jeshi halijawahi kuzirusha kufuatana na utaratibu ulivyo, tangu mwaka 1993 hazijarushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara (jeshi) lina utaratibu gani wa kuzifanyia matengenezo ndege hizo na baadaye kuzirusha? Lakini kwa sababu ndege hizo labda zimepitwa na wakati na siku za nyuma tulipewa *offer* ya kuzibadilisha ndege hizo kutoka China tupewe ndege nne aina ya *mig 29* ambazo ni za kisasa zaidi lakini bado tunakigugumizi, hakuna tunachokifanya mbali na kuzirudisha *Mwanza Airport* zikipigwa jua, ni vizuri yangefanyika maamuzi ya haraka vinginevyo tutakuwa kama ilivyokuwa kwa *ATC* kwa ndege zake aina ya *Foker Friendship* zilizoishia hewani.

Naomba nipate majibu ni lini ndege hizo pamoja na nilivyoshauri zitaondolewa sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie nyumba/makambi yanayokaliwa na maafisa wa jeshi katika maeneo ya Masaki, Kitangiri na Tabora. Nyumba hizo hapo awali zilikuwa zinakaliwa na wataalamu wa Kirusi, nyumba hizo ziko uraiani, Wizara ina utaratibu gani wa kuwauzia askari nyumba hizo ambazo kwa hali ilivyo ni nyumba sawa na zile za uraiani hasa baada ya watalaamu wa Kirusi kurudi kwao. Naunga mkono.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mchango wangu utahusu mgogoro wa ardhi kati ya JKT - Chita na wanakijiji wa Chita na Ikule. Katika Bunge la Bajeti la mwaka 2006/2007, nililetewa hapa Bungeni matatizo ya mahusiano kati ya JKT - Chita na wanakijiji wanaowazunguka. Pamoja na kwamba tulikubaliana kufanya mazungumzo ya pande zote ili kufikia muafaka, ninashukuru kwamba uongozi wa jeshi kwa nyakati tofauti walifika Chita na kufanya mazungumzo na uongozi wa wanakijiji.

Ombi langu ni kwamba ili hali ya amani iweze kudumu tunaomba upimaji wa mipaka ufanyike kwa kushirikisha pande zote mbili yaani jeshi na uongozi wa Serikali mbili za vijiji vya Chita na Ikule.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya mara kwa mara ya kuwabomolea wananchi hayatatuletea mahusiano mazuri. Naomba sana tuunde Tume ndogo ambayo itaangalia mipaka na kuweka *beacons* ili kuwepo na uhusiano mzuri baina ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu kuwa Waziri atalitolea taarifa jambo hili katika majumuisho yake, kwa vile analifahamu tatizo hili. Ahsante.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni Wizara nyeti ambayo inafanya kazi zake kimahiri, bila woga na ufanisi na Wizara ambayo inailetea sifa nchi yetu, kwa kulinda na kuihifadhi mipaka kutokana na maadui wanayoionea gere nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi wetu wamekuwa mahiri sana ingawa kazi zao ni ngumu lakini hawatetereki pamoja na hali ngumu ya maisha lakini wanafanya kazi zao kwa busara bila ya woga, hivyo basi Wizara iendelee kuwatafutia walinzi wetu utulivu wa maisha ikiwa ni pamoja na maslahi yaliyo bora zaidi.

Kwa kuwa wapiganaji wetu huishi katika makambi hivyo watakapostaafu watahitaji kurudi uraiani hivyo ni bora kuwajengea nyumba za kuishi kabla ya kumaliza muda wao wa kazi. Mlinzi aliye *smart* ni yule ambaye amehudumiwa vizuri hasa kwa vifaa na vitendea kazi ikiwa ni pamoja na *uniform,* hivyo basi Wizara iendelee na mpango wake wa kuwapatia vifaa vinavyohitajika, tena mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, walinzi hawa wanaofanya kazi katika ulinzi wa nchi yetu, kabla ya kustaafu miezi mitatu kabla watayarishiwe mafao yao mapema ili kujitayarisha na maisha ya uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo mengi yanayotumiwa na majeshi yamekuwa chakavu kwa majengo na miundombinu yanayozunguka makambi, hivyo ni wajibu wa Wizara husika kukarabati majengo ili wapiganaji wetu kufanya kazi zao kwa uzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulimwengu unabadilika kutoka karne na karne hivyo wakati umefika kwa jeshi letu kwenda na mabadiliko yanayotokea ili liwe jeshi la kisasa pamoja na vifaa vya kileo ili kukabiliana na adui yeyote yule atakayejaribu kulichokoza.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Hai, naomba niwapongeze sana kwa kazi nzuri ninazofanya pamoja na mipango iliyopo nikianzia kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote Wizarani. Pamoja na pongezi hizo ninaomba nitoe ushauri wangu.

Napenda kwa dhati kabisa kurudishwa kwa mpango wa vijana wanaomaliza kidato cha sita kupitia Jeshi la Kujenga Taifa yaani ile kwa mujibu wa sheria angalau kwa kuanzia hata miezi sita kabla ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu. Naomba uzingatie mchango wangu wa kina mama wanataka asilimia 50 kwa 50 wakafaidi vizuri timu ya simba iwe ya Jeshi, JWTZ. Suala lolote linalokukela katika Wizara hiyo toa jibu sema mchango wa Mbunge wa Temeke. Simba oyee!

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kufika hapa nikiwa salama. Pia nachukua fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uongozi wako mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimpongeze Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Naibu wake Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa hotuba yao nzuri ambalo inaonyesha ulinzi wa nchi yetu pia na kuwapa mategemeo jeshi letu katika kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu katika Wizara husika. Kuhusu wanajeshi wetu huko Lebanon napenda kuipongeza Serikali/Wizara kwa kukubali kwao kutekeleza azma ya jeshi letu kulinda amani na kuweza kupeleka askari wetu huko Lebanon. Ni vyema sasa Serikali itujulishe hali ya askari hao ikoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kambi za wanajeshi wetu, kwa kuzingatia hali ya jeshi letu lilivyoiva kinidhamu, kisiasa na ukakamavu iko haja kuziboresha kambi zao. Kwa kweli kambi zetu hazikidhi haja jambo ambalo hupelekea mwanajeshi huvutika kuishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kambi ya JKT – Makutupora, Wabunge wako baadhi wana timu yao ya *Shabaha Club* ipo Makutupora. Ninalosema ni la uhakika kwani nami ni mwanachama wa *club* hiyo. Kuhusu kiwanja cha Shabaha cha Kambi hiyo kinahitaji kiwekwe katika hali iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa eneo hilo muhimu kwani ni sawa ya chuo, lakini hapana jengo la kupumzikia askari wetu na hapana vyoo. Sehemu hii ni eneo linaloweza kutokezea kuumia kwa askari, lakini hapana kituo cha afya, hapana hata gari inayotambulika kuwa ni gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu naomba eneo hili lipewe kipaumbele kwani ni eneo linalozalisha wanajeshi wenye shabaha. Nampongeza *CPL* Auleria Mlelwa na *SGT* Rashid Msham kwa ufundi wao wa kuitumia bunduki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi ya wanajeshi wetu, ipo haja kwa Serikali/Wizara kuwatupia jicho la rehema askari wetu kwani hali ya makazi yao siyo nzuri.

Kuhusu uhamisho wa askari, suala la kuhama askari kutoka hapa kwenda kule ni vizuri. Tatizo ni Serikali/Wizara katika kufanikisha uhamisho huo. Kuna baadhi ya askari waliotoka Pemba - Tanzania Bara tokea mwaka 2005 mpaka leo posho yao hawajapata. Ni vyema sasa askari wetu tuwapatie huduma zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nimpongeze tena Mheshimiwa Profesa Juma Othman Kapuya na Naibu wake Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa jitihada zao za kuwaenzi wanajeshi wetu kwa hali ya uwezo wao. Pia nilipongeze Jeshi letu kwa kazi zao nzuri za kulinda mipaka ya nchi yetu. Ahsante.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Kuhusu Kambi ya JKT – Mpwapwa, kijeshi Mpwapwa ina historia kubwa sana kama ukifuatilia kumbukumbu mbalimbali za Jeshi Mpwapwa ndipo palipokuwa pamependekezwa kujengwa hospitali kubwa ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hospitali ambayo baadaye ilijengwa Lugalo. Kwa msingi huu si busara kuiacha Mpwapwa ikiwa haina hata Kambi ya JKT tu.

Ombi/swali Wizara ina mipango gani ya kurudisha kambi ya JKT – Mpwapwa wakati eneo lipo, majengo japo yamebomolewa lakini yanahitaji ukarabati mdogo sana ambapo siyo sawa na kujenga kambi mpya? Wakati wa Bajeti ya mwaka jana yalitolewa mapendekezo kwamba Mpwapwa ni mojawapo ya Kambi zitakazoangaliwa kuona kama inaweza kurudishwa. Naomba maelezo.

Kuhusu wanajeshi waliopigana vita kuu ya pili ya dunia, manung'uniko ya wazee hawa yamekuwa ni ya muda mrefu na sasa kufuatia jibu la swali hili liliulizwa hapa Bungeni mwaka huu na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wazee hawa wanajua sasa kwamba fedha zao zinaliwa na wajanja wachache ambao wanajifanya ni viongozi wa wapiganaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi/swali naomba Serikali kupitia kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ieleze wazi na kwa ufasaha imelishughulikiaje jambo hili hadi sasa? Wanaohusika kula fedha za wenzao wamechukuliwa hatua gani? Na ni lini wapiganaji hawa wataanza kulipwa. Nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii wakiwemo Mkuu wa Majeshi na Makamanda wote wa Jeshi hili. Pongezi za pekee zimfikie Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa kuyaweka majeshi yake yakiwa na nidhamu ya kujituma na imara sana. Nampongeza sana.

Aidha, napongeza kila awaye yote aliyeshiriki kwa njia iwayo yote katika uandaaji wa hotuba hii. Ningependa hata hivyo nichangie katika maeneo matatu tu kama ifuatavyo:-

Kwanza makazi na haki zao wanazostahili, suala la makazi ya wanajeshi kutenganishwa na makazi ya raia ni muhimu sana. Nyumba nyingi za makazi kwa

wanajeshi zijengewe utaratibu mahususi ili uwe ni mradi unaojitegemea. Brigedia ya Ujenzi kama bado ipo ndiyo ingepewa jukumu la kujenga nyumba hizo. JKT wamefanyakazi nzuri kujenga nyumba za Mwangaza/Kisasa hapa Dodoma. Naamini wakiaminiwa, wakapewa kazi hii kwa makambi yote hapa nchini naamini hii itawezesha hata Jeshi lenyewe lijitegemee na kupata ujuzi zaidi.

Kuhusu stahili zingine, naomba sera ya Ulinzi wa Taifa iharakishwe ili wanajeshi wastaafu na wenye ulemavu waanze kupata haki halali na stahili kwa mazingira ya sasa.

Kuhusu elimu ya sekondari na ufundi nalipongeza sana Jeshi hili na Wizara hii kwa jumla kwa kutoa fursa kwa askari na familia ya elimu ya sekondari na ufundi kama ilivyofafanuliwa katika kitabu cha Bajeti. Kuna taarifa ambayo ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atolee ufafanuzi.

Katika eneo hili kuna maelezo kuwa askari wa kawaida ngazi za chini hawaruhusiwi kwenda kuchukua mafunzo ya ufundi zaidi ya *Diploma.* Kwa mfano askari aliyeajiriwa jeshini akiwa kidato cha nne na akafaulu vizuri katika kozi ya cheti *mechanical engineering* itolewayo na vyuo vya ufundi nchini na kupata *FTC,* askari huyu ameshindwa kupata kibali cha jeshi kwenda kuchukua mafunzo ya shahada ya kwanza ya *Mechanical Engineering* kwa maelezo kuwa licha ya kukubaliwa na vyuo vya elimu ya juu hawezi kujiunga na mafunzo hayo kwa kuwa cheo chake ni cha chini! Hayo kwa mujibu wa maelezo yake na wenzake wa aina hii maelezo hayo hutolewa na uongozi wa Jeshi unaohusiana na mafunzo.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri, akihitimisha mjadala huu namuomba atoe ufafanuzi wa utaratibu huu. Kwa imani na matarajio yangu kama askari huyo angeruhusiwa elimu hiyo ingekuwa ya manufaa jeshini kabla na baada ya kustaafu kwake. Kama huu ndiyo utaratibu je, hauwezi kurekebishwa? Naamini marekebisho yanaruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa vijana wa JKT, vijana wanapochukuliwa kujiunga na JKT huwa na umri wa miaka 18 hadi 22 hivi au zaidi kidogo. Baadhi yao umri wa miaka 25 huwakuta bado wako jeshini (JKT). Ajira za kujiunga na jeshi la wananchi na polisi na majeshi mengine yanahitaji vijana wenye umri wa miaka 25 tu. Kinachosikitisha vijana wanapomaliza mikataba yao JKT huwa tayari wamezidi miaka 25 na kwa kigezo cha umri hawawezi tena kujiunga na majeshi mengine kwa kuwa na umri mkubwa.

Ombi langu ni kuwa kwa maombi ya kujiunga na majeshi mengine kama Polisi, Magereza, JWTZ na kadhalika, kigezo cha umri kwa vijana wanaofikisha umri wa miaka 25 wakiwa JKT wafikiriwe kusamehewa. Kwa kuwa tayari alikuwa jeshini tayari kama ni kuenguliwa basi aenguliwe kwa vigezo vingine. Aidha, kwa vijana wanaopitia JKT kujiunga na majeshi mengine, zile kozi za awali, miezi 3 hadi 6 ya mwanzo wanagesamehewa wawe wakianzia ngazi ya juu kidogo. Kwa kijana aliyemaliza miaka miwili jeshini JKT kuingia kwenye jeshi lingine na kuwaanzishia mafunzo kama

mwingine ambaye hata kwata hajafanya ni kuidhalilisha miaka miwili ya kijana huyu ya kuwa JKT kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho langu ni kuwa makampuni yote ya Ulinzi yaajiri vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa. Waajiriwe kupitia kwa wakuu wa makambi ya JKT ya vijana hao kwa vile wao ndiyo wanawafahamu na kupitia kwa anwani za vijana hao zinajulikana kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri kuwapa kazi na kuishughulikia haraka sana mpaka sasa naendelea kushughulikia wengine, sihangaiki tena lakini nina mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa nini Jeshi linathaminiwa kipindi cha vita? Kwa sababu tangu vita imeisha sijawahi kuona Serikali kujali makazi ya wanajeshi kama ilivyokuwa mwanzoni kipindi cha vita vya Uganda na Kagera, hospitali walikuwa na ya kwao hata raia walikuwa wakitibiwa hapo.

Pili walikuwa na *Restaurant* Rwamishenye Kabora Twiga Biharamuro, je, kwa sasa Serikali haioni kuwa ni tatizo kubwa sana kwa askari waliostaafu na wale ambao wapo jeshini na wale wanaopenda kujiunga na kusikitika sana jeshini pale Twiga Biharamuro na panaitwa Makao Makuu ya Jeshi, kweli panafaa lakini panatia aibu.

Naomba nipewe majibu mazuri na lini Serikali inatakumbuka vikosi hivyo vyote vile Kagera ni sehemu mojawapo na kukumbukwa sana, sehemu ya upiganaji kambi hizo zote kuchakaa ilivyo, kwa sasa naomba nipate majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwa nini Wizara pamoja na Serikali kushirikiana na wananchi pamoja na mimi kupunguza usumbufu kwa sisi viongozi naelewa suala ni kuhusu pensheni pamoja na mirathi, wastaafu pamoja wategemezi katika Mikoa na gharama hawana na wakishafika hawajui waende wapi wenyewe wakienda Hazina wanawapiga chenga .

Naomba sana hili suala lisgughulikiwe mikoani wajue yapo wapi watangaziwe mambo yote yaishie huko, naomba Jeshi lithaminiwe sana hata huko na Mungu awabariki.

Mimi sitaunga mkono mpaka nipewe majibu mazuri ya kuridhisha na Wizara ijitahidi kujali makazi ya jeshi mkoa mzima. Ahsanteni.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza sana kwa hotuba yako nzuri na yenye ufafanuzi.

Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Nawapongeza wanajeshi wote wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi Jenerali George Waitara kwa kazi nzuri ya kulinda nchi yetu na mipaka yake. Nafahamu wanafanyakazi katika mazingira magumu ya ufinyu wa Bajeti, uhaba wa vitendea kazi na vifaa vya kisasa vya mawasiliano, hata hivyo wanajitahidi kutekeleza majukumu yao ya ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuwa katika kuendelea mafunzo ya JKT kwa vijana wetu ambapo hujifunza mambo mbalimbali ikiwemo uzalendo na Utaifa, je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuanzisha makambi ya JKT kila Wilaya likiwemo Kambi la Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma ili vijana wetu wapate mafunzo hayo na pia vijana wanaomaliza *form IV* kabla ya kujiunga na vyuo vikuu wapitie JKT ambapo watapata mafunzo ya uzalendo na Utaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo na miundombinu ya kambi ya JWTZ ya Ihumwa - Mkoani Dodoma na JKT Makutupora Dodoma pamoja na mpango gani wa kuboresha huduma mbalimbali, vitendea kazi kama vile magari, mawasiliano katika makambi hayo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha pensheni ya wanajeshi wanaostaafu na kuwalipa kwa wakati/mapema bila usumbufu wowote?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiaw Spik,a napenda kutoa shukrani zangu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari 14JK Wawi, Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa nyumba za askari wa Kikosi cha 14JK Wawi, Pemba. Naiomba Serikali izidi kupeleka fungu la fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za 14 JK Wawi - Pemba, naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kuwajengea nyumba na ukarabati wa ofisi za kikosi hiki cha 151 JK Wawi, Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya nyumba na ofisi za kikosi hiki ni mbovu sana, ni vyema askari wenu wafanye kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NSSF,* nalipongeza Shirika hili kwa kusaini mkataba wa kuwajengea nyumba askari wetu katika maeneo yao. Naiomba Serikali ishirikiane na shirika hili ili liweze kujenga nyumba za askari wa Pemba. Ahsante.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na uzima wa afya na kunipa uwezo wa kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyonayo na kufanikisha vizuri hotuba hii pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara kwa kumshauri vyema na mashirikiano mazuri na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeze Jeshi letu kwa kazi kubwa waliyonayo ya ulinzi wa nchi yetu pamoja na heshima kubwa waliyonayo ndani ya nchi na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilipongeze Jeshi la Kujenga Taifa kwa kusimamia majukumu yake kwa umahili na kwa nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika,hivi sasa nchi yetu imekabiliwa na janga la ujambazi, majambazi ambayo yanatumia silaha nzito za kivita hali ambayo inatia wasiwasi kwa wananchi na wawekezaji ambao ni sehemu mojawapo ya vyanzo vya mapato ya nchi yetu, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo pamoja na kazi kubwa waliyonayo vikosi hivi vya majeshi sasa imefika wakati kuungana na vikosi vingine vya ulinzi ili kuweka nchi hii katika hali ya utulivu pamoja na wananchi na wageni wetu. Hii hali ichukuliwe ni vita vya kuikomboa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu la Tanzania baada ya kazi za ulinzi pia hujishughulisha na mambo mengine ya uzalishaji na michezo pamoja na ujenzi wa Taifa.

Katika kazi ya ulinzi Jeshi letu limejipanga vizuri sana katika mipaka lakini katika suala la michezo Jeshi letu limerudi nyuma hasa katika mchezo wa mpira wa miguu, sijui ni sababu zipi zilizorudisha nyuma mchezo huu ambao unapendwa zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma Jeshi letu lilikuwa linaajiri vijana kwa vipaji vyao vya aina ya michezo lakini hivi sasa suala hili hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba Jeshi lirejeshe michezo kwa sababu michezo ni nidhamu na kutokana na nidhamu iliyopo katika Jeshi, Tanzania itakuwa na wachezaji wazuri wenye nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Jeshi hili lina mawasiliano mazuri na Bunge lako Tukufu na kutupa nafasi Wabunge kwenda kulenga shabaha katika Kambi ya Makutupora. Suala hili ni la kulipongeza Jeshi hili kwa namna wanavyotuelekeza na kutuhudumia bila kuchoka kwa kipindi chote tunachokuwepo katika uwanja wa shabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapokuwepo katika viwanja vya shabaha baada ya kupata mafunzo ya kulenga shabaha pia hufanya mashindano kwa makundi na badaye hupatikana mshindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mashindano hayo pia huwashirikisha askari wa kikosi hicho na safari zote tunazokwenda kuna askari wa kike *CPL* (jina sinalo) siku zote anakuwa mshindi na kwa kipindi tumemuombea aongezwe cheo ili awe *SGT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Majeshi tunaomba mlikubali ombi hili kwa kudumisha mchezo huu, pia kumpa moyo kijana wetu huyu pamoja na wengine ili waupende mchezo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Waziri Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Naibu Waziri wake Mheshimiwa OmarYussuf Mzee, pamoja na makamanda wote kwa kuisimamia Wizara na Jeshi letu lote.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuajiri askari wa JWTZ bado unalalamikiwa kuwa askari wengi ni watoto wa wakubwa kuliko vijana wa wananchi wakulima. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie wananchi watoto au vijana wao wapate.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majengo ya makambi ya kijeshi yote au mengi kazi ya kijeshi haijafikia kwa sababu wao ndiyo wanatufanya tuwe na uhuru wa nchi, tuwe tukifanya kukaa kwa raha kwa kuweka amani na utulivu nchini kwani tuna kiguguzi gani kwa kuwapatia fedha nyingi kwa usalama wa nchi yetu na kwenda na awamu ya nne kwa kuwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu basi twende na wakati kwa kambi zote hata kambi ya Welezi, Jimbo la Magogoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kambi hii ifanyiwe ujenzi wa nyumba za askari wetu za kuishi, kama bado basi uamuzi japo ukarabati wa ndani ya kambi, kuna zahanati njia za ndani zinahitaji kifusi au changarawe na vifaa vya mitambo mikuu yote iliyomo ndani ile ni kambi maalum na kama hatukufanya tuna sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanda vyeo kwa askari kwa wale askari wa miaka mingi na hawana cheo au wale walipata cheo lakini kwa miaka mingi na sifa zao nzuri. Naomba kupitia kwa Waziri na Serikali hii basi wapandishwe vyeo pamoja na wale wanaofanya kazi nzuri mipakani wanaonusuru mabaya na uharibifu usiingie ndani ya nchi yetu kwani mcheza kwao hutunzwa, wao tuna watunzaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkopo kwa askari, wapewe pia vifaa vya ujenzi na vipando/usafiri wao binafsi wakopeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Magogoni naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamanda wote na wapinagaji kwa kazi nzuri iliyotukuka kwa kutimiza wajibu wao.

Naomba nianze kwa kupendekeza yafuatayo:-

Kuhusu SUMA - JKT iboreshe kitengo chake cha ujenzi ili kiweze kushindana katika zabuni za ujenzi ambazo hutangazwa katika taasisi za Serikali, Halmashauri, Shule, Zahanati, na hata watu binafsi na pia SUMA - JKT ijitangaze ili wananchi waitambue katika fani hiyo. Hii itapunguza wingi wa udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wakandarasi binafsi kwa kutofanya/ kujenga kazi kwa ubora na kwa wakati unaotakiwa na kubwa zaidi vijana wengi watapata ajira kupitia JKT na vile vile watakuja ni vijana wenye nidhamu.

Pia JKT itafute mashamba makubwa zaidi kwa ajili ya kilimo ili kuwafunza vijana wengi washiriki katika kilimo cha kisasa kwa mazao ya biashara na kilimo. Kwa kuwa JKT ni tegemeo kubwa la kufunza na kuwajenga kimaadili vijana ili wawe raia wema na wenye moyo wa uzalendo na utafiti, ni vema Serikali ikaangalia uwezekano wa kuongezea uwezo wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo ndani ya makambi ya JKT kwa lengo la kutumia nguvu kazi za vijana kwa kuzalisha mali kama utengenezaji wa viatu vya ngozi za wanyama wa hapa nchini, nguo na kuziuza nje ya nchi. Nchi kama China mara nyingi huwatumia wanajeshi na wafungwa kuzalisha mali viwandani, maana wanajeshi hufanya kazi kwa nidhamu bila kutegemeana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kikosi cha utoaji wa huduma cha Morogoro, nashauri kiboreshwe kwa kufanyiwa matengenezo ya bwalo, *operation* katika kikosi hicho zifanyike mara kwa mara ili kujiweka tayari kama jeshi linavyotakiwa kuwa, fedha za mafuta ziongezwe katika kikosi hiki cha huduma na kikosi kipatiwe magari ya kutosha kwa jaili ya mazoezi ya kijeshil

Mwisho naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wa jeshi wanapaswa kuwepo katika makambi yao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na sio kuishi uraiani kama inavyoonekana hivi sasa jambo ambalo linapunguza nidhamu ya jeshi hilo. Pia wajengewe nyumba zinazokidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uajiri wa askari jeshi unapaswa kutekelezwa kwa vijana wa pande zote mbili za nchi yetu ya Bara na Zanzibar. Utaratibu wa kutoka vijana Tanzania Bara kuja kujaza nafasi za Zanzibar (Unguja na Pemba) kunawanyima nafasi vijana wa Zanzibar kujiunga na jeshi kama inavyostahili. Ni vyema hali hii ikaangaliwa ili isije ikatokea kuwa jeshi hilo ni la upande mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu la jeshi ni ulinzi na usalama wa nchi, ni vyema jeshi hilo kupatiwa vitendea kazi vilivyo bora na vya kisasa ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho za askari jeshi wastaafu yaboreshwe na yatolewe kwa wakati unaofaa ili kuondoa usumbufu wa maisha unaowakabili askari hao baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uzito wa majukumu yao ni vyema askari hawa wakaboreshewa maslahi yao mara kwa mara kadri hali itakavyoruhusu.

Suala la kupatiwa chakula bora na mavazi bora ni muhimu sana kwa askari jeshi pamoja na kuangaliwa afya zao.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara hii muhimu kwa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kupongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri wanayofanya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha usalama wa mipaka yetu. Naipongeza kazi nzuri inayofanywa na wafanyakazi wa Hospitali ya Jeshi ya Lugalo. Hospitali hii inafanya kazi nzuri ya mfano wa kuigwa katika kuhudumia wagonjwa, hivyo naomba hospitali hii ipanuliwe na kupewa vifaa vya kisasa zaidi ili iendelee kutoa huduma bora zaidi. Hongera sana maafisa wote na watendaji Hospitali ya Lugalo. Wizara iangalie uwezekano wa kuwapa motisha kwa wafanyakazi wa hospitali wakiwemo madaktari, wauguzi kama wanavyopata wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya umma, ili kuweza kujenga nyumba za walimu na shule za umma huko vijijini, nashauri Serikali iwatumie wanajeshi katika kusaidia vijiji vya jirani na kambi hizi kuwa na shule zenye ubora unaostahili, zoezi hili lishirikishe JKT pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isaidie wajane ambao waume zao wamefariki wakiwa kazini. Naomba Serikali pia ichukue jukumu la kuwasomesha yatima badala ya hawa wajane kupata mafao na kuachwa, pia kuwasaidia kupata kipato cha kuendelea kuhudumia familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za askari, nashauri ujenzi wa nyumba za askari ufanyike haraka ili askari wote wawe kambini au katika nyumba zilizojengwa na jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa nyumba za wanajeshi wa kada ya kawaida, nyumba za wafanyakazi hawa zina hali mbaya sana, hazifanyiwi ukarabati kwa mfano nyumba kama zile za Kigamboni na kadhalika. Nyumba zifanyiwe ukarabati ili ziendane na kazi nzuri ya kutulinda sisi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI elimu iendelee kutolewa kwa familia za wanajeshi. Mwisho kabisa naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapa pole wafiwa wote ndani na nje ya Bunge. Pia niwapongeze wale wote waliopiga hatua mbalimbali za kimaendeleo katika nyanja mbalimbali.

Napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hotuba nzuri iliyosomwa mbele yetu leo hii. Kutokana na hivyo napenda niunge mkono asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwenye hotuba hii nitapenda kuelezea katika maeneo machache kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza, ni kuhusu ulinzi mipakani, hali ya usalama wa nchi kwa ujumla wake si mbaya, ni nzuri, hata hivyo wimbi la ujambazi unaoendelea nchini kwa kiasi kikubwa unachangiwa na uingiaji wa wageni mipakani mwetu hasa kutoka katika nchi zenye migogoro ya kisiasa na wengi huingia na silaha. Wizara ya Ulinzi isaidie katika kuimarisha ulinzi mipakani hasa udhibiti wa wageni waingiao na silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu mafunzo na zana za kisasa, Wizara ihakikishe kwamba jeshi letu liko katika hali ya utayari kwani hatujui ni yupi kati ya majirani zetu anaweza kutubadilikia. Jeshi lipewe mafunzo na pia lipatiwe zana za kisasa, tunajua silaha ni ghali lakini upatikanaji wake utasaidia kuimarisha hali ya usalama tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma, tunaomba askari wote, maofisa na askari wengineo *(NCO's etc)* wapewe huduma zinazostahili ili kuwaweka katika hali tahadhali na utayari. Lakini wakati huu wa amani, basi askari wetu hasa wahandisi wa medani *(Field Engineers)* watumike katika kusaidia ujenzi wa huduma za muhimu kama madaraja na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu askari wastaafu, Wizara isaidie kuandaa mazingira ambapo askari waliostaafu wanaweza kujitegemea katika kujiendesha kimaisha kuliko hali ya sasa ambayo tunaona baadhi ya askari wastaafu hasa waliokuwa maafisa wakiwa katika hali zenye kudhalilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu walemavu na majeruhi wa vita, katika mkutano wa Novemba, 2006 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kutoa tamko la Serikali kuhusiana na askari waliojeruhiwa na waliopata ulemavu wakati wa vita vya Kagera. Mpaka sasa tamko hili halijatolewa, tamko hili liliahidiwa kutolewa katika mkutano huu unaoendelea. Wizara inategemea kulitoa lini hilo tamko? Askari wahusika ni wachache sana kwa nchi nzima lakini iwapo watashughulikiwa hii itasaidia kujenga morali miongoni mwa askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba hoja hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi kuipongeza Wizara na watumishi wake wote kwa kuandaa taarifa na Bajeti nzuri ya Wizara. Baada ya pongezi hizo napenda kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pongezi kwa jeshi la wananchi, napenda kutoa pongezi za jumla kwa viongozi na wapiganaji wote kwa kazi nzuri inayofanywa na jeshi hilo. Jeshi hili limekuwa mfano mzuri wa kufanya kazi hasa wakati wa maafa kama vile mafuriko ambayo huharibu miundombinu kama vile madaraja na kadhalika na jeshi hili hurejesha mawasiliano katika muda mfupi sana. Ili jeshi hili liweze kufanya kazi zake vizuri nashauri jeshi lipatiwe vifaa zaidi vya kazi vitakavyolisaidia kukabiliana na maafa na dharura kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kasoro ndogo ndogo, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na jeshi hili bado kumekuwa na kasoro ndogo ndogo kwa mfano baadhi ya askari wake kujihusisha na vurugu/fujo na kupiga raia, hali hii huharibu sifa nzuri ya jeshi hili. Ni kweli inawezekana raia ndiyo wanakuwa wakosaji, lakini hii haisababishi askari hawa kujichukulia sheria mkononi. Nashauri hili lirekebishwe ili jina la jeshi letu liendelee kuwa zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jeshi la kujenga Taifa, napenda pia kulipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kwa jinsi linavyofanya kazi zake vizuri hasa zile za ujenzi kupitia shirika lake la SUMA JKT. Hata hivyo napenda kushauri yafuatayo, kwanza, SUMA JKT iajiri wataalamu wa kutosha na wenye sifa watakaolifanya shirika hilo lifanye kazi zake kwa ufanisi vizuri zaidi. Aidha, nashauri SUMA JKT inunue vifaa vya kutosha vitakavyolifanya shirika lifanye kazi zake kwa wepesi na uharaka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shamba la Itaka linalomilikiwa na JKT Itende, Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Itende Mbeya ina *detach* ya kilimo kule Itaka Mbozi. Shamba la Itaka hutumika zaidi kwa shughuli za kilimo cha mahindi na shamba lina ukubwa unaokadiriwa kufikia ekari 400 hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba hili kwa sehemu kubwa sana halilimwi lote, pengine kwa sababu ya uwezo mdogo wa jeshi lenyewe au kwa sababu nyinginezo. Pamoja kwamba shamba hilo halilimwi lote bado kuna ugomvi wa mpaka wa shamba hilo pamoja na vijiji jirani vinavyozunguka shamba hilo yaani vijiji vya Halungu, Insani na Itaka. Ugomvi huo uliwahi kusababisha Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na JKT, awamu ya tatu, kutembelea eneo hilo ili kutatua tatizo hilo. Hata hivyo hadi leo bado ugomvi wa mipaka katika eneo hilo upo vile vile haujatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Wizara Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhakikisha kwamba ugomvi huo unamalizika. Kuendelea kwa ugomvi huo kunawafanya wananchi wengi kutoelewa hatma ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga hoja mkono iwapo tu nitapewa maelezo ya kutosha kuhusu mgogoro wa mipaka wa shamba la Itaka linalomilikiwa na JKT Itende. Ahsante sana.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Asalaam Aleykum,* nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu

Waziri wake kwa kazi wanayoifanya pamoja na kwamba kwa macho au kila siku hatuoni mnafanya nini lakini zinapotokea rabsha hakika tunaona kazi kubwa unayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi nikushukuru kupitia ofisi ya mgambo Mkoa wa Tanga, tuliweza kutoa mafunzo ya mgambo kwa vijana/watu wazima 10. Aidha, niwashukuru kwa kupatiwa kamanda wa mgambo ndani ya Wilaya japokuwa baada ya kazi na pengine wakati hana shughuli hulewa sana, lakini angalau tumekumbukwa. Suala langu ni kwamba baada ya mafunzo ya mgambo kule Monduli wahitimu hao wamejikuta hawana shughuli hivyo kuwa ni kero kupata elimu na mwisho wake kutoona mafanikio ya masomo hayo. Je, Waziri atakubaliana na mimi pamoja na mafunzo ya mgambo, watu hao wapewe mafunzo ya ujasiriamali ili pindi wanapomaliza wapatiwe mikopo, waanze kujitegemea kiuchumi na huku likiwa ni jeshi ambalo linasubiri suala la ukosefu wa amani waweze kuitwa. Hebu naomba uliangalie kwa jicho la umakini, naomba mawazo yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yako umeonyesha jinsi ambavyo mnawahudumia wanajeshi na watumishi wa umma kwa kuwalipa kwa masuala binafsi. Naomba nirejee tatizo ambalo niliwahi kukuletea kwa maandishi. Kuna dada anaitwa Faith-Lucy Matumbo, amepangisha nyumba yake kwa mwanajeshi Kanali Shinyambala kwa muda mrefu kule Ukonga, Dar es Salaam, lakini kwa miaka miwili sasa hajalipwa kodi ya nyumba yaani mwaka 2005 na mwaka 2006, kodi hadi leo ni hiyo hiyo shilingi100,000/= kwa mwezi. Kwa kuwa huyu mama ni mzazi pekee na kodi hiyo ndiyo anayotegemea kusomesha watoto wake na maisha ya kila siku naomba ofisi yako ijitahidi kumlipa mapema. Simu yake ni namba 0754 295920, naomba huruma yako ili niendelee na kusaidia wengine nikiamini mmemshughulikia kwani anaendelea kutoa huduma hiyo.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba nzuri sana aliyoitoa leo asubuhi katika Bunge lako Tukufu. Baada ya kusikiliza kwa makini naunga mkono hoja hii na ninayo matumaini kuwa azma ya Wizara na Serikali kwa ujumla ya kuwa na Jeshi dogo la kisasa lililo madhubuti na lenye uwezo na ufanisi mkubwa katika utendaji wa kivita inaonekana wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza mambo matatu, moja suala la kupeleka askari wetu kwenye majukumu ya kulinda amani *(peace keeping missions)* lipewe kipaumbele. Kwa faida kubwa sana na ni vema tutumie nafasi hiyo, napongeza sana hatua ya kupeleka vijana wetu nje na naomba tuendelee.

Pili, kuhusu michezo, tunaomba suala la michezo Jeshini lipewe kipaumbele kama inawezekana, kuwe na makambi maalumu kwa ajili ya michezo tu ya aina mbalimbali. Zamani, Jeshi lilikuwa linatoa wachezaji wazuri sana. Ninaamini tukifanya hivyo, tutapata mahali ambapo makocha wetu watachagua wachezaji bora. Narudia, vijana wenye vipaji vya michezo, wawe *re-recruited* jeshini na wapelekwe kwenye kambi maalumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Jimbo langu la Mtama linalo eneo zuri sana ambalo linafaa kwa Kambi ya JKT la kilimo. Eneo hilo lina bonde zuri sana na kuna majengo ambayo Shirika moja la nje liliyajenga na wakayaacha.

Naomba wahusika kwenye Jeshi letu la kujenga Taifa nikutane nao ili wafike kwenye eneo husika na kufanya tathmini ya iwapo mazingira yanaruhusu eneo hilo kutumika kama Kambi ya Jeshi. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pili, naipongeza hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yenye mpangilio wenye kueleweka na ufanisi. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo kama walivyozungumza wengi nami pia nasisitiza maslahi ya wanajeshi wetu yaongezwe yakiwemo malazi, makazi na kadhalika. Pia sehemu za mipaka yetu kunahitajika kuboreshwa zaidi vituo na vifaa ili kuwe na ulinzi imara zaidi na madhubuti kwani huwa tunashangaa tunaposikia watu wanapenya mpaka na kufika katikati ya Mikoa

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu JKT lizidi kuimarishwa kwani limetoa mchango mkubwa zaidi katika Taifa letu toka kuanzishwa na wote waliopitia hapo ni watu ambao wako wakakamavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena naunga mkono hoja hii na ninaitakia Wizara kazi njema.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza kazi nzuri ya Wizara hii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Iringa unalo eneo la JKT Mafinga. Serikali ina mpango gani wa kuboresha kituo hichkatika sekta ya ujenzi, useremala, *engineering* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, JKT Mafinga kwa muda mrefu imeachwa, ni muhimu sana vituo hivi nchini vikatunzwa, je, Serikali imeweka mikakati gani juu ya JKT nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulinzi, Wizara hii inafanya kazi zake kwa siri bila kutoa siri, *which is good*. Lakini hatujaona kesi Mahakamani juu ya masuala ya ulinzi mfano, *Intruders, Money Laundering*, *Terrorist Act,* tungependa kuona moto (kasi) ya Wizara hii. *Tangible Acts* za Wizara ya Ulinzi. Je, Wizara hii imefungua kesi ngapi za ulinzi majini, ulinzi katika anga na mipakani? Pia Wizara hii ambayo ipo *very centralised* ngazi ya Taifa ina mpango gani wa kuwashirikisha *local people* mfano wananchi wa vijiji vya Ludewa na Makete maana hawana ofisi ngazi ya Kata, je, Serikali ina mpango gani wa kufanya hizo shughuli katika *local authorities?*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo na baada ya kupata ufafanuzi wa hoja zilizotajwa hapo juu ndiyo nitaunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Katibu Mkuu, Bwana Abel Mwaisumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeza Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania kwa namna linavyofanya kazi ya ulinzi na shughuli zote za Jeshi la Kujenga Taifa, nawapongeza Makamanda na wapiganaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao ushauri mchache kwa mafanikio ya Wizara hii kwa shughuli zake kwa kipindi cha mwaka 2007/2008. Jeshi la Kujenga Taifa linafanya kazi nzuri sana ikiwa ni pamoja na kazi mbalimbali za kiufundi na kadhalika. Naomba Jeshi hili lijihusishe zaidi kufanya kazi za kuliongezea pato Jeshi ikiwa ni pamoja na kuomba zabuni mbalimbali kama za ujenzi na zile za kutengeneza barabara na kadhalika kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa liendelee na utaratibu wake wa kuchukua vijana wa kujitolea kutoka vijijini kwa utaratibu ule ule wa kudhaminiwa na vijiji vyao, hii itajenga vijana na itasaidia kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Wananchi, nashauri wapiganaji wote wajengewe nyumba makambini na sio kujibanza mitaani kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, marupurupu na maslahi mengine yatolewe kwa wapiganaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja iliyowasilishwa na kwamba nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao.

Hata hivyo, ningeomba Wizara izingatie yafuatayo yanayotendwa katika Jimbo langu. Askari wa JWTZ waliopo kwenye *detach* za Karago, Kirando (Lubengela) na Sigunga na Rukoma wamekuwa wanalalamikiwa kutoza au kudai fedha kwa matumizi yao ya chakula na mahitaji mengine. Wananchi wanapohoji wanaelezwa kuwa wao wapo pale kuwalinda, hivyo ni wajibu wao wapewe mahitaji na wananchi hao.

Katika *detach* za Sigunga na Rukoma wamekuwa wanachangishwa lita tano za petroli kwa kila mtumbwi kwa ajili ya doria, kuchangia doria siyo jambo baya, lakini lita tano kwa kila mvuvi maana wavuvi wapo zaidi 100 kila kijiji ni mafuta ambayo hayawezi kutumika kila siku. Kuna haja ya kuwepo na mwongozo mzuri wa kuchangia ukawa wa wazi na shirikishi ili kusiwepo manung'uniko. Ushauri wangu ni Serikali na wananchi washirikishwe kiulinzi kwa hali ambayo kila upande utachangia kwa uwazi na haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naipongeza JKT kwa juhudi walizozionyesha katika kufanikisha elimu Kigoma. Mkakati wa uejnzi wa Sekondari za Kata katika Jimbo la Kigoma Kusini umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na Kikosi cha Ujenzi cha JKT, kiimarishwe kimafunzo ili kiwe ni kikosi cha kiuchumi na kuweza kuzalisha kitaalamu, JKT ikiwezeshwa kivifaa na kitaalamu inaweza kuwa kitega uchumi katika fani ya ujenzi.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamanda, Maafisa na watalaamu na watumishi wote wa Wizara, Majeshi na Asasi zilizo chini ya Wizara hii kwa hotuba nzuri sana na kwa kazi nzuri na mahiri ya kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nina maoni yangu kwamba Jeshi la Kujenga Taifa sio tu muhimu bali lina nafasi kubwa sana ya kujenga uzalendo, ukakamavu, mafunzo ya stadi mbalimbali, ulinzi na shughuli nyingine muhimu za ujenzi wa Taifa. Hivyo kuna umuhimu mkubwa sana wa kulipanua na kuliboresha Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Jeshi la Kujenga Taifa lina nafasi nzuri sana ya kuchangia katika kuongeza na kuboresha kilimo kwa faida ya JKT yenyewe na Taifa kwa ujumla. Nyingi ya Kambi za JKT zina maeneo makubwa sana ya ardhi yenye rutuba safi. Nina hakika wakipatiwa vifaa vya kisasa vya kutosha wataweza kuleta mapinduzi makubwa ya kilimo, kuongeza sana mazao na kuwa mfano wa shamba la darasa kwa wananchi wa jirani.

Mheshimiwa Spika, nne, JKT vile vile inayo nafasi kubwa ya kuendeleza mafunzo ya stadi mbalimbali na hivyo kuongeza kujitegemea kwa wananchi wetu. Naiomba Wizara ifanye mipango na mikakati maalumu ya kupanua na kuendeleza shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, zaidi ya hayo ya juu SUMA JKT ina nafasi nzuri ya kupanua shughuli zake katika ujenzi wa majengo na miundombinu mbalimbali ili mradi SUMA JKT inapatiwa vifaa na vitendea kazi vya kisasa na vya kutosha. Kubwa zaidi ipo haja ya kujengea SUMA JKT nidhamu na uhodari wa kuongeza tija na kuwa na kasi bora ya utekelezaji. Nasikitika kwamba ujenzi wa Boma na Nyumba za viongozi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, Kasera umekuwa ukisuasua ingawa kasi yao inaongezeka wanapopata msukumo kutoka juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Kambi ya JKT Maramba iliyopo Wilayani Mkinga inahitaji vifaa na majengo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, ipo haja ya kurudisha mkakati wa kujiunga na JKT kwa lazima haraka iwezekanavyo,

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, ipo haja ya kuongeza mafunzo ya mgambo hasa katika Wilaya za mipakani kama Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kuitakia Wizara utekelezaji mwema.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Amiri Jeshi Mkuu, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Jeshi zima kwa kazi nzuri sana. Naunga mkono hoja. Nina ushauri ufuatao:-

Kuhusu mgambo, uzoefu umeonyesha kwamba mgambo wamekuwa msaada mkubwa katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao vijijini ambako kwa sehemu kubwa hakuna vituo vya polisi wala polisi. Raia na mgambo hufundishwa na Jeshi lakini wakufunzi hawatoshi. Mgambo watano kila kijiji Tanzania nzima. Naunga mkono hoja.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutamka moja kwa moja kuwa naiunga mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina moja tu la kuchangia katika Wizara hii. Kambi ya JWTZ pale Nachingwea imekuwa na tabia ya kujitanua *physically*. Kujitanua huku kumesababisha mgogoro wa ardhi baina ya Jeshi na Wananchi wa Kijiji cha Kilimani hewa. Wapo wananchi wasiopungua 65 ambao wameniletea malalamiko ya ardhi yao kuchukuliwa na Jeshi bila kulipwa fidia. Jambo hili nilimkabidhi Mheshimiwa Waziri, lakini nasikitika kuwa hadi leo hii hapana hatua yoyote iliyochukuliwa. Tatizo hili ni kubwa na nyeti na ni vyema kuwa Waziri alichukulie kwa uzito ule ule ambao utasaidia kuondosha migogoro baina ya wananchi na Jeshi letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea Mheshimiwa Waziri atazungumzia tatizo hili na kuwapa moyo wananchi wa Nachingwea kuwa watalipwa fidia yao hivi karibuni. Wananchi hawana upinzani kuruhusu Jeshi kuchukua ardhi yao bali ni haki yao ya fidia ndiyo wanayelalamikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga tena mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara hiyo katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la watu waliopigana vita ya pili kutokulipwa malipo yao. Kwa muda mrefu watu wa aina hiyo sasa wapo ambao wameshapoteza maisha yao bila ya kufaidi malipo hayo. Wakati Waziri wa Ulinzi akijibu swali langu humu Bungeni, alikubali kuwa ni kweli Jeshi la Uingereza linalipa fedha hizo kwa Serikali ya Tanzania ili wapiganaji hao walipwe. Wadai hao ambao wapo nchi nzima wanazo taarifa hizo na wanailalamikia Serikali kuhusu malipo yao. Waziri anaeleza nini kuhusu hilo? Hatua za kuchukua ni zipi kwa wale ambao wamekuwa wakila fedha hizo na pia Waziri aeleze ni lini watu hao ambao sasa

wamekuwa ni wazee watalipwa? Hili lipewe kipaumbele kwa sababu kila viongozi wa Kitaifa wanaposafiri Mikoani na Wilayani hoja hiyo kutolewa kwa mtindo wa madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya huduma mbovu kwa baadhi ya *detach* zilizoko nje kwa kutokuwa na mahema ya kulala badala ya nyumba. Kutokuwa na mahema hayo, Wanajeshi wanajikuta wakiishi uraiani na wengine wasio waaminifu kupata vishawishi vya maisha tofauti na maadili ya mpiganaji. Vishawishi vinaweza kuwa kama vile ulevi, wizi kwa kutumia silaha walizonazo na vitendo vya umalaya. Mfano hai wa wapiganaji wenye tatizo la makazi ni askari walioko katika Mkoa wa Kigoma na hasa wale wanaolinda mpaka kama vile Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya vyombo vya usafiri na ujenzi kwa wanajeshi wetu ni hamasa mojawapo ambayo mpiganaji akipata anajiona ni sehemu ya raia mwema. Utaratibu huo ulifanyika miaka ya nyuma kwa askari kukopeshwa vyombo vya usafiri kwa kuzingatia ngazi *(rank).* Kwa kuwa sasa vyombo hivyo vimeshachakaa, nashauri kwa makusudi mazima Serikali iweke utaratibu mwingine wa kuwahamasisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwaacha askari kuendelea kuishi nje ya vikosi ni kitendo ambacho kimekuwa kikiliaibisha Jeshi hasa katika matukio ya ujambazi kama mifano hai ambayo imeshajitokeza. Naiomba Serikali kuliwekea mikakati ya makusudi ili kuhakikisha wapiganaji wote wanakaa kwenye vikosi. Kufanyika kwa hili ni lazima zitengwe fedha kwa ajili ya kujenga mahanga na nyumba kwa ajili ya askari waliooa ama kuolewa, iwe ni sheria ya askari kutokuishi nje ya kikosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya nyuma yalikuwepo mabasi mengi ya JW kwa ajili ya kuwabeba wapiganaji kwenda kazini na kurudi kutoka kazini. Hili lipewe kipaumbele ama kwa kununua magari (mabasi) ama kuwarudisha waishi vikosini. Mpiganaji atakuwa askari mzuri kutokana na huduma nzuri anayopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Naibu Waziri wake. Hali kadhalika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Katibu Mkuu na viongozi wakuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Jenerali George Waitara (Mkuu wa Majeshi), Mkuu wa JKT na viongozi wakuu wa JWTZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka kuchangia ni suala la makazi ya majeshi. Hili ni muhimu lizingatiwe sana kwani majeshi yanastahili kuwa na Kambi yenye majengo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kuchangia ni jinsi vijana wa JKT wanavyochaguliwa. Serikali imeweka nia njema kabisa kwamba JKT iwe na

mchanganyiko wa watu kutoka kila Wilaya. Kinachosikitisha ni kwamba wenye madaraka ya kusaili vijana hawa hawazingatii sera hii bali huitana na kupendeleana katika kupeana nafasi hizo. Wizara lazima iliangalie sana jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana ni kuangalia uwezo wa Jeshi katika nyanja ya ukandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, JWTZ limedhihirisha uwezo wake wa kutumia uwezo wao huu kuhudumia umma katika nyanja mbalimbali. JWTZ ni Jeshi ambalo lina wataalamu wa aina kwa aina; kwa mfano wapo mainjinia, wajenzi na kadhalika. Kwa kuwa Jeshi hili limedhihirisha kwamba lina uwezo wa kujenga nyumba, madaraja na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa amani tulitumie Jeshi letu kwa manufaa makubwa sana. Hivi sasa kumetolewa fedha za ujenzi wa nyumba za walimu na madarasa, Jeshi wangeweza kupewa kandarasi ya nyumba hizi. Madaraja na barabara zote za Wilaya zingeweza kutengenezwa na Jeshi kwani uwezo huo wanao. Hii itapunguza wizi wa fedha hizo huko Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya malipo ya wastaafu na walemavu imechelewa na kwa kuwa sasa imekumbukwa ni vema ikaharakishwa ili maslahi ya askari hao yatimizwe haraka. Naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja ya Wizara hii mkono kwa asilimia mia moja. Hii ni Wizara nyeti na ni uti wa mgongo wa nchi yoyote ile duniani. Utulivu wa nchi katika mipaka na kwa jamii kwa jumla inategemea sana umadhubuti wa Jeshi katika nchi.

Maoni yangu ni kuwa tujitahidi kulijenga Jeshi letu hili wakati wa utulivu kama huu tuliona au kwa lugha nyingine tutoe jasho jingi wakati wa amani ili tumwage damu chache wakati wa vita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeshuhudia vita au mapambano si chini ya matatu, lakini ninayokumbuka ya haraka haraka ni pambano baina ya Malawi, Tanzania, Ziwa Nyasa na kadhalika vile pambano baina ya Tanzania na Uganda haya yalikuwa ni ya wazi kila mmoja wetu anayatambua ukiacha yaliyojificha ambayo huzuka mipakani mwetu. Kama nchi tujiulize tunajipanga vipi? Hivi sasa tunashuhudia machafuko/mapigano kwenye mpaka baina ya Kenya na Uganda. Sisi Tanzania tunajifunza nini na tunajipanga vipi. Tunasikia kwanza vyombo vya habari kwa nchi jirani miaka ya hivi karibuni inaongeza Bajeti yake ya ulinzi maradufu (sisi tunajipanga vipi). Haya sio mambo ya kuyachukulia juu juu au kwa wepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ununuzi wa silaha ni uimarishaji wa jeshi kwa nchi jirani na mapigano yanayotokea mipakani kuna funzo kubwa la kutoamini moja kwa moja. Lazima kujitayarisha na tujiandae. Nchi yetu imezungukwa na mito kwa eneo kubwa na bahari hatuna boti za ulinzi za kutosha. Ushauri wangu ni kuwa tuimarishe Jeshi la majini kwa vifaa vya aina yote kuanzia vyombo vya mawasiliano na hata

manuari za vita, ni wakati sasa muafaka kwa jeshi la majini liwe moja baina ya Tanzania Bara mengine visiwani KMKM. Pia JKT na JKU viunganishwe viwe chini ya Serikali moja ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sio sahihi kwa mawazo yangu JKT kuwa sio Jeshi la Muungano na kuwa ni chombo cha Tanzania Bara peke yake kuunganishawa kwa chombo hiki kitaleta siri halisi ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulipongeza Jeshi kwa kujenga Hospitali mwanana na safi kabisa ya Bububu, Zanzibar tunashauri wasaa ukipatikana pajengwe Hospitali kama ile Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za makazi/jeshi tunaliomba Jeshi kimaadili na hata kutokana na mazingira ya kazi zao. Wizara ifanye kila njia kuboresha makazi ya wanajeshi kwa kuwajengea nyumba na wabaki makambini mwao badala ya kubaki uraiani. Uraiani kuna vishawishi vingi tu na kuna hatari ya hata upotevu wa silaha na risasi. Kutokana na wanajeshi kubaki uraiani, pia majengo yaliyopo sasa yaani kambini yanahitaji ukarabati mkubwa sana hasa kambi ya za Bavuwai, Mtoni, Chukwani na Mwanyanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba hazina vyoo na hata mazingira yao hayaridhishi, zaidi ni kwamba kwenye Kambi hizo unaweza kuingia na kutoka kama uko marikiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri wafanye ziara wazingatie kambi kipo na watayathibitisha haya ninayosema, lakini kubwa zaidi Kambi hizi hazina *fence* zinazotenganisha maeneo yao na maeneo ya raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nawaombeeni mafanikio mema katika kupitisha Bajeti hii.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa vijana wetu wa Jeshi la Wananchi waliishafikia hatua kubwa katika uhandisi na hata kuunda gari la kwanza la Kitanzania jambo ambalo licha ya sababu za kiuchumi tu lina manufaa makubwa katika kuuza jina letu (Taifa) na kwa kuwa kampuni ya *Meremeta Ltd.* ilianzishwa mahususi kwa lengo la kusaidia shughuli za kikosi na uundwaji wa nyumbu je, ni kitu gani hasa kinaendelea katika karakana za Nyumbu na hasa uzalishaji wa magari? Hii ni kwa sababu magari ya Nyumbu hayaonekani tena mitaani na Serikali haijawahi kutoa taarifa rasmi kuhusu utengenezaji huo wa magari kwa manufaa ya jeshi letu na hata kwa matumizi ya kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa kamili kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile lengo la kampuni ya Meremeta iliyoundwa na kukabidhiwa mgodi wa dhahabu wa Buhemba ambayo yote kampuni na mgodi ilimilikiwa na bado unamilikiwa na jeshi letu la wananchi, tangu shughuli za kampuni ya

Meremeta zilipoanza hadi leo ni fedha kiasi gani zimepokelewa na kikosi chetu cha Nyumbu kama ilivyokubaliwa na kukusudiwa toka awali?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wazee wastaafu wa vita vya pili ya dunia na fedha zao zilizotolewa na wenzao wa Uingereza bado halijapata muafaka. Wazee wengi wameanza kukata tamaa na wengine wengi pia wamefariki bila kupata fedha zao sasa je, suala hilo limefikia hatua gani baada ya Serikali kuahidi kuwa inalifuata mwaka juzi na hata mwaka jana? Ni kwa nini wazee wetu hao kwa vile walijitolea uhai wao na nafsi zao kupigania haki na Uhuru ambao leo sisi sote tunafurahia, isichukue jukumu la kuwafidia fedha hizo zilizopotea na Serikali ichukue sasa jukumu la kuwadai waliodhulumu au kutumia vibaya fedha hizo na ikawa lazima kuwafilisi mali zao ili kuzirejesha fedha hizo zilizopotea?

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za hivi karibuni kumekuwa na taarifa zenye utata kwenye vyombo vya habari kuhusu manunuzi ya helikopta kwa matumizi ya jeshi letu. Je, nani hasa alipewa zabuni ya kununua hizo helikopta na mktaba uliwekwa saini tarehe gani/ipi ya mwaka gani? Utaratibu wa kumtafuta *tenderer* ulikuwa upi na ni makampuni mangapi yaliyoomba zabuni hiyo na mchakato wa kumpata mshindi ulikuwaje? Helikopta zilikuwa ngapi, zinanunuliwa/au zimenunuliwa toka kampuni gani, ya nchi gani kwa kiasi gani kwa kila helikopta?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili linastahili kupewa taarifa kamili katika swali hili ili tusiliiingize Taifa letu katika gharama kubwa ambapo bila sababu za msingi leo Watanzania wanatakiwa kulipa zaidi ya shilingi bilioni 60 kutokana na zabuni ya manunuzi ya vifaa vya kijeshi wakati wa vita vya Idi Amin toka kwa kampuni ya Bwana Nolan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa nitapata majibu ya kina naomba kuwasilisha.

**MHE. PAUL KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitangulize pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Katibu Mkuu wake Ndugu Abel Mwaisumo wakisaidiana na watendaji wakuu wa Wizara hii. Naunga mkono hoja hii ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii Mheshimiwa Waziri amejumuisha taarifa kuhusu askari wetu walioshiriki katika kulinda amani katika nchi ya Lebanon, je, anaweza kuelezea kwa kifupi hali ya usalama wao na utaratibu mzima wa bima ya maisha yao? Ninaendelea kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi hizo. Lakini je, Waziri haoni kupeleka askari Waafrika kwenye nchi za wazungu kunaweza kuwafanya ni *target* ya kuangamizwa kama wabaguzi wa rangi wakiamua kutekeleza azma hiyo mbaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara imefanya nini kuendeleza azma yao katika kuendeleza tafiti za uzalishaji wa bidhaa za kijeshi hasa kwa vikosi vya SUMA na Nyumbu. Kwa suala la kikosi cha Nyumbu, naelewa Serikali ya Ireland ilikuwa mstari

wa mbele kukisaidia kituo hiki. Nini kimetokea hali hiyo ikabadilika na kwa nini tusiendelee kuwaomba watekeleze azma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti nashauri Serikai iweke kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza kuwa na jeshi dogo lenye vifaa na zana za kisasa na wanajeshi wenye kulelewa vizuri kimaslahi. Bado posho ya chakula ni ndogo sana; bado kuna umuhimu wa kuangalia upya umri wa kustaafu; bado suala la muda wa kuoa au kuolewa liangaliwe katika mazingira haya ya magonjwa ya UKIMWI na bado ujenzi wa makazi kwa wapiganaji upewe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka yetu mingi bado haijakuwa na ulinzi wa kutosha na mipaka yake kuingiliwa kila mara na wananchi wa upande wa pili wa nchi kama inavyotokea katika mpaka wetu na Uganda sehemu ya Kakunyu. Tusikubali mipaka hii ikawa chanzo cha machafuko. Tuandae pia vikosi vya kutosha katika mipaka pembeni mwa ziara Tanganyika. Tatizo la *DRC* lisipuuzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie pia nafasi hii kumpongeza Jenerali George Waitara na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Abraham Shimbu. Kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao kwa misingi bora ya kijeshi na kusaidia nchi hii iendelee kuishi kwa utulivu na amani. Pia la msingi ni jinsi jeshi hili lilivyoamua kusaidiana na jeshi la polisi katika kupambana na uhalifu ndani ya nchi. Naiomba Serikali iendelee kuwashirikisha katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hii, maana matukio ya uhalifu yanaonekana kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja timu yake yote kwa Bajeti yao nzuri iliyo na mwelekeo kwa kuleta mabadiliko na kuimarisha jeshi letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii, Wizara hii ni Wizara nyeti katika nchi yetu lakini wanajeshi wanapata matatizo makubwa kwenye utendaji wao wa kazi kutokana na kukosa mahitaji ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari hao wanafanya kazi katika mazingira magumu hawana nyumba za kuishi, wanajeshi wengi wanaishi uraiani kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwajengee nyumba za kutosha, vifaa vya kutendea kazi, waongezwe maslahi yao yaani yaboreshwe na vile vile wanapostaafu wapewe mafao yao bila ya kupata matatizo kwa sababu wastaafu hawapati mafao kwa muda unaotakiwa anadai mpaka atakufa

hapati kwa hiyo, Serikali tunaiomba iwatendee haki majeshi hawa kuongezwa posho angalau fedha za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI ni tatizo kubwa katika Taifa letu wanajeshi wanapewa muda wa miaka mitano bila kuoa au kuolewa hii Serikali iangalie upya sheria hii ili waipuke na vishawishi wa kufanya ngono kiholela na kuwapelekea kuathirika. Kwa hiyo, kijana anapoajiriwa apunguziwe mtihani huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza wanajeshi kwa kujiunga na michezo mbalimbali kwa kuzingatia kuwa michezo ni afya na vile vile tunaiomba Serikali wawaajiri majeshi wa kike nao waweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Waziri na Naibu Waziri na nawatakia kila la kheri katika utendaji wa kazi zenu Mungu awape kheri.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza watendaji na Mawaziri wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu maeneo ya mipakani. Nchi yetu izingatie sana mipaka yetu na iweke utaratibu wa kujenga nyumba katika mipaka hiyo, Serikali itoe pesa kujenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pensheni kuwepo na utaratibu mzuri kwa wale ambao wanatarajia kustaafu kwa kuwaandalia taratibu nzuri kwa ajili ya pensheni zao kwa kuzipata kwa wakati ili kuwapunguzia usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, ni vyema kurudisha mahusiano na nchi rafiki ili kupeleka vijana wetu wa Jeshi kupata elimu huko. Mfano udaktari na urubani, kwani hapa nchini hakuna elimu ya kutosha na bado hata Serikali inapopeleka wafanya kazi nje ya nchi hawarudi kwa hiyo jeshi ndio la kutuokoa. Napenda kufahamu nchi yetu ina uhusiano wa kirafiki kijeshi na nchi ngapi na yapi mafanikio?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza timu za Jeshi Tabora kwa kuingia daraja la kwanza *RhinoTabora* nashauri jeshi lizidi kuimarisha michezo.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi wa Biharamulo hawana nyumba, hulazimika kupanga vyumba katika nyumba za watu kwa gharama kubwa. Pia Biharamulo wanajeshi hawana usafiri, kila siku wanajeshi huzagaa barabarani wakienda kazini na kurudi kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao yao hasa posho ya chakula huchelewa kufikia wahusika. Wajane wa marehemu wanajeshi huchelewa kupata malipo na wengine kukosa kabisa. Wakati wa *Twiga Brigade* Jeshi lilichukua sehemu kubwa ya ardhi ambayo kwa sasa hailiendelezi, kama jeshi halina mpango wa kuendeleza ardhi hiyo sehemu isiyoweza kuendelezwa wapewe wananchi kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Brigedia ya Twiga ilipovunjwa sehemu ya Tutuu iliyokuwa sehemu ya kambi ya Jeshi iliombwa na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge na kupewa. Baada ya kikosi kidogo cha jeshi kurudi wanajeshi wanadai kuwa sehemu ya Tutuu ni yao na kuleta mkanganyiko au utata, Wilaya inaomba Serikali, Wizara ya Ulinzi, isaidie kuondoa utata uliopo ili sehemu hiyo iweze kuendelezwa.

Kuhusu mpango wa kufundisha wananchi mbinu za kijeshi kama vile wanamgambo wanajeshi wanaostaafu na wanajeshi wa Jeshi la Kujenga Taifa na Serikali kukaa bila kufahamu watu hao wanakoishi na wanafanya nini inaweza kuwa moja ya sababu za kuongezeka kuwa moja ya sababu za kuongezeka kwa ujambazi nchini. Nchi kama Israel na nyingine watu wote wenye ujuzi wa kijeshi huundiwa vikosi na mara kwa mara hufanya mazoezi. Pia huweza kujulikana wanakoishi pamoja na mwenendo wa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi wanaolemaa wakiwa kazini hulipwa kiasi kidogo cha pesa kwa mfano, Kapteni Naftali Kibandwa wa Biharamulo mjini hulipwa wa shilingi 2,000 kwa mwezi wakati alipoteza jicho akiwa katika utumishi wa jeshi.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa hotuba nzuri sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa kazi nzuri. Aidha, nalipongeza Jeshi letu kwa utayari, uwezo mkubwa na kuendelea kuogopwa na maadui zetu. Tuongeze mafunzo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu leo ni ahadi ambayo Jeshi la Wananchi walitupa la kutusaidia kutengeneza barabara yetu ya kutoka Usangi kwenda Butu na ya Vuchama kwenda Ngofi kama sehemu ya mafunzo ya *field engineering.* Wakati wa nyuma JWTZ walianza kupasua mawe ya Ngofi na baadaye aliyekuwa Waziri wa Ulinzi Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, alituma timu ya *Military Engineers* wakaja wakapima maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya muda mrefu tukaletewa bili ya vifaa vinavyohitajika vyenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 22 ili barabara hizo ziweze kujengwa. Sisi hatuna dola hizo hivyo dau hilo likawa zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaanza wenyewe tukatumia Msaragambo na shilingi milioni 21 tukafika pahali tukamwomba Waziri kama bila vifaa aghali haiwezekani, basi watusaidie (kupitia Halmashauri ya Mwanga) shilingi milioni 25 kazi hiyo tutaimaliza wenyewe na wanajeshi waje waangalie, Waziri akakubali. Sasa namwomba Waziri atimize ahadi yake na amtume Naibu Waziri aje aone kazi iliyofanywa kwa Msaragambo. Ahsante sana.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, viongozi wakuu wote wa majeshi yetu kwa matayarisho mazuri ya Bajeti hii. Aidha, nawapongeza Wanajeshi wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuhakikisha hali ya amani na utulivu inaendelea hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mbunge wa Tabora Mjini nilijaribu kupata idhini ya kiongozi wa Brigedi ya Magharibi ili nipate fursa ya kufika katika makambi ya Jeshi letu Mjini Tabora kwa madhumuni ya kuona hali halisi ya makambi pamoja na kusikiliza mawazo ya wanajeshi wetu kuhusu matatizo yanyowakabili ili niweze kuja kuyawasilisha katika ngazi za juu kwa ajili ya kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sikupata ruhusa ya kufanya hivyo. Kwa hiyo nimeshindwa kuelewa hali halisi ya matatizo ya askari wetu. Naiomba Wizara inipatie maelekezo ya namna ninavyoweza kuzungumza na askari wetu mjini Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa nyumba za askari wetu mjini Dar es Salaam. Hata hivyo naishauri Serikali ipanue wigo wa ukarabati na ujenzi wa nyumba za askari toka Dar Salaam mpaka makambi ya Tabora vile vile kwani nyumba za askari katika makambi ya Tabora ni chakavu, duni (nyingine zimejengwa kwa tofali za udongo wa kawaida) na hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ishirikishe Jeshi letu la Ulinzi katika ukarabati na kuupanua Uwanja wa Ndege wa Tabora ili uweze kukidhi mahitaji ya ndege kubwa za kijeshi na hasa matumizi ya dharura yanapotokea kama ilivyokuwa wakati wa vita ya Nduli Iddi Amini. Jeshi letu lililazimika kukitumia kiwanja hiki wakati wa usiku bila kuwa na taa za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha naomba kuchukua fursa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kama mipango iliyoainishwa itatekelezwa vizuri, tutapiga hatua kubwa ya kimaendeleo hasa katika suala zima la kuimarisha ulinzi wa nchi yetu na katika suala zima la kupatikana ajira kwa ajili ya vijana wetu. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake nzuri sana na aliyoisoma kwa ufanisi mkubwa na kasi inayokwenda na wakati. Naunga mkono hoja hii kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine napenda kuwapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Mkuu wa

Jeshi la Kujenga Taifa na wasaidizi wao wote kwa kumsaidia Waziri kwa juhudi, maarifa na ufanisi mkubwa na kumwezesha kutoa hotuba ya Bajeti inayoeleweka na kukubalika Bungeni. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wetu sisi Wabunge, tunapenda kutoa shukrani zetu kwa kutukubalia kutufanyia mazoezi ya kulenga shabaha katika kambi ya JKT Makutupora. Mazoezi hayo yanatusaidia sana kuelewa kanuni za matumizi ya silaha na utunzaji wake kwa walionazo na wanotegemea kumiliki silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeunda *Bunge Range Club* kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri wa kutumia fursa tuliyopewa vizuri zaidi. Kwa niaba ya wanachama wa *Bunge Range Club (BRC)* tunaomba mtufikishie shukrani zetu kwa Kamanda wa Jeshi la Kujenga Taifa Makutupora kwa jinsi wanavyotupokea kwa heshima na kutuelekeza kwa ufanisi unaozingatia mazingira ya Kijeshi ya ukakamavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunashukuru sana kwa huduma nzuri sana tunazopewa wakati wa mazoezi ambazo zinaboreka kiuendelevu. Vifungu 3 hadi 6 nimeviandika nikiwa ni mratibu wa *Bunge Range Club.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Waziri, Naibu Waziri na wapiganaji wake wote kwa kazi maridhawa za ulinzi wa mipaka ya nchi yetu, wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naipongeza Wizara kwa kukamilisha ujenzi wa hospitali ya Jeshi la Wananchi iliyoko Bububu, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuwaongezea mishahara Makamanda wetu. Serikali iendelee kuwaongeza mishahara yao pale panapokuwa na haja ya kufanya hivyo sambamba na malipo ya posho zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iipatie fedha za kutosha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kununulia silaha za kisasa kwa vile zile za zamani zimepitwa na wakati na nyingi ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuagiza magari ya askari wetu, hata hivyo ugawaji wa magari uwe kwa kila Wilaya za Kambi za Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi wetu makambini usichelewe kuanza, halikadhalika ugawiwe kwa kambi zote nchini hasa zile kongwe ikiwemo kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mwanyanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za askari uende sambamba na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba wanazoishi wanajeshi ambazo kwa miaka mingi zimekuwa hazifanyiwi matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, resheni ya chakula ya askari wetu iongezwe na ilipwe kwa wakati muafaka ili kuondosha manung'uniko kwa askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti Wizara ichukue hatua za makusudi za kuanza kujenga uzio kuzunguka Kambi ya Mwanyanya ambayo imezungukwa na nyumba za raia, kitu ambacho huliondolea heshima Jeshi letu kwa vile kila wafanyalo ndani ya kambi hiyo huonekana kwa urahisi na raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huo wa uzio uanze kwa awamu kwani upandaji wa miti kuzunguka kambi kama ilivyoshauriwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali langu, ukuaji wa miti huchukua miaka mingi, pia uzio uliozungushiwa kwa kupanda miti hauwezi kumzuia mtu au mnyama kuingia kwenye maeneo ya Kambi ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishwaji wa vyeo kwa baadhi ya askari huchukua miaka mingi na hivyo huwakatisha tamaa. Pamoja na kuwa sifa za kupandishwa vyeo huwa wanazo yaani elimu, juhudi, ujuzi na hata nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wasikae kwa muda wa miaka mingi kwenye kambi moja au eneo moja, wahamishwe kila baada ya miaka michache kwa kuzingatia maeneo mbalimbali ya kambi ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pensheni kwa wastaafu liangaliwe upya kwa vile fedha wanazolipwa wastaafu hazikidhi hali halisi ya maisha kwa nyakati husika. Nashauri kuwepo na *formula* zinazokidhi mabadiliko ya malipo ya pensheni kwa nyakati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *uniforms* zinazofanana na zile za kijeshi zidhibitiwe. Kwa sasa mavazi ya kufanana na *uniforms* hizo yanazidi kuzagaa mitaani na nyingine huvaliwa na wahalifu na kuonekana kuwa wahalifu hao ni wanajeshi wetu wakati sio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa asilimia zote.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii na pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wapiganaji wetu wote, wakiongozwa na Jenerali mahiri, George Waitara, hakika Jeshi letu la Wananchi ni jeshi la kujivunia kwa kila hali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze juhudi za Serikali za kulifanya Jeshi letu kituo cha umahiri *(Centre of Excellency)* katika sayansi na teknolojia, kwa utafiti na kufundisha, hasa kufundisha elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi duniani wamefanya hivyo na wamefikia mafanikio makubwa katika sayansi na teknolojia, nasi tunaweza kuendeleza haya na kupitia Jeshi tutafikia upeo mkubwa kama nchi na pia katika ubingwa wa wataalamu katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumuomba Mheshimiwa Waziri, wataalamu wake pamoja na wapiganaji wetu wajidhatiti katika kuendeleza hizo *centres of exellency* katika *medicine* na *engineering*. Wizara na Jeshi lenyewe waendelee na juhudi hizi ambazo ni muhimu sana katika kuliandaa na kuliimarisha pia Jeshi letu kuwa la kisasa, lenye uwezo mkubwa kitaaluma na katika mbinu za medani na pia kuwa na vifaa vya kisasa vinavyotumika kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni Profesa, nafarijika kwa maelezo haya machache niliyotoa kwamba atayatafsiri vizuri zaidi kama Wizara na kuziba au kuimarisha mtazamo wa kisera, kama itabidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilipongeze Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa ushirikiano ambao wameendelea kuuonyesha na wananchi wangu wa Masange/Ilolangulu, huko katika Wilaya ya Uyui, katika kufikia maelewano juu ya mipaka ya Kambi ya Jeshi pale wanapopakana na vijiji vya Masange, Ibiri na Ilolangulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Tabora Kaskazini, napenda niseme kuwa tutaendelea kufanya mazungumzo katika kutatua matatizo yetu ya mipaka na uhusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya ulinzi wa mipaka yetu ndani ya Ziwa Victoria inaendelea kuboreshwa. Hata hivyo bado kuna mahitaji makubwa ya boti zenye nguvu, boti ambazo Jeshi la Wananchi wa Tanzania watazitumia katika kuvinjari ndani ya Ziwa hilo kama ambavyo wanajeshi wa nchi jirani wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati shirikishi mithili ya ule unaoongozwa na Jeshi la Polisi wakishirikisha idara zingine kama vile *TRA,* Uvuvi, Uhamiaji na kadhalika hazitaweza kuchukua nafasi ya kipekee ambayo lazima Jeshi la Wananchi wa Tanzania tu ndiyo waichukue katika ulinzi wa mipaka yetu ndani ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale ambao walikuwa wachangie mchana huu wamekwishachangia. Sasa tutaingia upande wa mtoa hoja, tutaanza kumwita Naibu Waziri, atatumia dakika zake 20, baadaye mtoa hoja atatumia dakika 40.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kabla sijatoa mchango wangu kwa dhati kabisa naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kiembesamaki, naungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa familia za Watanzania ambao wamefiwa na ndugu zao ikiwa ni pamoja na familia ya marehemu Akukweti, marehemu Amina Chifupa Mpakanjia na Wabunge wote waliofiwa na ndugu na jamaa zao. Vilevile natoa pole kwa familia ya aliyekuwa Katibu mwenezi wa tawi langu la Kiembesamaki kwa kifo cha mtoto wao mpenzi, marehemu Ally Kombo. Marehemu alikuwa mchapa kazi hodari na siku zote alikuwa karibu na wananchi, Mungu azilaze pema roho za marehemu hao. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Waziri Mkuu akiwa ni kiongozi mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni, kwa kutuongoza sisi Mawaziri katika kutekeleza majukumu yetu. Vilevile namshukuru sana Waziri wangu Alhaj Prof. Juma A. Kapuya, kwa miongozo na nasaha zake kwangu. Muda wote tukiwa kazini na nje ya shughuli za kazi, namwomba Mheshimiwa Juma Kapuya asichoke kuniongoza kwani wahenga wanasema jungu kuu halikosi ukoko. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kiembesamaki kwa kushirikiana na mimi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, ninawaahidi siku zote nitakuwa pamoja nao kwa manufaa ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano ninaoupata kutoka kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote ni wa kiwango cha juu. Nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwaomba tuendelee kushirikiana.

Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzani, Mkuu wa JKT na wapiganaji wote kwa msaada na ushirikiano wanaonipa muda wote toka nimeteuliwa kushika nafasi hii. Nawaomba waendelee kufanya hivyo kwani msaada wao unahitajika sana kwangu na nawaahidi nitakuwa msikivu kwao na kufanya kazi zangu kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru mke wangu Bi Narriman na watoto wangu kwa kunisaidia katika kazi zangu za kila siku na kunifariji pale kwenye matatizo na kunifurahisha pale kwenye raha, nawaomba waendelee kunivumilia na kukubali kutokuwa nao karibu mara kwa mara kutokana na kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo sasa naomba na mimi nichangie hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja mbalimbali zilizoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, hoja ni nyingi, tutajaribu kuzijibu kadri ya muda utakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ambayo imetolewa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ilikuwa ni kuhusu Nyumbu haijapatiwa fedha katika bajeti ya mwaka huu. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Nyumbu katika bajeti ya mwaka huu imepatiwa fedha za *recurrent* shilingi bilioni 1.859 ili ziweze kutekeleza majukumu yake ya kazi za kawaida, hatujaweza

kuwapatia fedha za maendeleo kwa sababu wana majukumu madogo madogo na hawataweza kuzalisha magari kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imeulizwa ilikuwa ni uimarishaji wa JKT kwa kuwapatia wataalamu na vitendea kazi. Waliouliza hoja hiyo walikuwa ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Masoud Aballah Salim, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba JKT tumeipatia wataalamu wa kutosha na kila inapohitajika tunajaribu kutafuta wataalamu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Aidha, katika mwaka jana na mwaka juzi tumeweza kuwapatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na matrekta, vyerehani kwa ajili ya viwanda vyao mbalimbali, bado tutaendelea kununua vitendea kazi ili kuweza kuliimarisha zaidi Jeshi letu la JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imeulizwa kwa upande wa JKT ilikuwa ni suala zima la kupima maeneo ya JKT. Mheshimiwa Janeth Massaburi alitaka kuelewa shamba la Itaka Mbeya kama limekwishapimwa, nataka nimuarifu kwamba shamba hili tayari limekwishapimwa na maelekezo yapo na *beckon* zipo. Naye Mheshimiwa Castor Ligallama vilevile alitaka kuelewa kama Kambi ya Chita imeshapimwa, nataka nimhakikishie kwamba Kambi ya Chita, tumekwishaipima na *beckon* zipo na zinaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo nataka niliarifu Bunge lako iliyoulizwa na Waheshimiwa mbalimbali ni suala la kuimarisha michezo jeshini pamoja na JKT na siyo kuimarisha mpira wa miguu tu. Hapa nitamke kuwa na mimi vilevile ni mpenzi wa simba kama alivyo Waziri Kapuya. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Leo tumepata tabu, vitabu vyote ni simba tu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imeulizwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Aziza Ally. Nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Aziza Ally kwa kuifadhili timu ya Raino iliyoko kule Tabora. Naomba vilevile Waheshimiwa Wabunge wengine waige mfano wa Mheshimiwa Aziza Ally, kwa kuzifadhili timu zilizoko katika majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleza kwa upande wa michezo, nia na lengo la jeshi ni kuimarisha michezo ndani ya jeshi, tunafanya hivyo siyo kwa mipira ya miguu tu; tunafanya hivyo pia kwa mipira ya mikono; kwa ngumi; mpira wa magogo; mpira wa pete na kadhalika. Na kwa kuthibitisha hili asiliamia 70 ya wachezaji wa ngumi katika timu yetu ya Taifa ni wanajeshi na juzi katika wanamichezo, katika wapiganaji saba waliokwenda *Liverpool* wanajeshi walikuwa ni watano. Hii ni kudhihirisha kwamba tunaimarisha michezo jeshini na sasa hivi tumeanzisha mashindano ya Afrika Mashariki kwa timu za jeshi na hivi karibuni tu kule Zanzibar, mnamo mwezi wa Mei timu yetu au wanajeshi wetu walikuwa washindi wa kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo iliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge ni kurejesha JKT kwa mujibu wa sheria. Hoja hii iliulizwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita, nataka nieleza kwamba kama nilivyoeleza katika maswali na majibu wiki iliyopita kwamba itakapofika mwaka 2010 JKT tutairejesha kwa mujibu wa sheria na kila ambaye ana wajibu wa kuingia kwa mujibu wa sheria atajiunga na JKT.

Hoja nyingine ambayo imeulizwa ilikuwa ni kurejesha Kambi ya Mpwapwa chini ya JKT, hoja hii iliulizwa na Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa George Simbachawene. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa hawa kwamba kambi hii tayari tumeshaipitia lakini ukarabati wake utakuwa na gharama kubwa. Hata hivyo, tutajitahidi ili tuweze kuona kwamba tunairejesha. Inawezekana tukashindwa katika mwaka wa kesho lakini tutajitahidi ili tuweze kuirejesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imeulizwa ni kuwa na Kambi ya JKT Singida. Mheshimiwa Mohamed Missanga aliuliza kwamba Singida kuna tatizo gani kwani kuna ardhi nzuri, hali ya hewa nzuri na kadhalika.

Nataka nikubaliane naye Mheshimiwa Mohamed Missanga, kwamba kweli Singida kuna hali ya hewa nzuri, kuna ardhi nzuri lakini lazima tukubali kwamba Waheshimiwa Wabunge maelekezo ya Serikali yapo, JKT tuna wajibu wa kwenda chini katika kila Wilaya lakini hii itategemeana na uwezo wa Serikali, tutafanya hivyo kila pale uwezo wa Serikali utakapokuwa mzuri na tutaenda kwa awamu. Mheshimiwa Mohamed Missanga nataka nikuahidi kwamba tutafika Singida na wala usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo iliulizwa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni suala zima la kuitumia SUMA JKT kusaidia ujenzi katika maendeleo ya vijiji pamoja na miradi ya Serikali. Hoja hii imeulizwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Benito Malangalali na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. Nataka niwahakikishieni kwamba kwanza Serikali inatupatia kazi za kutosha za kutekelezwa na JKT, tuna majengo pale Dar es Salaam tunayajenga na mengine tumeshakamilisha, tuna majengo katika Wilaya mpya ambazo Serikali imetupa tujenge Makao Makuu zake, tunajenga na tunaendeleo nayo na mengine tutayakamilisha hivi karibuni. Vilevile tumejenga shule kwa kushirikiana na wanakijiji katika maeneo mbalimbali na hivi sasa tumeshaanzisha mazungumzo na Wizara ya Elimu ili kusaidiana nao katika kujenga madarasa pamoja na maabara katika shule mbalimbali. Kwa hiyo, suala la Serikali kutupatia kazi tunashukuru, wanatupatia kazi na kila zitakapoongezeka kwetu sisi tunafurahi vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo iliyoulizwa ni Kambi ya JKT Mafinga igeuzwe na iwe Kambi ya JWTZ, hoja hii imeulizwa na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Benito Malangalila. Nataka nieleze tu kwamba Jeshi la Wanachi wa Tanzania linapoihitaji kutumia Kambi hii kwa shughuli zao wanaitumia. Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ni waoto pacha, tuko pamoja hatuna matatizo, lakini vilevile tukumbuke kwamba bado sisi kama JKT tunahitajia makambi zaidi. Kuitoa kambi hii kuipeleka JWTZ maana yake ule uwezo wa kufika kila Wilaya mtatupunguzia. Kwa sasa tunaomba kambi hii iendelee kuwa chini ya JKT na JWTZ

watakapoihitajia kwa matumizi mengine, basi tutaweza kuwapatia ili waweze kutumia kwa muda ule wanaohitajia.

Hoja nyingine ambayo iliulizwa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni suala la ujenzi wa Makao Makuu ya Mkinga kwamba unaenda taratibu. Hoja hii imeulizwa na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro. Nataka nimhakikishie kwamba hapo awali kweli ujenzi ulikuwa unaenda taratibu, lakini ujenzi siku zote unategemeana na fedha zinavyotolewa. Hata hivyo, ujenzi huu unakaribia kukamilika na tutaukabidhi kwa mamlaka husika kabla ya kwisha kwa mwezi wa Agosti mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imeulizwa na Waheshimiwa Wabunge ni vigezo vinavyotumika katika kuwasajili vijana kujinga na JKT. Mheshimiwa Hamza aliuliza swali hili. Nataka niseme kwamba suala hili nilishalijibu hapo awali lakini kwa manufaa na faida ya Wabunge. Vigezo vinavyotumika kwa vijana kujiunga na JKT kwanza awe ni raia wa Tanzania, pili, awe amemaliza angalau darasa la saba, tatu, umri wake usiwe chini ya miaka 16. Chini ya umri huo hatuwezi kumchukua kijana kujiunga na JKT. Nne awe na afya nzuri na mwadilifu. Hatuwezi tukamchukua mtoto ambaye tunahisi kwamba afya yake si nzuri. Hatuwezi kumchukua kijana ambaye si mwadilifu. Na tano awe amepitishwa na Serikali ya Mitaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ambayo imeulizwa kwa upande wa JKT ni hoja ambayo imeletwa kwetu na Mheshimiwa William Shellukindo. Mheshimiwa Shellukindo alishukuru sana kwa Bunge *Range Club* kupata fursa tunazotoa katika kambi yetu ya Makutupora kwa ajili ya kupiga shabaha. Aliwaomba sana Waheshimiwa Wabunge wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kupiga shabaha na alitutaka sisi tuwe tayari kuwahudumia wakati wote Wabunge watakapokuwepo pale. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Shellukindo na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kama kawaida yetu mtakapokwenda Makutupora kwa ajili ya shabaha, tutawapa kila kinachostahili kupewa na tutajitahidi tuwafundishe shabaha kwa mujibu wa mafunzo ambayo tunayatoa kwa vijana. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mjitokeze kwa wingi sana ili muweze kujifunza katika suala zima la kupiga shabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga tena mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa tena fursa hii kutoa shukrani zangu kwako kwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala wa hotuba yangu kwa maandishi na kwa mdomo. Lakini katika shukrani hizi hizi naomba sasa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi na wapiga kura wa Urambo Magharibi kwa msaada wanaonipa wa kuelewa kwamba Wizara tuliyopewa ni nyeti na ziara tulizokuwa tumezoea za kutembeleana mara kwa mara sasa hivi kidogo zinapungua. Lakini nina hakika ndugu zangu mnajua kwamba kazi tuliyonayo ni kwa niaba ya Taifa tutaendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla michango yote iliyotolewa inalenga katika kuboresha utendaji katika vyombo vyetu vya ulinzi, maoni na ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Kambi ya Upinzani ambayo kimsingi mengi waliyoyatoa katika mchango wao kwa kweli yamezingatiwa katika sera ya Chama cha Mapinduzi. Pamoja na Waheshimiwa Wabunge yatazingatiwa na Wizara itayatekeleza kadri ya uwezo wa kifedha unavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutaendelea kutumia ushauri wa wataalamu na maoni mbalimbali juu ya namna ya kuboresha utendaji wa vyombo vyetu vya ulinzi. Tunatambua kwamba amani na utulivu ni nguzo muhimu ya maendeleo ya Taifa letu lakini tunatambua pia kwamba tatizo lipo la ufinyu wa bajeti kitaifa kwa ajili ya kugharamia mambo ya ulinzi. Tutafanya kila juhudi ili kuhakikisha kwamba fedha kidogo zitakazoidhinishwa zinaelekezwa katika kutekeleza mambo yatakayotuletea kishindolengwa yaani *impact*. Aidha, tutaendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti kama ilivyokwishaagizwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kikao cha kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tarehe 15 Aprili, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo inahusiana na Wizara hii, Wizara nyingine na waliochangia katika hotuba yangu kwa leo hii kwa mdomo na kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Eng. Dr. James Msekela, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Said Omar, MheshimiwaRiziki Omar Juma, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Willium Shellukindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe, Mheshimiwa Manju Salum Msambya, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Omar Ally Mzee, Mheshimiwa Ameir Ally Ameir, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Lucy Msafiri, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Uledi Khamis, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Wilbrod Slaa,

Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, Mheshimiwa John S. Malecela, hawa ndio waliochangia kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa mdomo ni Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Col. Saleh Farrah, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mbunge wa Kiembesamaki na Naibu Waziri wa Ulinzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia wakati wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu walikuwa ni Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Ally Said Salim, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge hawa ambao walichangia naomba sasa nichukue fursa hii kutoa maoni na majibu ya Wizara yangu kwa hoja zilizojitokeza wakati wa mjadala wa hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu, hoja ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, hoja ya Kambi ya Upinzani na hoja za Waheshimiwa Wabunge wote zilizotolewa kwa maandishi na kwa mdomo leo. Kutokana na muda hoja zitakazosalia bila kuzijibu naomba nikiri kwamba tutawasilisha majibu yake kwa maandishi na kusambaza kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Suala la kwanza lililojitokeza ni ufinyu wa bajeti, juhudi zinaendelezwa kuiomba Serikali iweke mipango ya maendeleo ya Jeshi katika kipaumbele kutimiza azma hiyo. Aidha, kiasi kidogo cha fedha kitakachopatikana kitaelekezwa kwenye maeneo yenye kuleta kishindolengwa yaani *impact* na tuendelee kuimarisha udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili naomba niseme kwamba tangu tumeingia madarakani kuanzia Serikali ya Awamu ya Tatu na sasa ni Serikali ya Awamu ya Nne kwa kweli kumekuwa na mabadiliko japo ni kidogo lakini inaelekea sasa shida za Jeshi zimeanza kutambulika na fedha zimeanza kuongezeka. Tunachoomba ni kwamba huko tuendako siku za usoni hali itaendelea kuwa bora. Posho ya Chakula ni kweli ongezeko ni dogo lakini Serikali inalitambua hilo na inaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka majukumu ya ziada ya kitaifa na kimataifa bila kuwepo sambamba na fedha, hili ni Jeshi, yapo mambo ambayo yanatokea ghafla na yanapotokea ghafla kama alivyokuwa akizungumza Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha kwamba yanapotokea mambo ya ghafla utekelezaji unaanza mara moja, mambo ya posho na mambo ya fedha yanafuata baadaye.

Tulipopata dharura ya kwenda *Lebanon* na kwa sababu sisi tulishakubali kwamba tutakwenda kusaidia katika ulinzi wa amani ilibidi kwanza tutumie fedha zetu za ndani na kuahirisha mipango mingine kwa kuamini kwamba Umoja wa Mataifa utatulipa na hivyo ndivyo wanavyofanya yaani wanatulipa. Mipango ambayo inapoturuhusu kupanga, kama

hivi sasa tunakwenda *Comoro*, tunapata muda wa kupanga. Tumepanga vizuri na tumeshirikiana na Hazina na itatuwezesha.

Kwa hiyo, yapo mambo ya kidharura na tunayashughulikia kidharura na yapo mambo ambayo tutapata muda wa kupanga na tutapanga ili kuweza kupata fedha za kuandaa.

Uondoshaji wa bidhaa bandarini unachukua muda mrefu. Hili tutaendelea kuzungumza na Hazina na *TRA* ili nao waendelee kuliona kwa sababu ni kweli vifaa vingine ni nyeti na vifaa vingine vikikaa hapo vitaharibika, kwa hiyo, tutaendelea kushauriana na Serikali.

Sera ya Ulinzi ikamilishwe haraka, nataka kukiri kwamba Sera ya Ulinzi hivi sasa iko katika hatua za mwisho mwisho za maandalizi na kisha Sheria ya Ulinzi ya Taifa itafanyiwa mapitio baada ya Sera kupitishwa.

Pensheni kwa Majenerali Wastaaafu, Wizara yangu italifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na Hazina na Wizara ya Katiba ya Sheria. Kuhusu matatizo ya mipaka (*beacons*) kuondolewa mpaka wa Malawi na Tanzania, wafugaji kuvuka mipaka, yanashughulikiwa kwa pamoja na vyombo vingine kwa sababu hili si la Wizara moja, kuna Wizara nyingi ambazo zinahusika.

Jukumu la ulinzi ni kutoa taarifa tunapoona kuna matatizo na ndivyo tunavyofanya ili wadau wote wanaohusika walizingatie na kuanza kulishughulikia. Matatizo haya yatafuatiliwa kupitia Wizara zinazohusika na pia kushirikisha Wilaya na Mikoa ya mipakani pamoja na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa husika.

Wataalamu kustaafu na Wataalamu wanaostaafu waajiriwe kwa mikataba, utaratibu huu tunao ila tunazingatia vilevile kuendelea kuhitajika kwa Mtaalamu huyo na umri wake na afya yake wakati anapostaafu na uwezo wenyewe wa kifedha.

Kuanzishwa *Sub Vote* za *Navy* na *Air Defence*, tathmini tumeshaifanya kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfumo kama huo kwa kuwa tunadhani vilevile kwamba utaongeza udhibiti na uwajibikaji. Suala hili litahusu Vikosi vyote vya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizingatie maoni ya Kambi ya Upinzani ambayo kwa kweli ukikaa hapa na kumsikiliza utadhani kwamba nchi hii kwa kweli haina Jeshi kabisa. Nadhani haya yanatokana na kukataa ukweli au kuangalia kifaa kimoja kimoja wakati wa kutembelea kambi hizi. Tumekuwa naye na tunashirikiana naye na tunampa kila taarifa anayohitaji lakini tumeshangaa taarifa aliyoitoa hapa leo kwamba kila kitu kilicho katika Jeshi na katika Wizara ni kibovu, vile vizima havioni, vile vipya vinavyokuja havioni. Sasa tunashangaa mwenzetu macho alikuwa anaelekeza wapi.

Nidhamu Jeshini, Jeshi letu lina Wanajeshi watiifu kwelikweli, nidhamu ni kigezo muhimu na sharti la msingi la kuwepo Jeshini. Matukio yanatokea moja moja ni ya kupigwa vita kwa nguvu zote, makosa ya Askari mmoja mmoja yasichukuliwe kama ndiyo makosa ya kitaasisi na watovu wa nidhamu wamechukuliwa hatua kwa mujibu wa

taratibu za kijeshi. Waheshimiwa Wabunge walizungumzia pia suala la Askari aliyepatikana na risasi, sidhani kama yupo Kamanda au Jenerali au kiongozi yeyote ambaye anajivunia tukio hili, ni tukio ambalo linatupaka matope na ninataka nikuhakikishie kwamba taratibu zinafuatwa kujaribu kujua chanzo chake hasa kikoje na mpaka zile risasi zikaweza kumfikia askari yule.

Makazi ya askari ni kweli tuna tatizo la makazi ya askari lakini wewe mwenyewe umeshuhudia juhudi ambazo tunazifanya, Lugalo umetembelea nyumba zinazojengwa hivi sasa. Arusha kuna nyumba zinazojengwa hivi sasa, juhudi za kutafuta vianzio vingine unazifahamu tunaendelea nazo. Lakini kwa kuzingatia taratibu za fedha si kitu ambacho unaweza ukakiamua harakaharaka kwa sababu nyinyi wenyewe mmeshuhudia hapa mnatuletea taarifa nyingi ambazo mnasema kwamba Serikali imeingia mkenge. Sasa yapo mambo ambazo ni lazima uyabaini kabla hujaingia mikataba katika vianzio vingine vya fedha, ni lazima tuwe waangalifu.

Kuhusu Jeshi la kisasa Serikali imekusudia kujenga Jeshi la kisasa lenye vifaa bora na Serikali itazingatia hili kwa kadri ya uwezo wa kifedha kama tunavyozungumza. Lakini napenda niseme kwamba tunapozungumza Jeshi la kisasa tusidhani kwamba ndiyo tunaanza alifu kabisa katika kulijenga Jeshi hili. Waheshimiwa Wabunge, ujenzi wa Jeshi la kisasa umekwishaanza kwa wale ambao wanapata fursa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama wanaona na wanajua tunayoyafanya. Ni vitu ambavyo mimi siwezi kusimama hapa na kueleza, kwa mfano, katika hatua hii katika ndege tunafanya hivi na katika meli tunafanya hivi. Nyinyi mnajua na wewe unajua meli.

Juu ya ajira katika Jeshi la Wananchi, Naibu Waziri ameshalifafanua hili, kwa kweli sisi hatuzingatii sana mambo ya itikadi lakini tunachozingatia ni utimamu wa kijana na tabia na adabu nzuri . Kwa hiyo, wala usiwe na wasiwasi kwamba sisi tunabagua. Lakini vilevile Waheshimiwa Wabunge ni vema tukatambua kwamba Jeshi ni mahali ambapo kama tukikosea tukarundika vijana wasiofaa, uwezekano wa kupata matatizo ni mkubwa sana. Kwa hiyo, tunapofanya zoezi la kuchuja, tafadhali sana muungane na sisi pamoja. Kama unahisi kwamba kuna mtu ameachwa kwa sababu ya itikadi na kama unahisi kwamba ni kijana mzuri, njia za kuweza kuonana na Viongozi wa kisiasa wenzako ziko wazi, saa yoyote unakaribishwa katika ofisi za wanasiasa wenzako. Wastaafu na stahili zao nimekwishazungumzia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mafunzo ya mgambo pia yalijitokeza. Wizara kupitia Ngome imekwishatoa mwongozo wa kusisitiza mafunzo ya mgambo kwa mikoa yote. Viongozi wa mikoa na wilaya wana wajibu wa kuhakikisha mafunzo yanafanyika na hili nalo viongozi wa wilaya na mikoa wana tabia ya kutaka kuitenga mgambo kama vile si yao. Mgambo wangechukuliwa kama ni sehemu ya utawala wao wa mkoa na utawala wa Serikali za Mitaa huko kwa sababu tunachokijenga ni chombo ambacho hata wenyewe kinawafaa wakati wa matatizo.

Ianzishwe *detach* ya Jeshi katika kijiji cha Sali ili kukabiliana na wahalifu wa Kisomali. Kuhusu hoja hii, ili kukabiliana na uhalifu katika maeneo ya mipakani maagizo

yalikwishatolewa kuhusu kuanzisha vituo vya Polisi ambavyo vitakuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama wa maeneo hayo kwa kuwashirikisha wananchi katika maeneo waliopo na zinapohitajika nguvu za ziada za ulinzi uongozi wa Brigedia au vikosi kwa kupitia Kamati za Ulinzi za Mikoa husika hushirikishwa. Hili nalo ninapenda kulifafanua kidogo. Kuna siku nilipigiwa simu nikiwa Jimboni, nikaelezwa kuwa kuna tatizo kule mpakani wasomali wanaingia tu, sasa wewe Waziri wa Ulinzi unasemaje? Mahali pa kwanza pa kuuliza pawe ni Wizara ya Usalama wa Raia si Wizara ya Ulinzi. Tumegawana majukumu haya, na wenzetu kwa kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ndiyo watatuarifu kwamba sasa yamefikia mahali ambapo na sisi tunapaswa kushirikiana nao. Lakini wewe unaona wasomali wawili au watatu wameingia unampigia Waziri wa Ulinzi, si sahihi!

Mhehimiwa Capt. John D. Komba alisema kwamba wavuvi wa Malawi wanavua katika maeneo ya Tanzania kwenye Ziwa Nyasa, Ulinzi uimarishwe katika mpaka wa Ziwa Nyasa, ianzishwe *detach* ya Jeshi itakayohusika na Ulinzi katika maeneo ya Ziwa Nyasa. Wananchi wa maeneo hayo wahamasishwe kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vya Wilaya pamoja na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, Mikoa katika kutathmini na kuratibu mienendo ya wavuvi wanaovua bila utaratibu na kuchukua hatua stahili. Aidha, Jeshi halina utaratibu wa kuanzisha *detach* kwa maeneo ambayo hayaonyeshi dalili za wazi kwa matishio.

Ni kweli Ziwa Nyasa kuna matatizo ya mpaka lakini hatujapata dalili za waziwazi kwamba kuna tishio la usalama wetu. Lakini vilevile tungeendelea basi kuwaandaa wananchi kwa sababu huko huko Ziwa Nyasa tuna malalamiko makubwa juu ya kituo chetu kidogo kilichopo cha Rada. Je, tutapoanzisha hiyo *detach* anayosema Mheshimiwa Capt. John D. Komba si itakuwa balaa? Kwa hiyo, tuanze kuhamasisha basi wananchi vilevile wajue kwamba kuna umuhimu wa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir alisema kwamba nyumba za jeshi katika Kambi ya Potoa Zanzibar zifanyiwe ukarabati, ukarabati wa nyumba za makazi za maofisa unaendelea kadri yauwezo wa kifedha unavyoruhusu. Maeneo yanayohitaji ukarabati ni mengi na kazi za ukarabati zinafanywa kwa hatua kulingana na uwezo. Nadhani katika hotuba yangu nimezungumzia jinsi ambavyo sehemu ya nyumba hizi za Potoa ambazo tumeanza kuzishughulikia.

Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula alisema kwamba Serikali idhibiti uingiaji wa silaha holela kupitia mipaka ya Rwanda na Uganda. Hili ni tatizo la kikanda ambalo limetokana na mwingiliano wa kijamii unaotokana na wakimbizi na machafuko katika nchi jirani. Juhudi za pamoja za kikanda zinahitajika kufanyika ili kudhibiti hali hii, wananchi washirikishwe na kuhamasishwa katika masuala ya ulinzi na usalama ili kuwafichua wahalifu na kutoa habari zitakazosaidia kutambua maeneoe yanayotumika kuingiza silaha kiholela.

Hili nalo ni tatizo kwa ndugu zetu mnaokaa mipakani. Wakati vyombo vya usalama vinapoamua kushughulikia sawa sawa masuala haya ya mawimbi ya uhalifu, inakuwa ni tatizo kwa ndugu zetu wanaokaa pale kuwafichua wale wahalifu, wanadhani

wanafanya vema kwa kuwaficha ndugu zao. Tulipata matatizo ya mpakani kule Tarime wakati walipovunja vunja *beacons* zetu. Mpaka leo hatujaweza kuwagundua waliosababisha matatizo hayo kwa sababu wanadhani wale kumfichua yule mhalifu ni kumsaliti badala ya kufikiria athari kubwa ambayo inapatikana kwa nchi yao.

Kuhusu Madeni ya wazabuni, Wizara inakiri kupokea malalamiko kuhusu madeni ya wazabuni. Hatua zimekwishaanza kuchukuliwa kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunaweza kuhitaji vielelezo kutokana na madeni kuwa ya muda mrefu. Tutafanya juhudi kuhakikisha kwamba suala hili linafikia hatima yake mwaka huu ili kama anastahili kulipwa basi alipwe.

Hili tunazungumzia yale matatizo uliyokuwa unazungumzia Mheshimiwa Issa Kassim Issa kwa sababu tuna tatizo kusema kweli. Wakati mwingine mtu analeta nyaraka ambazo si sahihi, sasa tunapozipata si kwamba ndiyo tayari umeshakuwa na haki ya kulipwa, ni lazima zikaguliwe, zifanyiwe uhakiki na zinapokuwa zimethibitika basi ndipo ambapo tunaweza tukalipa. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba Mheshimiwa Issa Kassim Issa na wengine kama wewe *documents* zenu tunazo, tunaanza kuzihakikiki kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Tutakapofikia mahali ambapo tumeridhika kwamba zinastahili kulipwa tutahakikisha tunakulipa mwaka huu lakini kama tutahitaji vielelezo zaidi au maelezo zaidi tunakuomba usisite kuja kufika kutupa maelezo hayo tutakapokuita.

Kuhusu likizo na uhamisho, kwa sasa hivi kwa kweli nadhani analolizungumzia hapa ni historia, hali si mbaya kama ilivyokuwa inazungumzwa zamani, wanajeshi wanakwenda likizo kwa wakati na wanalipwa kabla hawajaondoka, raia wanakwenda likizo kwa wakati na wanalipwa kabla hawajaondoka.

Uchakavu wa majengo ya Jeshi, majengo ya makazi ya wanajeshi yana hali mbaya hii ni kweli kwamba hali ya makazi kwenye Kambi nyingi ni mbaya, kiini chake ni muda mrefu kupita bila ukarabati. Hatua zimekwishaanza kutekelezwa. Kama nilivyozungumza katika hotuba yangu kwa mfano, kutekeleza ukarabati wa majengo ya vikosi mbalimbali kulingana na uwezo wa kifedha unavyoruhusu. Pia kwa kuzingatia vipaumbele. Kwa makubaliano na *NSSF* kwa kuanzia na maeneo ya Dar es Salaam na Arusha na kama tulivyosema juhudi zingine zinaendelea kufanywa ili kujaribu kupata vianzio vingine vya fedha ili kuweza kujaribu kuhakikisha kwamba tunajaribu kulitatua tatizo hili kwa kasi kubwa zaidi.

Kuhusu maeneo ya Jeshi kwamba Jeshi limechukua maeneo makubwa ambayo hawayatumii. Waheshimiwa Wabunge dhana ya kuyaona maeneo ya Jeshi kuwa makubwa au hayatumiki ni potofu, maeneo mengine yanamilikiwa na Jeshi kwa kuzingatia mpango mkakati wenye maslahi kwa ulinzi wa taifa kwa miaka ijayo. (*Makofi*)

Kitendo cha kuwaruhusu wananchi kutumia ardhi hiyo kitapelekea kuanza kujenga maiundombinu ya kudumu na Jeshi kupoteza rasilimali zake. Aidha, wakati wa mazoezi ya kijeshi na hata wakati wa operesheni mahitaji ya maeneo hujidhihirisha kuwa

ni makubwa kuliko inavyoonekana, inafaa wananchi waelimishwe kwamba ulinzi siyo jukumu la wakati wa vita tu bali unaanzia wakati wa amani kwa kujiandaa kwa mazoezi na kutenga nafasi stahili za ulinzi.

Kimsingi hata wakuu wa Vikosi wanapowaruhusu wananchi kuendesha shughuli zao za kilimo katika maeneo ya Jeshi wanawapotosha wananchi. Lakini napenda nisisitize vilevile kwamba Jeshi mahali popote duniani *resource* yake ya kwanza ni ardhi, lazima wawe na eneo kubwa la kuweza kuweka makazi na kufanya mazoezi yao lakini vilevile kuweza kujihifadhi kwa sababu viko vitengo fulani vya kijeshi ambavyo havipaswi kuonekana. Sasa kama utakuwa unaweka mipaka ya Jeshi, hapa na raia anaanzisha pale pale usiri wa kijeshi ambao unatakikana hauwezi kupatikana, ndiyo maana mnaweza mkaona maeneo mengine yamekaa tu kama vile hayatumiki kumbe ni *buffer zones.* Ni maeneo ambayo yanapaswa kulinda usiri wa Jeshi kule wanakokaa. Kwa hiyo, mimi naomba hili Waheshimiwa Wabunge tuelewane.

Walemavu wa vita kwamba huduma kwa walemavu wa vita hairidhishi, walemavu wa vita wamekuwa wakipatiwa huduma mbalimbali kadri inavyostahili hasa zinazohusu tiba, kwa mfano, viungo vya bandia, vyombo vya usafiri na ajira kadri ya utalaamu wa mlemavu. Baadhi ya walemavu wanachanganya tatizo la ulemavu na matatizo mengine ya maradhi ya kawaida au yaliyojiri kutokana na umri. Vilevile napenda niseme kwamba wanapokuja kwenye hospitali zetu za Jeshi wao wanapewa kipaumbele sawasawa na askari aliye kazini. Kama ni kulazwa atalazwa kwa daraja lile lile, kama ni chakula atakula chakula kilekile na kama akihitaji matibabu ya nje kutokana na uzito na kutegemeana na fedha tulizonazo anaweza akapelekwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati fulani wako walemavu hasa wale wa wakati ule wa awali walipelekwa mpaka Ujerumani kwenda kutengeneza viungo maalumu. Unaweza ukaona jinsi ambavyo tunawaenzi, tatizo ndugu zangu ni fedha kutokutosha, kwa hiyo, tunaweza tukalaumiana. Hata ukizungumza na wale askari waliopo makambini hivi sasa tena wengine ni maafisa wakubwa tu lakini kutokana na hali ya kifedha inabidi wasubiri. Wanaendelea kuteseka, sasa isichukuliwe kwamba hawa wanabaguliwa.

Baadhi ya wanajeshi kukaa eneo moja kwa muda mrefu, napenda kusema kwamba misingi ya wanajeshi kukaa kikosi fulani ni mahitaji ya aina ya kazi za kijeshi zinapohitajika kutekelezwa na taaluma ya mhusika, hivyo ndivyo vigezo. Unaweza ukakuta mwanajeshi fulani kazi yake inamuhitaji kukaa eneo moja tu, sasa unaposema kakaa miaka 30 tufanyaje? Ndipo penye kazi yake, siwezi kumpeleka Tabora hakuna taaluma hiyo, haihitajiki! Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hili nalo ninapenda mlielewe hivyo.

Utaratibu wa kupanga nani anakwenda wapi tungewaachia wanajeshi wenyewe kuzingatia mahitaji yalivyo, tukianza kuwapanga wanajeshi kisiasa tutakuwa tumeleta tatizo kubwa zaidi. *Rational allowance*, posho ya chakula nadhani nimeshajibu.

Fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo, idadi ya wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa na Jeshi wangapi wamelipwa? Hadi kufikia mwaka 2002-2006, ni

2039 kama ifuatavyo: Tondoroni Kiluvya 1650, Ueleza 42, Oldonyo Sambu 316, Msangani 30 na Changanyikeni 1. Kwa hiyo, juhudi za kulipa fidia zinaendelea kutokana na uwezo tulionao.

Upimaji wa maeneo ya Jeshi, maeneo mengi ya Jeshi hayajapimwa na hayana hatimiliki. Tangu mwaka 1987 - Juni, 2007 zaidi ya 70% ya maeneo ya Jeshi yamepimwa kwa kutumia timu ya wapima ardhi wa Wizara ya Ulinzi na JKT. Maeneo ya Jeshi yaliyopimwa ni katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Mwanza, Kagera, Ruvuma, Arusha, Iringa, Tabora, Mbeya, Mtwara, Lindi, Shinyanga, Mara na Kigoma. Zoezi la upimaji wa maeneo ya Jeshi linaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha. Kuhusu hatimiliki kwa maeneo ya Jeshi, Serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaendelea kutafuta utaratibu wa kumilikisha ardhi kwa Wizara, Idara na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge, michezo katika Jeshi, Wizara inajikita katika michezo yote na tungependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa hivi karibuni katika michezo ya majeshi nchi za Afrika Mashariki, Jeshi lilichukua nafasi ya kwanza katika michezo hiyo. Aidha, tunaomba ieleweke kwamba Jeshi lina timu mbili katika daraja la kwanza nalo ni Ruvu *Stars* na Ruvu *Shooting Stars. (Makofi)*

Kulituhumu Jeshi kwamba linajikita katika michezo ya mpira wa miguu tu si sahihi, sisi ndiyo tunaongoza katika masuala ya ngumi; sisi ndiyo tunaongoza katika masuala ya riadha, ninyi wenyewe ni mashahidi, tukitoka huko nje tunaleta medali mpaka za dhahabu. Kwa hiyo, Jeshi kwa kweli linajaribu kujizatiti katika michezo yote na hivi kutokana na jinsi uwezo unavyozidi kuongezeka tutaendelea kurudi katika hali yetu ile ya kawaida ya kuongoza michezo katika bara hili la Afrika na pengine ulimwenguni.

Sheria za Kijeshi kufanyiwa marekebisho, tunakiri kwamba Sheria za kijeshi zimedumu kwa muda mrefu lakini pia ieleweke kuwa Sheria hubadilika iwapo kuna mabadiliko ya msingi katika mazingira ya utekelezaji wake. Sheria za Kijeshi kadhaa nazo pia zimekuwa zikifanyiwa mabadiliko pale inapobidi. Tunapenda kuelezea pia kuwa umri wa kuoa au kuolewa ni miaka sita, umewekwa kutokana na majukumu ya askari wa ngazi husika kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, hawa askari wanapoanza kazi ya uaskari kitu cha kwanza wanachofanya ni mafunzo, kwa hivi sasa wako hapa Makutupora watamaliza miezi sita au tisa wanahitimu kama makuruta. Baada ya hapo ndiyo hasa maandalizi ya askari yanapoanza. Tunatumia miaka mitano au sita kumwandaa awe askari aliyekamilika, sasa ukishambebesha majukumu ya kubeba mimba, kunyonyesha, kuwa baba mtoto, haya mengine atayakamilisha vipi? (*Makofi*)

Jeshi letu katika Bara la Afrika linaendelea kutisha na kuheshimika kwa sababu lina askari waliopata mafunzo yaliyokamilika, vinginevyo itabidi muwe na askari ambao mnawafundisha nusunusu na ukimtuma atakujibu kwa sababu afande leo sikulala sawasawa, kazi hiyo siiwezi, vipi? Mtoto alikuwa na malaria, mara tumeambiwa twende

kwa mganga wa kienyeji kwa sababu hospitali wamesema vipimo vyote havioni. Sasa kwa kuzingatia haya yote ndiyo maana tunasema wapeni nafasi hawa. Kila kazi ina nidhamu zake.

Kustaafu kutokana na umri, katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kijeshi, umri ni kigezo muhimu, hata hivyo, sheria za kijeshi zinamruhusu Mkuu wa Majeshi kumwongezea umri mwanajeshi pale anapoona inabidi. Tunaomba aachiwe jukumu la kuongeza miaka ya utumishi jeshini kwa askari wake, hoja ya ajira kwa mkataba kwa wataalamu Jeshini inafanyiwa kazi. Hivi sasa, ajira hii itatokana na aina ya taaluma na athari yake katika ufanisi wa taaluma husika Jeshini.

Lakini vilevile kwa ujumla nataka niseme ukizingatia miaka ya nyuma umri wa kustaafu jeshini ulikuwa chini zaidi lakini jinsi mazingira yanavyozidi kubadilika, lishe inavyozidi kubadilika, mazingira ya afya yanavyozidi kubadilika, umri unazidi kupanda na kupanda. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho siyo *static* ni kitu ambacho kimeendelea kubadilika na ni kitu ambacho ni *dynamic,* itakuwa inaendelea kuangaliwa kutokana na hali halisi ilivyo lakini tumwachie Mkuu wa Majeshi awe na uwezo wa kuamua ni nani aendelee na kwa misingi ipi.

Kero za usafiri, Wizara yangu imeendelea na mipango mizuri ya kutoa huduma za usafiri kwa wanajeshi, hata hivyo, napenda kukiri kuwa tatizo bado lipo na tutaendelea kuikumbusha Serikali kila inapowezekana kuendelea kulipatia Jeshi vyombo vya usafiri.

Lakini nataka nizungumze kidogo zaidi katika hili, kwamba katika hotuba yangu ya mwaka 2006 nilizungumzia jinsi ambavyo Serikali inanunua magari 628, ndani ya magari hayo yamo na magari ya usafiri kwa kuonyesha jinsi ambavyo Serikali inavyozingatia tatizo la usafiri. Ni kweli inasikitisha kuwakuta askari wanapanda Daladala na kuona wanasukumwa kwenye basi, inabidi abembeleze na nchi yetu hii ni nchi inayozingatia utawala bora, hawawezi kutumia mabavu. Lakini nataka niwaambie kuwa Serikali inalijua hilo na ndiyo maana inawekeza sasa katika kutafuta magari mapya ili kuweza kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, marupurupu ya Majenerali, cheo ya Ubrigedia Jenerali ni ngazi ya Ujenerali na Kijeshi cheo hiki kinaitwa pia *One Star General*, hoja ya kupata marupurupu kulingana na wanayopewa Mameja Jenerali ni ya msingi na suala hilo litapelekwa katika ngazi husika ili liweze kurekebishwa ikiwa ni pamoja na marupurupu yote ya maafisa na maaskari wanapostaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya miundombinu ya Kijeshi, miundo ya kijeshi hutokana na mazingira ya kiulinzi wakati husika, Wizara yangu imeanza kuifanyia kazi marekebisho miundo na mifumo ya ukaaji jeshini.

Upanuzi wa Jeshi kufikia Vikosi mbalimbali linafanyiwa kazi, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa suala la kufahamu nguvu na uwezo wa majeshi ya nchi jirani ni suala la kawaida na endelevu kwa Jeshi letu. Aidha, kwa askari wa Jeshi

la Ulinzi ni kazi yake ya msingi na hufanya kazi saa 24, hivyo halihusiani na kupewa malipo yaani *allowances* dhidi ya majukumu yao ya kiulinzi.

Wanajeshi waliopigana Vita Kuu vya Pili ya Dunia, malalamiko ya wazee waliopigana Vita Kuu vya Pili ninakiri ni ya muda mrefu. Kumekuwepo na mgogoro wa pande mbili zinazogongana kwa kutotambua uongozi uliopo madarakani unaoongozwa na Mzee Silvester Lubala. Hivi sasa wanachama kadhaa wamefungua kesi mbili Mahakama ya Kisutu zikiwa ni kutotambua uongozi uliopo madarakani na kuwepo kwa madai ya ubadhirifu wa mali za Tanzania *Legion Club*.

Serikali imelishughulikia suala hilo kama ifuatavyo: imeunda Kamati ya Wajumbe kutoka Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Ulinzi na JKT, Kabidhi Wasii Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Afya ya Ustawi wa Jamii. Kamati hii imefikia uamuzi kuwa mali zote za Chama cha Wazee waliopigana Vita Kuu vya Pili vya Dunia, Tanzania *Legion Club* zitakabidhiwa kwa Kabidhi Wasii Mkuu ili azisimamie mpaka maamuzi ya kesi hiyo yatakapotolewa na Mahakama. Waliohusika na ufujaji na ubadhirifu wa mali za Tanzania *Legion Club* watachukuliwa hatua, Polisi na TAKURU wamekwishafahamishwa ili washughulikie suala hili.

Lakini kuhusu hiyo Tanzania *Legion Club,* fedha zilikuwa zikija, zilikuwa zikiletwa na Serikali ya Uingereza. Hivi sasa wamesimamisha wakisubiri mgogoro huu kwanza uishe ili wajue ni nani wa kumkabidhi fedha hizo. Kwa hiyo, hakuna anayepokea fedha hizo kwa hivi sasa. Ujenzi na ukarabati wa nyumba za kuishi Maskari nimeshaungumzia.

Zoezi la kupima maeneo yote ya Jeshi linaendelea kwa kushirikisha Halmashauri za Wilaya zote zinazohusika ili kuhakikisha migogoro yote inakwisha. Pale panapokuwa na stahili ya kulipa fidia Wizara inalipa fidia kama nilivyosema katika hotuba yangu lakini suala la fidia tuna tatizo nalo. Wananchi ama wenyewe kwa wenyewe kwa kuhamasishwa na watu tusiowajua wakishasikia kwamba eneo hili sasa linatwaliwa na Jeshi ndiyo wanaharakisha kwenda kujenga vibanda ama nyumba pale ili waweze kama vile kulikomoa Jeshi wakati wanapokuja kuanza shughuli zao pale.

Sasa hii tabia tunaomba Waheshimiwa Wabunge ninyi mnaojua uzito wa Jeshi na kazi linazozifanya katika kuweka usalama wa nchi mtusaidie ku-*discourage* mambo haya, wanapofanya hivyo wanamkomoa nani? Hivi sasa tunatafuta Kambi ya Mafunzo sehemu fulani wananchi walipotangaziwa kwamba Jeshi linakuja hapa kuanzisha Kambi ya Mafunzo tayari watu wameshaanza kwenda kujenga pale. Sasa hili linakuwa ni tatizo. Tunaomba tusaidiane katika hilo. Mafao kwa wastaafu nimeshazungumza na kero ya usafiri nimeshazunguza.

Mahusiano ya askari na raia, kwa ujumla mahusiano kati ya askari wa Jeshi la Wananchi na Wananchi ni mazuri hata hivyo yapo matukio moja moja *(isolated)* yaliyotokea kama vile Kaboya na Kibaha na wahusika wanachukuliwa hatua kwa taratibu za kijeshi. Lakini ningependa nizungumzie hili kwa zaidi kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, katika nchi ambazo zina bahati ya kuwa na askari wenye nidhamu, hakuna nchi kama Tanzania katika Bara zima la Afrika. Mheshimiwa Ruth B. Msafiri alipoanza kuongea mimi nilifurahi kweli kweli, akasema mimi wanajeshi ni wapiga kura wangu na wale wananchi wa kawaida ni wapiga kura wangu. Lakini akaendelea kuja kuwahukumu wanajeshi kabla hata hatua za uchunguzi hazijakamilika, hiyo nadhani si sahihi, kwa sababu wakati mwingine huwa tunadhani kwamba askari kupigwa ni haki yake, askari kuvuja damu ni haki yake, tunadhani kwamba huyu hapaswi kusikia uchungu. Hivi ninavyozungumza taarifa niliyoletewa mimi leo ni kwamba kuna wanajeshi vilevile wameumia na wamelazwa hospitali wanatibiwa.

Sasa ni kitu ambacho tungekuwa tunakizungumza kwa uangalifu sana ili tukaacha vyombo vinavyohusiana na uchunguzi vifanye uchunguzi lakini kuendelea kuhukumu hapa na kutoa madai kwamba sasa Serikali iwalipe matibabu wale waliumia wamekwenda kulazwa katika hospitali za watu binafsi na kwa nini hawakwenda katika hospitali za Serikali, mimi sijui. Mambo ambayo ndugu zangu yanawaumiza askari wa Jeshi la Wananchi wanaposikia, kwa sababu na wao ni watu pamoja na kwamba ni wanajeshi lakini ni watu na ni watoto wa nchi hii. Askari hao wanauawa na raia hakuna anayejali.

Mwaka jana kuna askari alipigwa karibu na Kituo cha Vingunguti, alikuwa anasubiri basi kwenda kazini saa 9 usiku, akavamiwa na kupigwa na kuuawa. Sasa wenzake walipoona hakukuwa na hatua zinazoonekana kuchukuliwa ndiyo maana walijikuta wakijihamasisha kwenda kufanya vurugu ya aina hii. Lakini hatusemi sisi tunaunga mkono vurugu hizo. Sasa hiki ni kitu ambacho tunapaswa kukifanyia *political management*. Kuboresha kitengo cha mgambo, kama nilivyokwishaeleza katika taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Walemavu za Serikali Bungeni ni kwamba hili linashughulikiwa, tuko imara katika Mikoa yote 21. Walemavu wa kivita nimeshalishughulikia lakini hasa maslahi yao tunategemea katika hii sera ambayo tunakaribia kuikaribisha hivi sasa yaangaliwe upya kutokana na agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama mnakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama hapa akaagiza, na sisi akishasema ni agizo ambalo linatakiwa litekelezwe kwa ukamilifu, kwa hiyo, tunalifanyia kazi kwa kuangalia namna ambavyo tunaweza tukahuisha maslahi ya hawa walemavu wa kivita.

Waheshimiwa Wabunge kutembelea makambi ya Jeshi la Wananchi ni kuomba kibali kutoka Makao Makuu ya Jeshi kwa sababu si eneo ambalo unaweza ukasema unapiga hodi leo halafu unatembezwa. Ni lazima utoe taarifa mapema kwa Mkuu wa Jeshi ajue ni sehemu gani atakutembeza, ni vitu gani ambavyo kutokana na wewe ulivyo kama uko *vetted* au si *vetted* ajue jinsi ambavyo anaweza akakutembeleza katika maeneo mbalimbali.

Ununuzi na ukarabati wa zana, utaratibu wa kununua na kukarabati zana za kijeshi unaendelea kulingana na kipaumbele na uwezo. Aidha, ununuzi unafuata taratibu zilizopo za *tender* za kijeshi. Utaratibu wa kuanzisha mfumo wa Kamandi, umeanza kufanyiwa kazi na iko Kamati maalumu inayoshughulikia suala hili, taarifa ikikamilika na ikaonekana kwamba inafaa itatekelezwa mara moja.

Jeshi kusaidia Mamlaka za Kiraia, Jeshi linashiriki katika shughuli za uokoaji katika maafa mbalimbali nchini kama nilivyoeleza katika hotuba yangu. Jeshi kutafuta miradi ya kuongeza kipato, kwa Jeshi la Wananchi *proper* si vizuri kuanza kujiingiza katika biashara na ndiyo maana halifanyi hiyo shughuli. Tunacho kitengo cha SUMA JKT, tumeeleza jinsi ambavyo kinafanya kazi ya biashara, tumeeleza jinsi ambavyo kinakua, tumeeleza jinsi kinavyoanza ku–*acquire* teknolojia ya kisasa. Hicho kitafanya kwa niaba ya Jeshi na kinapopata mapato lengo lake ni kutaka kusaidia kuboresha matumizi au kupunguza gharama za matumizi ya kijeshi na ya JKT lakini kusema Jeshi lifanye biashara itakuwa si vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafanya mawasiliano ya karibu na Wanajeshi wetu waliopo *Lebanon* na hii tunafanya karibu kila siku. Wao wana namna ya kuwasiliana na sisi karibu kila siku. Hata hivyo, upo mpango wa viongozi wa ngazi ya juu kutowatembelea wanajeshi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuanzisha Vituo vya utafiti, Wizara imepokea wazo hili zuri la kuanzisha Vituo vya Utafiti. Aidha, kwa wakati huu Wizara inaona ni vyema kuimarisha kwanza vituo vilivyopo kulingana na uwezo wa kifedha.

eshi limekwishapiga marufuku ufugaji wa mifugo yoyote kwenye Kambi za Jeshi. Aidha, pale ambapo utaratibu huu unakiukwa, Jeshi halitasita kuchukua hatua zinazohusika. Kuna wakati ilitolewa amri hiyo kusisitiza kabisa na kuna akina mama walikuwa wanafuga kuku kule, walitoa malalamiko makubwa ikabidi kuusihi Uongozi wa Jeshi kuwapa angalau mwezi mmoja, kuweza kuhakikisha kwamba wale kuku wamekua wamefikia hali ya kuuzwa na baada ya hapo iwe mwisho. Nina hakika, agizo hilo litatekelezwa na hivi sasa makambi yetu yanaendelea kuwa safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za askari kuzingatia pande zote za Muungano, kutokana na taratibu za ajira kwa askari, nafasi hutolewa kwa kila Mkoa nchi nzima. Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ndizo zinazofanya usaili. Tunaposema nchi nzima maana yake ni Mikoa 26 yote, Mikoa 21 Tanzania Bara na Mikoa 5 ya Tanzania Visiwani. Kwa hiyo, tunapata vijana kutoka Zanzibar na tunapata vijana kutoka Tanzania Bara. Hivi sasa vilevile tunachukua vijana kutoka Jeshi la Kujenga Taifa.

Suala la upandishwaji vyeo Jeshini linafanyika kwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa. Hili nilikwishalizungumza, Waheshimiwa Wabunge, tusifike mahali tuanze kuwekeana *quota.* Turuhusu vigezo vinavyotumika kuwapandisha vyeo Maafisa Jeshini viendelee kutumika hivyo isipokuwa anapokuwa ni Afisa au Kamanda awe ni Kamanda kweli kweli kutokana na vigezo, siyo Kamanda kwa sababu tu ameingizwa kutimiza *quota* fulani itakuwa si vizuri. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ili tusiingie kwenye mkanganyiko, napenda kuwaarifu kwamba, Fungu 38 ndilo lile alilokuwa analisema Mheshimiwa Felix N. Kijiko - Ngome. Kwa hiyo, hakuna mshahara wa Waziri hata wenyewe hamjui. Halafu Fungu 39 ni Jeshi la Kujenga Taifa, mshahara wa Waziri haupo hapo. Fungu 57 ndipo kazi yetu inaendelea hapo. Kwa hiyo, tupo pamoja. Ahsante.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 38 - Ngome**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … Sh. 198,693,067,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … … Sh.47,650,625,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … … Sh. 7,945,321,480

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Godrefy W. Zambi, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Said Ali Said, Mheshimiwa Benson M. Mpesya na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid. Tunaanza na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Niko kwenye Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niligusia suala ambalo nafikiri katika hotuba pia limeandikwa, lakini kidogo tu ni kifungu 55 kwenye kitabu cha hotuba yake. Suala la walemavu walioumia wakati wa Vita vya Kagera. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea kwamba kuna wakati niliuliza swali la nyongeza hapa akatoa ahadi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, ingekuja kauli lakini ile ni *statement* fupi sana, kusimama kama ni kauli ya Serikali siyo lazima Waziri Mkuu. Lakini kusimama kama kauli ya Serikali kwa ajili ya wale ambao waliumia wakati wa Vita vya Kagera. Sasa nilikuwa naomba nipate maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala hili.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa swali lake zuri. Katika hotuba yangu, nimesema kutokana na upana wa suala hili, ilibidi kwanza tuiangalie sera yenyewe ina mapungufu gani na ilibidi vilevile tuangalie hivi wenzetu wanaliangalia namna gani hili la walemavu wa kivita. Yote haya tunayaainisha sasa ili tuje na *comprehensive and proposal* kwa Serikali.

Vile vile katika sera ili tunapokuja kutoa jibu liwe jibu ambalo limekamilika. Nimezungumza hapa kwamba, *paper* yenyewe ya sera ipo katika hatua za mwisho mwisho na mambo mengine ya uchunguzi katika nchi za wenzetu waliozingatia walemavu wa kivita, tumeshayakamilisha. Tutayazingatia yote katika hii sera tunayoiandaa ili kuhakikisha walemavu hao wanaangaliwa ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unasimama halafu ninakuita unaendelea kuongea. Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nadhani ninaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa kuwa wenyewe wapo hivi sasa wanatusikiliza, namwomba Mheshimiwa Waziri, atupe ahadi hiki kitu kitakamilika lini kwa sababu wamechoka kustahimili na wanaendelea kupata tabu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema ni mwaka huu wa fedha, kwa sababu si vizuri kuji-*commit* kwamba, baada ya miezi miwili. Lakini katika mwaka huu wa fedha, hili litakuwa limekamilika. Kwa sababu ninasema ni kitu ambacho *once* tukishakiweka katika taratibu, kiwe kitu ambacho kitaweza kutekelezwa kuanzia sasa na kuendelea. Kwa hiyo, lazima kipangwe vizuri.

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, amenyoosha kidole kwambao ameridhika na majibu.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 57, Programu ya 10, *Sub-vote* 1001 - Mshahara wa Waziri. Nilikuwa naomba tu kupata ufafanuzi. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea juu ya umuhimu wa lishe bora kwa askari wetu na bado ninaamini lishe na afya bora ni mhimili mkuu kwa afya ya askari. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, suala zima la posho ya chakula, wanalifanyia kazi. Ningependa tu kujua, Serikali itakuwa tayari kuharakisha hili maana kiwango cha shilingi 2,500 hakitoshi, mimi nilikuwa nimependekeza kiwe shilingi 5,000 kwa maana ya milo mitatu kwa siku.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya.

Nimeeleza jinsi ambavyo Serikali inalitambua suala zima la lishe kwa askari na kwa kutambua hilo, ndiyo maana safari ya kwanza kuongeza posho, yaani *ration*

*allowance* imeanza. Tulikuwa kwenye shilingi 2,000 sasa tupo kwenye 2,500. Hatusemi hapo ndipo mwisho, lakini vilevile lazima tuzingatie uwezo wenyewe. Kama jinsi unavyoishi katika nyumba yako, unavyoweza ukabadilisha mlo kutoka mlo mmoja kwenda mwingine, ndivyo na sisi tunavyoishi katika Serikali. Kutokana na uwezo tulionao, tunajaribu kujibana katika shilingi 2,500, lakini vilevile tukitambua kwamba, hapo tulipo iwe ni mwanzo tu siyo kwamba ni mwisho wa safari. Hakuna aliye ndani ya Serikali ambaye yupo *comfortable* au ameridhika na kiwango hicho. Lakini kutokana na uwezo tulionao, kwa hivi sasa hicho ndicho tunachoweza. Sasa ni lini tutafika kwenye kiwango cha shilingi 5,000, itategemea uwezo na jinsi ambavyo Hazina inavyozidi kukusanya mapato ya kutosha. Lakini mimi nina hakika, Hazina wanalijua na Hazina ni watu *very sensitive* katika masuala ya kulilea Jeshi lao. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. *Vote* 57, Programu ya 10, *Sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia tatizo la mipaka ya ardhi katika Kambi ya JKT Itaka. Lakini pia nataka nimshukuru Naibu Waziri, alipokuwa anajibu ameligusia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme pamoja na kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu hoja alisema kwamba, *beacons* zipo na mipaka inaeleweka. Mimi kabla sijaja kwenye Bunge hili, nimetoka ziarani katika Kijiji cha Harungu, ambapo ni moja ya eneo lenye matatizo ya mpaka na Kambi ya JKT Itaka. Bado matatizo yapo. Wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu, nakumbuka aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi, aliwahi kwenda kwenye sehemu ile kwa ajili ya matatizo ya mipaka.

Sasa naomba maelezo zaidi, kadri Mheshimiwa Waziri anavyolijua tatizo hili. Mimi nafikiri tatizo lipo. Ninaomba sasa aniahidi mimi na wananchi hao wasikie kwamba, yeye mwenyewe Waziri au Naibu Waziri, yupo tayari kwenda tena Itaka kwa ajili ya kuzungumza na viongozi wa vijiji vinavyohusika, pamoja na uongozi wa Kambi ile ili kumalizika kabisa tatizo la mpaka katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda na kuzungumza na wananchi, mimi na yeye.

**MWENYKEITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri lini?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** baada ya kuahirisha Bunge hili tutakwenda pamoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 57, Programu ya 10, *Sub-vote* 1001 - Mshahara wa Waziri. Wakati wa mjadala wa Waziri ukiwa unaendelea hapa Bungeni, nilipotoka nje nilikutana na wazee wawili na mmoja anatoka Tabora, wamekuja hapa Bungeni kutaka kujua hatma yao na walikuwa na maelezo yafuatayo, ambayo kwa niaba yao nitaomba Waziri ayatolee ufafanuzi:-

Wanadai wao walipigana Vita ya Ukombozi Msumbiji, Angola Seychelles na hata ya Uganda na wakaweza kuacha Jeshi kwa taratibu mbalimbali, wapo ambao waliacha kwa hiari na wengine walistaafu, lakini hawakuwa kwenye nafasi zenye pensheni. Walipolipwa kwa mkupuo walilipwa kiasi shilingi 15,000, ambazo kwa kweli hazikuwasaidia hata kujenga nyumba za kuishi. Hali ambayo inapelekea leo wanaishi kwa shida na familia zao hazina mafanikio yoyote, hata watoto wao wameshindwa kuwasomesha. Nataka kujua kwa niaba yao na pengine Waziri atoe ufafanuzi ili na wao waweze kusikia kama Serikali ina taratibu gani au ina mpango gani wa kuwasaidia watu hao waliopigana vita kwa ajili ya kusaidia heshima ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua suala alilouliza Mheshimiwa B. George Simbachawene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmoja wa wazee hao na mimi nimeonana naye. Ninachoweza kusema ni kwamba, kama walistaafu kama Wanajeshi, tuna taratibu zetu ambazo tunazizingatia katika mafao. Ni kiasi gani walilipwa, inategemea ni wakati gani wamestaafu. Inawezekana shilingi 15,000 ni ndogo hivi sasa, lakini wakati ule pengine ilikuwa kubwa sana. Nazungumzia inategemea ni wakati gani walipostaafu kazi. Kwa mfano, unaweza ukakuta nilipokuwa Waziri wa Kazi, mfanyakazi ambaye alikuwa akiumia na viungo vyake vyote vinakuwa havifanyi kazi, alikuwa analipwa shilingi 108,000. Lakini 108,000 kwa wakati ule, ilikuwa anaweza akajenga nyumba za maghorofa hata 10, kwa mwaka 1966 ilikuwa ni hela nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema na hao inategemea walistaafu kazi wakati gani. Lakini nilimwambia mzee huyo kwamba, atuachie hilo suala tukalifanyie kazi, tuangalie jinsi ambavyo tunaweza tukapata ukweli uko wapi. Kama kuna stahili yoyote wanayostahili, sisi hatutasita kuwalipa, hicho ndicho nilichomwambia. Ametupa makaratasi yake na makaratasi yale tumeyachukua tumeyapeleka Dar es Salaam. Hivi sasa yapo Ngome yanafanyiwa kazi. Kwa hiyo, siwezi kuwa na jibu la haraka haraka hivi sasa, atupe muda ili kwanza, tuangalie taratibu nzima za wao kushiriki katika Jeshi, walishiriki kama akina nani, kama ni Mgambo, kama ni Wanajeshi, kama ni Jeshi la Kujenga Taifa na kadhalika. Hilo moja.

Lakini la pili, waliacha kazi kwa utaratibu upi na la tatu, maslahi gani walikuwa wakilipwa wote waliostaafu kwa wakati huo ili kuhakikisha kwamba, haki yake au haki zao zinapatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii haihusu hao wawili, inahusu na wale wengine wote, wanaofanana na hao. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Fungu 57, Programu ya 10, *Sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Wakati Mheshimiwa Waziri, akijibu hoja, mimi nilikuwa nimeuliza juu ya hatma ya wale wananchi waliopigwa. Sababu ya kwenda kwenye hospitali ya binafsi ni kwa sababu sisi hatuna hospitali yoyote ya Serikali katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Hospitali hiyo ipo karibu kilomita moja na nusu kutoka eneo ambalo tukio lilitokea. Kwa hiyo, isingewezekana kuwapeleka mbali, ambapo kuna kama kilomita 35 mpaka 40 kuweza kufika kwenye Hospitali ya Serikali. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kusema, askari kweli ni watoto wetu, tena mimi ni wakwe zangu na shemeji zangu, kwa sababu pale walipo ni mahali ambapo kuna mahusiano ya kijamii. Lakini suala dogo tu ni kwamba; je, inaruhusiwa raia kujichukulia madaraka mkononi? Kama walionewa kwa nini hawakuweza kuchukua hatua za kwenda kutafuta suluhu katika vyombo vya dola vinavyoshughulikia hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye Kambi ya Kaboya, ikishafika saa 12.00 jioni hakuna hata mwananchi anayeruhusiwa kukatisha pale kwenye Kambi. Hilo tukio lilitokea kwenye kijiji saa 3.00 za usiku, kwa maana ya kwamba hao wanajeshi waliwafuata wananchi huko. Kama ni mgogoro huo umejitokeza ni vizuri Mheshimiwa Waziri, asijibu kwamba ninatafuta pengine kuwahukumu hapana. Ninapenda mahusiano mazuri kati ya wananchi hao na wanajeshi kwa sababu wanakaa pamoja. Kwa hiyo, nilikuwa napenda pengine Mheshimiwa Waziri, aeleze vizuri umuhimu wa mahusiano hayo, badala ya kueleza kwamba, tunawahukumu na wengine wameumizwa. Mimi nadhani labda walijipiga wenyewe kwa sababu ilikuwa ni usiku wa giza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua hoja ya Mheshimiwa Ruth B. Msafiri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna askari wa Jeshi la Wananchi, wala raia wa nchi hii, anayeruhusiwa kuchukulia sheria mkononi, hatukubaliani kabisa na kitendo hicho. Ila ninachosema ni kwamba, sisi ambao ndiyo walezi kwa maana ya Waheshimiwa Wabunge, Serikali za Mitaa na Serikali nyingine zilizopo hapo, zijaribu kuangalia tatizo hili chanzo chake kimekuwa namna gani na nani ambaye alifanya makosa na wenye kuhusika wataadhibiwa. Ila kusema wale walifanya makosa hivi sasa, si vizuri. Tuache uchunguzi huo ufanyike ukamilike. Kwa mfano, mimi nilipokuwa nikizungumza ni kwamba, sisi tuliletewa taarifa kwamba, kuna Maaskari waliumia, sasa ukisema walijipiga wenyewe, mimi sijui, inawezekana kweli walijipiga wenyewe kama alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini acha uchunguzi utudhihirishie kama walijipiga wenyewe katika giza lile. Mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba,

sisi kama Wizara na sisi kama Jeshi, huwa hatuvumilii vitendo vya utovu wa nidhamu, vinachafua sifa nzuri ya Jeshi letu. Hili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ruth B. Msafiri kabisa na yeyote atakayebainika, atachukuliwa hatua kali za kinidhamu. Wapo ambao huwa wanafukuzwa kazi na wapo ambao huwa wanafungwa kwenye jela zetu za kijeshi. Kwa hiyo, atupe nafasi, uchunguzi ufanyike na ukamilike, wenye hatia wajulikane.

**MWENYEKITI:** Nadhani ni sahihi. Tunakwenda kwa Mheshimiwa John M. Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Nitatumia kifungu ambacho umeshakutubalia tukitumie kwa hiyo sitakitaja.

Kambi ya Upinzani, imezungumzia juu ya kuwapatia makazi wanajeshi. Tumeonesha kutoridhika na dhana ya kukopa kutoka Taasisi ya Hifadhi za Jamii kama *NSSF*. Nilikuwa naangalia hapa hesabu za Wizara hii, sioni hata kipengele kimoja ni jinsi gani shilingi bilioni 21, zitaweza kurudishwa kwa *NSSF*. Kama kila upande wa Serikali utakopa fedha kwenye Mifuko hii na juzi nimeona kuna Wizara nyingine imekopa kama shilingi bilioni 41, itafika mahali Mifuko hiyo itakuwa haina fedha, wakati zinahitajika kwa ajili ya watumishi ambao wanastaafu kazi.

Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo, hizo fedha ambazo wamekopa watazirudisha kwa njia gani? Pia nimefurahishwa na taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri kwamba, yeye hapendelei kutumia Jeshi kibiashara. Tunafahamu kuwa kumekuwa na wakati ambapo Jeshi linajenga nyumba mbalimbali. Nataka kujua tu kama Jeshi likilipwa na Serikali; hizo fedha zinakwenda wapi; ni fedha za Jeshi au ni fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na *accounting* yake inakuwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu, naomba kupata ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ufafanuzi juu ya hoja ambazo amezieleza Mheshimiwa John M. Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, ametoa hoja kidogo naiona kama ni mpya ya kusema kwamba, wao Kambi ya Upinzani, wamesema hawakufurahishwa na Wizara hii kukopa kutoka *NSSF*. Kwa sababu ukizingatia mchango wa Waziri Kivuli, pale ambapo alikuwa akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, aliunga mkono ukopaji huo, ila akasema ni vizuri vikaangaliwa na vyanzo vingine ili kuharakisha utatuzi wa jambo hili ambalo ni kero. Ndivyo alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nije basi tunalipa namna gani hizo fedha ambazo tunakopa kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa John M. Cheyo, fedha hizo tumekopa na si sadaka. Kwa tathmini iliyofanywa ya kiuchumi, Mfuko wa *NSSF* wameona ni endelevu *(sustainable)* na sisi

tutalipa kutokana na *allocation* za bajeti tunazopewa na Serikali kila mwaka. Tumekadiria kulipa mkopo huu kwa miaka minane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana kulipa mkopo huu kwa miaka minane kwa riba, wala siyo kwamba, tutarudisha fedha hizo jinsi tulivyokopa, hapana. Tutazilipa fedha hizo kwa riba ambayo tume-*negotiate* tukakubaliana.

Kwa hiyo, ni mkopo ambao tulikwenda kukopa kama mtu mwingine yeyote anavyokwenda kukopa, wao wakaona ni *sustainable* na sisi tukaona unajibu hoja yetu ya ujenzi wa nyumba hizo na tukaendelea. Ndiyo maana wakaweza kutuongeza mkopo wa pili wa kununua mitambo. Kwa hiyo, si sadaka, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tutalipa na hatutatumia fedha ambazo ni za wafanyakazi, walizowekeza pale kama vile kudanganya, hapana. *(Makofi)*

La pili, ndiyo maana nikasema Jeshi kama Jeshi, haliingii katika kufanya biashara, lakini ipo JKT. JKT ni *economic wing,* ni kama vile dirisha la wafanyabiashara la Jeshi. Hii JKT imeanzisha Kampuni ambayo inaitwa SUMA JKT. SUMA JKT yenyewe inafanya kazi kama mkandarasi mwingine yeyote. Kwa hiyo, inaweza ikashtaki na ikashtakiwa. Kwa hiyo, fedha zinapolipwa zinaingia katika mzunguko wake. Lakini SUMA JKT inajua mwenye hisa ni JKT kwa hiyo ni lazima ilipe *dividend*. Inapolipa *dividend,* ndiyo inasaidia sasa katika kuendesha mipango fulani ya Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo, inaipunguzia Serikali mzigo katika kulihudumia Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeuliza *specific questioin* kwamba, nimeangalia makadirio haya, nilikuwa nataka kipengele ambacho kinasema kurudisha fedha za *NSSF, allocation* yake iko wapi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hatuwezi kuiweka hapo. Kwa mfano, ukiangalia *development,* kasma ile ya 57, kuna fedha imeandikwa shilingi bilioni 54. Katika shilingi bilioni 54 hizo, kuna fedha za kulipa madeni ya magari ambayo tumenunua na zana mbalimbali na kuna deni la *NSSF* lipo ndani yake. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote* 57, Programu ya 10, *Sub-vote* 1001, *item* 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulimwengu wa leo wa sayansi na teknolojia, hali ya Jeshi la nchi yoyote inajulikana, hata kama nchi husika ikiamua kuficha. Kwa mfano, sisi Tanzania, tukiamua kuficha kama tuna silaha chakavu, wakubwa wa dunia wanajua. Lakini cha msingi, tunatakiwa tuwe na Jeshi dogo, lenye utaalamu wa kutosha na silaha za kisasa. Je, katika hili sisi tuko vipi? La pili, mahusiano yetu na nchi jirani, tunalingana namna gani katika mambo hayo? Asante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali la kwanza unataka utujibu hapa tuwaambie ulimwengu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema, labda nitajibu kipengele cha kwanza tu. Katika ulimwengu wa kisasa, nchi ikiwa na Jeshi si siri. Nataka nimhakikishie, nchi nyingi ikiwemo Tanzania, majeshi yake ni siri. Upo ushahidi wa kutosha, hata hivi sasa kuna nchi hizo kubwa alizozisema, zimekwenda zimevamia nchi kwa sababu tofauti ambazo walidhani zipo na wakajikuta kwamba kumbe sababu hizo si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unafahamu na kama ingekuwa ni rahisi kiasi hicho ninachosema, basi ingekuwa hakuna haja hata ya upelelezi unaoendelea hivi sasa. Lakini tunapelelezwa usiku na mchana. Kwa hiyo, mimi nataka nikuhakikishie kwamba, Jeshi letu linajua kuficha siri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli suala lile lilikuwa sio sahihi kwa kikao kama hiki.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Mimi niko kwenye *Vote* 57, Programu ya 10, *sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri.

Wakati nachangia asubuhi, nilizungumza suala la yule askari mstaafu, Said Abdallah Bakar. Nilipata taarifa kwamba, amestaafishwa lakini baada ya kurudi na kumwuliza akanithibitishia kwamba, yeye hajastaafishwa na nilipomwona yule mama anayehusika na Shughuli za Bunge hapa akaniambia basi lete *documents* zake, tufuatilie lakini bahati mbaya tumekaa karibu mwaka mzima hata kuwasiliana hatuwasiliani.

Kwa hiyo, nikawa na wasi wasi kwamba, inawezekana kweli ameshastaafishwa lakini maslahi yake yamemalizikia huku huku juu, yeye hayakumfikia. Naomba maelezo na ninasikitika Mheshimiwa Waziri wala Naibu Waziri, hilo suala wakati wa kufanya majumuisho, hawakuligusia. Mheshimiwa Waziri naomba maelezo.

Lakini la pili, Mheshimiwa Waziri katika bajeti ya mwaka jana wakati nachangia suala hili hili, nilikuomba utakapokuja Pemba, uweze kumfikia huyu askari angalau kumfariji na Waziri akaahidi kwamba angefika, lakini mpaka leo bado hajafika na vilevile safari hii bado hajasema lolote. Naomba maelezo, asante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua masuala hayo mawili kama ifuatavyo: Ni kweli hilo suala nimejaribu kumwuliza afisa mhusika na ameniambia ni kweli alikutana na Mheshimiwa Mbunge. Baada ya kulileta hapa tena tumelipokea na tutakwenda kulifanyia ufuatiliaji wa karibu zaidi ili tuweze kujua. Taarifa alizonipa afisa yule ni kwamba, kweli taarifa zilizoko zinaendelea kuonesha kwamba alikuwa amestaafu. Lakini tumekubaliana kwamba, tutatumia maafisa wetu walioko huko kwenda kumtembelea na kukaa naye ili aweze kutoa historia yake kamili ili iweze kujulikana ukweli uko wapi, kuliko kuendelea kubishana hapa Bungeni. Suala la pili la Pemba, ilikuwa nitakapotembelea Pemba nifike kumtembelea. Sasa kwa bahati mbaya sijafika

Pemba. Kwa hiyo, sijaweza kumtembelea kwa sababu sijafika Pemba. Nitakapofanya ziara kwenda Pemba kutembelea vikosi vyangu, naendelea kurudia na kuahidi tena, nitamtembelea ili nimwone hali yake.

**MWENYEKITI:** Asante. Lakini kama huyo aliyepewa *document* ni afisa anayesaidia ofisi yako, basi huyo ni ofisa sio mama. Mimi nikashangaa kuona kwamba, unampa mama tu *documents* muhimu sasa inakuwaje! Tofautisheni bwana mtu akiwa kazini anaitwa ofisa, akiwa mama nyumbani anaitwa mama. Kwa hiyo, nadhani imeeleweka. *(Kicheko/Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .. … … Sh.184,552,280
Kif. 1003 - *Policy and Planning…* … … Sh.482,569,080
Kif. 2001 – *Industries, Construction and Agriculture*...Sh.246,828,160

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 38 - Ulinzi**

Kif. 1001 *Administration and General…* … … Sh.203,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service Force…* … Sh.203,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 2001 – *Industries, Construction and Agriculture*...sh. 54,028,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
*Bunge lilirudia*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa taarifa, naomba kumtambua Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magomeni, ambaye naye alichangia kwa maandishi na nilimruka wakati natamka orodha ya Waheshimiwa Wabunge, waliokuwa wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mwaka 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liyakubali. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru kwa kazi njema. Vikosi vyetu vyote vya Majeshi na pia sisi wote tuliopitia *National Service,* tunafahamu jinsi tulivyokuwa wakakamavu. Kwa hiyo, nadhani hii azma ya Serikali kurudisha jeshi hili ni jambo zuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja tu. Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi, ambaye ndiyo Spika, anaeleza kwamba, kesho tarehe 2 Agosti, 2007, saa 7.30 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi, kwa maana Kamati ya Wenyeviti wote katika Ukumbi wa Spika, saa 7.30 nadhani baada ya kuahirisha hapa kesho.Baada ya kusema hayo, napenda kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.09 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 2 Agosti, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*